JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# TUME YA MABADILIKO YA KATIBA

# MAONI YA MABARAZA YA KATIBA KUHUSU RASIMU YA KATIBA YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

DISEMBA, 2013

# YALIYOMO

**UTANGULIZI** ........ **iv**

**UTANGULIZI WA RASIMU** ........ **1**

**SURA YA KWANZA YA RASIMU** ........ **4**

1.0 SEHEMU YA KWANZA: MIPAKA, ALAMA, LUGHA,UTAMADUNI NA TUNU ZA TAIFA ........ 4

1.1 SEHEMU YA PILI: MAMLAKA YA WANANCHI UTII, NA HIFADHI YA KATIBA ........ 28

**SURA YA PILI YA RASIMU** ........ **39**

2.0 MALENGO MUHIMU, MISINGI YA MWELEKEO WA SHUGHULI ZA SERIKALI NA SERA ZA KITAIFA ........ 39

**SURA YA TATU YA RASIMU** ........ **52**

3.0 SEHEMU YA KWANZA: MAADILI NA MIIKO YA UONGOZI WA UMMA ........ 52

3.1 SEHEMU YA PILI: MIIKO YA UONGOZI WA UMMA ........ 63

**SURA YA NNE YA RASIMU** ........ **69**

4.0 SEHEMU YA KWANZA: HAKI ZA BINADAMU, WAJIBU WA RAIA NA MAMLAKA ZA NCHI ........ 69

4.1 SEHEMU YA PILI: WAJIBU WA RAIA NA MAMLAKA ZA NCHI ........ 109

**SURA YA TANO YA RASIMU** ........ **115**

5.1 URAIA KATIKA JAMHURI YA MUUNGANO ........ 115

**SURA YA SITA YA RASIMU** ........ **128**

6.0 MUUNDO WA JAMHURI YA MUUNGANO ........ 128

**SURA YA SABA YA RASIMU** ........ **177**

7.0 SEHEMU YA KWANZA: SERIKALI, RAIS NA MAKAMU WA RAIS ........ 177

7.1 SEHEMU YA PILI: BARAZA LA MAWAZIRI LA SERIKALI YA JAMHURI YA MUUNGANO ........ 207

**SURA YA NANE YA RASIMU** ... **222**
8.0 URATIBU WA MAHUSIANO YA WASHIRIKA WA MUUNGANO ... 222
**SURA YA TISA YA RASIMU** ... **234**
9.0 SEHEMU YA KWANZA: KUUNDWA KWA BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO ... 234
9.1 SEHEMU YA PILI:WABUNGE ... 248
9.2 SEHEMU YA TATU:UONGOZI WA BUNGE ... 269
9.3 SEHEMU YA NNE: UTARATIBU WA SHUGHULI BUNGENI ... 278
9.4 SEHEMU YA TANO:MADARAKA NA HAKI ZA BUNGE ... 284
**SURA YA KUMI YA RASIMU** ... **287**
10.0 SEHEMU YA KWANZA: MISINGI YA UTOAJI HAKI NA UHURU WA MAHAKAMA ... 287
10.1 SEHEMU YA PILI:MUUNDO WA MAHAKAMA ... 290
10.2 SEHEMU YA TATU:TUME YA UTUMISHI WA MAHAKAMA NA MFUKO WA MAHAKAMA ... 318
**SURA YA KUMI NA MOJA YA RASIMU** ... **323**
11.0 SEHEMU YA KWANZA: UTUMISHI KATIKA JAMHURI YA MUUNGANO ... 323
**SURA YA KUMI NA MBILI YA RASIMU** ... **432**
12.0 SEHEMU YA KWANZA: UCHAGUZI KATIKA VYOMBO VYA UWAKILISHI NA VYAMA VYA SIADA ... 432
12.1 SEHEMU YA PILI: TUME HURU YA UCHAGUZI ... 437
**SURA YA KUMI NA TATU YA RASIMU** ... **456**
13.0 SEHEMU YA KWANZA:TUME YA MAADILI YA UONGOZI NA UWAJIBIKAJI ... 456
13.1 SEHEMU YA PILI:TUME YA HAKI ZA BINADAMU ... 463
13.2 SEHEMU YA TATU:MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI ... 483
**SURA YA KUMI NA NNE YA RASIMU** ... **514**

14.0 MASHARTI KUHUSU FEDHA ZA JAMHURI YA MUUNGANO ..... 514

**SURA YA KUMI NA TANO YA RASIMU ..... 548**

15.0 SEHEMU YA KWANZA: ULINZI NA USALAMA KATIKA JAMHURI YA MUUNGANO ..... 548

**SURA YA KUMI NA SITA YA RASIMU ..... 592**

MENGINEYO ..... 592

MAPENDEKEZO MAPYA ..... 598

NYONGEZA ..... 608

# UTANGULIZI

Baada ya kukamilisha kazi ya kuandaa Rasimu ya Awali ya Katiba, Tume ya Mabadiliko ya Katiba ilichapisha na kusambaza Rasimu ya Katiba katika maeneo yote nchini na katika tovuti na mitandao mbalimbali ya intaneti. Madhumuni ya hatua hiyo ilikuwa ni kuwawezesha wananchi kupitia mikutano ya mabaraza ya katiba kuichambua na kuitolea maoni Rasimu ya Katiba kwa lengo la kuiboresha. Tume iliwajibika kwa kuzingatia masharti ya Kifungu cha 18 (3) cha Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, Sura ya 83, kuunda mabaraza ya katiba katika kila wilaya, ngazi ya mamlaka za serikali za mitaa. Hata hivyo, kwa kuzingatia changamoto za kijiografia za mkoa wa Dar es Salaam na idadi kubwa ya wakazi wa Dar es Salaam, Tume iliona umuhimu wa kuongeza idadi ya Mabaraza ya Katiba na kuamua kuwa na mabaraza mawili kwa kila halmashauri za mkoa wa Dar es Salaam. Hali hiyo ilifanya jumla ya mabaraza ya wilaya, ngazi ya mamlaka ya serikali za mitaa kuwa 177 ikiwa ni mabaraza 164 kwa Tanzania Bara na mabaraza 13 kwa upande wa Zanzibar.

Mabaraza ya Wilaya yaliwakutanisha wawakilishi wa wananchi katika makundi yao mbalimbali. Wajumbe wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya walijumuisha wawakilishi wa wananchi waliochaguliwa kupitia kata zao kwa Tanzania Bara na shehia kwa upande wa Zanzibar. Uchaguzi wa wajumbe wa mabaraza ulifanywa na wananchi wenyewe kwa kuzingatia uwakilishi wa watu wazima, wanawake, vijana na jiografia ya kata au shehia husika. Wajumbe wengine wa mabaraza walikuwa ni madiwani wote waliopo katika wilaya husika. Mabaraza haya yaliwawezesha wawakilishi wa wananchi kutoa maoni juu ya Rasimu ya Katiba mpya katika mikutano iliyokuwa imeitishwa na Tume.

Tume pia ilipokea maoni juu ya Rasimu kutoka kwa mabaraza ya Katiba ya asasi, taasisi na makundi ya watu wenye malengo yanayofanana. Mabaraza hayo yaliundwa kwa mujibu wa kifungu cha 18 (6) cha Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, kinachoiwezesha Tume kuruhusu asasi, taasisi au makundi ya watu yenye malengo yanayofanana kuandaa mikutano kwa ajili ya kutoa fursa kwa wanachama wake kutoa maoni yao juu ya Rasimu ya Katiba na kisha kuwasilisha maoni hayo kwa Tume. Mabaraza hayo yalijiendesha yenyewe kwa kuzingatia mwongozo uliokuwa umetolewa na Tume. Hata hivyo, Tume iligharamia uendeshaji wa mabaraza mawili ya watu wenye ulemavu. Baraza la kwanza liliandaliwa na Shirikisho la Vyama vya Watu wenye Ulemavu Tanzania Bara (SHIVYAWATA) na baraza la pili liliandaliwa na Shirikisho la Jumuiya za Watu Wenye Ulemavu Zanzibar (SHIJUWAZA). Mabaraza hayo yaliwashirikisha watu wenye ulemavu wa aina zote.

Miongoni mwa asasi, taasisi na makundi ya watu wenye malengo yanayofanana yaliyounda mabaraza ya Katiba ni pamoja na:

(1) Jumuiya za Kidini.
(2) Vyama vya Siasa.
(3) Asasi za Kiraia.
(4) Jumuiya za Wakulima.
(5) Jumuiya za Wafugaji.
(6) Taasisi za Elimu ya Juu.
(7) Jumuiya za Wanahabari.
(8) Taasisi za Wafanyabiashara.
(9) Jumuiya za Wanawake.
(10) Jumuiya za Vijana.
(11) Jumuiya za Kitaaluma.
(12) Jumuiya za Wafanyakazi..
(13) Wizara, Idara na Taaasisi za Serikali
(14) Jumuiya za Waajiri.
(15) Jumuiya za Wanasheria
(16) Jumuiya za Watanzania waishio nje ya Nchi (Diaspora).
(17) Jumuiya za Watu wenye Ulemavu.

Mabaraza hayo yaliwawezesha wananchi kupitia asasi, taasisi au makundi yao mbalimbali kutoa maoni juu ya Rasimu ya Katiba. Kwa ujumla, kulikuwa na mabaraza 614 yaliyoundwa na asasi, taasisi na makundi ya watu wenye malengo yanayofanana.

Baada ya kupokea maoni na mapendekezo kuhusu Rasimu ya Katiba mpya, Tume ilipitia na kuchambua maoni ya wananchi na kuyaweka katika maeneo mbalimbali sambamba na ibara husika za Rasimu ya Katiba. Tume ilifanya tathmini ya maoni na mapendekezo ya Mabaraza ya Katiba kwa namna ambayo yanakubaliana na au kutokubaliana na masharti ya Ibara za Rasimu ya Katiba. Katika uchambuzi huo wa maoni ya Mabaraza, Tume ilizingatia uzito wa hoja zilizotolewa na hadidu za rejea zilizowekwa na Sheria ya Mabadiliko ya Katiba katika kuamua kubadilisha ama kubakiza vifungu vya ibara husika za Rasimu ya Katiba. Pia, Tume iliyapa hadhi sawa maoni na mapendekezo kutoka kwenye mabaraza ya aina zote mbili, kwa kuwa yote ni maoni ya wananchi.

Taarifa hii inaonyesha muhtasari wa maoni ya wananchi, kupitia mabaraza ya katiba juu ya Rasimu ya Katiba kuanzia na Utangulizi na Ibara zote 240. Taarifa inakusanya mawazo yote kwa muhtasari baada ya kuangalia kiini cha ujumbe uliokusudiwa katika maoni yaliyotolewa. Pia, taarifa hii inajumuisha sababu zilizotolewa na wananchi walipotoa maoni yao katika sehemu na Ibara husika. Hata hivyo, kuna baadhi ya vifungu ambavyo wananchi walitoa maoni bila kuainisha sababu. Ieleweke kwamba, wananchi katika mabaraza mengi ya katiba walitoa maoni katika maeneo ambayo waliona yanahitaji maboresho na hawakutoa maoni kwa maeneo walioyoona kuwa hayahitaji mabadiliko. Aidha, ingawa maoni ya wananchi yaligusa kila sehemu ya Rasimu, maoni mengi yalikuwa juu ya vifungu vinavyohusiana na mamlaka ya serikali ya muungano, mamlaka ya serikali za nchi washirika, uraia na uhamiaji, muundo wa muungano na mambo ya muungano. Maeneo mengine yaliyotolewa maoni kwa wingi na wananchi ni pamoja na maadili ya viongozi na miiko ya viongozi, haki za binadamu, masuala ya fedha, mikopo na madeni. Taarifa hii inaonyesha pia vifungu vilivyofanyiwa marekebisho kutokana na maoni ya mabaraza ya katiba. Marekebisho hayo ni pamoja na kubadili baadhi ya masharti ya ibara za Rasimu ya Katiba kwa kuondoa baadhi ya maneno, kuongeza maneno au kuandika upya vifungu vya ibara husika katika Rasimu kama inavyojionyesha katika taarifa hii. Baadhi ya vifungu vilivyorekebishwa viko kwenye ibara zinazohusu mamlaka ya wananchi, utii na hifadhi ya katiba. pamoja na utambulisho wa Jamhuri ya Muungano, ukuu wa katiba, maadili ya viongozi wa umma na miiko ya viongozi, utumishi katika Jamhuri ya Muungano. Hata hivyo, baada ya kutathmini maoni ya wananchi yaliyounga mkono ibara zibaki kama zilivyo na yale yaliyokuwa tofauti na baadhi ya vifungu vya Rasimu ya Katiba, Tume iliona ni vyema vifungu hivyo vibaki kama vilivyo.

# UTANGULIZI WA RASIMU

| ***Ibara Na.*** | ***Kichwa cha habari*** | ***Maoni ya Mabaraza*** | ***Sababu ya Maoni*** | ***Marekebisho ya Tume*** |
|---|---|---|---|---|
| | UTANGULIZI | (i) Katika utangulizi Katiba ionyeshe jinsi mamlaka kuu (sovereignity) yatakavyogaiwa baina ya nchi washirika wa Muungano kwa mambo ambayo si ya Muungano.<br>Aidha, maelezo hayo yazingatie kuwepo kwa nchi mbili huru pamoja na kutaja makubaliano ya Muungano "Articles of the Union" kuwa ni msingi mkuu wa Muungano pamoja na Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964 kama ulivyotajwa uhuru wa Tanganyika wa 1961.<br>(ii) Ili kuonyesha ya kwamba Muungano wetu uliundwa na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar na Jamhuri ya Tanganyika utangulizi usomeke. KWA KUWA, Sisi wananchi wa Tanganyika na Zanzibar tumeamua rasmi na kwa dhati kujenga katika Shirikisho la Muungano wa Jamhuri za Tanzania tunaloliunda jamii inayoheshimu na kuzingatia misingi ya utu, uhuru, haki, usawa, udugu, amani, umoja na mshikamano katika Nyanja zote za maisha yetu. | | Ubaki kama ulivyo |
| | | (iii) Utangulizi utoe fursa kwa nchi nyengine zinazotaka kujiunga na Muungano huu ziweze kujiunga, ili kujenga ile dhana ya kwamba Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ni hatua ya mwanzo tu ya Muungano mkubwa zaidi wa nchi za Afrika, ambayo ni mojawapo ya sababu iliyotajwa katika Mkataba wa Muungano katika maelezo ya utangulizi wa Mkataba | Ni utaratibu kama ule uliomo katika kifungu cha 3(1) cha Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambao unatoa uhuru na fursa kwa nchi nyengine kujiunga iwapo itakubaliana na masharti yaliyowekwa. | |

| Ibara Na. | Kichwa cha habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | wa Muungano wa 1964. | | |
| | | (iv) Aya ya kwanza iandikwe kama ifuatavyo: "KWA KUWA SISI wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tunamheshimu Mungu aliyetuumba na kutupatia nchi hii nzuri, tumeamua rasmi na kwa dhati kujenga katika nchi yetu jamii inayoheshimu na kuzingatia misingi ya utu, uhuru, haki, usawa, udugu, amani, umoja na mshikamano katika Nyanja zote za maisha yetu"; | | |
| | | (v) Utangulizi uanze kama ifuatavyo: "KWA KUWA MWENYEZI MUNGU muumba wa mbingu na nchi ametujalia nchi hii nzuri sisi wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania …"<br><br>(vi) Ni vema Katiba itambulishe nafasi za Serikali katika masuala ya DINI kuwa Serikali hazitafuata dini mahsusi bali watu wake watambuliwe na Katiba kuwa wana dini mahsusi wanazofuata ndani ya jamii inayounda Katiba hii. | (a) Kuonyesha jinsi watanzania tunavyomheshimu Mwenyezi Mungu aliyetuumba.<br>(b) Ingawa nchi yetu haina dini lakini watu wake wana dini na tunatambua uwepo wa Mwenyezi Mungu bila kujali itikadi za dini au madhehebu yetu. | |
| | | (vii) Aya ya pili ya Utangulizi isomeke kama ifuatavyo: "Serikali isiyokuwa na Dini, yenye kufuata misingi ya demokrasia, utawala bora na kujitegemea na Bunge lenye wabunge waliochaguliwa" | | |
| | | (viii) Aya ya mwisho ya utangulizi isomeke kama ifuatavyo: HIVYO BASI, KATIBA HII YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA ILIYOPENDEKEZWA NA BUNGE MAALUM LA KATIBA imetungwa na SISI WANANCHI WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA kupitia | Kwa lengo la kujenga jamii yenye kuheshimu HAKI za watu wenye DINI mbalimbali | |

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Maoni* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| | | KURA YA MAONI kwa madhumuni ya kujenga jamii kama hiyo, na kuhakikisha kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaongozwa na Serikali yenye kufuata misingi ya demokrasia na utawala wa sheria, kujitegemea na isiyofuata dini yoyote rasmi bali yenye watu wenye dini mbalimbali. | | |
| | | (ix) Katika Para ya tano neno "Umajimui" lifutwe na litafutwe neno lingine linaloleta maana kwa wepesi. | Kitumike Kiswahili chepesi ambacho kitakuwa rahisi kueleweka kwa watu wote. | |
| | | (x) Kuwepo kipengele kinachoeleza mambo ya utamaduni ambacho kitaeleza kama ifuatavyo:<br>(xi) "Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itaenzi na kuendeleza utamaduni na michezo kwa watu wote". | | |
| | | (xii) Mwisho wa utangulizi yaandikwe maneno yafuatayo:<br>"MUNGU IBARIKI TANZANIA". | | |
| | | (xiii) Katika Utangulizi iwekwe kipengele kitakachoeleza "Hati ya Makubaliano ya Muungano". | Ili kuienzi historia ya muungano. | |

# SURA YA KWANZA YA RASIMU

## 1.0 SEHEMU YA KWANZA: MIPAKA, ALAMA, LUGHA,UTAMADUNI NA TUNU ZA TAIFA

| Ibara Na. | Kichwa cha habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | (i) Kichwa cha habari kiandikwe: MIPAKA, UTAMADUNI, ALAMA, LUGHA NA TUNU ZA TAIFA. | Halikutumika. | |
| | | (ii) Neno "UTAMADUNI" katika kichwa cha habari lifutwe. | | |
| 1. | Jamhuri ya Muungano | (i) Kuwe na muundo wa Serikali mbili;<br>(ii) Tanzania ni muungano wa Nchi mbili sio shirikisho;<br><br>(iii) Kutamka neno "Shirikisho" maana yake ni nchi mbili kamili zinaungana na kuwa shirikisho zinaungana na kuwa shirikisho. Kwa msingi huu inakinzana na kifungu cha 9(2)(i) cha Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ambacho kimetamka wazi kuwa Tume itaongozwa na misingi mikuu ya kitaifa na maadili ya jamii.<br>(iv) Shirikisho ni kwenda kinyume na makubaliano ya Muungano ya mwaka 1964;<br>(v) Shirikisho la Serikali Tatu ni mzigo kwa wananchi;<br>(vi) shirikisho la Serikali tatu litasababisha mgongano wa kisiasa;<br>(vii) Muungano ni mfumo wenye | (a) Zilizoungana ni nchi sio watu.<br>(b) Matumizi ya neno hilo linapunguza maana ya Muungano na linalenga kuvunja Muungano.<br>(c) Asili ya neno Tanzania ni Tanganyika na Zanzibar, hivyo kutumia neno Tanzania Bara ni kuimeza Zanzibar.<br>(d) Linaleta utata. | Katika ibara ndogo ya (1), neno "nchi na" liongezwe kabla ya neno "shirikisho" |

| Ibara Na. | Kichwa cha habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | Serikali yenye mamlaka kamili sio Shirikisho;<br>(viii) Litumike jina moja kati ya 'shirikisho' na 'muungano'<br>(ix) Litumike Jina Tanganyika badala ya Tanzania Bara<br>(x) Neno "watu wa Zanzibar" lifutwe isomeke "Zanzibar".<br>(xi) Neno "Shirikisho" lifutwe liandikwe "nchi".<br>(xii) Neno Shirikisho lisifutwe.<br><br>(xiii) Katika ibara ndogo ya (1) na (3) neno "ya" libadilishwe isomeke "za"<br><br>(xiv) Neno shirikisho ndio msingi muhimu wa Serikali tatu. | | |
| | | (xv) Katika Ibara ndogo ya (1) inapendekezwa maneno "…Shirikisho lenye mamlaka kamili" yatolewe na badala yake yawekwe maneno "Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi yenye mamlaka kamili ambayo imetokana na Muungano wa nchi mbili".<br>(xvi) Neno Shirikisho linapunguza maana ya Muungano. | Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haiwezi kuelezeka kuwa ni shirikisho kwani shirikisho ni mfumo wa Serikali au utawala na hakiakisi nchi bali Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi yenye mamlaka kamili. | |
| | | (xvii) Ibara ya 1 ibadilishwe na iandikwe kama ifuatavyo:<br>"(1) Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mamlaka kamili | Tanzania ni nchi moja yenye mamlaka kamili. | |

| Ibara Na. | Kichwa cha habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | ambayo imetokana na Muungano wa Nchi mbili za Jamhuri ya Tanganyika na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar wa mwaka 1964.<br>(2) Jamhuri ya Muungano ni nchi ya kidemokrasia inayofuata mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa, Usawa wa binadamu, kujitegemea, utawala wa sheria na kuheshimu haki za binadamu”. | | |
| | | (xviii) Jina rasmi la nchi liwe Jamhuri za Muungano wa Tanganyika na Zanzibar | | |
| | | (xix) Ibara 1(1) Maneno “Shirikisho lenye mamlaka kamili” yatolewe na isomeke “Jamhuri ya Muungano ni nchi yenye mamlaka kamili ambayo imetokana na Muungano wa nchi mbili…” | | |
| | | (xx) Makao Makuu ya mihimili ya dola yawe maeneo tofauti katika sehemu zote mbili za muungano.<br>(xxi) Makao Makuu ya mihimili ya dola yawe maeneo tofauti katika sehemu zote mbili za muungano. | | |
| | | (xxii) Utambulisho wa Jamhuri ya Muungano ujumuishe misingi ya demokrasia, vyama vingi, usawa, utawala wa sheria na haki za binadamu. | | |
| | | (xxiii) Utambulisho wa Jamhuri ya Muungano ujumuishe misingi ya demokrasia, vyama vingi, usawa, utawala wa sheria na haki za | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | binadamu. | | |
| | | (xxiv) Haki ya kujitoa kwenye muungano iwepo | | |
| | | (xxv) Haki ya kujitoa kwenye muungano iwepo | | |
| | | (xxvi) Ibara ndogo ya (1) ibadilishwe na iandikwe kama ifuatavyo:<br>(xxvii) "(1) Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Shirikisho lenye mamlaka kamili ambayo imetokana na Muungano wa nchi mbili za Jamhuri ya Tanganyika na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar ambazo kabla ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar mwaka 1964". | | |
| | | (xxviii) Ibara ndogo ya (1) ibadilishwe na iandikwe kama ifuatavyo:<br>"(1) Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Shirikisho lenye mamlaka kamili ambayo imetokana na Muungano wa nchi mbili za Jamhuri ya Tanganyika na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar ambazo kabla ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar mwaka 1964". | | |
| | | (xxix) Ibara ndogo ya (2) inapendekezwa isomeke kama ifuatavyo:<br>(xxx) "Jamhuri ya Muungano ni nchi ya kidemokrasia, isiyokuwa na dini, inayofuata mfumo wa vyama vingi vya siasa, usawa wa binadamu, kujitegemea, utawala wa sheria na kuheshimu haki za binadamu." | | |
| | | (xxxi) Hati ya makubaliano ibaki kuwa | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | ni msingi wa makubaliano ya Tanganyika na Zanzibar kama ilivyotambuliwa kwenye Ibara 1(1) na isiwe ndiyo dhamana ya msingi wa Katiba hii kwani Katiba hii ni makubaliano ya Wananchi wote. | | |
| | | (xxxii) Iongezwe ibara ndogo mpya itakayoweka utaratibu wa kurekebisha Makubaliano ya Muungano. | Ndio iwe msingi wa kubalidisha makubaliano ya Muungano. | |
| | | (xxxiii) Maneno "Hati ya Makubaliano" yafutwe na badala yake yasomeke "Makubaliano ya wananchi" na ibara hiyo iandikwe kama ifuatavyo:<br>(xxxiv) "1(1) Makubaliano ya wananchi ndio msingi mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na yatalindwa na Katiba hii kwa kadri itakavyokuwa ikirekebishwa". | | |
| | | (xxxv) Ibara ndogo ya (2) irekebishwe kwa kuweka mfumo wa serikali mbili. | Serikali Tatu:<br>(a) zitavunja makubaliano ya Muungano;<br>(b) zitavunja umoja wa kitaifa;<br>(c) zinaweza kuleta mgongano katika umiliki wa mali na kimaslahi. | |
| | | (xxxvi) Ibara ndogo ya (1) irekebishwe kwa kufuta neno "Shirikisho" na badala yake litumike neno "nchi". | (a) Inasababisha mkanganyiko kwa kueleza Muungano na Shirikisho.<br>(b) Sio sahihi kutumia neno Muungano na | |

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Maoni* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| | | | Shirikisho kwa wakati mmoja.<br>(c) Linaleta utata. | |
| | | (xxxvii) Ibara ndogo ya (1) irekebishwe ili isomeke kama ilivyo Katiba ya sasa. | Kuipa nguvu Katiba. | |
| | | (xxxviii) Ibara ndogo ya (2) yaongezwe maneno "isiyokuwa na dini" mwisho wa sentensi. | Ili ijulikane waziwazi kuwa Serikali haina dini. | |
| | | (xxxix) Ibara ndogo ya (1) irekebishwe kwa kufuta neno "Shirikisho" na badala yake litumike neno "nchi". | (d) Inasababisha mkanganyiko kwa kueleza Muungano na Shirikisho.<br>(e) Sio sahihi kutumia neno Muungano na Shirikisho kwa wakati mmoja.<br>(f) Linaleta utata. | |
| | | (xl) 1(2) isomeke, "Jamhuri ya Muungano ni nchi ya kidemokrasia,isiyokuwa na dini, inayofuata mfumo wa vyama vingi vya siasa, usawa wa binadamu, kujitegemea, utawala wa sheria na kuheshimu haki za binadamu." | | |
| | | (xli) Ibara ndogo ya (2) inapendekezwa, ibadilishwe na iandikwe kama ifuatavyo:<br>(xlii) "(2) Jamhuri ya Muungano ni shirikisho la kidemokrasia na kijamaa linalofuata mfumo wa vyama vingi vya saisa, usawa wa binadamu, kujitegemea, utawala wa sheria na kuheshimu haki za | Nchi yetu toka ilipoasisiwa ilijengeka katika kufuata misingi ya ujamaa na kujitegemea iliyojaa utu, haki, usawa na ushirikiano baina ya watu wake hivyo ujamaa na demokrasia vikienda kwa pamoja tutajenga taifa lenye ustawi. | |

| Ibara Na. | Kichwa cha habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | binadamu." | | |
| | | (xliii) Ibara ndogo ya (2) maneno "mfumo wa vyama vya siasa na usawa wa haki za binadamu" yafutwe. | (a) Kila nchi itasimamia vyama vya siasa yenyewe.<br>(b) Vyama vya siasa na haki za binadamu hazikuwemo katika hati ya makubaliano ya Muungano. | |
| | | (xliv) Ibara ndogo ya (3) iboreshwe kwa kueleza kuwa Hati ya Muungano ni sehemu ya Katiba. | Ili hati hiyo isiwe chini ya Katiba.<br>Ili wananchi waifahamu Hati hiyo. | |
| | | (xlv) Kuwe na Nyongeza ya Pili katika Rasimu ya Katiba itakayoeleza Hati ya Muungano. | (a) Kuipa nguvu Katiba.<br>(b) Nchi Washirika kuifuata Katiba katika kutunga katiba zao.<br>(c) Ili wananchi waifahamu Hati hiyo. | |

| Ibara Na. | Kichwa cha habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | (xlvi) Ibara ndogo ya (3) irekebishwe na iandikwe kama ifuatavyo:<br>(xlvii) "(3) Makubaliano ya wananchi ndiyo Msingi Mkuu wa Jamhuri ya Mungano wa Tanzania na Katiba hii kwa kadri yatakavyorekebishwa itakuwa ni mwendelezo wa makubaliano hayo." | (a) Italeta utatanishi mkubwa kwa kuwa Hati ya Muungano inazungumzia Serikali mbili tofauti na Rasimu inayopendekeza serikali tatu;<br>(b) Katiba mpya haiwezi kuwa mwendelezo wa Hati ya makubaliano ya Muungano ya 1964.<br>(c) Iwapo Rasimu ya Katiba msingi wake ni huo maneno "upon union day and forever after" hayaruhusu kurekebisha au kuvunjwa kwa Muungano. | |
| | | (xlviii) Ibara ndogo ya (3) ifutwe. | | |
| | | (xlix) Iongezwe ibara ndogo mpya ya (4) ambayo itaeleza Makao Makuu ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo itakuwa Dar es Salaam, Makao Makuu ya Mahakama ya Rufaa na Mahakama ya Juu itakuwa Zanzibar na Makao Makuu ya Bunge itakuwa Dodoma. | | |
| | | (l) Ibara 1(3) isomeke: "Hati ya | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | Makubaliano ya Muungano iliyorejewa katika ibara 1(1) ndiyo msingi mkuu wa Jamhuri ya Muungano waTanzania." | | |
| | | (li) Iongezwe ibara ndogo mpya itakayoeleza makubaliano ya Muungano ya mwaka 1964, na kisha hati ya muungano iwekwe kwenye nyongeza mwisho wa Rasimu. | Hati ya Makubaliano ya Muungano hairuhusu mabadiliko. | |
| | | (lii) Ibara ndogo ya (3) ifutwe. | | |
| | | (liii) Ibara ndogo ya (3) ifutwe na badala yake iandikwe kwa mfumo wa Muungano wa Serikali Moja. | | |
| | | (liv) iongezwe ibara ndogo nyingine kuzungumzia makao makuu ya Jamhuri ya Muungano kuwa ni Dar Es Salaam. | | |
| | | (lv) Iongezwe ibara ndogo mpya ya (4) itakayoruhusu nchi nyingine zikitaka ziweze kujiunga na shirikisho hili. | | |
| | | (lvi) Mfumo wa uchumi wa nchi ubainishwe kwenye katiba | | |
| | | (lvii) Ibara ndogo ya (3) maneno "kadri itakavyorekebishwa" yafutwe.<br>(lviii) Katika ibara ndogo ya (1), neno "nchi na" liongezwe kabla ya neno "shirikisho"<br>(i) | | |
| 2. | Eneo la Jamhuri ya Muungano | (i) Maneno "Tanzania Bara" yafutwe na badala yake iandikwe "Tanganyika"; | (i) Neno "Tanganyika" ndilo lililotumika wakati wa makubaliano ya Muungano mwaka | Katika Ibara ya (2) na mahali pengine popote kwenye rasimu hii neno Tanzania Bara |

| Ibara Na. | Kichwa cha habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | 1964; | lisomeke “Tanganyika.“ |
| | | (ii) Neno “Zanzibar” liandikwe “Tanzania Visiwani”; | | |
| | | (iii) Isomeke” eneo lote la Tanzania Bara na eneo lote la Zanzibar pamoja na sehemu zake zote za bahari, maziwa, mito na maeneo mengine yatakayoongezwa.” | | |
| | | (iv) Yaongezwe maneno “mito, maziwa na vyanzo vyote vya maji” mwisho wa sentensi; | | |
| | | (v) Ibara hii iandikwe kama ifuatavyo: “Eneo la Jamhuri ya Muungano ni pamoja na bahari, maziwa, mito na anga na eneo lote la Zanzibar ikijumuisha sehemu yake ya bahari na anga”; “Eneo la Jamhuri ya Muungano linajumuisha nchi kavu na sehemu yote ya bahari ya hindi, ziwa nyasa, ziwa Tanganyika na ziwa Viktoria”; | (a) Tanzania inapakana na nchi mbalimbali baharini, katika maziwa, mito na nchi kavu, ni vyema mipaka ikatambulika ili kuepusha migogoro na nchi zinazopakana nazo hapo baadae; (b) Usalama unahusisha nchi kavu, baharini na angani. (c) Tanzania inapakana na nchi mbalimbali baharini, katika maziwa, mito na nchi kavu, nivyema mipaka ikatambulika ili kuepusha migogoro na nchi zinazopakana nazo hapo baadae; (d) Usalama unahusisha nchi kavu, baharini na angani. | |

| Ibara Na. | Kichwa cha habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | (vi) Ibara ya 2 ifutwe na badala yake isomeke kama ifuatavyo: "Eneo la Jamhuri ya Muungano ni eneo lote la Tanzania Bara na eneo lote la Zanzibar pamoja na sehemu zake zote za bahari, maziwa, mito na maeneo mengine yatakayoongezwa." | Mipaka ya Tanzania Bara na Zanzibar imezungukwa na bahari, maziwa na mito hivyo ni vyema viashiria vyote vya mipaka vikatajwa. Vile vile kuna uwezekano wa kupanuka/ kupanuliwa kwa mipaka ya nchi. | |
| | | (vii) Ibara hii irekebishwe ili iainishe eneo la Tanganyika na mipaka yake na eneo la Zanzibar na mipaka yake na pamoja na eneo la Ukanda wa Bahari Kuu (EEZ). | | |
| | | (viii) Makubaliano ya Exclusive Economic Zone na mipaka ya nchi Washirika yabainishwe kikatiba. | | |
| | | Nchi zote mbili ziainishwe mipaka yake.<br>(ii) Maneno visiwa, maziwa yaongezwe.<br>(iii)Ibara hii ifutwe. | (a) Ili kuondosha migogoro.<br>(b) Kulinda usalama wa nchi.<br>(c) Haikuonesha mipaka ya Washirika wa Muungano. | |
| | | (ix) Ibara hii irekebishwe ili mipaka ya kila nchi itajwe kwa idadi ya kilomita za mraba. | Kuondoa utata unaoweza kutokea na nchi jirani. Rasimu haikuonesha mipaka ya Washirika wa Muungano. | |
| | | (x) Katika ibara hii maneno "Tanzania Bara" yafutwe na badala yake iandikwe "Tanganyika;" | (a) Neno "Tanganyika" ndilo lililotumika wakati wa makubaliano ya Muungano mwaka 1964;<br>(b) Hakujawahi kuwepo | |

| Ibara Na. | Kichwa cha habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | nchi inayoitwa Tanzania Bara, bali kulikuwepo nchi ya Tanganyika kabla ya hati za Makubaliano ya Muungano;<br>(c) Katika hati ya makubaliano ya Muungano nchi zilizoungana ni Tanganyika na Zanzibar, hakukuwa na nchi nayojulikana kwa jina la Tanzania Bara.<br>(d) kutambuliwa kwa Jamhuri ya watu wa Tanganyika ili kuonyesha uzalendo wa utu wa watanganyika kama ilivyo kwa Jamhuri ya watu wa Zanzibar. | |
| | | (xi) Iongezwe ibara ndogo mpya ya (2) na (3) ambazo zitatoa tafsiri ya mipaka ya Tanganyika na Zanzibar, zitakazosomeka kama ifuatavyo:<br>"(2) Tanganyika ni nchi ambayo eneo la mipaka yake ni eneo lote ambalo kabla ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar liliitwa Jamhuri ya Tanganyika, pamoja na eneo lake la bahari."<br>"(3) Zanzibar ni nchi ambayo eneo la mipaka yake ni eneo lote la visiwa | Masuala ya utafutaji mafuta na gesi asilia na uvuvi katika bahari kuu sio mambo ya Muungano tena, kwa hiyo ni lazima mipaka ya washirika wa Muungano itajwe wazi ili kuepuka migogoro ya mipaka wakati wa utafutaji au uchimbaji wa mafuta na gesi asilia katika bahari kuu au shughuli za uvuvi katika eneo la bahari kuu. | |

| Ibara Na. | Kichwa cha habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | vya Unguja na Pemba na visiwa vidogo vinavyoizunguka ambavyo kabla ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar iliitwa Jamhuri ya watu wa Zanzibar.” | | |
| | | (xii) Ibara hii irekebishwe ili ibaki kama ilivyo Katiba ya sasa. | | |
| | | (xiii) GPS Longitudo na latitudo zitumike kubainisha mipaka | | |
| | | (xiv) Eneo la Jamhuri lijumuishe sehemu ya anga, bahari, na ardhi ya Zanzibar na Tanganyika | | |
| | | (xv) Rasilimali za mipakani zibainishwe | Kulinda raslimali na usalama wa nchi. | |
| | | (xvi) Ugawaji wa nchi katika mikoa umshirikishe Rais wa Zanzibar | Ili kuondosha migogoro. | |
| 3. | Alama na Siku Kuu za Taifa | (i) Maelezo ya pembeni (marginal note) yasomeke “Alama za Taifa na Sikukuu za Kitaifa”. | Ili kuondoa mkanganyiko baina ya sikukuu za Taifa na Sikukuu za Kitaifa, na iweze kutoa fursa kwa siku nyingine kutangazwa kuwa sikukuu za Kitaifa kwa mujibu wa sheria zitakazotungwa. | 1. Ibara ibaki kama ilivyo.<br>2. Katika Ibara ya (2), 2(d) na ya 3 neno “siku kuu” lisomeke “sikukuu” |
| | | (ii) Maelezo ya pembeni (marginal note) yasomeke “Siku Kuu za Kitaifa na Siku ya Taifa”. | | |
| | | (iii) Siku Kuu za Kitaifa na Siku za Taifa zitajwe kwenye katiba | Ni alama zinazoitambulisha Jamhuri ya Muungano | |
| | | (iv) Skukuu za kitaifa zifutwe ziingizwe kwenye sheria. | (a) Zikiwa kwenye sheria ni rahisi kuziongeza au kuzipunguza;<br>(b) Sikukuu za kitaifa zinaweza kubadilika kwa kuongezeka au | |

| Ibara Na. | Kichwa cha habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | kupungua, hivyo itakuwa ni rahisi kuifanyia Sheria ya kawaida marekebisho kuliko Katiba ambayo utaratibu wa kuifanyia mabadiliko ni mrefu. | |
| | | (v) Ibara hii iandikwe upya kwa kuzingatia mazingira ya sehemu zote mbili za Muungano. | (a) Washirika wa Muungano (Tanganyika na Zanzibar) wakubaliane kuanzisha wimbo, nembo na bendera mpya za Taifa zitakazozingatia usawa wa uwakilishi wa nchi zote mbili. Katika kutengeneza mambo yote matatu mambo yafuatayo yazingatiwe.<br>(i) Viongozi wa kwanza wa Zanzibar huru na Tanganyika huru.<br>(i) Raslimali za Zanzibar na Tanganyika<br>(ii) Utamaduni wa Zanzibar na Tanganyika<br>(iii) Watu na silka za Zanzibar na Tanganyika. | |
| | | (vi) Bendera iwe na rangi zinazoashiria nchi zote mbili, nyeupe kuashiria amani, kijani kuashiria kilimo kwa upande wa Tanganyika, buluu | Rangi iliyomo katika bendera ya sasa inaashiria upande mmoja wa Shirikisho. | |

| Ibara Na. | Kichwa cha habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | kuashiria bahari kwa upande wa Zanzibar na nyeusi kuashiria watu (kwa | | |
| | | (vii) Katika Ibara ndogo ya (2) ziongezwe sikukuu ya kumbukumbu ya kifo cha Baba wa Taifa tarehe 14/10 na Rais Karume tarehe 7/4. | Kuwaenzi waasisi wa Muungano na Historia ya nchi yetu. | |
| | | (viii) Aya (c) ya Ibara ndogo ya (2) maneno "ambayo pia ni Siku ya Taifa" yaongezwe baina ya maneno "Zanzibar" na "itakayoadhimishwa". | | |
| | | (ix) Ibara ndogo ya (2)(d) na (3) zifutwe na badala yake kuwekwa ibara ndogo ifuatayo:<br>"(3) Kutakuwa na siku kuu nyingine za kitaifa zitakazowekwa kwa mujibu wa sheria itakayotungwa na Bunge". | | |
| | | (x) Utamaduni wa Taifa uwe moja ya alama za Taifa | Ili kuwa na sura ya kimuungano | |
| | | (xi) Siku Kuu ya Shirikisho iwe ni siku pekee ya kitaifa zingine zibaki kwa washirika.<br>Siku Kuu ya shirikisho itumike badala ya siku ya Muungano. | Iwe sikukuu ya Taifa. | |
| | | (xii) utamaduni wa nchi, Vazi la Taifa, Wimbo wa Taifa wa washirika, Kitambulisho cha Taifa viwe Alama ya Taifa | Kuonyesha mamlaka kwa nchi Washirika. | |
| | | (xiii) Nembo ya Taifa kuwa na viashiria vya pande zote mbili | Alama zilizopo sasa zina vielelezo vyote vya Tanganyika. | |
| | | (xiv) Alama za Taifa ziwekwe kwenye sheria na siyo katiba | Ni rahisi kuifanyia Sheria ya kawaida marekebisho | |

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Maoni* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| | | | kuliko Katiba | |
| | | (xv) Siku za Ibada zitajwe kwenye katiba | | |
| | | (xvi) Rangi za bendera zisibadilishwe bila ridhaa ya wananchi.<br>Rangi za Bendera zitajwe kwenye katiba | | |
| | | (xvii) Twiga atumike kama Alama ya Taifa | | |
| | | (xviii) Wimbo wa Taifa usifanane na za nchi zingine<br>Wimbo wa Taifa na maneno yake uwekwe kwenye katiba | | |
| | | (xix) Ibara hii ibaki kama ilivyo. | | |
| | | (xx) Tarehe ya uhuru wa Zanzibar wa 1963 iingizwe katika orodha ya sikukuu ya Taifa. | Iwe sikukuu ya Taifa. | |
| | | (xxi) Ibara hii isomeke kama ifuatavyo:<br>“Kutakuwa na sikukuu za kitaifa zitakazoratibiwa na sheria zitakazotungwa na Bunge. | | |
| | | (xxii) Katika Ibara hii iongezwe alama zifuatazo kama alama za Taifa:<br>Vazi la Taifa;<br>Fedha ya Taifa; na<br>Mwenge wa Uhuru. | | |
| | | (xxiii) Ibara ndogo ya (1) isomeke “alama na sikukuu za Shirikisho”. | Utaifa upo katika nchi Washirika na sio katika Muungano. | |
| | | (xxiv) Nembo ibadilishwe iwe na alama zifuatazo:<br>(a) Ramani ya Zanzibar na ya Tanganyika.<br>(b) Mazao ya kilimo ya pande | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | zote mbili mfano karafuu, pamba. | | |
| | | (xxv) Ibara ndogo ya (2)(a) na (b) zifutwe | | |
| | | (xxvi) Ibara ndogo ya (2)(d) yaongezwe maneno "nchi Washirika". | Sikukuu zisherehekewe na nchi Washirika wenyewe. | |
| | | | | |
| 4. | Lugha ya Taifa na lugha za alama | (i) Katika ibara ndogo ya (1) maneno "na kiserikali" yafutwe na badala yake iandikwe "katika mihimili yote ya dola". | Ili kuweka msisitizo wa kutumia lugha ya Kiswahili katika shughuli zote Serikalini. | 1) Ibara ndogo ya (1) ibaki kama ilivyo.<br>2) Ibara ndogo ya (2) iongezewe maneno, "au lugha nyingine" baada ya neno kiingereza<br>3) Ibara ndogo ya (3) isomeke, "serikali itaweka mazingira yatakayowezesha kuwepo kwa mawasiliano mbadala zikiwemo lugha za alama, maandishi, yaliyokuzwa na nukta nundu kwenye sehemu muhimu za umma na katika vyombo vya habari |
| | | (ii) Katika ibara ndogo ya (1) yaongezwe maneno yafutayo:<br>"katika mihimili yote ya dola na lugha nyengine za asili ziheshimiwe." | | |
| | | (iii) Kiswahili kiwe lugha ya shirikisho badala ya lugha ya Taifa | Kuweka mkazo wa kuimarisha na kuthaminiwa kwa lugha ya Kiswahili. | |
| | | (iv) Lugha ya Kiswahili itumike katika mawasiliano rasmi kitaifa na kimataifa | Kiswahili ndio lugha ya Taifa lazima idumishwe. | |
| | | (v) Lugha za kiasili zidumishwe, kuheshimiwa na kuendelezwa. | Baadhi ya wananchi hawafahamu lugha ya Kiswahili. | |
| | | (vi) Ibara ndogo ya (1) iandikwe kama ifuatavyo:<br>"(1) Lugha ya Taifa ya Jamhuri ya Muungano ni Kiswahili na itatumika katika mawasiliano rasmi ya kitaifa na kiserikali ikiwemo za Mahakama." | Ni muhimu Mahakama zote kutumia lugha ya Taifa inayotumika kwa wengi katika kutoa nakala za hukumu. | |
| | | (vii) Ibara ndogo ya (1) aindikwe upya na | Ni kukifanya Kiswahili | |

| Ibara Na. | Kichwa cha habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | iwe kama ifuatavyo: "(1) Lugha ya Taifa ya Jamhuri ya Muungano itakuwa Kiswahili na itatumika katika mawasiliano yote ya kiserikali na kitaifa na kila muswada wa sheria utakaopendekezwa, au sheria yeyote itakayotungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano, au Mabunge ya Washirika itakuwa katika Lugha ya Kiswahili." | kuwa lugha rasmi ya mawasiliano katika Jamhuri ya Muungano na pia sheria zote ziweze kutungwa kwa Kiswahili. | vinavyotangaza habari zake kitaifa kwa ajili ya watu wenye mahitaji maalum." |
| | | (viii) Ibara ndogo ya (2) irekebishwe kwa kuongeza maneno "na itakuwa lugha ya lazima ya kufundishwa kwenye mitaala" baada ya neno inapohitajika. | Kuwajengea uwezo wa kufahamu lugha ya kiingereza kwa ufasaha watanzania na hasa mashuleni na kwenye taasisi za elimu. | |
| | | (ix) Ibara ndogo ya (2) ifutwe. | Hakuna haja ya kutaja lugha ya kigeni katika mazingira tuliyonayo ya utandawazi. | |
| | | (x) Ibara ndogo ya (2) irekebishwe ili kuruhusu lugha nyingine yoyote ya kimataifa kuweza kutumika. | Ili kurahisisha mawasiliano. | |
| | | (xi) Lugha ya kiingereza itumike kama lugha rasmi ya mawasiliano | | |
| | | (xii) Kiingereza na Kiarabu zitumike kama lugha rasmi za mawasiliano ya shirikisho | | |
| | | (xiii) Ibara ndogo ya (2) neno "Kiingereza" lifutwe na badala yake isomeke "lugha za kigeni". | | |
| | | (xiv) Ibara ndogo ya (2) irekebishwe kwa kufuta neno "inaweza" na weka neno "itatumika". | Neno "inaweza" inaondoa lugha ya Kiingereza kuweza kutumika sambamba na | |

| Ibara Na. | Kichwa cha habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | lugha ya Kiswahili. | |
| | | (xv) Ibara ndogo ya (2) irekebishwe ili kuwe na uwezekano wa kutumia lugha zingine zaidi ya kiingereza na kiswahili kama lugha rasmi ya mawasiliano. | | |
| | | (xvi) Ibara ndogo ya (3) ibadilishwe na iandikwe kama ifuatavyo:<br>"(3) Bila ya kuathiri masharti ya Ibara ndogo ya (1), lugha nyingine za kitaifa zitapewa msisitizo maalumu kama lugha muhimu kwa Taifa letu". | Lugha za kigeni zinazotumika katika shughuli za kibiashara ni muhimu kupewa umuhimu. | |
| | | (xvii) Ibara ndogo ya (3) isomeke "Serikali itaweka mazingira yatakayowezesha kuwepo kwa mawasiliano mbadala yakiwemo ya lugha ya alama, nukta nundu na maandishi yaliyokuzwa kwenye sehemu za huduma na zile muhimu za umma na katika vyombo vya habari vinavyotangaza habari za kitaifa kwa ajili ya watu wenye mahitaji maalum". | | |
| | | (xviii) Ibara ndogo ya (3) iongezwe maneno "lugha rasmi kwa viziwi na viziwi wasioona." | Ili kuhakikisha taarifa zote zinazotolewa kwa umma zinawafikia watu wote kwa kuona na kusikia. | |
| | | (xix) Ibara ndogo ya (3) iongezwe maneno ''Lugha ya alama na maandishi ya nukta nundu itatumika katika taasisi zote za serikali" | Kuwawezesha walemavu wasioona na viziwi kuweza kupata taarifa kwa urahisi. | |

| Ibara Na. | Kichwa cha habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | (xx) Iongezwe ibara ndogo mpya ya (3) ambayo itaandikwa kama ifuatavyo: "(3) Mamlaka ya Jamhuri ya Muungano na mamlaka za washirika na Muungano zitalinda, kuhifadhi na kuendeleza lugha za asili za watu wa Jamhuri ya Muungano". | Kuweza kuendeleza na kuenzi utamaduni wa lugha za asili za wananchi wa Jamhuri ya Muungano na kuufanya urithi kwa ajili ya vizazi vya sasa na vijavyo. | |
| | | (xxi) Iongezwe ibara ndogo ya (4) isomeke: "(4) Mamlaka ya Jamhuri ya Muungano na mamlaka za washirika wa Muungano zitahamasisha maendeleo na matumizi ya lugha za asili na lugha mbadala zikiwemo lugha za alama na nukta nundu katika sehemu muhimu za umma na katika vyombo vya habari kwa ajili ya watu wenye mahitaji maalum". | Kutambua rasmi lugha za asili na nukta nundu hasa kwa watu ambao wanamahitaji maalum. Aidha, nchi kama Kenya inatambua lugha nyingine za watu wa Kenya zikiwemo za makabila ya nchi hiyo. | |
| 5. | Tunu za Taifa | (i) iongezwe aya (h) inayosomeka "ukarimu"; | | Ibara inabaki kama ilivyo. |
| | | (ii) yaongezwe maneno "uhuru na haki" katika tunu za Taifa; | Yote haya ni tunu za Taifa. | |
| | | (iii) Neno Tunu liondolewe badala yake itumike misingi ya kitaifa au misingi ya Maadili.<br>(iv) Aya ya (g) isomeke lugha ya Taifa | | |
| | | (v) aya (e) iandikwe "uwazi na ukweli"; | | |
| | | (vi) aya (e) iandikwe "usawa wa binadamu"; | Uwazi si moja wapo ya tunu za Taifa. | |
| | | (vii) Aya (g) ifutwe badala yake isomeke "lugha ya Kiswahili". | | |
| | | (viii) iongezwe aya nyengine | Amani ndiyo nguzo ya nchi | |

| Ibara Na. | Kichwa cha habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | itakayoandikwa "amani na utulivu"; | yetu. | |
| | | (ix) utamaduni nao iorodheshwe kama Tunu ya Taifa. | | |
| | | (x) maneno "haki na usawa" yaongezwe kama tunu za Taifa; | Baada ya utu, haki inafuata kabla ya jambo lingine, bila ya haki hakuna tunu nyingine zote hazitakuwa na maana. | |
| | | (xi) yaongezwe maneno "Utawala bora na Utawala wa sheria". | | |
| | | (xii) neno "uwazi" lifutwe. | Sio miongoni mwa tunu za Taifa. | |
| | | (xiii) Tunu ya uwazi iondolewe | Uwazi si mojawapo ya tunu za Taifa. | |
| | | (xiv) Yaongezwe maneno "uhuru wa vyombo vya habari, usawa wa kijinsia" kama tunu za Taifa. | | |
| | | (xv) iongezwe Ibara ndogo ambayo itafanana na Ibara ya 10(1) ya Katiba ya Kenya. | Utawala bora ni dhana inayobeba mambo mengi zaidi. | |
| | | (xvi) Ibara hii iandikwe upya kama ifuatavyo:<br>"Jamhuri ya Muungano itaenzi na kuzingatia tunu za taifa zifuatazo:-<br>(a) Utu, Haki na Usawa;<br>(b) Uzalendo;<br>(c) Uadilifu;<br>(d) Umoja na amani;<br>(e) Uwazi;<br>(f) Amani;<br>(g) uwajibikaji; na<br>(h) utamaduni na Lugha ya taifa". | Sote tunatambua kuwa, amani, haki, usawa na utamaduni pamoja na tunu nyinginezo zilizotajwa katika rasimu hii ndio msingi bora wa Taifa. | |
| | | (xvii) Ziongezwe Tunu za Taifa zifuatazo:<br>(a) Mlima Kilimanjaro; | (a) Kwenye Rasimu zimeandikwa Tunu zisizoshikika tu na zile | |

| Ibara Na. | Kichwa cha habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | (b) Vyombo vya habari;<br>(c) Mbuga za Wanyama;<br>(d) Demokrasia ya Vyama vingi;<br>(e) Utawala wa sheria;<br>(f) Haki za binadamu;<br>(g) Madini;<br>(h) Azimio la Arusha;<br>(i) Ardhi/Misitu;<br>(j) Utamaduni;<br>(k) Maji/Maziwa;<br>(l) Utawala Bora;<br>(m) Mito; na<br>(n) nyinginezo zitakazobaonishwa na Sheria ya Bunge. | zinazoshikika hazikutajwa na hali ipekee nafasi kwa viongozi na wenye nafasi kuhujumu;<br>(b) Sheria itakayotungwa na Bunge ieleze wazi kuwa watakaozihujumu wachukuliwe hatua kali za kisheria;<br>(c) Ni muhimu Demokrasia ya Vyama vingi, Utawala wa sheria na Haki za binadamu zikatambuliwa kama Tunu za Taifa ili kila mmoja alazimike kuhifadhi Tunu hizi adhimu. | |
| | | (xviii) "Amani na Kufanya kazi" iwe ni miongoni mwa tunu za Taifa. | (a) imekuwa kisiwa cha amani kwa miaka mingi, na itaendelea kuwa hivyo.<br>(b) wanaokusudia kutaka kuharibu amani na utulivu uliopo waone kuwa wanaharibu moja ya tunu muhimu zinazolindwa na Katiba hii,<br>(c) Ni utamaduni wa Watanzania kufanya kazi kutokana na dhana ya kujitegemea ambayo | |

| Ibara Na. | Kichwa cha habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | tumekuwa nayo tangu Uhuru, hivyo "kufanya kazi" kuchukuliwe kuwa ni moja ya tunu muhimu ambayo kila Mtazania atawajibika kuilinda kwa kujituma na kufanya kazi kwa bidii popote iwe ni nje au ndani ya nchi, au awe kwenye utumishi wa umma au kwenye ajira binafsi (private sector). | |
| | | (xix) Vazi la taifa liongezwe kama Tunu ya Taifa. | Itasaidia kudumisha utamaduni wa Mtanzania. | |
| | | (xx) Aya (a) hadi (g) zifutwe na badala yake ziandikwe mpya kama ifuatavyo:<br>(a) utu;<br>(b) uzalendo na utaifa;<br>(c) amani na utulizu;<br>(d) uadilifu;<br>(e) upendo na kuvumiliana;<br>(f) umoja na mshikamano;<br>(g) uwajibikaji na kujitegemea;<br>(h) haki na usawa;<br>(i) lugha ya Kiswahili. | | |
| | | (xxi) Ziongezeke Tunu za uaminifu, utawala wa sheria, amani, lugha ya kiswahili, maliasili, utamaduni wetu, kufanya kazi na umakini, usawa wa binadamu na demokrasia | | |
| | | (xxii) Tunu zingine ni: upendo, ukweli na usawa wa kijinsia, Ushiriki na | Bila amani na utulivu hakuna maendeleo. | |

| Ibara Na. | Kichwa cha habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | ushirikishwaji, kupata, kutafuta na kutunza habari, udugu, ardhi, haki, heshima, madini na kujitegemea. | Bila haki, uhuru na ukweli hakuna utulivu.<br>Usawa wa binadamu ni suala la taswira ya nchi yetu. | |

## 1.1 SEHEMU YA PILI: MAMLAKA YA WANANCHI UTII, NA HIFADHI YA KATIBA

| ***Ibara Na.*** | ***Kichwa cha Habari*** | ***Maoni ya Mabaraza*** | ***Sababu ya maoni*** | ***Marekebisho ya Tume*** |
|---|---|---|---|---|
| 6. | Mamlaka ya Wananchi | (i) ibara hii ibadilishwe kwa kufuta neno "nchi" na badala yake iandikwe "shirikisho". | | 1. Ibara ya 6 (a) "mamlaka za nchi" isomeke "mamlaka yote".<br>2. Vifungu vingine kwenye Ibara hii vibaki kama vilivyo kwenye Rasimu. |
| | | (ii) ibara hii ibadilishwe kwa kufuta maneno "Jamhuri ya Muungano" na badala yake iandikwe "Jamhuri za Muungano". | Neno "za" linamaanisha Serikali za Shirikisho. | |
| | | (iii) Aya (a) maneno "mamlaka za nchi" iandikwe "mamlaka ya nchi". | | |
| | | (iv) Aya (b) iunganishwe na Ibara ya 7(1). | Haiendani na maelezo ya pembeni (marginal note). | |
| | | (v) Aya (b) ifutwe. | Hii ni miongoni mwa malengo. | |
| | | (vi) Iongezwe aya (e) mpya ambayo itakuwa kama ifuatavyo:<br>"(e) Endapo Serikali itawajibika kwa wananchi, wananchi wawajibishe Serikali kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii". | | |
| | | (vii) Ibara hii irekebishwe ili kueleza dhana ya Serikali za Mitaa chini ya msingi wa kupeleka madaraka kwa wananchi. | | |
| | | (viii) Iongezwe "haki ya kupiga kura" | Ili wananchi wote wenye haki ya kupiga kura waweze kufanya hivyo | |
| | | (ix) Isomeke "Jamhuri ya Muungano ni nchi inayofuata misingi ya kidemokrasia yenye mfumo wa vyama vingi vya siasa, inayozingatia haki ya kijamii na kwa hiyo:<br>a) wananchi ndiyo msingi wa | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | mamlaka ya nchi na serikali itapat mamlaka na madaraka yake kutoka kwa wananchi ambao kwa ujumla wao wanaimilki na kuipatia katiba hii uhalali; | | |
| 7. | Watu na Serikali | (i) Ibara ndogo ya (1) irekebishwe na iandikwe kama ifuatavyo: "(1) Ulinzi na usalama, maendeleo na ustawi wa wananchi, amani na utulivu na azma ya kukuza umoja wa kitaifa na kudumisha heshima ya Taifa." | | Katika Ibara ya 7(2) zimeongezwa ibara ndogo ambazo zitasomeka kama ifuatavyo: a) "utu, heshima na haki nyingine za binadamu zinalindwa, zinathaminiwa, zinahifadhiwa na kudumishwa kwa kuzingatia mila na desturi za Watanzania na mikataba mbalimbali iliyoridhiwa na Jamhuri ya Muungano." d) ardhi ikiwa rasilimali kuu na msingi wa Taifa, inalindwa, inatunzwa na kutumiwa na wananchi wa |
| | | (ii) Ibara ndogo ya (2) irekebishwe kwa kuongeza neno "na sheria" baina ya maneno "sera" na "na". | | |
| | | (iii) Ibara ndogo ya (2) ifutwe. | Mambo yaliyoelezwa katika ibara hiyo sio mambo ya Muungano. | |
| | | (iv) Aya ya (a) na (g) ya Ibara ndogo ya (2) ziunganishwe. | Zinafanana. | |
| | | | | |
| | | (v) Aya ya (e) ya ibara ndogo ya (2) irekebishwe kwa kufuta maneno "kwa pamoja" na badala yake yaiandikwe maneno "uwiano mzuri". | | |
| | | (vi) Ziongezwe aya mpya (c), (d) na (h) katika ibara ndogo ya (2) zitakazosomeka kama ifuatavyo: (c) itikadi ya siasa iongezwe; (d) upatikanaji na ugawaji wa ardhi ufanywe na Serikali za Washirika; (h) sera na sheria za ardhi zioanishwe (harmonized). | Kuzuia ubaguzi wa kisiasa kutokana na utofauti wa vyama. | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | (vii) aya ya (g) ya ibara ndogo ya (2) irekebishwe kwa kuongeza neno "nzuri" baina ya maneno "desturi" na "za" na kufuta maneno "Jamhuri ya Muungano" na kuandika maneno "kuwa sehemu ya sheria za nchi". | | Tanzania kwa manufaa, maslahi na ustawi wa kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.<br>g) kunakuwepo fursa na haki zilizo sawa kwa wananchi wote, wanawake na wanaume, bila ya kujali rangi, kabila, nasaba, itikadi, dini au hali ya mtu;<br>j) nchi inaongozwa kwa kufuata misingi ya demokrasia, utawala wa sheria na kujitegemea. |
| | | (viii) iongezwe aya mpya itakayoeleza masharti ya kulinda na kuhifadhi mazingira katika utekelezaji wa shughuli za kibinadamu. | Mazingira ni muhimu kwa maendeleo endelevu. | |
| | | (ix) Katika ibara ndogo ya (2) iongezwe aya (d) mpya itakayoandikwa kama ifuatavyo:<br>"(d) Ardhi na rasilimali zote zilizopo chini na juu ni mali ya wananchi wa Tanzania, hivyo kila mwananchi ana haki ya kumiliki ardhi na kunufaika kwa pamoja"; | | |
| | | (x) Aya (d) irekebishwe na iwe (e) na kuendelea kwa mpangilio wake. | | |
| | | (xi) Aya (f) iandikwe upya kama ifuatavyo:<br>"(f) Kila mtu mwenye uwezo wa kufanya kazi anafanya kazi; na kazi maana yake ni shughuli yoyote ya halali inayokubalika kijamii na kisheria inayompatia mtu riziki yake." | Shughuli yoyote halali inakuwa halali pale tu inapokuwa inatambuliwa kisheria au kijamii siyo kwa kadiri ya utashi wa mtu, na pia, "kipato", ni neno linalotoa tafsiri inayolenga mapato ya kifedha tu, lakini riziki inalenga na kutoa tafsiri pana ya namna zote za malipo yanayowezesha mtu kukimu maisha. | |
| | | (xii) Aya (g) irekebishwe na iandikwe upya kama ifuatavyo: | Ili kuhifadhi haki za Watanzania, ikiwemo uhai, | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | "(g) utu, haki, heshima na haki nyingine zote za binadamu zinahifadhiwa na kudumishwa kwa kuzingatia mila na desturi za kitanzania na kwa kufuata mikataba mbalimbali iliyoridhiwa na Jamhuri ya Muungano"; | imani, mila na desturi zao. | |
| | | (xiii) Aya (g) ya ibara ndogo ya (2) irekebishwe kwa kuongeza maneno "mila na desturi, mavazi". | Itawezesha kuheshimu utamaduni wa nchi. | |
| | | (xiv) Aya ya (h) ya ibara ndogo ya (2) irekebishwe kwa kufuta maneno "mamlaka za nchi zinatoa" na badala yake kuweka maneno "wanawake na wanaume". | | |
| | | (xv) Aya (i) ya ibara ndogo ya (2) irekebishwe kwa kuongeza maneno "inapiga vita" mwanzoni mwa aya hiyo na maneno 'zinaondolewa nchini" . | | |
| | | (xvi) Aya ya (j) ya ibara ndogo ya (2) ifutwe. | Maudhui yake yapo 7(2)(c). | |
| | | (xvii) Aya (j) ya ibara ndogo ya (2) iandikwe kama ifuatavyo:<br>"(j) Utajiri wa rasilimali na maliasili za Taifa unaendelezwa katika kuleta maendeleo, kuboresha huduma za afya, elimu na huduma nyingine za jamii"; | | |
| | | (xviii) Aya ya (k) ya ibara ndogo ya (2) irekebishwe kwa kufuta neno | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | "kujitegemea" na kuweka maneno "utawala wa Sheria". | | |
| | | (xix) Neno "kujitegemea" liliopo katika aya (k) litafsiriwe katika ibara ya ufafanuzi. | | |
| | | (xx) Aya (k) ya Ibara ndogo ya (2) irekebishwe kwa kuongeza neno "haki" baada ya neno "misingi ya"; | Haki ndiyo msingi katika utawala bora unaofuata misingi ya kujitegemea ili kuleta ustawi wa watu katika nchi. | |
| | | (xxi) Iongezwe ibara ndogo mpya itakayoeleza kama ifuatvyo:- "Sheria ya umiliki wa ardhi kwa wawekezaji wa nje usizidi miaka ishirini na tano tu (25)". | | |
| | | (xxii) Iongezwe Ibara ndogo mpya itakayoandikwa kama ifuatavyo: "Uundaji wa mamlaka mbalimbali za umma zitakazoanzishwa kwa mujibu wa Katiba hii na uendeshaji wa shughuli zake mbalimbali utazingatia usawa wa kijinsia, umoja wa kitaifa na kukuza usawa miongoni mwa Watanzania. | Kwa kuzingatia umuhimu wa aya hii, inapendekezwa iwekwe mara tu baada ya aya (b) ya ibara hii. | |
| | | (xxiii) Aya (c), (d), (e) na (j) katika Ibara ndogo ya (2) zifutwe. | Hazihusiani na mambo ya Muungano. | |
| | | (xxiv) Ziongezwe ibara ndogo mpya zitakazoeleza mambo yafuatayo:<br>(a) Kulinda na kudumisha amani na usalama wa Taifa ;<br>(b) Kuimarisha mahusiano mema na nchi nyingine;<br>(c) Kuheshimu sheria na mikataba ya Kimataifa ambayo Serikali ya Shirikisho imeridhia kabla na au | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | baada ya kupatikana kwa Katiba Mpya;<br>(d) Kuhakikisha kuwa migogoro ya kisiasa na kijamii inamalizwa kwa njia za mazungumzo na usuluhishi;<br>(e) Kuhakikisha kuwa kila raia wa Tanzania anapata fursa sawa katika ajira na nafasi za kuchaguliwa katika serikali ya Muungano; na<br>(f) Serikali zinalinda Hakimiliki za wasanii. | | |
| 8. | Mamlaka na utii wa Katiba | (i) Ibara ndogo ya (1) irekebishwe kwa kufuta maneno "Bila ya kuathiri masharti ya Katiba za Washirika wa Muungano kwa mambo yasiyo ya Muungano". | (a) Ibara ya 8(1) na (2) ina maana nchi Washirika hazitabanwa na mambo ambayo sio ya Muungano. Hii maana yake ni kuwa Katiba za Nchi Washirika ndio zenye nguvu.<br>(b) Katiba zote za Muungano au mashirikisho kama ilivyo kwa nchi ya Nigeria, Marekani na nyinginezo hutamka kwa uwazi Ukuu wa Katiba ya Muungano au shirikisho lakini Rasimu haibainishi ukuu wa Katiba. | Ibara hii imeandikwa upya na itasomeka kama ifuatavyo:<br>8(1) Katiba hii ni sheria kuu katika Jamhuri ya Muungano kwa kuzingatia masharti ya Katiba hii.<br>(2) Kwa madhumuni ya Ibara ndogo ya (1), endapo masharti ya sheria yoyote yatatofautiana na masharti ya Katiba hii, masharti ya sheria hiyo yatakuwa batili na yatatenguka kwa kiwango kile kinachotofautiana |
| | | (ii) Katika ibara ndogo (1) maneno Katiba uwe kwa mambo ya Muungano tu. | Katiba ni kwa mambo ya Muungano na sio vyinginevyo. | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | (iii) Katika ibara ndogo (1) maneno "Bila ya kuathiri masharti ya Katiba za Washirika wa Muungano kwa mambo yasiyo ya Muungano" yafutwe na badala yake isomeke "Bila kuathiri masharti ya Katiba ya Zanzibar." | | na masharti ya Katiba hii.<br>(3) Mtu yeyote, chombo, taasisi, jumuiya na wakala wowote wa mamlaka ya nchi na mamlaka binafsi zinao wajibu wa kuzingatia masharti ya Katiba hii na sheria za nchi na kuzitii.<br>(4) Sheria yoyote, mila, desturi au uamuzi wowote wa chombo cha dola, Ofisa wa Serikali au mtu binafsi ni sharti ufuate na kuendana na masharti yaliyomo kwenye Katiba hii na kwamba, sheria, mila, desturi au uamuzi wowote ambao hautawiana au kwenda sambamba na masharti ya Katiba hii utakuwa batili.<br>5) Serikali itaweka utaratibu wa kuwawezesha wananchi kuifahamu, kuilinda |
| | | (iv) Ibara ndogo ya (1) irekebishwe ili Katiba ya Muungano iwe Kuu na iwe na nguvu kwa mambo ya Muungano tu na kuacha Katiba za Nchi Washirika ziwe Kuu na ziwe na nguvu kwa mambo yaliyo katika mamlaka zao. | | |
| | | (v) Ibara ndogo ya (1) ibadilishwe na iandikwe kama ifuatavyo:<br>"(1) Bila kuathiri kutumia kwa Katiba za Washirika wa Muungano kwa mambo yote ya washirika yasiyo mambo ya Muungano, Katiba hii itakuwa na nguvu ya kisheria katika Jamhuri ya Muungano nzima na endapo sheria nyingine yoyote iliyotungwa na washirika wa Muungano au mamlaka nyingine yeyote itakiuka, kwa kiasi inachokiuka Katiba, itakuwa batili." | Hiki ni kipengele cha ukuu wa Katiba (Supremacy Clause) ambacho kinaipa Katiba ya Jamhuri ya Muungano ukuu wa Katiba (Supremacy of Constitution). Hii ndio itaifanya Rasimu kuwa Katiba mama. | |
| | | (vi) Ibara ndogo ya (1) irekebishwe. | Ili kuondoa mkanganyiko kwa mamlaka ya Serikali za Washirika na Serikali ya Muungano. | |
| | | (vii) Katika Ibara ndogo ya (3) maneno "mila na desturi" yafutwe. | Kila nchi Washirika ina mila na desturi zake ambazo zinatofautiana. | |
| | | (viii) Ibara ndogo ya (3) | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | iandikwe kama ifuatavyo:<br>“(3) Sheria yoyote, mila, desturi au uamuzi wowote wa chombo cha dola, taasisi, jumuiya, wakala, ofisa wa serikali au mtu binafsi ni sharti ufuate na kuendana na masharti yaliyomo katika Katiba hii”. | | na kuitii Katiba. |
| | | (ix) Iongezwe ibara ndogo ya (4) itakayoeleza maana ya mila na desturi kama ifuatavyo:<br>“(4) Mila na desturi maana yake ni kanuni zinazoongoza na kudhibiti fikra, mienendo, tabia, ujuzi na matendo ya watu katika jamii zao kulingana na jinsi, jinsia, umri wao, hadhi zao na maslahi halisi ya jamii hizo”. | | |
| | | (x) Katika ibara ndogo ya (3) yaongezwe maneno “kwa kadiri utakavyokuwa unahusu utekelezaji wa mambo ya Muungano kama yalivyoorodheshwa kwenye nyongeza ya Katiba hii” mwisho wa sentensi. | Katiba inahusu mambo ya Muungano tu.<br>Kuzuia Katiba isiingilie sheria, mila na desturi za Washirika. | |
| | | (xi) Ibara ndogo ya (3) ifutwe na iandikwe upya kama ifuatavyo:<br>“(3) Sheria yoyote, mila, desturi au uamuzi wowote wa chombo cha dola, Ofisa wa Serikali au mtu binafsi unaokiuka masharti ya Katiba hii basi sheria, mila, desturi au uamuzi huo kwa kiasi unachokiuka Katiba hii utakuwa batili”. | Rasimu ya Katiba haionyeshi ukuu wa Katiba kwa maana ya kubatilisha sheria, maamuzi au mambo au vitendo vinavyokiuka masharti ya Katiba na hivyo kufifisha utekelezaji wake. | |
| | | (xii) Iongezwe ibara ndogo mpya ya (4) itakayoandikwa kama ifuatavyo: | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | "(4) Katiba yoyote ya washirika wa Muungano itakayopingana na vifungu vya Katiba hii kuhusu mambo ya Muungano, vifungu vya Katiba hiyo itakua batili kadiri ya kupingana huko". | | |
| | | (xiii) Iongezwe ibara ndogo ya (4) inayosomeka kama ifuatavyo: "(4) Hakuna mtu yeyote au chombo chochote kitakachokuwa juu ya Katiba". | Ili kusisitiza dhana ya ukuu wa Katiba. | |
| | | (xiv) Ibara ndogo ya (3) ifutwe na badala yake iandikwe kama ilivyo Ibara ya 64(5) ya Katiba ya sasa. | Katiba za Washirika zitakuwa na nguvu zaidi. | |
| 9. | Hifadhi ya Katiba | (i) Ibara ndogo ya (1) ifutwe na badala yake iandikwe kama ilivyo Ibara ya 26(1) ya Katiba ya sasa. | Jamhuri ya Muungano ni Shirikisho sio nchi. Kutumia neno nchi itasababisha utata kati ya Tanzania, Tanganyika na Zanzibar. | Ibara hii imerekebishwa na kuongezwa vifungu vifuatavyo: (1)Katika Ibara ndogo ya (1) yameongezwa maneno "kwa mujibu wa" mbele ya neno "isipokuwa". Ibara ndogo ya (2), isomeke Kitendo chochote kinachokiuka masharti ya Ibara ndogo ya (1) ni batili na ni kitendo cha uhaini kama itakavyoelezwa |
| | | (ii) Katika ibara ndogo ya (1) maneno "mamlaka ya nchi" yafutwe na badala yake iandikwe "mamlaka ya shirikisho". | | |
| | | (iii) Ibara ndogo ya (2) isomeke kama ifuatavyo: "(2) Serikali itaweka utaratibu wa kuwezesha wananchi kuifahamu, kuilinda na kuitii Katiba." | Ili kuilazimisha serikali kusimamia elimu. | |
| | | (iv) Ibara ndogo ya (3) maneno "itaweka" yafutwe na badala yake iandikwe "iweke". | Ili kuilazimisha serikali kusimamia elimu. | |
| | | (v) Ibara ndogo ya (3) irekebishwe kwa kufuta maneno "mitaala ya elimu". | Masuala ya elimu sio mambo ya Muungano. | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | (vi) Ibara ndogo ya (3) ifutwe. | Elimu si mojawapo ya mambo ya Muungano. | katika sheria za nchi. |
| | | (vii) Ibara ndogo ya (3) ifutwe na badala yake iwekwe kwenye sheria. | Kupitia Katiba itakuwa ni vigumu kutekelezeka. | |
| | | (viii) Iongezwe ibara ndogo itakayoweka utaratibu kwa Serikali kusambaza Katiba kwa wananchi. | Ili wananchi wapate fursa ya kuifahamu Katiba yao. | |
| | | (ix) Kuongeza ibara ndogo mpya ya (4) ambayo itaanzisha Tume ya Hifadhi ya Katiba, kazi ya Tume hiyo ielezwe kama ifuatavyo:<br>"Kwa madhumuni ya kuhifadhi masharti ya Katiba hii, Tume ya Hifadhi ya Katiba itakuwa na wajibu wa kuwezesha wananchi kuifahamu, kuilinda na kuitii Katiba. Au<br>Kwa madhumuni ya kuhifadhi masharti ya Katiba hii, Tume ya Hifadhi ya Katiba, itakuwa ndiyo chombo muhimu cha usimamizi na wajibu wa kuwezesha wananchi kuifahamu, kuilinda na kutii Katiba, sheria za nchi zitaweka namna ya tume itakavyotekeleza wajibu huu."<br>(x) Iandikwe -(1) Kila mtu ana wajibu wa kufuata na kutii Katiba hii na sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.<br>(2) Serikali itaweka utaratibu wa kuwawezesha wananchi kuifahamu, kuilinda na kuitii Katiba.<br>(3) Kitendo chochote kinachokiuka masharti ya Ibara ndogo ya (1) ni batili na ni kitendo cha jinai kama itakavyoelezwa katika sheria za nchi. | | |

| ***Ibara Na.*** | ***Kichwa cha Habari*** | ***Maoni ya Mabaraza*** | ***Sababu ya maoni*** | ***Marekebisho ya Tume*** |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |

# SURA YA PILI YA RASIMU

## 2.0 MALENGO MUHIMU, MISINGI YA MWELEKEO WA SHUGHULI ZA SERIKALI NA SERA ZA KITAIFA

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Maoni* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| 10. | Utekelezaji wa malengo ya Taifa | (i) Ibara hii ifutwe. | Ibara hii inatoa mwongozo kwa Serikali ya Shirikisho kwa mambo ambayo hayasimamiwi na Serikali hiyo. | 1. Ibara ya 10 imekuwa ya 11:<br>2. Ibara imerekebishwa na imeongezwa kifungu kidogo cha 3(b)(v) ambacho kitasomeka: Kuwezesha upatikanaji na utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria kwa wananchi wasiokuwa na uwezo wa kumudu gharama za uwakili.<br>3. Aidha, katika Ibara ndogo ya 3(c) Ibara imeongezwa vifungu vidogo vifuatavyo:<br>(xi) Kuhamasisha uwekezaji wa pamoja baina ya raia na wasio raia katika miundo mbinu ya uchumi, uvunaji wa rasilimali na maliasili za Taifa.<br>(xii) Kuweka utaratibu wa usimamizi wa kiuchumi na uandaaji wa mipango, |
| | | (iv) Ibara ndogo ya (1) sentensi iishie na maneno "Vyama vya Siasa" na maneno yote yanayofuata baada ya hapo yafutwe. | Chini ya mfumo wa vyama vingi vya siasa kila chama kinakuwa na sera zake. Hivyo kuna uwezekano wa nchi kukosa uelekeo mmoja. | |
| | | (v) Ibara ndogo ya (1) irekebishwe kwa kuongeza maneno "inayojitegemea, inayoheshimiwa" baina ya maneno "makini" na "na". | | |
| | | (vi) Katika ibara ndogo ya (2) maneno "mara moja" yafutwe na badala yake iandikwe "mara nne". | Inapendekezwa Serikali itoe taarifa mara nne kwa mwaka ili Wananchi wapate taarifa zaidi. | |
| | | (vii) Katika ibara ndogo ya (2) neno "Serikali" lifutwe na badala yake liandikwe neno "Rais". | Rais ndiye mwenye jukumu la kutoa taarifa kwenye chombo cha | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | uwakilishi wa wananchi. | kuwezesha malengo ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu kuendelezwa.<br>(xiii)Kuwezesha na kuendeleza matumizi ya Sayansi na Teknolojia na kukuza ubunifu katika shughuli za kiuchumi na maendeleo ya Taifa kwa ujumla.<br>4. Katika Ibara ndogo ya 3(e) zimeongezwa aya ndogo zifuatazo:<br>(ii) Kuhakikisha kuwa Taasisi za Umma na Asasi za Kiraia zinawajibika kusimamia utekelezaji na uzingatiaji wa matakwa ya kisheria katika kulinda na kuhifadhi mazingira.<br>(iii) Kuhakikisha kuwa wananchi wa Tanzania ndio wenye haki ya kumiliki rasilimali za kijenetiki za |
| | | (viii) Ibara ndogo ya (2) iandikwe kama ifuatavyo:<br>“(2) Serikali itatoa taarifa Bungeni na kujadiliwa si chini ya mara moja katika kila mwaka kuhusu hatua zinazochukuliwa na mamlaka za nchi ili kuhakikisha utekelezaji wa malengo ya taifa yaliyoainishwa katika Katiba hii”. | Itatoa fursa hasa kwa masuala muhimu ya malengo na mwelekeo wa Taifa kupata fursa pana ya kueleweka vyema, namna utekelezaji wa Serikali ulivyokuwa ili kuondoa sintofahamu kwa wananchi hasa tukizingatia uzoefu wa nyuma pale taarifa muhimu zilipohitaji ufafanuzi, zikakosekana ilhali wananchi wakiambiwa ziko kwa Spika hivyo kuzima mjadala kwa maslahi ya Taifa. | |
| | | (ix) Ziongezwe Ibara ndogo mpya za (2) na (3) kama ifuatavyo:<br>“(2) Katika kutekeleza majukumu yao, Serikali, Bunge, Mahakama, vyama vya siasa, taasisi, asasi na mamlaka nyingine na kila mwananchi atazingatia na kuheshimu malengo yaliyowekwa ndani ya Katiba hii.<br>(3) Ilani za uchaguzi za vyama vya siasa zitazingatia malengo makuu yaliyoainishea ndani ya Katiba hii.” | | |
| | | (x) Ibara ndogo ya (2) iwe ibara ndogo ya (4). | | |
| | | (xi) Iongezwe Ibara ndogo mpya ya (3) | Masharti haya yabaki | |

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Maoni* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| | | itakayokuwa na maelezo kama ilivyo Ibara ya 7(2) ya Katiba ya sasa. | kuwa malengo muhimu yanayoonyesha azma ya Serikali ya kuyafikia kwa manufaa ya watu wake. Endapo yatatiliwa nguvu za kisheria itakuwa vigumu kwa Serikali kupata fursa ya kutimiza mipango yake kwani itakuwa ikishtakiwa mara kwa mara. | Tanzania kwa manufaa ya Taifa. |
| | | (xii) Iongezwe ibara ndogo mpya itakayoeleza tafsiri ya neno "Taifa".<br>(xiii) kuwezesha upatikanaji na utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria kwa wananchi wasiokuwa na uwezo wa kumudu gharama za uwakili;<br>(xiv) kuweka utaratibu unaofaa kwa ajili ya kufanikisha utekelezaji wa haki ya mtu kujipatia elimu na kuwa huru kupata fursa sawa ya kutafuta elimu katika fani anayoipenda hadi kufikia upeo wowote kulingana na stahili na uwezo wake;<br>(xv) kuhamasisha uwekezaji wa pamoja kwa raia na wasio raia katika miundombinu ya uchumi katika uvunaji wa rasilimali na maliasili za Taifa;<br>(xvi) kuweka utaratibu wa usimamizi wa kiuchumi na uandaaji wa mipango, kuwezesha malengo ya muda mfupi, muda wa | Ili kuepusha tafsiri potofu. | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | kati na muda mrefu kuendelezwa;<br>(xvii) kuwezesha na kuendeleza matumizi ya sayansi na teknolojia na kukuza ubunifu katika shughuli za kiuchumi na maendeleo ya Taifa kwa jumla;<br>(xviii) kimazingira, Serikali itachukua hatua zinazofaa ili:-<br>(xix) kuhakikisha kuwa ni haki na wajibu wa kila mtu kulinda na kudumisha mazingira kwa faida ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo;<br>(xx) kuhakikisha kuwa taasisi za umma na asasi za kiraia zinawajibika kusimamia utekelezaji na uzingatiaji wa matakwa ya kisheria katika kulinda na kuhifadhi mazingira; na<br>(xxi) kuhakikisha kuwa wananchi wa Tanzania ndiyo wenye haki ya kumiliki rasilimali za kijenetiki za Tanzania kwa manufaa ya Taifa. | | |
| 11. | Malengo Makuu | (i) Ibara ndogo ya (1) ifutwe na badala yake iandikwe kama ilivyo Ibara ya 11(1) ya Katiba ya sasa. | Ili kutekeleza haki za binadamu zinazohusiana na huduma ya afya kwa watumishi wa umma. | Ibara ya 11 imekuwa Ibara ya 10 na imebakia kama ilivyo. |
| | | (ii) Ibara ndogo ya (1) irekebishwe kwa kuongeza maneno “maendeleo endelevu” baada ya maneno “utawala bora”. Pia yaongezwe maneno “dira na” baina ya maneno “kutekeleza” na “malengo ya Taifa”. | Lengo Kuu la Katiba hii ni kulinda, kuimarisha na kudumisha udugu, amani, umoja na utengamano wa wananchi wa Jamhuri ya Muungano kwa kuzingatia ustawi wa wananchi na kujenga | |

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Maoni* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| | | | Taifa huru lenye demokrasia, utawala bora na kujitegemea. | |
| | | (iii) Ibara ndogo ya (1) irekebishwe kwa kufuta maneno “demokrasia, utawala bora na kujitegemea” na badala yake kuweka maneno “utulivu, demokrasia, utawala wa sheria na linalojitegemea.” | | |
| | | (iii) Ibara ya 11(2) iongezwe nyanja moja ya kijadi. | Jadi husimamia mila na desturi ya sehemu husika | |
| | | (iv) Ibara ndogo ya (2) na (3) zifutwe. | Ibara hizi zinahusu utekelezaji wa malengo. | |
| | | (v) Katika Ibara ndogo ya (3) kila ambapo neno “Serikali” linajitokeza lifuatiwe na maneno “Bunge, Mahakama, vyama vya siasa, taasisi, asasi na mamlaka nyinginezo na kila mwananchi”. | | |
| | | (vi) Aya (a), (c), (d) na (e) za Ibara ndogo ya (3) zifutwe. | Malengo haya si ya kikatiba yawekwe kwenye sheria. | |
| | | (vii) Aya (a) ya Ibara ndogo ya (3) irekebishwe kwa kuongeza neno “uchochezi” baina ya maneno “rushwa” na “uonevu”. | | |
| | | (viii) Aya (i) ya Ibara ndogo ya (3)(b) ifutwe na badala yake iandikwe kama ifuatavyo:<br>“(i) kuhakikisha kwamba heshima ya binadamu inahifadhiwa na kudumishwa kwa kufuata mila, desturi, imani za dini na Kanuni za Tangazo la Dunia kuhusu Haki za Binadamu na mikataba mingine | Imani za dini ni muhimu kuzingatiwa katika kuhifadhi na kudumisha heshima ya binadamu wanaoamini Mungu. | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | ya kimataifa iliyoridhiwa na Tanzania; | | |
| | | (ix) Ibara ndogo ya (3) aya (b)(i) irekebishwe ili kusisitiza kuheshimu Matangazo ya Dunia yanayoendana na mila na desturi za Taifa letu. | | |
| | | (x) Katika aya (ii) ya ibara ndogo ya (3)(a) yaongezwe maneno "utulivu" kila baada ya neno "amani" linapojitokeza. | | |
| | | (xi) Aya (ii) ya ibara ndogo ya (3)(c) iandikwe upya kama ifuatavyo: | | |
| | | "(ii) Serikali itahakikisha kuwa rasilimali za Taifa zinaendelezwa, zinahifadhiwa na zinatumiwa kwa manufaa ya wananchi wote"; | | |
| | | (xii) Aya (iv) ya ibara ndogo ya (3)(b) iandikwe kama ilivyo ibara ya 11(1) ya Katiba ya sasa. | | |
| | | (xiii) Aya (iii) na (viii) ya ibara ndogo ya (3)(c) zifutwe na badala yake iandikwe kama aya moja ya (iii) kama ifuatavyo:<br>"(iii) Serikali itaweka utaratibu wa usimamizi wa kiuchumi na uandaaji wa mipango kuwezesha malengo ya muda mfupi, wa kati na mrefu kuendelezwa"; | Maudhui yake yapo katika ibara ya 11(3)(c)(i), na pia vinaleta ubaguzi wa kutambua baadhi ya makundi. | |
| | | (xiv) Aya ya (xi) ya ibara ndogo ya (3)(c) ihamishiwe katika ibara ndogo ya (3)(b) inayohusu masuala ya kijamii na iandikwe kama ilivyo Ibara ya 11(2) ya Katiba ya sasa. | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | (xv) Iongezwe aya mpya katika ibara ndogo ya (3)(c) itakayosomeka kama ifuatavyo:<br>"Kuwezesha na kuendeleza matumizi ya sayansi na teknolojia na kukuza ubunifu katika shughuli za uchumi na maendeleo ya Taifa kwa ujumla;" | | |
| | | (xvi) Iongezwe aya mpya ya (f) katika ibara ndogo ya (3) kama ifuatavyo:<br>"(f) kiulinzi, Serikali itachukua hatua zinazofaa ili kuhakikisha uwepo wa ulinzi wa Taifa, ikijumuisha kuandaa umma kulinda Taifa dhidi ya vitendo vya uadui;" | | |
| | | (xvii) Ziongezwe aya nyingine mpya katika aya (e) ya ibara ndogo ya (3) na kuwa mojawapo ya hatua zinazofaa zitakazochukuliwa na Serikali kwa upande wa mazingira, ambazo ziwe kama ifuatavyo:<br>"(f) kuhakikisha kuwa ni haki na jukumu la kila kizazi kulinda na kudumisha mazingira kwa faida ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo;<br>(g) kuhakikisha kuwa taasisi za umma na taasisi za kiraia zinawajibika kusimamia utekelezaji na uzingatiaji wa matakwa ya kisheria katika kulinda na kuhifadhi | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | mazingira;<br>(h) kuhakikisha kuwa miradi yote mikubwa ya maendeleo inayoweza kusababisha athari katika mazingira inafanyiwa Tathmini ya Kimkakati ya Mazingira na Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) kabla ya kuanza utekelezaji wake; na<br>(i) kuhakikisha kuwa wananchi wa Tanzania ndiyo wenye haki ya kumiliki rasilimali za kijenetiki za Tanzania kwa manufaa ya Taifa". | | |
| | | (xviii) Aya ya (i) ya Ibara ndogo ya (3)(c) irekebishwe na iandikwe kama ifuatavyo:<br>"(i) Kuwaletea wananchi maisha bora kwa kukuza uchumi na kuondoa umaskini". | Katika kutekeleza malengo ya taifa serikali ihakikishe kwamba itawapatia wananchi maisha bora kwa kuondoa umaskini. | |
| | | (xix) Aya ya (ii) ya Ibara ndogo ya (3)(c) irekebishwe na iandikwe kama ifuatavyo:<br>"(ii) Kuhakikisha kwamba shughuli za Serikali zinatekelezwa kwa njia ambazo zitahakikisha kuwa rasilimali za Taifa zinaendelezwa, zinahifadhiwa na zinatumiwa kwa manufaa ya wananchi wote kwa jumla".<br>(xx) Ziongezwe aya mpya mara baada ya aya (c) katika ibara ndogo ya (3) kama ifuatavyo: | Kuhakikisha kwamba shughuli za serikali zinatekelezwa kwa njia ambazo zitahakikisha kuwa utajiri wa taifa unaendelezwa, unahifadhiwa na unatumiwa kwa manufaa ya wananchi wote kwa jumla na pia kuzuia mtu kumnyonya mtu mwingine. | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | (a) "Serikali itahakikisha kuwa inaimarisha miundombinu ya barabara, reli, usafiri wa majini na viwanja vya ndege inayoimarisha uchumi wa nchi;<br>(b) Serikali kwa makusudi ishiriki katika kujenga viwanda vya kati na vikubwa. Chuma, mbolea, zana za kilimo kwa kuingia ubia au yenyewe;<br>(c) Serikali kwa makusudi inaandaa wataalam wazawa wa fani mbalimbali ili kushiriki na kushika uongozi katika mashirika ya umma au ubia". | | |
| | | (xx) Aya ya (iii) ya Ibara ndogo ya (3)(c) ibadilishe kwa kuweka mazingira bora kwa ajili ya kuanzisha vyombo vya uwakilishi wa wakulima, wafugaji, wavuvi na wachimbaji wadogo wadogo na vyombo vya makundi mengine kwa kadri itakavyojitokeza. | Mapendekezo ya maneno hayo yanalenga maeneo yote muhimu ya uzalishaji na kutambuliwa kwa vyombo vya makundi hayo kiuchumi, hivyo kutambuliwa kwa makundi ya kilimo na ufugaji tu sio tija kwa uchumi wa nchi, japo tunatambua kilimo kina umuhimu wa pekee kwa watanzania walio wengi. | |
| | | (xxi) Iongezwe aya mpya katika ibara ndogo ya (3)(c) itakayozungumzia masuala ya wafanyabiashara na wafanyakazi. | Kifungu hiki kimeacha kuainisha makundi mengine ya msingi kwa mfano wafanya kazi, | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | wafanyabiashara. | |
| | | (xxii) Aya ya (i) ya Ibara ndogo ya (3)(d) maneno "wa asili" yafutwe na badala yake iandikwe "utamaduni usioshikika na unaoshikika". | Kuleta maana iliyokusudiwa. | |
| | | (xxiii) Aya (c) ya Ibara ndogo ya (3) iandikwe kama ifuatavyo:<br>"(c) kiuchumi, Serikali itachukua hatua kuwaletea wananchi maisha bora kwa kuondoa umasikini kwa kuchukua hatua zinazofaa ili:"<br>Hivyo aya (ii) iwe (i) na kuendelea. | | |
| | | (xxiv) Aya ya (vii) ya Ibara ndogo ya (3)(c) neno "upangaji" lifutwe. | (a) Neno hili linakinzana na kanuni za ushindani hasa katika kipengele cha kupanga bei.<br>(b) Serikali ilikwishafuta Tume ya Bei, hivyo hakuna haja ya kuwepo kipengele kinachozungumzia masuala ya kupanga bei. | |
| | | (xxv) Iongezwe ibara ndogo mpya itakayoeleza namna jamii itakavyoshirikishwa katika utekelezaji wa malengo yaliyomo katika Rasimu. | Serikali haiwezi kufanya haya peke yake. | |
| 12. | Sera kuhusu Mambo ya Nje | (i) Maelezo ya pembeni (Marginal note) yarekebishwe na yasomeke "Uhusiano wa Kimataifa na ulinzi." | | Katika Ibara ndogo ya 12(1) (a)(b) na (c) zimefanyiwa marekebisho na kusomeka kama ifuatavyo : |
| | | (ii) Ibara hii irekebishwe ili kuzungumzia sera za Kitaifa na sio | Katiba itoe mwelekeo wa Sera za Kitaifa kuhusu | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | Sera ya Mambo ya Nje pekee. | utayarishaji na usimamizi wake. | a) kukuza ujirani mwema, ushirikiano wa kikanda na wa kimataifa;<br>b) kukuza maendeleo na ushirikiano wa kiuchumi wenye tija kwa Taifa na raia wake;<br>c) kuunga mkono na kuendeleza jitihada za kuimarisha Umoja wa Afrika, sera ya kutofungamana na upande wowote na ushirikiano na nchi zinazostawi duniani;<br>d) kuheshimu sheria za kimataifa;<br>e) Kuzingatia mikataba ya kimataifa na ya kikanda yenye maslahi kwa Jamhuri ya Muungano na kutatua migogoro ya kimataifa kwa njia ya majadiliano, usuluhishi, maridhiano na mahakama".<br>Imeongezwa Ibara ndogo ya 2, ambayo itasomeka : Bunge litatunga sheria, pamoja na mambo mengine, itakayoelekeza |
| | | (iii) Ibara hii irekebishwe ili ieleze misingi ya Sera ya Mambo ya Nje na Sera ya Ulinzi na Usalama na izingatie mambo yafuatayo:<br>(a) kujenga uhusiano mzuri na mataifa mengine sambamba na kutambua, kulinda, kusimamia na kuendeleza maslahi na heshima ya nchi;<br>(b) kuwa na jeshi la kisasa lenye uwezo, nidhamu na utii. | | |
| | | (iv) Ibara hii iandikwe upya kama ifuatavyo:<br>"12(1) Sera ya Mambo ya Nje ya Jamhuri ya Muungano inalinda maslahi ya Taifa na mamlaka kamili ya nchi na kwamba itatekelezwa kwa uwazi ili:<br>(a) kulinda uhuru wa kujiamulia, heshima ya mipaka ya nchi, uhuru wa kisiasa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;<br>(b) kulinda uhuru, haki za binadamu, usawa na demokrasia;<br>(c) kukuza ujirani mwema;<br>(d) kuendeleza umoja wa Afrika;<br>(e) kukuza ushirikiano wa kiuchumi na wabia wa maendeleo;<br>(f) kuunga mkono utekelezaji wa sera ya kutofungamana na upande wowote na ushirikiano | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | wa nchi maskini duniani;<br>(g) kuunga mkono Umoja wa Mataifa katika jitihada zake za kuimarisha maendeleo ya uchumi wa kimataifa, amani na usalama; na<br>(h) Kuwatambua na kuwashirikisha raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wanaoishi nje ya mipaka ya Tanzania (Diaspora) katika shughuli za maendeleo na uchumi wa Tanzania.<br>(2) Bunge litatunga sheria itakayosimamia utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje. | | na kusimamia utekelezaji wa sera ya mambo ya nje. |
| | | (v) Aya (d) ifutwe na badala yake iandikwe kama ifuatavyo:<br>"(d) kuheshimu sheria za kimataifa zisizovunja Katiba hii". | Sheria yoyote ya kimataifa itakayokuwa kinyume na Katiba hii isiruhusiwe kutumika. | |
| | | (vi) Aya (d), (e) na (h) zirekebishwe ili kulifanya Shirikisho la Tanzania kuwa mshawishi katika kufikia mikataba ya kimataifa. | | |
| | | (vii) Aya (g) ifutwe na badala yake iandikwe kama ifuatavyo:<br>"(g) kupambana na makosa ya kimataifa ya kijinai kwa kuzingatia masharti ya Katiba hii". | | |
| | | (viii) Iongezwe ibara ndogo mpya itakayoeleza wazi kuwa masuala yote ya uhusiano wa kimataifa lazima yahakikishe yanalinda rasilimali za taifa na kwamba | Ibara hii haijaonyesha kwamba itazingatia kulinda maslahi na rasilimali za taifa | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | yatalenga kumnufaisha kwanza raia wa Tanzania. | | |
| | | (ix) Iongezwe Ibara ndogo mpya ili kuifanya Serikali ya Muungano kuwa na uwezo wa kushawishi katika mikataba ya Kimataifa kwa nchi Washirika wa Muungano. | | |
| | | (x) Iongezwe ibara ndogo mpya itakayotoa tafsiri ya neno “Taifa” | Ili kuondoa utata unaoweza kutokea wakati wa kusimamia sera. | |
| | | (xi) Iongezwe ibara ndogo mpya itakayoweka mipaka baina mambo ya nje na ushirikiano wa kimataifa. | Ili kuondoa utata unaoweza kujitokeza. | |

# SURA YA TATU YA RASIMU

## 3.0 SEHEMU YA KWANZA: MAADILI NA MIIKO YA UONGOZI WA UMMA

| ***Ibara Na.*** | ***Kichwa cha Habari*** | ***Maoni ya Mabaraza*** | ***Sababu ya Maoni*** | ***Marekebisho ya Tume*** |
|---|---|---|---|---|
| | SURA YA TATU | Misingi mikuu ya maadili, miiko ya viongozi na Tume ya Maadili na Uwajibikaji iainishwe katika Katiba. Aidha, itungwe sheria maalum itakayoweka bayana maadili na miiko ya viongozi na kuitambua rasmi Tume ya Maadili na Uwajibikaji. | Katiba ni sheria mama inayobeba misingi mikuu na taratibu za jumla za sheria nyingine zote.<br><br>Hivyo, sheria ya kawaida ndiyo inayopaswa kueleza kwa kina jambo husika, utaratibu wa kulitekeleza jambo hilo, masharti na adhabu inayoweza kutolewa ikiwa jambo hilo litakiukwa.<br><br>Aidha, sheria ina utaratibu mwepesi utakaowezesha maadili na miiko inayotajwa kuainishwa kwa kina, kuimarishwa, kufafanuliwa au kuongezwa vipengele vipya kwa urahisi zaidi kuliko ikikaa kwenye Katiba ambo utaratibu | |

| ***Ibara Na.*** | ***Kichwa cha Habari*** | ***Maoni ya Mabaraza*** | ***Sababu ya Maoni*** | ***Marekebisho ya Tume*** |
|---|---|---|---|---|
| | | | wake wa mabadiliko ni mrefu. | |
| | | SEHEMU YA KWANZA NA YA PILI ziunganishwe na isomeke "MAADILI NA MIIKO YA VIONGOZI WA UMMA".<br>Eneo hili liwahusu viongozi wa Umma tu, na si watumishi wote wa umma;<br>Eneo hili liainishe misingi ya ujumla tu, taratibu za utekelezaji ziwe katika Sheria husika. | Ni vigumu kuyatenganisha.<br><br>Sheria ni rahisi kubadilisha. | Kichwa cha habari kimebadilishwa na kinasomeka : "MAADILI YA UONGOZI NA WATUMISHI WA UMMA". |
| 13. | Dhamana ya Uongozi wa Umma | (i) Ibara hii ifutwe. | Maadili, Miiko na misingi ya Utumishi wa umma inaweza kuimarishwa au kuongezwa vipengele vipya kwa urahisi zaidi kuliko ikikaa kwenye Katiba ambayo utaratibu wake wa marekebisho ni mrefu. | 1. Katika Ibara ndogo ya 2(c) (i) yameongezwa maneno :<br>Dhana za "ukweli", na "uwazi".<br>2. Aidha, kwenye 2(c) (e) limeongezwa neno : "uadilifu", kama mambo ya kuzingatiwa katika dhana nzima ya uongozi na heshima kwa kiongozi wa umma. |
| | | (ii) Aya (a) ya Ibara ndogo ya (1) irekebishwe na isomeke kama ifuatavyo:<br>(i) kuzingatia masharti ya Katiba hii, Sheria, kanuni na taratibu zitakazowekwa;<br>(ii) kuheshimu mamlaka na wananchi;<br>(iii) namna inayokuza hadhi ya taifa na kulinda heshima ya ofisi anayoitumikia; na<br>(iv) kukuza imani na heshima ya ofisi, na utumishi wa umma machoni mwa | | |

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Maoni* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| | | wananchi." | | |
| | | (iii) Iongezwe ibara ndogo mpya itakayotoa tafsiri ya maneno "Kiongozi wa umma". | | |
| | | (iv) Aya (b) ya ibara ndogo ya (1) ifutwe. | Makundi ya watu hawa yanahitaji malezi kwani msaada unaotolewa hautoshelezi. | |
| | | (v) Iongezwe aya mpya ya (f) katika Ibara ndogo ya (2) ambayo itasomeka kama ifuatavyo:<br>"(f) anayeongoza na kuthamini na kutunza familia". | | |
| | | (vi) Aya ya (iv) ya Ibara ndogo ya (3)(b) ifutwe na badala yake iandikwe kama ifuatavyo:<br>"(iv) kuwalea watu wasiojiweza, wazee, wagonjwa, watoto na watu wenye ulemavu". | | |
| | | (vii) Aya ya (iv) ya Ibara ndogo ya (3) ifutwe na badala yake iandikwe upya kama ifuatavyo:<br>"(iv) kuhakikisha kuwa msaada wa hifadhi ya jamii na haki ya hifadhi ya jamii inatolewa kwa watu wasiojiweza, wazee, wagonjwa, watoto na watu wenye ulemavu". | Ni vema kuweka wazi hifadhi hizi kwani zinatofautiana na ni muhimu kwa nchi kama Tanzania kuhakikisha upatikanaji wake kwa walengwa. | |
| | | (viii) Ziongezwe ibara nyingine mpya zitakazoeleza dhamana ya uongozi na heshima kwa kiongozi wa umma katika mambo ya msingi kama vile:<br>(a) Rushwa;<br>(b) Kujilimbikizia mali; | | |

| ***Ibara Na.*** | ***Kichwa cha Habari*** | ***Maoni ya Mabaraza*** | ***Sababu ya Maoni*** | ***Marekebisho ya Tume*** |
|---|---|---|---|---|
| | | (c) Utunzaji wa siri za Serikali. | | |
| | | (ix) Inapendekezwa kwamba sura hii na Ibara zake ibaki kama ilivyo. Aidha, kutambuliwa kwa maadili na miiko ya Uongozi na Utumishi wa Umma tu haitoshi bila kuzungumzia maadili ya jamii ya kitanzania na namna watakaochangia kumomonyoa maadili watakavyowajibishwa ili kuweka msingi imara wa jamii yetu kwa kuzingatia maadili na miiko ya mtanzania. Mambo hayo ndio chimbuko la maadili na miiko ya viongozi na watumishi wa Umma. | | |
| | | (x) Ibaki kama ilivyo ili maadili na miiko ya uongozi katika utumishi wa umma yawekwe bayana na kupewa nguvu stahiki ya kisheria | | |
| 14. | Kanuni za Uongozi wa Umma | i. Ibara hii ifutwe. | Maadili, Miiko na misingi ya Utumishi wa umma inaweza kuimarishwa au kuongezwa vipengele vipya kwa urahisi zaidi kuliko ikikaa kwenye Katiba ambayo utaratibu wake wa marekebisho ni mrefu. | 1. Ibara ndogo ya (2) imerekebishwa na inasomeka ''Kwa madhumuni ya Ibara ndogo ya (1), Mamlaka ya nchi itaweka utaratibu wa sheria utakaowezesha Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji kusimamia utekelezaji wa masharti yanayohusu kanuni za Uongozi wa |
| | | ii. Ibara hii ibaki | Mmomonyoko wa maadili ya umma umeongezeka. | |
| | | iii. Iongezwe ibara kuhusu maadili ya wananchi | Ili wananchi wawe na maadili na tabia | |

<table>
<tr><th>Ibara Na.</th><th>Kichwa cha Habari</th><th>Maoni ya Mabaraza</th><th>Sababu ya Maoni</th><th>Marekebisho ya Tume</th></tr>
<tr><td></td><td></td><td></td><td>inavyostahili na kusaidia utunzaji wa dhima na Tunu za Taifa.</td><td>Umma”.<br><br>2. Aidha, Ibara ndogo ya (3) yameongezwa maneno sheria za nchi mwisho wa sentensi.</td></tr>
<tr><td rowspan="5">15.</td><td rowspan="5">Zawadi katika Utumishi wa Umma</td><td>(i) Ibara hii ifutwe.</td><td>Masuala ya Zawadi yatatoa fursa ya kuwepo kwa Rushwa.</td><td rowspan="4">1. Marginal note imefanyiwa marekebisho na itasomeka ‘’ Zawadi katika Utumishi wa Umma”<br><br>2. Ibara ya 15 (1) imerekebishwa na imeandikwa upya kama ifuatavyo: Kiongozi wa umma wakati anapotekeleza shughuli za kiserikali, akipewa zawadi au kitu chochote, zawadi au kitu hicho kitakuwa ni mali ya Jamhuri ya Muungano na ataiwasilisha kwa Katibu Mkuu Kiongozi kupitia kwa Katibu Mkuu wa Wizara au kiongozi wa taasisi ya Serikali inayohusika, “akiainisha”…</td></tr>
<tr><td>(ii) Ibara 15(1) iandikwe kama ifuatavyo: Kiongozi au mtumishi wa umma wakati anapotekeleza shughuli za kiserikali, akipewa zawadi au kitu chochote, zawadi au kitu hicho kitakuwa ni mali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kitawasilishwa kwa Katibu Mkuu Kiongozi kupitia kwa Katibu Mkuu wa Wizara au taasisi ya Serikali inayohusika, akiainisha</td><td rowspan="2">Masharti hayo yaende katika sheria husika.</td></tr>
<tr><td>(iii) Ibara ndogo ya (1) irekebishwe kwa kufuta maneno “mtumishi wa umma” na badala yake iandikwe “kiongozi wa umma”.</td></tr>
<tr><td>(iv) Aya (a) katika ibara ndogo ya (2) maneno “Bila kuathiri Katiba hii” yawekwe kabla ya neno “hatafungua”.</td><td></td></tr>
<tr><td></td><td></td><td>Imeongezwa ibara mpya ya 16 inayosomeka kama</td></tr>
</table>

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Maoni* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| | | | | ifuatavyo:<br>"Akaunti nje ya nchi na mikopo" na itasomeka;<br>"Kiongozi wa umma -<br>(a) hatafungua au kumiliki akaunti ya benki nje ya Jamhuri ya Muungano isipokuwa tu kwa namna ambayo sheria za nchi zinaruhusu; na<br>(b) hataomba au kupokea mkopo au faida yoyote kwa namna au mazingira ambayo yanashusha hadhi au heshima ya utumishi wa umma." |
| 16. | Wajibu wa kutangaza mali na madeni | 1) Ziongezwe ibara ndogo kama ifuatvyo:<br>(i) watoto wake walio chini ya umri wa miaka kumi na nane, mara moja kila mwaka kwa Tume ya Maadili na Uwajibikaji.<br>(ii) Bunge litatunga sheria itakayosimamia, pamoja na mambo mengine:<br>a) ngazi au orodha ya viongozi wa umma, wanaopaswa kutangaza mali na madeni yao; na<br>b) utaratibu wa kuwasilisha taarifa ya mali na madeni kwa Tume ya Maadili.<br>2). Ibara hii ifutwe. | (1) Maadili, Miiko na misingi ya Utumishi wa umma inaweza kuimarishwa au kuongezwa vipengele vipya kwa urahisi zaidi kuliko ikikaa kwenye Katiba ambayo utaratibu wake wa marekebisho ni mrefu.<br>(2) Masharti hayo yaende katika sheria husika. | Ibara ya 16 sasa inakuwa Ibara ya 17, ambayo imeongezwa ibara ndogo kama ifuatavyo:<br>2(c) itakayosomeka kama ifuatavyo:<br>"watoto wake walio chini ya umri wa miaka kumi na nane, mara moja kila mwaka kwa Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji.<br>(3) Bunge litatunga sheria itakayosimamia, pamoja na mambo mengine:<br>(a)ngazi au orodha ya |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | (iii) Iongezwe ibara ndogo mpya ya (3) ambayo iandikwe kama ifuatavyo: “(3) Mtu yeyote mtanzania au si mtanzania lakini anafanya kazi au biashara au uwekezaji Tanzania anaweza kuchunguzwa kuhusu uhalali wa umiliki wa mali zake na inaweza kutaifishwa ama kufilisiwa iwapo ameipata isivyo halali”. | | viongozi wa umma, wanaopaswa kutangaza mali na madeni yao; na (b)utaratibu wa kuwasilisha taarifa ya mali na madeni kwa Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji kwa mujibu wa Katiba hii. |
| | | (iv) Ibara hii irekebishwe ili Bunge liwe na mamlaka ya kutunga sheria itakayoainisha ngazi ya viongozi husika, thamani ya mali na adhabu kwa watakaokiuka sheria. | | |
| | | (v) Ibara ya 16(1) iongezwe maneno “kiongozi wa umma na viongozi wa kada mbalimbali. | Kuepuka kwa viongozi wa kada mabalimbali kujilimbikizia mali. | |
| 17. | Mgongano wa kimaslahi | (i) Ibara hii ifutwe. | Maadili, Miiko na misingi ya Utumishi wa umma inaweza kuimarishwa au kuongezwa vipengele vipya kwa urahisi zaidi kuliko ikikaa kwenye Katiba ambayo utaratibu wake wa marekebisho ni mrefu. | 1. Ibara hii itakuwa Ibara ya 18 na imefanyiwa marekebisho yafuatayo: Katika Ibara ndogo ya (3) yameongezwa maneno: “Muda wa kukaa katika nafasi ya madaraka iliyompatia fursa ya kushiriki katika kuamua maslahi husika”. 2. Ibara ndogo ya (4) isomeke: |
| | | (ii) Ibara ndogo ya (1) irekebishwe kwa kufuta maneno “au mtu yeyote wake wa karibu”. | Yamejirudia. | |
| | | (iii) Ibara ndogo ya (1) irekebishwe na ieleze kuwa mgongano wa maslahi utokane na utendaji na wadhifa wa kiongozi husika. | Mtumishi asibanwe kujishughulisha na shughuli zisizokinzana na sheria na taratibu za | |

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Maoni* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| | | (iv) Ibara ndogo itakayosomeka kama ifuatavyo iongezwe: Masharti ya Ibara ndogo ya (3), hayatahusu kiongozi yeyote wa umma ambaye kutokana na asili ya nafasi ya madaraka au aina ya kazi zake anapaswa kushiriki katika upangaji wa mishahara au maslahi mengine ya watumishi wa umma. | utumishi wa umma kuondoa utata katika kujua kiongozi anayekusudiwa katika Ibara hii. | "Masharti ya Ibara ndogo ya (3), hayatahusu kiongozi yeyote wa umma ambaye kutokana na asili ya nafasi ya madaraka au aina ya kazi zake anapaswa kushiriki katika upangaji wa mishahara au maslahi mengine ya watumishi wa umma." |
| | | (v) Maneno "kiongozi wa Umma" katika ibara ndogo ya (1) yatolewe tafsiri.<br>(vi) Kiongozi wa Umma hataruhusiwa kushika nyadhifa mbili au zaidi au kutumikia Mihimili ya Dola zaidi ya mmoja kwa wakati mmoja. | | |
| | | (vii) Ziongezwe aya mpya (f) na (g) katika ibara ndogo ya (4) kama ifuatavyo:<br>"(f) uanzishaji wa mitaala ya elimu;<br>(g) Bila ya kuathiri masharti ya aya (c) uanzishaji wa mitaala ya elimu ya dini na uendelezaji wa masomo ya dini utafanywa na wanadini husika". | (a) Mitaala ni mkusanyiko wa masomo mbalimbali yanayofundishwa katika nchi yakiwemo siasa, maadili, falsafa nk. Bunge halitaweza kutunga sheria kusimamia mitaala ya somo moja moja.<br>(b) Nchi nyingi duniani zinaruhusu watu wa dini mbalimbali kuwa na mfumo wao wa elimu ili kutoa nafasi ya kufundisha watoto wao imani, mila na desturi zao. | |

| ***Ibara Na.*** | ***Kichwa cha Habari*** | ***Maoni ya Mabaraza*** | ***Sababu ya Maoni*** | ***Marekebisho ya Tume*** |
|---|---|---|---|---|
| | | (viii) Ibara ndogo ya (3) ifutwe. | Haina mantiki kumzuia Kiongozi kushiriki kuongeza maslahi ya watumishi wake ambapo naye anaweza kushiriki. | |
| | | (ix) Ibara ndogo ya (5) irekebishwe ili kuruhusu mtu mmoja kuwa katika nyadhifa zaidi ya moja. | Hii ni kutokana na utamaduni uliopo, mfano mtumishi kuteuliwa katika Bodi ya Wakurugenzi ya mamlaka tofauti na alipoajiriwa. | |
| | | (x) Ibara ndogo ya (5) irekebishwe. | Suala hili ni vigumu kutekelezeka na huenda likaathiri mfumo na sheria au taratibu za nchi washirika, kuna baadhi ya nyadhifa zinahitaji mtu kutoka muhimili mwingine, mfano, Katiba ya Zanzibar inaeleza kuwa Mjumbe mmoja wa Tume ya Uchaguzi lazima awe Jaji wa Mahakama Kuu ya Zanzibar. | |
| | | (xi) Iongezwe ibara ndogo ya (6) ambayo iandikwe kama ifuatavyo: “(6) Kiongozi wa umma hatashiriki katika maamuzi ya jambo au shughuli yoyote ambayo ana maslahi nayo yeye binafsi, mwenza wake, mtoto wake, jamaa yake, rafiki yake au mtu wake yeyote wa karibu”. | | |
| | | (xii) Ibara ya 17. Ibaki kama ilivyo | Kulinda maadili. Imejitosheleza | |

| ***Ibara Na.*** | ***Kichwa cha Habari*** | ***Maoni ya Mabaraza*** | ***Sababu ya Maoni*** | ***Marekebisho ya Tume*** |
|---|---|---|---|---|
| 18. | Matumizi ya mali ya umma | (i) Ibara hii ifutwe. | Maadili, Miiko na misingi ya Utumishi wa umma inaweza kuimarishwa au kuongezwa vipengele vipya kwa urahisi zaidi kuliko ikikaa kwenye Katiba ambayo utaratibu wake wa marekebisho ni mrefu. | 1. Ibara ya 18 imekuwa Ibara ya 19.<br>2. Ibara imeandikwa upya na itasomeka kama ifuatavyo: ''Kiongozi wa Umma hataruhusiwa kutumia au kuruhusu kutumika kwa mali yoyote ya umma, zikiwemo zilizokodishwa kwa Serikali, kwa madhumuni ya kujipatia yeye binafsi au kumpatia mtu mwingine yeyote manufaa yoyote. |
| | | (ii) Ibara hii ifutwe na badala yake iandikwe upya kama ifuatavyo: "18. Haitaruhusiwa kwa kiongozi, mfanyakazi yeyote wa Umma kutumia au kuruhusu kutumika kwa mali yoyote ya umma, zikiwemo zilizokodishwa kwa Serikali, kwa madhumuni ya kumpatia yeye binafsi au mtu mwingine yeyote manufaa ya kiuchumi". | Mali za umma kama nyumba, magari (vipando), idara za utendaji na mali asili hutumika kama sehemu ya mtu kujiona ni chake wengine hawana haki na kujinufaisha mwenyewe kiuchumi na hata kisiasa na umaarufu. | |
| | | (iii) Iongezwe maneno "ni marufuku kwa kiongozi wa umma kuuza mali za umma"<br>(iv) Kuwe na ibara mpya itakayoelekeza utekelezaji ma masharti ya maadili. | Ni vigumu kupata eneo mbadala.<br>Ni marufuku kuuza eneo lililotengwa kwa manufaa ya wananchi. | Aidha imeongezwa Ibara mpya ya 20, kuhusiana na utekelezaji wa masharti ya maadili na kulipa Bunge mamlaka ya kutunga sheria ya kutaifisha mali zilizopatikana kwa njia zisizo halali na pia kuwe na mitaala ya katiba na maadili shuleni. |
| | | | | |
| 19. | Matumizi ya masharti ya maadili kwa watumishi wa umma | (i) Ibara hii ifutwe. | Maadili, Miiko na misingi ya Utumishi wa umma inaweza kuimarishwa au kuongezwa vipengele vipya kwa urahisi zaidi | Ibara ya 19 imeingizwa ndani ya Ibara ya 20 na imekuwa Ibara ndogo ya 2. |

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Maoni* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| | | | kuliko ikikaa kwenye Katiba ambayo utaratibu wake wa marekebisho ni mrefu. | |
| | | (ii) Mwisho wa ibara hii yaongezwe maneno "katika sheria itakayotungwa na Bunge". | | |
| | | (iii) Iongezwe ibara ndogo ya (3) ambayo itasomeka kama ifuatavyo:<br>"(3) Masharti yaliyoainishwa katika ibara ya 13 hadi 18 yatawahusu pia viongozi na watumishi wa umma wa nchi washirika wa Muungano". | | |

## 3.1 SEHEMU YA PILI: MIIKO YA UONGOZI WA UMMA

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Baraza* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| | MIIKO YA UONGOZI WA UMMA | Kichwa cha habari cha Sura ya Tatu kiandikwe kama ifuatavyo: "MAADILI YA TAIFA NA MIIKO YA UONGOZI NA UTUMISHI WA UMMA" | Maadili ya Taifa ni kinga ya haki za wananchi, uhuru wa wananchi na vitu vyote ambavyo wanavithamini. Maadili ya Taifa yanapaswa kumbana kiongozi na asiyekuwa kiongozi. | |
| 20. | Utii wa Miiko ya Uongozi wa Umma | (i) Ibara ndogo ya (1) hadi ya (3) zifutwe. | Vinahusu utekelezaji hivyo viwekwe kwenye sheria. | 1. Ibara ya 20 imekuwa ya 21.<br>2. Ibara ndogo ya 21(2)(b)(iii) imerekebishwa na kusomeka "kutenganisha biashara na shughuli binafsi na masuala yanayohusiana na uongozi". |
| | | (ii) Iongezwe aya ya (ii) mpya katika ibara ndogo ya (2)(a) kama ifuatavyo:<br>"(ii) kuvunja au kukiuka masharti ya sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa kwa mujibu wa sheria"; | | |
| | | (iii) Aya ya (iii) katika ibara ndogo ya (2)(b) ibadilishwe na isomeke:<br>"(iii) Wafanya biashara wasiruhusiwe kugombea nafasi yeyote ya uongozi". | Ili kutoa fursa kwa wananchi kuchagua kati ya kufanya biashara na uongozi. | |
| | | (iv) Iongezwe aya ya (ii) mpya katika ibara ndogo ya (2)(a) kama ifuatavyo:<br>"(ii) kuvunja au kukiuka masharti ya sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa kwa mujibu wa sheria"; | | |
| | | | (i) Neno "kutenganisha" | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Baraza | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | lifutwe lisomeke "kutojihusisha". | |
| | | | (ii) Isomeke kiongozi atenganishe shughuli binafsi na shughuli za uongozi. | |
| | | 1. Ibara ya 20(3)c iongezwe maneno "mwizi au mbadhirifu wa mali za umma asimamishwe kazi, ashtakiwe, afilisiwe mali zake na achukuliwe hatua za kisheria. | | |
| | | Ibara ya 20(1) iongezwe maneno "miiko ya viongozi wa umma na wa vyama vya siasa". | | |
| 21. | Marufuku kwa baadhi ya vitendo | (i) Ibara hii ifutwe. | Masharti hayo yaende katika Sheria husika. | 1. Ibara ya 21 imekuwa Ibara ya 22.<br>2. Ibara ya 22(2) imefanyiwa marekebisho na inasomeka kama ifuatavyo:<br>Mtumishi wa umma haruhusiwi kugombea, kuchaguliwa au kuteuliwa kushika nafasi ya madaraka katika chama cha siasa au nafasi ya kisiasa ya aina yoyote chini ya Katiba hii.<br><br>3. Ibara ndogo ya (3) imeandikwa upya na itasomeka kama ifuatavyo:<br>(3)Endapo mtumishi wa |
| | | (ii) Ibara hii ihamishiwe katika ibara ya 11. | Inahusu masuala ya Utumishi wa Umma. | |
| | | (iii) Ibara ndogo ya (1) hadi ya (3) zifutwe. | Vinahusu utekelezaji hivyo viwekwe kwenye sheria kwa sababu masuala ya miiko na maadili huwa yanabadilika mara kwa mara. | |
| | | (iv) Ibara ndogo ya (1) ifutwe. | (a) Wafanyakazi wanaruhusiwa kuwa na ajira zaidi ya moja ili mradi muda hauingiliani kwa mfano madaktari, wanataaluma, n.k.<br>(b) Hii ni njia mojawapo ya kuongeza kipato kwa wafanyakazi na | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Baraza | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | kuwa na maisha bora. | umma ataamua kugombea, kuchaguliwa au kuteuliwa kushika-<br>(a) nafasi ya madaraka ya kisiasa ya aina yoyote chini ya Katiba hii; au<br>(b) uongozi wa ngazi yoyote katika chama cha siasa,mtumishi huyo atachukuliwa kuwa utumishi wake umekoma tangu siku ya kuteuliwa kuwa mgombea, kuchaguliwa au kuteuliwa kushika nafasi ya kisiasa au uongozi katika chama cha siasa. |
| | | (v) Ibara ndogo ya (1) irekebishwe kwa kuongeza maneno "ya kudumu" baina ya maneno "yoyote" na "yenye". | | |
| | | (vi) Ibara ndogo ya (1) irekebishwe ili kutoa fursa kwa mtumishi wa umma kufanya kazi nyingine baada ya muda wa kazi. | (i) Ili mtumishi aliye katika ajira ya kudumu aweze kufanya kazi nyingine baada ya kukamilisha muda wa kazi katika utumishi wa umma;<br>(ii) Ili watumishi waweze kujipatia kipato halali cha kutosha waweze kujikimu kimaisha. | |
| | | (vii) Ibara ndogo ya (1) yaongezwe maneno "ya kudumu" baina ya neno "yoyote" na neno "yenye". | | |
| | | (viii) Ibara ndogo ya (1) ibadilishwe na iandikwe kama ifuatavyo:<br>"(1) Mtumishi wa Umma aliye katika ajira ya kudumu ataruhusiwa kuingia katika ajira nyingine yoyote yenye malipo ya mshahara baada ya kutimiza masharti ya mwajiri wake katika taasisi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano tu". | | |
| | | (ix) Ibara ndogo ya (1) iainishe maadili ya Taifa. Inapendekezwa maadili ya Taifa yawe:<br>(a) Kuheshimiana;<br>(b) Kujipatia mali kwa njia halali; | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Baraza | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | (c) Kuheshimu haki za binadamu;<br>(d) Kutokubaguana;<br>(e) Kutojilimbikizia mali;<br>(f) Matumizi ya utajiri wa nchi kwa manufaa ya watu wote;<br>(g) Kufanya kazi kwa kujituma;<br>(h) Kuheshimu na kutii utawala wa sheria na sheria za nchi;<br>(i) Uwajibikaji. | | |
| | | (x) Ibara ndogo ya (2) ifutwe na badala yake iandikwe upya kama ifuatavyo:-<br>"(2) Mtumishi wa umma haruhusiwi kuchaguliwa au kuteuliwa kushika madaraka katika chama cha siasa kuanzia ngazi ya Tawi hadi Taifa". | Hali hii itaondoa uwezekano wa watumishi wa umma katika ngazi zote kushabikia mambo ya siasa sehemu za kazi. | |
| | | (xi) Ibara ndogo ya (3) irekebishwe ili wastaafu waruhusiwe kuendelea kutumia ujuzi wao katika nafasi watakazokuwa wamepewa kwa kuzingatia vigezo na uwezo wao wa kumudu majukumu hayo. | Hoja hii inaondoa fursa ya kutumia ujuzi na utaalamu walionao watumishi wa umma waliostaafu. Aidha, Ibara hii inakinzana na mapendekezo yaliyomo katika Ibara ya 47(2) inayohusu haki ya wazee kupewa fursa ya kuendelea kutumia utaalam na ujuzi wao kwa faida ya jamii. | |
| | | (xxvi) Aya ya (i) ya Ibara ndogo ya (3)(c) irekebishwe na iandikwe kama ifuatavyo:<br>"(i) Kuwaletea wananchi maisha | Katika kutekeleza malengo ya taifa serikali ihakikishe kwamba itawapatia wananchi | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Baraza | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | bora kwa kukuza uchumi na kuondoa umaskini". | maisha bora kwa kuondoa umaskini. | |
| | | (xxvii) Aya ya (ii) ya Ibara ndogo ya (3)(c) irekebishwe na iandikwe kama ifuatavyo:<br>"(ii) Kuhakikisha kwamba shughuli za Serikali zinatekelezwa kwa njia ambazo zitahakikisha kuwa rasilimali za Taifa zinaendelezwa, zinahifadhiwa na zinatumiwa kwa manufaa ya wananchi wote kwa jumla". | Kuhakikisha kwamba shughuli za serikali zinatekelezwa kwa njia ambazo zitahakikisha kuwa utajiri wa taifa unaendelezwa, unahifadhiwa na unatumiwa kwa manufaa ya wananchi wote kwa jumla na pia kuzuia mtu kumnyonya mtu mwingine. | |
| | | (xxviii) Ziongezwe aya mpya mara baada ya aya (c) katika ibara ndogo ya (3) kama ifuatavyo:<br>(d) "Serikali itahakikisha kuwa inaimarisha miundombinu ya barabara, reli, usafiri wa majini na viwanja vya ndege inayoimarisha uchumi wa nchi;<br>(e) Serikali kwa makusudi ishiriki katika kujenga viwanda vya kati na vikubwa. Chuma, mbolea, zana za kilimo kwa kuingia ubia au yenyewe;<br>(f) Serikali kwa makusudi inaandaa wataalam wazawa wa fani mbalimbali ili kushiriki na kushika uongozi katika mashirika | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Baraza | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | ya umma au ubia”. | | |
| | | (xii) Kichea cha habari kiwe MAADILI YA UONGOZI WA UMMA | | |
| | | (xiii) baada Ibara ya 21 iongezwe ibara mpya itakayoeleza kama ifutavyo: “Maadili ya Taifa yaliyotajwa katika Sura ya tatu ya Katiba hii yatambana kila mtu ama mamlaka yatakayotafsiri ama kutekeleza Katiba hii au sheria, yatakayotunga ama kutekeleza sera au kutoa maamuzi ya kisera.” | | |
| | | (xiv) katika Ibara ndogo ya (3) yaongezwe maneno “Kwa kuzingatia elimu, ujuzi na uzoefu” mwanzo wa sentensi. | | |
| | | (xv) iongezwe ibara mpya itakayoeleza dhana nzima ya maadili ya viongozi wa umma katika Sura ya Tatu. | Hakuna dhana ya maadili ya viongozi katika Rasimu. | |
| | | (xvi) Isomeke “watumishi wa umma waruhusiwe kuchagua au kuchaguliwa, lakini utumishi wao ukome baada ya kuchaguliwa. | | |

# SURA YA NNE YA RASIMU

## 4.0 SEHEMU YA KWANZA: HAKI ZA BINADAMU, WAJIBU WA RAIA NA MAMLAKA ZA NCHI

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Baraza | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| 22. | Uhuru, utu na usawa wa binadamu | (i) Inapendekezwa kwamba Sehemu ya Kwanza yote ya Sura ya Nne inayohusu (Haki za Binadamu) kuanzia Ibara ya 22 hadi 47 ifutwe. | Suala la haki za binadamu ziachiwe nchi washirika wa Muungano wenyewe ili:<br>(a) kutoa fursa kwa nchi washirika wa Muungano kupitisha Haki za Binadamu katika Katiba zao husika kwa kupitia vyombo vyao vya kutunga sheria.<br>(b) Rasimu haijaorodhesha haki za Binadamu kuwa ni miongoni mwa mambo ya Muungano.<br>(c) Haki za Binadamu zinakwenda sambamba na utamaduni na desturi za nchi husika.<br>(d) Katika hali hii Tanganyika na Zanzibar zinatofautiana kiutamaduni na kidesturi. | Ibara ya 22 imekuwa ya 23 na itabaki kama ilivyo. |
| | | (ii) Iongezwe ibara mpya ya 22 ambayo itasomeka kama ifuatavyo:<br>"22. Masharti ya ibara hii yatawahusu pia viongozi na watumishi wa Nchi Washirika wa Muungano"; | | |
| | | (iii) Ibara ya 22 ya sasa iwe 23 na kuendelea. | | |
| 23. | Haki ya kuwa hai | (i) Iongezwe ibara ndogo ya (2) na (3) ambazo zitasomeka kama | (a) Haki ya kuishi haiko madhubuti (Absolute) | 1. Ibara ya 23 imekuwa ya 24 na itabaki |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Baraza | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | ifuatavyo:<br>"(2) Haki ya kuishi itaanzia pale mimba inapotungwa.<br>(3) Utoaji mimba hautaruhusiwa". | bado haki hii imefungiwa katika sheria ikiwa na maana kuwa haki ya kuishi inaweza kuminywa na sheria.<br>(b) Hali hii inaacha mwanya wa kuwepo kwa adhabu ya kifo.<br>(c) Pia ibara ya 69(2)(k) inayoelezea kazi za Rais imezitaja kuwa ni pamoja na 'Kuidhinisha utekelezaji wa adhabu ya kifo iliyotolewa kwa mujibu wa sheria. | kama ilivyo.<br>2. Marginal Note imerekebishwa na itasomeka " Haki ya kuishi" badala ya "Haki ya kuwa hai" |
| 24. | Marufuku kuhusu ubaguzi | Aya ya (b) ya ibara ndogo ya (7) irekebishwe na iandikwe kama ifuatavyo:<br>"(b) ni marufuku kwa mtu aliyeshtakiwa kwa kosa la jinai au kosa lingine kutendewa kama mtu aliyehukumiwa kwa kutenda kosa hilo hadi itakapothibitika mahakamani au kwenye chombo kingine chenye dhamana kuwa anayo hatia ya kutenda kosa hilo". | | 1. Ibara ya 24 itakuwa ya 25 na imefanyiwa marekebisho katika Ibara ndogo ya 7(b) kwa kubadilisha maneno "isipokuwa tu kama itathibitika" badala ya maneno "hadi itakapothibitika",<br>2. katika Ibara ndogo ya 7(e) neno "masharti" lisomeke "mashtaka" |
| 25. | Haki ya kutokuwa mtumwa | (i) Ibara ndogo ya (1) iishie katika neno "kutweza", maneno yaliyobaki yafutwe. | Kuondoa kujirudia kwa maneno. | 1. Ibara ya 25 itakuwa ya 26.<br>2. Ibara ndogo ya 26(2) isomeke "Biashara |
| | | (ii) Ibara ndogo ya (1) irekebishwe ili | Maelezo ya Ibara ya 25 ya | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Baraza | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | itambue wajibu wa kufanya kazi kama ilivyo Ibara ya 25 ya Katiba ya sasa. | Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya sasa yanajitosheleza zaidi kuliko ilivyowekwa kwenye Rasimu. | haramu ya kusafirisha na kuuza binadamu ni marufuku katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania” |
| | | (iii) Ibara ndogo ya (2) irekebishwe kwa kuongeza neno “haramu” kati ya maneno “Biashara” na “ya kusafirisha.” | Biashara ya kusafirisha binadamu kama ilivyowekwa katika Ibara ya 25(2) si kosa na hivyo haiwezi kupigwa marufuku na Katiba. | |
| | | (iv) Ibara ndogo ya (2) ifutwe. | (a) Ipo sheria inayojitosheleza.<br>(b) Biashara ya kusafirisha binadamu inajumuisha biashara halali ya usafirishaji wa abiria na ibara ndogo ya 25(1)(c) inakidhi matakwa yanayokusudiwa. | |
| | | (v) Iongezwe ibara ndogo mpya itakayoeleza kwamba, kila mtu ana haki ya kupata msaada wa sheria. | | |
| | | (vi) Ibara ya 25(c) neno “kufanyiwa” lisomeke “kufanywa” | | |
| 26. | Uhuru wa mtu binafsi | (i) Ibara hii irekebishwe ili uhuru wa mtu usisitishwe mpaka vyombo vya ulinzi na usalama viwe vimekamilisha uchunguzi wao. | Uhuru wa mtu binafsi umekuwa ukisitishwa au kuingiliwa na vyombo vya dola bila ya sababu ya msingi. | Ibara ya 26 itakuwa ya 27 na itabaki kama ilivyo. |
| | | (ii) Aya (a) ya Ibara ndogo ya (2) ifutwe. | Kukiacha kipengele hiki ni kuendeleza utamaduni wa huko nyuma wa kutoa | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Baraza | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | haki kwa mkono mmoja na kunyan'ganya kwa mkono wa pili (vifungu nyakuzi) hii itahalalisha matumizi ya sheria kandamizi kutungwa kama ilivyowahi kutumika vibaya kama vile kutungwa kwa sheria za kuweka watu vizuizini ya mwaka 1962, sheria ya kuhamisha watu kwa nguvu nk. | |
| | | (iii) Iongezwe aya mpya ya (c) katika ibara ndogo ya (2) ambayo iandikwe kama ifuatavyo:<br>"(c) Ndugu wajulishwe na mamlaka husika pindi mtu anapofariki". | | |
| | | (iv) Ibara ya 26(1) iongezwe maneno "bila ya kuvunja sheria"<br>(v) Ongeza maneno "uhuru uwekewe mipaka"<br>(vi) Iongezwe isomeke "mtu yeyote aliewekwa kizuizini na ikathibitika hana hatia afidiwe" | Kutilia mkazo | |
| 27. | Haki ya faragha na usalama wa mtu | (i) Iongezwe ibara ndogo mpya ya (2) itakayokuwa kama ifuatavyo, na ibara ndogo ya (2) iwe (3):<br>"(2) Haitaruhusiwa mtu yeyote kuunda na kuwa na familia ya jinsia moja kwa mujibu wa mila na desturi za Mtanzania." | Kipengele hiki kitaepusha kuwa na ndoa za jinsia moja ambayo ni kinyume na maadili, mila na desturi za nchi yetu. | 1. Ibara ya 27 inakuwa Ibara ya 28.<br>2. Ibara ndogo ya (2) imeongezwa maneno "Itaweka utaratibu wa sheria kuhusu hali" mbele ya maneno "mamlaka ya nchi" |
| | | Ibara ndogo ya (2) irekebishwe ili | Haijaelezewa vizuri | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Baraza | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | iweke bayana kuwa utaratibu utakaoowekwa kisheria uwe wa wazi na ueleweke. | umuhimu wa utaratibu utakaoowekwa kisheria kuwa wazi ili ujulikane vyema na wote. | |
| | | (ii) Ibara ya 27(1)isomeke "Kila mtu ana haki ya kuwa faragha ikiwa ni pamoja na<br>(a) haki ya kuheshimiwa na kupata hifadhi kwa nafsi yake, maisha yake binafsi, familia yake na nyumbani kwake;<br>(b) kutopekuliwa yeye mwenyewe, ofisini au nyumbani kwake au mali yake;<br>(c) taarifa zake binafsi kutotolewa bila ya ridhaa yake;<br>(d) uhuru wa kufanya mawasiliano bila ya kuingiliwa | | |
| | | (iii) Ibara ya 27(2) isomeke "Kwa madhumuni ya kuhifadhi haki ya mtu, mamlaka ya nchi itaweka utaratibu wa sheria kuhusu hali, namna na kiasi ambacho haki ya mtu ya faragha na usalama wa nafsi yake, mali na maskani yake, yanaweza kuingiliwa bila ya kuathiri masharti ya ibara hii ili mradi masharti hayo yawe kwa mujibu wa ibara ya 53" | | |
| 28. | Uhuru wa mtu kwenda anakotaka | Katika Ibara ndogo ya (1) yaongezwe maneno "kwa mujibu wa sheria" mwisho wa ibara hii. | | Ibara ya 28 inakuwa Ibara ya 29 na itabaki kama ilivyo. |
| | | Ibara ya 28(2) isomeke "Kwa | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Baraza | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | madhumuni ya kuhifadhi haki ya mtu kwenda anakotaka mamlaka ya nchi itaweka utaratibu wa sheria kuhusu hali, wakati, namna na kiasi ambacho haki ya kwenda anakotaka yaweza kuingiliwa bila ya kuathiri masharti ya ibara hii ilimradi masharti hayo yawe kwa mujibu wa ibara ya 53” | | |
| 29. | Uhuru wa maoni | (i) Ibara ibadilishwe | Kutoa ufafanuzi aina ya mawasiliano yaliyokusudiwa katika Ibara hii. | 1. Ibara ya 29 inakuwa Ibara ya 30.<br>2. Katika Ibara ndogo ya 30(1)(a) isomeke: “ ana haki na uhuru wa :-…………..”<br>3. 30(1)(iii) Isomeke ‘’ugunduzi, ubunifu na utafiti wa sanaa, sayansi na mapokeo ya asili. |
| | | (ii) Aya (a) katika ibara ndogo ya (2) iandikwe kama ifuatavyo: “(a) Haki zilizotajwa katika ibara ndogo ya (1) hazitatumika kwa madhumuni ya propaganda za vita au kuleta machafuko ya kisiasa au ushawishi wa chuki, ubaguzi wa kijinsia, dini au masuala yoyote yanayoweza kuleta madhara kwa taifa”. | | |
| | | (iii) Sehemu inayohusu masuala ya tasnia ya habari na uhuru wa habari iwe na kichwa cha habari cha pekee kwa ajili ya Ibara ya 29, 30, 30A, 30B na 30C chini ya Sehemu ya Pili mpya katika Sura ya Nne. | | |
| | | (iv) Sehemu ya pili ya Rasimu iwe Sehemu ya Tatu (badala ya kuwa chini ya kichwa cha habari cha *HAKI ZA BINADAMU* kinachojumuisha Ibara zote tangu | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Baraza | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | Ibara ya 22 hadi Ibara ya 47). | | |
| | | (v) Kichwa cha habari kiwe *UHURU WA HABARI NA VYOMBO VYA HABARI.* Kichwa cha habari hiki kipya pamoja na Ibara zake za 29 na 30, 30A, 30B na 30C, vihamishwe na kuorodheshwa baada ya Ibara ya 47. | Ili mfululizo wa Ibara zinazohusu haki za binadamu usikatishwe na Ibara za mambo ya habari. | |
| | | (vi) Marginal notes ya ibara hii ipanuliwe kusomeka "uhuru wa kujieleza" kwani maoni ni sehemu ndogo tu; | | |
| | | (vii) Ibara za 29(1)(b) (iii) na (vi) viunganishwe na kusomeka "haki za ubunifu wa sanaa; ugunduzi wa sayansi; uandishi; utafiti wa sanaa na sayansi" | | |
| | | (viii) Ibara ya 29(1)(a) irekebishwe na isomeke "kutafuta na kupata habari au taarifa kutoka serikali na mamlaka/taasisi zinginezo" | | |
| | | (ix) Ibara ya 29(1)(b) isomeke "kutumia habari na taarifa zilizopatikana au kusambaza taarifa"<br>(x) haki na uhuru wa ugunduzi, ubunifu na utafiti wa sanaa, sayansi na mapokeo ya asili. | | |
| 30. | Uhuru wa habari na vyombo vya habari | (i) Ibara ndogo ya (2) irekebishwe na kuboreshwa kwa namna ambayo haitahalalisha usambazaji wa habari kutoka kwenye vyanzo visivyo rasmi na visivyoaminika. | Uhuru wa vyombo vya habari ni lazima uzingatie uwajibikaji utakaohakikisha haki ya watu wengine | 1. Ibara ya 30 inakuwa Ibara ya 31.<br>2. Ibara ya 31(4) isomeke: "Bunge litatunga sheria kwa ajili ya kulinda: |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Baraza | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | kutochafuliwa sifa na haiba zao inalindwa. | Haki na uhuru wa vyombo vya habari, habari na taarifa kwa madhumuni ya usalama wa Taifa, Amani , maadili ya umma, haki, staha na uhuru wa watu wengine”. |
| | | (ii) Katika aya ya (b)(ii) ya ibara ndogo ya (2) yaongezwe maneno “kwa kuzingatia maadili ya Kitanzania” baada ya neno “kuzisambaza”. | | |
| | | (iii) Iongezwe ibara mpya ambayo inazungumzia wajibu wa vyombo vya habari ambao ni kutoa taarifa sahihi kwa wananchi wote bila ubaguzi au upendeleo wowote na taarifa kutolewa bila ubaguzi wowote. | | |
| | | (iv) Iongezwe Ibara mpya ambayo inayozungumzia wajibu wa vyombo vya habari kwa kutoa kipaumbele kwa makundi ya watu wenye ulemavu, wanawake, wazee, watoto na habari za kundi lolote linaloonekana kuhitaji msaada wa haraka kutoka kwa jamii. | | |
| | | (v) Inapendekezwa kuwepo na mpangilio mbadala wa ibara kuanzia ibara ya 29 na kupendekeza ibara mpya 3OA,30B na 30C kama ifuatavyo:<br>*Uhuru wa maoni*<br>29. (isomeke kama Rasimu ya sasa ilivyo).<br><br>*Uhuru wa mtu binafsi*<br>30(1). Kila mtu anao uhuru wa kutafuta, kupata na kutumia habari na taarifa na kusambaza | (a) Madhumuni ni kutenganisha haki mahsusi za tasnia ya habari na haki za jumla ambazo zitawahusu hata wasio katika tasnia hiyo kwani hiyo ni haki yao ya msingi.<br>(b) Vile vile hii itarahisisha kutunga na kukuza sheria na kanuni mahsusi kwa | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Baraza | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | taarifa hizo.<br>(2) Serikali na taasisi zake, asasi za kiraia na watu binafsi watakuwa na wajibu wa kutoa habari kwa umma juu ya shughuli na utekelezaji wa shughuli zao.<br><br>*Uhuru wa vyombo vya habari*<br>30A-(1) Vyombo vya habari vitakuwa huru na vilevile vitakuwa na-<br>(a) haki ya kutafuta, kupata, kutumia na kusambaza habari na taarifa wanazopata;<br>(b) wajibu wa-<br>(i) kusambaza habari na taarifa kwa wananchi; na<br>(ii) kuheshimu na kulinda utu, heshima, uhuru, staha ya wananchi dhidi ya habari na taarifa wanazozitumia, wanazozitayarisha na kuzisambaza.<br>(2) Kutakuwa na vyombo huru vya habari vya umma ambavyo-<br>(a) havitaegemea upande wowote,<br>(b) vitakuwa huru kufuata sera zake za uhariri na vitawajibika kutoa kwa usawa maoni ya watu na vikundi tofauti katika jamii,<br>(c) vitapata fedha za kujiendesha kupitia Bunge.<br><br>*Mipaka ya uhuru na haki*<br>30B. Uhuru wa kujieleza, haki | fani ya wanahabari (specialisation) kama ilivyo kwa maeneo ya sheria nyingine mbalimbali. | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Baraza | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | ya kupata habari na uhuru wa vyombo vya habari kama ilivyoainishwa katika Ibara ya 29, 30 na Ibara ya 30A hautahusu matamshi, maandishi au mawasiliano ya aina yoyote yenye kashfa, yanayoshabikia ukatili, chuki, propaganda za kuchochea vita, ubaguzi, kuchochea tofauti za kidini au kikabila.<br><br>*Sheria za vyombo vya habari*<br>30C.-(1) Bila ya kuathiri Katiba hii, Bunge litatunga sheria kwa madhumuni ya kulinda usalama wa taifa, amani, maadili ya umma, haki, staha na uhuru wa watu wengine.<br>(2) Bila ya kujali maudhui ya jumla ya aya ya (a), Bunge litatunga sheria itakayoelekeza uhuru na haki ya vyombo vya habari na uhuru wa kupata habari." | | |
| | | (vi) Ibara ndogo ya (4) iandikwe upya kama ifuatavyo:<br>"(4) uhuru wa habari na vyombo vya habari hautahusu ukusanyaji na usambazaji wa habari:<br>(a) Zinazohamasisha vita au mapigano;<br>(b) Zinazohamasisha chuki, za kikabila, kidini au kisiasa;<br>(c) Ambazo msingi wake ni sababu yeyote ya kibaguzi ilikatazwa na ibara ya 24 ya | Ibara hii kama ilivyo sasa inaruhusu uwepo wa sheria ambazo zimetumika kukiuka haki na uhuru wa habari kama vile sheria ya magazeti ya mwaka 1970. | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Baraza | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | katiba hii". | | |
| | | (vii) Ibara hii itoe tafsiri ya maneno yanayotumika kuzingatia haki na uhuru uliotolewa kama vile usalama wa taifa, maadili ya umma, n.k. | Haki hii imewekewa kifungo cha sheria kuwa itabidi kuzingatia sheria ya nchi itakayotungwa kwa ajili ya kuilinda haki hii kwa madhumuni ya usalama wa Taifa, amani, maaadili ya umma, haki, staha na uhuru. | |
| | | (viii) Ibara ndogo ya (1) ibadilishwe na iandikwe kama ifuatavyo:<br>"(1) Bila kuathiri maslahi ya nchi kila mtu anao uhuru wa kutafuta, kupata na kutumia habari na taarifa na kusambaza taarifa hizo na kuanzisha habari kwa kuzingatia mazingira ya kijiografia na mipaka ya nchi". | | |
| | | (ix) Aya (b) ya ibara ndogo ya (1) ifutwe. | | |
| 31. | Uhuru wa imani ya dini | (i) Ibara hii irekebishwe na ieleze wazi kwamba, Serikali haina dini na izuie Viongozi kutumia majukwaa ya dini kujiimarisha kisiasa. | | 1. Ibara ya 31 itakuwa Ibara ya 32.<br>2. Ibara ndogo ya (5) ifanyiwe marekebisho na isomeke kama ifuatavyo:<br>"Ni marufuku kwa mtu, kikundi au taasisi ya dini kutumia uhuru wa kutangaza dini kwa namna ambayo italeta uvunjifu wa amani, kujenga chuki au kuchochea vurugu na |
| | | (ii) Ibara hii irekebishwe vizuri na itamke bayana kuwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haina dini. Ndani ya katiba itajwe misingi mikuu ya imani ya dini kama vile Ibara ndogo (5).<br>(iii) Neno kashifu katika ibara ndogo ya (5) libadilishwe | (a) Kuepuka migogoro ya kidini nchini.<br>(b) Suala la Serikali kutokuwa na dini ni lazima liwe wazi ndani ya Katiba kwa kutofautisha haki ya kuabudu na kuwapo kwa dola isiyoegemea | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Baraza | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | imani yoyote ya kidini. | ghasia kwa madai ya kutetea imani au dini hiyo.” |
| | | (iv) Ibara ndogo ya (1) irekebishwe na isomeke kama ifuatavyo: “(1) Kila mtu anao uhuru wa mawazo, imani na uchaguzi katika mambo ya imani ya dini na anao uhuru pia wa kubadilisha dini, imani yake au kutokuwa na imani au dini.” | Kuondoa utata katika matumizi ya maneno katika Ibara hii. | |
| | | (v) Katika ibara ndogo ya (1) yaongezwe maneno “haki na uhuru” baada ya neno “anayo”. | Haki ni jambo la mwanzo linalotakiwa kudumishwa na Katiba. | |
| | | (vi) Katika ibara ndogo ya (2) yaongezwe maneno “haki na uhuru” baada ya neno “itakuwa ni”. | Haki ni jambo la mwanzo linalotakiwa kudumishwa na Katiba. | |
| | | (vii) Ibara ndogo ya (3) ifutwe. | Ili kuzipa uhuru nchi Washirika kuweka masharti ya ibada katika nchi zao. | |
| | | (viii) Ibara ndogo ya (3) irekebishwe na iandikwe kama ifuatavyo: “(3) Shughuli ya uendeshaji wa ibada na jumuiya za dini itakuwa nje ya shughuli za mamlaka ya serikali”. | | |
| | | (ix) Ibara ndogo ya (3) irekebishwe kwa kuongeza ufafanuzi au vipengele vitakavyohusu mwenendo wa viongozi na ushiriki wao rasmi katika shughuli za dini kwa namna ambayo itatenganisha nyadhifa za kiserikali katika shughuli hizo na ushiriki wao kama mtu binfsi. | Mwenendo ulivyo hivi sasa ni viongozi kushiriki katika shughuli za kidini kwa nyadhifa zao si rahisi kutenganisha sura ya dini na mtu binafsi. | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Baraza | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | (x) Ibara ndogo ya (5) ifutwe. | (x) Ibara ndogo ya (5) ifutwe. | |
| | | Itasababisha ukandamizwaji wa watu wanaoabudu na wanaoeneza dini zao kwa kutumia njia halali na za kidemokrasia na ambazo zimekuwa halali zaidi ya miaka 1000 iliyopita. | Itasababisha ukandamizwaji wa watu wanaoabudu na wanaoeneza dini zao kwa kutumia njia halali na za kidemokrasia na ambazo zimekuwa halali zaidi ya miaka 1000 iliyopita. | |
| | | (e) Maneno "kwa mujibu wa sheria za nchi" katika ibara ndogo ya (4) yatolewe ufafanuzi. | (xi) Maneno "kwa mujibu wa sheria za nchi" katika ibara ndogo ya (4) yatolewe ufafanuzi. | |
| | | (xii) Ibara ndogo ya (5) irekebishwe na iandikwe kama ifuatavyo: "(5) Ni marufuku kwa mtu, kikundi au taasisi ya dini kutumia uhuru wa kutangaza dini kwa kukashifu imani na dini nyingine kwa kutumia lugha au matendo kujenga chuki au kuchochea vurugu na ghasia kwa madai ya kutetea imani au dini." | | |
| | | (xiii) Ibara ndogo ya (5) irekebishwe na iandikwe kama ifuatavyo: "(5) Ni marufuku kwa mtu, kikundi au taasisi ya dini kutumia uhuru wa kutangaza dini kwa kukufuru imani na dini nyingine kwa kutumia lugha au vitendo kwa taadhira yake vinaweza kujenga chuki au kuchochea vurugu na ghasia kwa kuhatarisha amani ya nchi kwa | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Baraza | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | madai ya kutetea imani au dini". | | |
| | | (xiv) Ibara ndogo ya (6) irekebishwe na iandikwe kama ifuatavyo:<br>"(6) Dini na imani ya dini haitatumika kujipatia nafasi za kisiasa na haitatumika kwa namna yoyote itakayowagawa wananchi, kuleta uhasama au kuharibu amani miongoni mwa wananchi". | | |
| | | (xv)Iongezwe ibara ndogo mpya ya (7) ambayo itakuwa kama ifuatavyo:<br>"(7) Dini, imani au ibada yoyote lazima itokane na misingi ya utu na haki". | Ni muhimu kuweka udhibiti wa watu wanaoweza kuanzisha ibada zinazokwenda kinyume na haki na utu kama mauaji ya watoto, vikongwe, walemavu au kufanya ibada wakiwa uchi. | |
| | | (xvi) Iongezwe ibara ndogo mpya ya (8) ambayo itakuwa kama ifuatavyo:<br>"(8) Serikali haitatumia pesa za umma katika uendeshaji wa huduma binafsi kwa taasisi za kidini, imani, ibada au watu binafsi". | Ni muhimu jukumu la huduma za umma libaki mikononi mwa Serikali, huduma binafsi zijiendeshe zenyewe kuepusha mgongano wa maslahi. | |
| | | (xvii) Ibara ndogo ya (7) ibadilishwe iwe (9) na iwe kama ifuatavyo:<br>"(9) Bila ya kuathiri masharti ya ibara ndogo ya (7), neno dini na ibada kama yalivyotumika katika ibara hii, yatafsiriwa kwa mujibu wa tafsiri ya dini husika". | Tafsiri ya neno dini na ibada yanatofautiana kutoka dini moja hadi nyingine, kwa mfano kwa waislamu neno dini haliwezi kutafsiriwa kama madhehebu. | |
| | | (xviii) Iongezwe ibara ndogo mpya | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Baraza | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | itakayozuia utambulisho wa dini kwenye sare za shule za Serikali. | | |
| | | (xix) Ibara ya 31(5) isomeke "Ni marufuku …….kutangaza dini kwa kutumia maneno ya matusi, kujenga chuki……kutetea imani na dini" | | |
| 32. | Uhuru wa watu kujumuika na kushirikiana na wengine | (i) Ibara hii itenganishwe ili kila haki iliyotajwa ijitegemee. | | Ibara ya 32 inakuwa ya 33 na inabaki kama ilivyo |
| | | (ii) Katika Ibara ndogo ya (1) maneno "bila kuathiri sheria za nchi" yafutwe. | Maneno hayo yanahalalisha uwepo wa sheria zinazofifisha haki ya kukusanyika. | |
| | | (iii) Katika ibara ndogo ya (2) inapendekezwa kuongeza maneno "aliyefikisha umri wa miaka 18" baada ya neno "kila mtu". | | |
| | | (iv) Ziongezwe ibara ndogo mbili ambazo zitakuwa kama ifuatavyo: "(2) Bila ya kuathiri masharti ya ibara ndogo ya (1), itakuwa ni ruhusa kwa watu kuanzisha vyama vya siasa vya kidini. (3) Bila ya kuathiri masharti ya ibara ndogo ya (1), wanadini watakuwa na vyombo huru vinavyounganisha makundi mbalimbali ya wanadini husika na vyombo hivyo vitakuwa na nafasi sawa katika uwakilishi wa masuala mbalimbali ya kitaifa na kimataifa". | Ili kupatikana kwa maslahi ya waislamu baada ya kutopatikana kwa kukosa muelekeo wa maadili ya kidini katika vyama vya siasa viliyopo. Nchi nyingi duniani zinafuata utaratibu huu mfano Ujerumani, Australia, Uingereza, Kanada, Rwanda, Ubelgiji, Afrika ya Kusini nk. Na wala hakuna matatizo yoyote. | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Baraza | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | (v) Inongezwe Ibara ndogo mpya ya (2) ambayo itaeleza kama ifuatavyo: "(2) Kila mtu ana haki, kwa amani na bila kubeba silaha, kusanyika, kuandamana, kuzuia njia (to picket) na kuwasilisha malalamiko kwa mamlaka ya umma". | Haki ya kuandamana kwa amani ndiyo nguzo kuu. | |
| | | (vi) Iongezwe ibara ndogo mpya itakayotaja aina ya sheria zinazozungumziwa vinginevyo sheria zinaweza kutungwa ambazo zitaminya kabisa hiyo haki. | Sheria zinazozungumziwa katika haki hii ni za ujumla si mahsusi. | |
| 33. | Uhuru wa kushiriki shughuli za umma | (i) Ibara ya 180 (1) (2) ziingie ibara hii<br>(ii) ibara ndogo ya (1) iongeze maneno "kwa kuzingatia utaratibu uliowekwa kwa mujibu wa sheria." | Haki za raia | 1. Ibara ya 33 inakuwa ya 34.<br>2. Ibara ndogo ya (1) iongezwe maneno "kwa kuzingatia utaratibu uliowekwa kwa mujibu wa sheria za nchi." mwishoni mwa sentensi. |
| 34. | Haki ya kufanya kazi | (i) Ibara ndogo ya (1) ibadilishwe na iandikwe kama ifuatavyo: "(1) Kila mtu ana haki ya kufanya kazi ya halali ya kuajiriwa au kujiajiri mwenyewe". | | Ibara ya 34 inakuwa ya 35, na inabaki kama ilivyo |
| | | (ii) Ibara ndogo ya (1) iandikwe kama ilivyo ibara ya 22 ya Katiba ya sasa. | | |
| | | (iii) Katika Ibara ndogo ya (2) mwisho yaongezwe maneno "kulingana na sifa zinazohitajika katika nafasi hiyo". | | |
| | | (iv) Iongezwe ibara ndogo mpya ya (4) itakayoandikwa kam ifuatavyo: | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Baraza | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | "(4) Bunge litatunga sheria itakayofafanua haki hizo na kuzilinda". | | |
| | | (v) Iongezwe ibara ndogo mpya itakayozuia mwanandoa kumzuia mwenzi wake kufanya kazi ama kuajiriwa au kujiajiri. | | |
| | | (v) Iongezwe ibara ya 34(3) na isomeke "Kila mtu anayo haki ya kupata ulinzi na usalama kwa kazi yoyote halali anayofanya bila ya kubughudhiwa" | | |
| | | (vi) Iongezwe ibara ya 34(4) na isomeke "Serikali ina wajibu wa kutoa elimu ya ufundi au utaalamu mwengine, kuweka mazingira bora ya kisera na sheria kuwezesha watu kuajiriwa au kujiajiri na kulinda wafanyakazi dhidi ya vitendo vyote visivyokuwa vya haki" | | |
| 35. | Haki za wafanyakazi na waajiri | (i) Aya ya (b) ya ibara ndogo ya (1) irekebishwe kwa kuongeza maneno "kwa wakati" baada ya neno "anayofanya". | | Ibara ya 35 inakuwa ya 36, na inabaki kama ilivyo |
| | | (ii) Iongezwe aya mpya (e) katika ibara ndogo ya (1) itakayoeleza kama ifuatavyo:<br>"(e) kugoma au kusitisha nguvukazi yake mahali pa ajira." | Haki ya kugoma ndio silaha pekee aliyonayo mfanyakazi ya kulinda haki zake nyingine mahali pa ajira; | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Baraza | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | (iii) Ibara ndogo ya (1) irekebishwe kwa kuongeza aya mpya (e) ambayo itasomeka kama ifuatavyo: “(e) Wafanyakazi wanahaki ya kugoma”. | | |
| | | (iv) Iongezwe aya mpya (e) katika ibara ndogo ya (1) ambayo itaeleza kama ifuatavyo: “(e) Kila mwananchi mwenye sifa ya kuajiriwa apewe fursa kwanza na wageni ndio wafuate”. | Makampuni huwapa wageni nafasi kubwa za ajira na wazawa kukosa kuajiriwa kabisa na kubaki kuwa kibarua na mwisho mapato mengi hutoka na kunufaisha nchi zao na sisi kubaki wachakavu. | |
| | | (v) Iongezwe aya mpya katika ibara ndogo ya (1) itakayoeleza kama ifuatavyo: “kujiunga na Mfuko wowote wa Hifadhi ya Jamii”. | Kutoa uhuru kwa mfanyakazi kuchagua mfuko wenye maslahi kwake. | |
| | | (vi) Ibara ndogo ya (1) hadi (3) zifutwe. | Sheria ya kazi tayari imeshaeleza mambo hayo. | |
| | | (vii) iongezwe ibara ndogo mpya itakayoeleza kama ifuatavyo: “kila mtu ana haki ya kufanya kazi katika mazingira bora na salama. | | |
| | | (viii) iongezwe ibara ndogo mpya itakayoeleza kwamba, Wafanyakazi wenye sifa zinazofanana katika kada moja katika Taasisi za Serikali wanahaki ya kulipwa maslahi yanayofanana. | Kuondoa manung’uniko ya watumishi husika ambao wamesoma vyuo vile vile, wanatekeleza majukumu yale yale kwa mwananchi yule yule ndani ya nchi hiyo hiyo, na wanalipwa na Serikali | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Baraza | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | hiyo hiyo. | |
| | | (ix) Iongezwe ibara ndogo mpya itakayoruhusu mfanyakazi kulipwa pensheni kila baada ya miaka 10. | | |
| 36. | Haki ya kumiliki mali | (i) Ibara ndogo ya (1) irekebishwe na iandikwe kama ifuatavyo: "(1) Kila mtu anayo haki ya kumiliki mali ikiwemo ardhi na hifadhi ya mali yake aliyonayo kwa mujibu wa sheria". | | 1. Ibara ya 36 inakuwa ya 37.<br>2. Katika Ibara ndogo ya 37 (2) yametumika maneno ''kuchukuliwa'' badala ya ''kunyang'anywa''. |
| | | (ii) Katika Ibara ndogo ya (2) kuongezwa sharti la manufaa ya umma katika masharti ya mtu kunyang'anywa mali.<br>(iii) Ibara ya 36(1) isomeke "Kila mwanamme na mwanamke anayo haki ……." Katika jamii yetu neno "mtu" humaanisha mwanamme tu hasa katika mazingira ya kumiliki mali.<br>(iv) Iongewe ibara ya 36(4) na isomeke "Kwa madhumuni ya ibara hii, mali inaweza kupatikana kwa njia ya kupewa, kurithi au kununua"<br>(v) Ibara ya 36(2) isomeke "Bila ya kuathiri …..madhumuni ya kutaifisha kwa misingi ya ukatili wa kijinsia au …." | | |
| 37. | Haki ya uraia | (i) Maneno "na pale inapohitajika" yafutwe. | Yanasababisha kuleta maana inayokinzana na Ibara ya 28 ya Rasimu ya Katiba hii. | Ibara ya 37 inakuwa ya 38, na inabaki kama ilivyo |
| | | (ii) Ziongezwe ibara ndogo zifuatazo: | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Baraza | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | “(1) Raia yeyote wa kuzaliwa wa Tanzania hatapoteza uraia wake kwa kupata uraia wa nchi nyingine, na asinyang’anywe uraia wake kwa sababu yoyote ile.<br>(2) Mtu yeyote ambaye angalau mmoja kati ya Wazazi wake ni raia wa kuzaliwa wa Tanzania ana haki ya kupata uraia wa Tanzania bila vikwazo vyovyote vile, na hatalazimika kuukana uraia wa nchi nyingine kama anao.<br>(3) Mtu anayetaka kupata uraia wa Tanzania, ili awe na uraia wa zaidi ya nchi moja, na ambaye Mume au Mke wake wa ndoa ni Mtanzania atahitajika kutimiza masharti yafuatao:<br>(a) Ndoa yao iwe imesajiliwa rasmi katika Mamlaka za Tanzania na kudumu kwa kipindi kisichopungua miaka 10 toka siku ya usajili;<br>(b) Awe na uthibitisho wa kujifunza na kuimudu lugha ya Kiswahili, uliohakikiwa na Taasisi teule za Tanzania;<br>(c) Awe anaziheshimu na kuzithamini tamaduni za Tanzania;<br>(d) Awe anayaheshimu na kuyathamini maadili ya Kitanzania.<br>(4) Mtu mwingine yeyote anayeomba uraia wa kujiandisha | | |

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Baraza* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| | | wa Tanzania, ambaye mmoja kati ya Wazazi wake siyo Mtanzania sharti:<br>(a) awe na uthibitisho wa kujifunza na kuimudu lugha ya Kiswahili uliohakikiwa na Taasisi teule za Tazania;<br>(b) awe anaziheshimu na kuzithamini tamaduni za Tanzania;<br>(c) awe anayaheshimu na kuyathamini maadili ya Kitanzania". | | |
| 38. | Haki ya mtuhumiwa na mfungwa | (i) Ibara hii ifutwe. | (a) Haki ya watuhumiwa na wafungwa ziendelee kuwa kwenye sheria.<br>(b) Makosa mengine kama ya uhalifu wa kimataifa yanasimamiwa na sheria na mikataba ya kimataifa. | Ibara ya 38 inakuwa ya 39. Katika Ibara ndogo ya 1(a) yameongezwa maneno "au lugha ya alama" |
| | | (ii) Aya (a) ya Ibara ndogo ya (1) irekebishwe na isomeke kama ifuatavyo:-<br>(a) Kuelezwa kwa lugha anayoifahamu, haki ya kutoa au kutokutoa maelezo yoyote; na matokeo ya kutoa au kutokutoa maelezo. | Kuunganisha haki ya mtuhumiwa ya kutoa au kutotoa maelezo na Matokeo ya kutoa au kutokutoa maelezo. | |
| | | (iii) Aya (b) ya Ibara ndogo ya (1) irekebishwe na isomeke kama ifuatavyo:-<br>"(b) kutoa au kutokutoa maelezo". | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Baraza | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | (iv) katika Ibara ndogo ya (1) na (2) maneno "Mtuhumiwa na mwenendo wa mashtaka" yafutwe na badala yake yaandikwe maneno "Washitakiwa au Wafungwa na mwenendo wa shauri". | | |
| | | (v) aya (d) ya Ibara ndogo ya (1) iandikwe kama ifuatavyo: "(d) Kutoteswa kwa madhumuni ya kulazimishwa kutoa maelezo ya kukiri kosa ambayo yatatumika kama ushahidi dhidi yake." | Wafungwa na watuhumiwa wamekuwa wakiteswa ili wakiri kutenda makosa wanayotuhumiwa nayo hivyo ni vema neno kutoteswa likaongezwa katika ibara hii. | |
| | | (vi) Katika aya (e) ya Ibara ndogo ya (1) irekebishwe kwa kuwekwa ukomo wa muda wa kuwekwa kizuizini. | Neno mapema iwezekana halina ukomo wa muda hivyo linaweza likatumiwa vibaya kuwaweka watuhumiwa ndani kwa muda mrefu. | |
| | | (vii) Aya (c) katika Ibara ndogo ya (2) ifutwe na badala yake iandikwe kama ifuatavyo; "(c) Mtuhumiwa au mfungwa kufikishwa mahakamani kwa wakati ili kuthibitisha uwepo wake". | Ili kuhakikisha muda utakaotamkwa na sheria itakayotungwa na Bunge unazingatiwa. | |
| | | (viii) Iongezwe aya mpya (d) katika ibara ndogo ya (2) itakayoruhusu mtuhumiwa au mfungwa kupiga kura.<br>(ix) Lugha ya ishara ijumuishwe | Kupiga kura ni moja ya haki za msingi za raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.<br>Kwa ajili ya wafungwa wenye mahitaji maalum. | |
| | | (x) Ziongezwe ibara ndogo ya (3) na | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Baraza | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | (4) zitakazoeleza kama ifuatavyo:<br>"(3) Bunge litatunga sheria itakayoweka utaratibu wa kupata uwakilishi wa kisheria kwa makosa ya jinai.<br>(4) Ieleze utaratibu kuhusu kuhesabiwa kwa muda ambao mshtakiwa amekaa kizuizini au rumande wakati wa kutoa adhabu". | | |
| 39. | Haki ya watu walio chini ya ulinzi | (i) Katika ibara ndogo ya (3) maneno kwa "ridhaa yake" yafutwe na badala yake kuwekwa maneno kwa "ridhaa ya Serikali". | Kulinda raia dhidi ya udikteta wa watawala. | 1. Ibara ya 39 inakuwa ya 40.<br>2. Katika Ibara ndogo ya 3 yameongezwa maneno "isipokuwa kwa mujibu wa sheria na mikataba ya kimataifa na wajibu wa nchi katika uhusiano wa kimataifa." katika ibara ndogo ya tatu. |
| | | (ii) Katika ibara ndogo ya (3) irekebishwe kwa kufuta maneno "kinyume cha ridhaa yake" na badala yake kuweka maneno "isipokuwa kwa mujibu wa sheria za nchi na mikataba ya kikanda na kimataifa na wajibu wa nchi katika uhusiano wa kimataifa." | | |
| | | (iii) Ibara ndogo ya (3) iandikwe upya kama ifuatavyo:<br>"(3) Raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hatapelekwa katika nchi za nje kufungwa au kuwekwa kuzuizini kujibu mashitaka au kufanyiwa mahojiano ya aina yoyote bila kufuata taratibu za kisheria za nchi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania". | | |
| | | (iv) Iongezwe ibara ndogo mpya ya (4) itakayokuwa kama ifuatavyo: | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Baraza | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | "(4) Raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hatahojiwa na Maafisa Usalama wa Nchi za nje katika eneo la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania bila kufuata taratibu za sheria za nchi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania au kwa ridhaa yake". | | |
| | | (v) Ibara hii irekebishwe kwa kuongeza ibara ndogo mpya ya (4) ambayo iandikwe kama ifuatavyo:<br>"(4) Ni marufuku raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania:<br>(a) Kufungwa au kuwekwa kizuizini nje ya nchi bila ya kufuata taratibu na sheria ya nchi hiyo;<br>(b) Kuhojiwa na maafisa ujasusi au usalama wa nchi za nje bila kuhusisha vyombo vya usalama katika eneo la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania." | | |
| | | (vi) Ibara ndogo ya (3) maneno "aina yoyote kinyume cha ridhaa yake" yafutwe na badala yake yaingizwe maneno "kwa ridhaa au mamlaka ya nchi yake" na maneno "Bila kuathiri katiba hii" yawekwe kabla ya neno "Raia". | Ili isimpe ridhaa mtuhumiwa badala yake ridhaa itoke kwa nchi. | |
| | | (vii) Ibara ndogo ya (3) iandikwe upya kama ifuatavyo:<br>"(3) Raia wa Jamhuri ya Muungano hatapelekwa katika | Ili kisije kikasababisha kuvunjwa kwa sheria za kimataifa. | |

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Baraza* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| | | nchi yeyote ya nje kujibu mashtaka au kufanyiwa mahojiano ya aina yoyote isipokuwa kwa mujibu wa sheria". | | |
| | | (viii) Ziongezwe ibara ndogo mpya ya (4) na (5) ambazo zitakuwa kama ifuatavyo: "(4) Ni marufuku raia wa Tanzania kufungwa au kuwekwa kizuizini nchi ya nje bila ya kufuata sheria ya Tanzania. (5) Ni marufuku raia wa Tanzania kuhojiwa na maafisa wa ujasusi au usalama wa nchi za nje katika eneo la Tanzania." | Ili kulinda usalama wa raia wakiwa ndani na nje ya nchi. | |
| | | (ix) Ziongezwe ibara ndogo mpya ya (4) na (5) zitakazoeleza kama ifuatavyo: "(4) Bila kuathiri masharti ya ibara ndogo ya (3), raia yeyote wa Jamhuri ya Muungano anaweza kupelekwa nchi yoyote ya nje kujibu mashtaka ya jinai au kufanyiwa mahojiano, endapo nchi hiyo ina mkataba wa kubadilishana wafungwa au wahalifu na Jamhuri ya Muungano; (5) Bila kuathiri masharti ya ibara ndogo ya (3), raia yeyote wa Jamhuri ya Muungano anaweza kupelekwa nchi yoyote ya nje kujibu mashtaka au kufanyiwa mahojiano kwa mujibu wa mkataba wowote wa kimataifa | Mapendekezo haya mapya yanawezesha Jamhuri ya Muungano kutekeleza matakwa ya mikataba ya kubadilishana wafungwa na wahalifu na nchi nyingine ambayo Jamhuri ya Muungano ni mwanachama, na vile vile kutekeleza masharti ya Mkataba wa Roma wa 1999 uliounda Mahakama ya Uhalifu wa Kimataifa (the International Criminal Court – ICC). | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Baraza | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | ambao Jamhuri ya Muungano ni mwanachama." | | |
| 40. | Uhuru na haki ya mazingira safi na salama | (i) Katika Ibara ndogo ya (1) na (2) maneno "mazingira salama ya kiafya" yafutwe na badala yake yasomeke "mazingira safi na bora". | | Ibara ya 40 inakuwa ya 41, na inabaki kama ilivyo. |
| | | (ii) Ibara ndogo ya (3) irekebishwe na iandikwe upya kama ifuatavyo:<br>"(3) Serikali na mtu yeyote anayeishi Tanzania anao wajibu wa kutunza na kuendeleza mazingira na kutoa taarifa kwa mamlaka za nchi kuhusu shughuli au jambo lolote ambalo ni hatarishi au linauwezekano mkubwa wa kuharibu au kuathiri mazingira". | Kuweka wajibu wa kulinda mazingira kwa Serikali. | |
| | | (iii) Iongezwe ibara ndogo ya (4) kama ifuatavyo:<br>"(4) Kila mtu anayechafua au kuharibu mazingira atawajibishwa kwa mujibu wa sheria". | | |
| | | (iv) Ibara ya 40(1) isomeke "Kila mtu ……… na ya kiafya, siha ya tiba asili." | | |
| | | (v) Ibara ya 40(3) isomeke "Mtu yeyote anayeishi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anao wajibu …..kuharibu au kuathiri miti dawa asili na mazingira" | | |
| 41. | Haki ya elimu na kujifunza | (i) Katika aya (a) ya ibara ndogo ya (1) yaongezwe maneno "kwa ujuzi" | | 1. Ibara ya 41 inakuwa ya 42. |

| ***Ibara Na.*** | ***Kichwa cha Habari*** | ***Maoni ya Mabaraza*** | ***Sababu ya Baraza*** | ***Marekebisho ya Tume*** |
|---|---|---|---|---|
| | | mwisho wa sentensi. | | 2. Katika Ibara ndogo ya (1) imefanyiwa marekebisho yafuatayo:<br>(a) maneno ‘’kupata elimu” yasomeke “kupata elimu bora”.<br>(b) isomeke ‘’elimu bora ya msingi bila malipo.<br>(c) ‘’neno kupata elimu kwa gharama nafuu” ‘’lisomeke kupata elimu bora kwa gharama nafuu” |
| | | (ii) Ibara hii iandikwe kama ilivyo ibara ya 11 ya Katiba ya sasa. | | |
| | | (iii) Iongezwe ibara ndogo mpya itakayoeleza kuhusu Serikali kuchukua hatua za ziada kuhakikisha kuwa mtoto wa kike anapata fursa ya elimu bila vikwazo. | | |
| | | (iv) Aya (b) ya ibara ndogo ya (1) iandikwe upya kama ifuatavyo:<br>“(b) Kupata elimu bora ya msingi inayomtayarisha kikamilifu wanafunzi ama kuendelea na elimu ya ngazi inayofuatia au kuweka msingi wa kuanza kujitegemea”. | Sababu elimu ni gharama ambayo inabebwa na wananchi moja kwa moja au kupitia kodi. | |
| | | (v) Katika aya (b) ya ibara ndogo ya (1) maneno “bila ya malipo” yafutwe. | | |
| | | (vi) ibara hii irekebishwe na iandikwe kama ifuatavyo:<br>(1) Kila mtu ana haki ya:<br>(a) kupata fursa ya kupata elimu bila ya vikwazo wala ubaguzi;<br>(b) kupata elimu bora ya msingi bila ya malipo na pia elimu hadi kidato cha nne bila ya malipo ikiwa mzazi hana uwezo wa kulipa, inayomtayarisha kikamilifu mwanafunzi ama kuendelea na elimu ya ngazi inayofuata au kuweka msingi wa kuanza kujitegemea; | | |

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Baraza* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| | | (2) ……. <br>(3) Serikali itawajibika kuweka mazingira yatakayowezesha wasiojua kusoma na kuandika au walioshindwa kumaliza elimu ya msingi kupata elimu itakayowawezesha kujua kusoma na kuandika na kupata stadi za kazi ili waweze kumudu maisha yao". | | |
| | | (vii) iongezwe aya mpya ya (e) katika ibara ndogo ya (1) itakayokuwa kama ifuatavyo: <br>"(e) Kila mwanafunzi wa elimu ya juu atakuwa na haki ya kupata mkopo wa kugharamia masomo yake". | Upatikanaji wa mikopo utatoa fursa sawa kwa kila mtu kupata elimu ya juu kama inavyoelezwa kwenye ibara ya 41 (1) (a) na (d). | |
| | | (c) Ziongezwe aya mpya (f) na (g) katika ibara ndogo ya (1) kama ifuatavyo: <br>"(f) kuheshimiwa uchaguzi wake wa fursa za elimu anazoomba; <br>(g) Kutolazimishwa kuchukua mikopo ya elimu ambayo ni kinyume na imani ya dini yake au asiyohitaji". | Ili kuzuia wanafunzi wasichaguliwe katika fani walizokuwa hawakuomba na kuzuia wanafunzi kuchukua mikopo ya elimu hata kama wanao uwezo wa kujilipia. | |
| | | (d) Katiba iwaamuru washirika wa Muungano kuhakikisha kuwa wanatoa elimu bora katika ngazi zote kwa kufuata viwango stahiki vinavyokubalika kitaifa na kimataifa. | | |
| | | (e) Katiba ieleze elimu ya msingi kuwa ni hadi darara la 12 (kidato | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Baraza | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | cha nne). | | |
| | | (f) Elimu ya msingi iende sambamba na elimu ya ufundi stadi ili wahitimu wawe wamefikia taaluma ya ufundi stadi kamili [Full Technicians' Certificate] | | |
| | | (g) Nchi washirika katika mifumo yao ya elimu kuwa na Tume ya kudumu ya kudhibiti ubora na viwango vya Elimu tangu chekechea hadi kidato cha sita na pia tume za usajili na udhibiti wa ubora wa elimu za vyuo vya elimu ya juu na ufundi. | | |
| | | (h) Iongezwe ibara ya 41(3) na isomeke "Serikali itawajibika kuweka mazingira yatakayowezesha wasiojua kusoma na kuandika au walioshindwa kumaliza elimu ya msingi kupata elimu itakayowawezesha kujua kusoma na kuandika na kupata stadi za kazi ili waweze kumudu maisha yao" | | |
| | | (i) Iongezwe ibara ya 41(4) na isomeke "Mamlaka ya nchi itaweka utaratibu wenye lengo la kurekebisha matatizo mahsusi katika elimu kwa kuzingatia usawa wa kijinsia na mazingira ya kusoma" | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Baraza | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | (j) Kuwe na fursa sawa za kupata mikopo ya elimu ya juu hadi ngazi ya Shahada ya uzamili na uzamivu. | | |
| 42. | Haki ya mtoto | (i) Ibara ya 42 hadi 47 zifutwe, kwani maudhui ya Ibara hizo yamezingatiwa katika Ibara za 22 hadi 41. | Kutaja makundi maalum kwenye Katiba baadae linaweza kuja kuleta migogoro kwani inaonyesha makundi maalumu yamekuwa yakiongezeka kulingana na makundi. | 1. Ibara ya 42 itakuwa Ibara ya 43.<br>2. Katika Ibara ya 43(1)(c) yaongezwe maneno "bora" mbele ya neno elimu.<br>3. Katika Ibara ya 43(1)(e) yaongezwe maneno "na mazingira yanayomjenga kimaadili"<br>4. Iongezwe Ibara ndogo mpya ya 3 itakayosomeka. "Itakuwa ni wajibu wa kila mzazi, mlezi, jamii na mamlaka za nchi kuhakikisha kuwa watoto wanalelewa katika maadili stahiki kwa umri wao" |
| | | (ii) Kuongeza aya mpya katika ibara ndogo ya (1) itakayokuwa kama ifuatavyo:<br>"Kila mtoto anahaki ya kuishi". | Ili kuwalinda watoto. | |
| | | (iii) Ibara ndogo ya (1) iandikwe upya kama ifuatavyo:<br>"(1) Kila mtoto ana haki ya kuishi na kuishi huko ni tangu mimba inapotungwa na utoaji wa mimba lazima uzingatie ushauri wa kitabibu ili kulinda uhai na usalama wa mama na mtoto na mtoto akizaliwa ana haki ya:<br>(a) Kupewa jina na uraia<br>(b) Kutoa mawazo, kusikilizwa na kulindwa dhidi ya uonevu, ukatili na udhalilishaji<br>(c) Kucheza na kupata elimu;<br>(d) Kuhifadhiwa katika mazingira mazuri, kwa walio katika ukinzani na sheria;<br>(e) Kupata lishe bora, makazi na huduma ya afya; na | Kupunguza vitendo vya utoaji mimba. | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Baraza | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | (f) Kushiriki katika shughuli zinazolingana na umri alionao; na<br>(g) Kupata malezi na ulinzi wa wazazi, walezi au mamlaka ya nchi.<br>(h) Bila ya ubaguzi wa rangi, utaifa, lugha, mtazamo wa kisiasa, jamii anayotokea, mali, uzazi, kabila, dini, jinsi au aina nyingine za hadhi. | | |
| | | (iv) Aya ya (g) ya Ibara ndogo ya (1) irekebishwe na isomeke ifuatavyo:<br>"(g) kukua, kuendelezwa, kupendwa, kupata malezi na ulinzi wa wazazi, walezi au mamlaka ya nchi". | Lengo ni kuwalinda watoto na kuhakikisha wazazi au walezi wanatekeleza wajibu wao wa Kikatiba wa kumfanya mtoto akue, aendelezwe, apendwe ili asikimbilie mtaani nk. | |
| | | (v) Iongezwe ibara ndogo mpya itakayoeleza kama ifuatavyo:<br>"Kila Mshirika wa Muungano katika kutekeleza majukumu yake ya kiutawala, kisheria, na kisiasa na kiutamaduni ni lazima kuhakikisha kuwa maslahi ya watoto, utu wao na maendeleo ya ukuaji wao yanapewa kipaumbele siku zote". | | |
| | | (vi) Iongezwe ibara ya 42(3) na isomeke "Serikali, wazazi na walezi wanawajibika kuhakikisha kuwa watoto wanalelewa katika maadili stahili kwa umri wake" | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Baraza | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| | | (vii) Iongezwe ibara ya 42(4) na isomeke "Mtoto hataruhusiwa kwenye mikataba inayobeba majukumu mazito chini ya umri wa miaka kumi na nane" | | |
| 43. | Haki na wajibu wa vijana | (i) Ibara hii itoe tafsiri ya neno "kijana". | Rasimu haijamtafsiri kijana kuwa ni nani hivyo tafsiri iwe kama ilivyo katika Sera ya Taifa ya Vijana. | Ibara ya 43 inakuwa ya 44, na inabaki kama ilivyo. |
| | | (ii) Ibara hii irekebishwe kwa kufafanua umuhimu wa ulinzi wa Kijana kama ilivyo kwa Mtoto. | | |
| | | (iii) Ibara hii isomeke "Kila kijana ….mazingira mazuri, salama, ya kuwa raia ……." | | |
| 44. | Haki za watu wenye ulemavu | (i) Aya (e) ya ibara ndogo ya (1) irekebishwe ili kutoa nafasi kwa Mlemavu kupata nafasi ya uongozi, kazi kulingana na ulemavu alionao.<br>(ii) Neno kujifunza liongezwe baada ya neon kusoma katika (1) (e) | Rasimu haijaweka haki ya ulinzi kwa watu wenye ulemavu ulinzi ni dhidi ya kuuwawa, kutendewa maovu kama ubakaji n.k | Ibara ya 44 inakuwa ya 45, na inabaki kama ilivyo. |
| | | (iii) Katika aya ya (f) kuongeza maneno "ili mradi anazo sifa stahiki" baada ya neno "usawa" na hivyo aya hiyo iandikwe kama ifuatavyo: | | |
| | | (iv) "(f) haki ya kupata ajira na kugombea nafasi za uongozi katika nyadhifa mbalimbali kwa usawa ili mradi anazo sifa stahiki". | | |
| | | (v) Ibara ndogo ya (2) ibadilishwe na | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Baraza | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | iandikwe kama ifuatavyo:<br>"(2) Mamlaka ya nchi itaweka utaratibu utakaowawezesha watu wanaoishi na ulemavu kunufaika na haki zote ambazo zimetajwa na Katiba hii pamoja na haki nyinginezo". | | |
| | | (vi) iongezeke Ibara ndogo mpya ya (3) inayohusu haki za mlemavu ikiwemo:-<br>(a) haki ya kuishi;<br>(b) kuwa salama;<br>(c) kuishi kwa amani;<br>(d) kulindwa. | Katiba kutambua na kulinda haki za walemavu. | |
| 45. | Haki za makundi madogo katika jamii | (i) inapendekezwa itolewe tafsiri ya neno "makundi madogo katika jamii" ambayo isomeke kama ifuatavyo:<br>"makundi madogo" ni jamii za watu wanaoishi pembezoni wakitegemea ardhi pekee na mazingira yanayowazunguka kwa ajili ya kupata mahitaji muhimu". Tafsiri hii iwekwe pia katika ibara ya 238 ya ufafanuzi. | Kueleweka kwa maana ya maneno makundi madogo ni muhimu ili kupata uelewa wa pamoja na makundi haya yanatakiwa yasiende kinyume na maadili, mila, desturi na tamaduni za Watanzania kama ushoga. | 1. Ibara ya 45(1)(e) imefanyiwa marekebisho kwa kuongeza neno "kujifunza mbele ya neno kusoma".<br>2. Ibara ya 45 inakuwa ya 46 na imeongezwa Ibara ndogo ya 3 ambayo "itaelezea maana ya makundi madogo". |
| | | (ii) Katika ibara ndogo ya (1) neno "madogo" lifutwe na badala yake liandikwe neno "mbalimbali."<br>(iii) Maana ya makundi madogo ielezwe | Kuondoa utata wa kujua hayo madogo, je makubwa ni yapi? | |
| | | (iv) Ibara hii irekebishwe ili kuainisha makundi madogo yaliyokusudiwa. | Kuepuka makundi mengine madogo kujiingiza, mathalan, mashoga. | |
| | | (v) Ibara ya 45(1)(c) isomeke | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Baraza | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | "kutengewa maeneo …riziki ya chakula na dawa asili" | | |
| | | (vi) Ibara ya 45(2) isomeke "Serikali na mamlaka … na afya, siha tiba asili kwa ajili ya ……" | | |
| 46. | Haki za wanawake | (i) aya (a) ya ibara ndogo ya (1) irekebishwe na iandikwe kama ifuatavyo: "(a) kuheshimiwa utu wake na kuheshimu utu wa jinsia nyingine". | Pamoja na kutambua mfumo dume uliopo katika jamii yetu, tunaomba itambulike kwamba kumeanza kujitokeza viashiria vya wanawake kuwanyanyasa wanaume na kuwafanyia vitendo vya kikatili, hivyo kutambuliwa kwa utu wa mwanamke tu, hakutoshi bali utu na haki za jinsia zote ndio msingi. | 1. Ibara ya 46 inakuwa ya 47.<br>2. Ibara ndogo ya 47(1)(d) imefanyiwa marekebisho na itasomeka "Kupata fursa na ujira sawa na mwanamme katika kazi zenye sifa zinazofanana.<br>3. Ibara ya 47(1) (g) irekebishwe na isomeke "kupata huduma bora ya afya." |
| | | (ii) Aya (b) ya Ibara ndogo ya (1) irekebishwe na isomeke kama ifuatavyo: "(b) Kukingwa na unyonyaji, unyanyasaji, ukatili wa kijinsia na ubaguzi kwa misingi ya udini, uraia au hali ya ndoa." | Kuimarisha na kuweka misingi imara ya kikatiba yenye kulinda utu na haki za wanawake. | |
| | | | Kufafanua kwamba dhana ya ujira sawa kati ya mwanamke na mwanamume inahusu watu wenye sifa sawa na kazi inayolingana. | |
| | | (iii) aya (d) ya ibara ndogo ya (1) irekebishwe na iandikwe kama ifuatavyo: | (a) Kutoa ufafanuzi kwamba dhana ya ujira sawa kati ya | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Baraza | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | "(d) kupata ujira sawa kwa kazi inayofanana". | mwanamke na mawanamme inahusu watu wenye sifa sawa na kazi inayolingana.<br><br>(b) Mwanamke na mwanaume wenye kiwango sawa cha elimu na ujuzi wana haki ya kupata ujira sawa. | |
| | | (iv) ziongezwe aya mpya ya (h) na (i) katika Ibara ndogo ya (1) na ziandikwe kama ifuatavyo:<br>"(h) Umiliki wa mali uwe sawa na mwanaume na hata kuwa na haki ya kuongea na kusikilizwa;<br>(i) Mwanamke anahaki ya kusimamia na kumpangia mtoto wake bila kumngojea baba". | (a) Wanawake wengi wamekosa haki ya kumiliki nyumba, ardhi, mali.<br>(b) Wanawake wanaonekana hawana haki ya kupanga mipango juu ya mtoto wake hasa wa kike kama juu ya kumuozesha, kusoma na hata kumtuma kwa huduma zaidi juu yake na familia. | |
| | | (v) Iongezwe ibara mpya itakayoeleza haki ya kupata elimu sawa kati ya mtoto wa kike na wa kiume. | Pamoja na kuwa kuna haki ya elimu katika rasimu haki ya elimu ya Wanawake iwekwe bayana kwa vile kuna hali ya kuminya hii haki. | |
| | | (vi) Iongezwe ibara ndogo mpya ambayo itatamka wazi kuwa mwanamke mjamzito anayohaki ya kupata lishe bora na huduma | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Baraza | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | za afya (bure kwa asiyejiweza, wakiwemo wajane) wakati wote wa ujauzito, wakati wa kujifungua na mara baada ya kujifungua. | | |
| | | (vii) Iongezwe ibara ndogo mpya itakayoeleza juu ya ulinzi wa Wanawake dhidi ya mila na desturi potofu kwa kuoanisha na malengo makuu yaliyoelezwa katika ibara ya 11(3)(b)(i) inayotambua kanuni za tangazo la dunia kuhusu haki za binadamu na mikataba mingine ya kimataifa iliyoridhiwa na Tanzania na ibara ya 8(3). | Rasimu katika sehemu hii haikuweka bayana ulinzi wa Wanawake dhidi ya mila na desturi zinazovunja haki hizo. | |
| | | (viii) Ibara hii ibadilishwe na badala yake kisomeke “Haki za Kijinsia” badala ya “Haki za Wanawake”. | Haki za kijinsia zinajumuisha haki za wanawake na wanaume badala ya kuzungumzia wanawake peke yao. | |
| | | (ix) Ibara hii ibadilishwe na isomeke Haki za mtu binafsi. Ili haki hii iwahusu kwa pamoja wanaume na wanawake. | Tunapoelekea tutaweka tatizo la mfumo jike kwani kuna wanaume ambao hawatendewi haki, haki ya mtu binafsi ili kila mmoja alindwe dhidi ya maonevu ya aina yeyote na kupewa heshima. | |
| | | (x) Ibara ya 46(g) isomeke "kupata huduma ya afya, siha tiba asili inayopatikana” | | |
| | | (xi) Iongezwe ibara mpya ya 46(1)(g) na isomeke "kulindwa dhidi ya ubaguzi kwa misingi ya ujauzito au majukumu ya kifamilia wakati | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Baraza | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | wa kuomba kazi" | | |
| | | (xii) Ibara ya 46(1) (g) ya rasimu hii iwe ibara ya 46(1)(h) na isomeke "kupata huduma ya juu ya afya inayopatikana ikiwa ni pamoja na haki ya afya kulingana na mahitaji yake, haki ya uzazi salama, haki ya kupata taarifa muhimu kwa ajili ya kulinda afya yake na afya ya mtoto wake anapotelekeza majukumu yake, haki ya afya wakati wa dharura na miundombinu inayoendana na mahitaji ya kijinsi na jinsia zote." | | |
| | | (xiii) Iongezwe ibara ya 46(1)(i) na isomeke "kuwa na haki sawa na mumewe katika mali inayohamishika na isiyohamishika iliyochumwa wakati wa ndoa au wakati wa dhana ya ndoa" | | |
| | | (xiv) iv. Ibara ya 46(2) ihaririwe na isomeke "Mamlaka husika ….kisheria na kitaasisi utakaosimamia …..wakiwemo wajane utakaowajibika kwa Bunge" | | |
| 47. | Haki za wazee | (i) Maneno ya pembeni yarekebishwe na yasomeke "Haki za Wazee na Wastaafu"; | | 1. Ibara ya 47 inakuwa ya 48.<br>2. Ibara ndogo ya 48(d) imefanyiwa marekebisho na isomeke '' kupata mahitaji ya msingi kutoka kwenye |
| | | (ii) Maelezo ya mwanzo yafutwe na badala yake yasomeke "Mamlaka ya nchi itaweka utaratibu wa kisheria utakaowawezesha wastaafu na wazee kupata haki | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Baraza | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | ya:” | | familia zao, jamii na mamlaka ya nchi.<br>3. Ibara ndogo ya 47 (e), imefutwa. |
| | | (iii) Aya (d) irekebishwe na isomeke kama ifuatavyo<br>“(d) Kulelewa na kupata huduma na misaada kutoka katika familia zao, jamii na mamlaka ya nchi.” | Katika mambo yaliyotajwa katika ibara hii haijataja haki ya kuishi, hii ni kutokana na hali iliyopo sasa kwa baadhi ya makabila kuwauwa na kutowapa haki yao ya kuishi wazee, vikongwe na walemavu. | |
| | | (iv) Aya (e) iandikwe kama ifuatavyo:<br>“(e) kuendelea kutumia utaalamu na ujuzi wao kwa manufaa ya jamii”; | | |
| | | (v) Aya (f) ibadilishwe na isomeke kama ifuatavyo:<br>“(f) Wazee wajane wana haki ya kumiliki mali ambazo wamechuma na marehemu mume wake ili imwezeshe kwenye uzee wake bila kujali amezaa naye ama laa”. | Wajane na wazee hunyanyasika kwa kiasi ambacho huwapelekea kuonekana ndio chanzo aidha kufa kwa mwenzie na mali huchukuliwa na ndugu wa mume na pia kunyimwa haki hiyo. | |
| | | (vi) Ziongezwe aya nyingine mpya kama ifuatavyo:<br>**(f)** “Wastaafu wawe na nafasi ya uwakilishi katika Bunge la Jamhuri ya Muungano;<br>**(g)** iwe ni haki yao Kikatiba kupata huduma za matibabu bure katika Hospitali na Zahanati za Serikali;<br>**(h)** Wazee kupata haki ya kulipwa pensheni zitakazokidhi mahitaji yao ya msingi na lazima; | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Baraza | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | **(i)** Wastaafu kulipwa pensheni zao kwa kiwango cha asilimia themanini ya mishahara ya Watumishi wa ngazi zao waliopo kazini;<br>**(j)** Wazee wana haki ya kupata hifadhi za jamii kwa mujibu wa sheria". | | |
| | | (vii) Katika aya (d) neno "misaada" lifutwe na badala yake liwe "huduma"; | | |
| | | (viii) Iongezwe ibara ndogo mpya itakayoeleza kama ifuatavyo:<br>"Mamlaka ya nchi itaweka utaratibu unaofaa kwa ajili ya kufanikisha utekelezaji wa haki za watu wanaoishi na ulemavu, maradhi yasiyotibika, wazee na katika hali nyinginezo za mtu kuwa hajiwezi kupata hifadhi ya maisha yao kutoka katika Serikali kwa mujibu wa sheria". | | |
| | | (ix) Ziongezwe aya mpya zitakazozungumzia njia ambazo wazee watalindwa dhidi ya kuuwawa, kunyanyaswa.<br>(x) Pia kiongezeke kifungu kinachohusu haki ya kupata huduma ya afya na matibabu na kupata pensheni ya uzeeni kutoka serikalini kwa wazee wote. | | |
| | | (xi) Iongezwe aya itakayoeleza tafsiri ya neno mzee ambayo iandikwe kama ifuatavyo:<br>"Mzee" maana yake ni mtu yeyote | Umri wa miaka 60 ndiyo umri wa kustaafu utumishi wa umma. | |

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Baraza* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| | | aliyezidi miaka 60". | | |

## 4.1 SEHEMU YA PILI: WAJIBU WA RAIA NA MAMLAKA ZA NCHI

### (a) Wajibu wa Raia kwa Taifa

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Baraza* | *Sababu ya Baraza* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| 48. | Wajibu wa kushiriki kazi | (i) Ibara ya 48 hadi 50 zifutwe na badala yake kuboresha Ibara ya 34 na 35. | | Ibara ya 48 inakuwa ya 49 na inabaki kama ilivyo. |
| | | (ii) Ibara irekebishwe ili kutoa mwongozo wa mamlaka za nchi kutengeza mifumo ya kielimu au vinginevyo itakayowawezesha watu wa nchi hii kuweza kupata kazi za kujiajiri au za ajira. | Rasimu haijaelekeza mamalaka za nchi kuweka mazingira yatakayowezesha kila mtu aweze kushiriki katika kazi, ikiwa ni pamoja na elimu itakayowajengea watu uwezo wa kujiajiri au kuwa na uwezo wa kufanya kazi zilizopo. | |
| | | (iii) Iongezwe Ibara ndogo itakayoeleza wajibu wa raia uongezwe kama ifuatavyo:<br>(a) Kuilinda na kuitetea katiba;<br>(b) Kulinda na kuheshimu Tunu za Taifa na vitu muhimu vya utambulisho na urithi wa taifa;<br>(c) Kuheshimu haki na uhuru na maslahi ya wengine;<br>(d) Kufanya kazi;<br>(e) Kulinda na kutunza mali za umma, kupambana na matumizi mabaya ya mali na fedha za umma na ufisadi pamoja na aina zote za rushwa; | | |

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Baraza* | *Sababu ya Baraza* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| | | (f) Kutojihusisha na uuzaji au utumiaji wa dawa za kulevya;<br>(g) Kuchangia katika ustawi wa jamii anayoishi;<br>(h) Kuilinda Tanzania na kushiriki katika ulinzi wa taifa;<br>(i) Kuzilinda na kufuata sheria na taratibu za nchi;<br>(j) Kulipa kodi kwa hiari;<br>(k) Kulinda na kuheshimu utamaduni na maadili ya taifa;<br>(l) Kulinda na kutunza mazingira;<br>(m) Kujitahidi kuzuia maradhi, ujinga na umaskini. | | |
| | | | | Imeongezwa Ibara mpya ya 50 inayozungumzia wajibu wa raia kwa Taifa |
| 49. | Ulinzi wa mali ya umma | Ibara ndogo ya (1) irekebishwe kwa na iandikwe kama ifuatavyo:<br>“(1) Kila raia anao wajibu wa kulinda maliasili ya Taifa, mali ya mamlaka ya nchi mali za taasisi mbalimbali za umma na mali yoyote inayomilikiwa kwa pamoja na wananchi, na pia kuiheshimu mali ya mtu mwingine”. | | Ibara ya 49 inakuwa ya 51 na inabaki kama ilivyo |
| 50. | Haki na wajibu muhimu | (i) Ibara hii ifupishwe na irudishwe katika Sehemu ya Kwanza ya sura ya Nne. | Uandishi mzuri wa sheria ni kuhakikisha vipengele vya aina moja vinapatikana sehemu moja kwa urahisi na kwa lugha nyepesi. | Ibara ya 50 inakuwa ya 52 na inabaki kama ilivyo |
| | | (ii) Ibara ndogo ya (3) ifutwe. | Haina mantiki kwani huko ni kuingilia uhuru mila na desturi za jamii mbalimbali. | |

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Baraza* | *Sababu ya Baraza* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| | | (iii) Ibara ndogo ya (3) ibadilishwe na iandikwe kama ifuatavyo:<br>"(3) Mtu yeyote katika Jamhuri ya Muungano hatakuwa na haki, hadhi au cheo maalum kwa misingi ya nasaba, jadi au urithi wake, dini, kabila, hali yake ya kiuchumi au jinsi yake". | | |
| | | (iv) Ibara ya 50 hadi 53 zifupishwe na zirudushwe Katika Sura ya Nne. | | |
| | | (v) Iongezwe ibara ndogo mpya itakayoeleza tafsiri ya maneno "maslahi ya umma" ambayo isomeke kama ifuatavyo:<br>"maslahi ya Umma" ni suala lolote ambalo ni kwa faida ya maendeleo ya wananchi wote. | Neno maslahi ya umma halina ufafanuzi jambo ambalo ni hatari katika jinsi kila mamlaka au mtu atakavyoweza kulitafsiri. | |

### (b) Wajibu wa Mamlaka za Nchi

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Baraza* | *Sababu ya Maoni* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| 51. | Hifadhi ya haki za binadamu | (i) Ibara hii ifupishwe na irudishwe katika Sehemu ya Kwanza ya sura ya Nne. | Uandishi mzuri wa sheria ni kuhakikisha vipengele vya aina moja vinapatikana sehemu moja kwa urahisi na kwa lugha nyepesi. | 1. Ibara ya 51 inakuwa ya 53.<br>2. Ibara ndogo ya (3) imerekebishwa kwa kuweka maneno ''mikataba ya kikanda na ya kimataifa" badala ya maneno ''mikataba ya kimataifa" |
| | | (ii) ibara ndogo ya (3) ifutwe. | Mazingira yanaweza kubadilika. | |
| | | (iii) Katika ibara ndogo ya (3) yaongezwe maneno "na Kikanda" baada ya neno "kimataifa". | Tanzania inaridhia mikataba ya kimataifa na kikanda. | |
| | | (iv) Iongezwe ibara ndogo mpya itakayoeleza bayana kuwa haki za Binadamu zilizopo katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zitapaswa kuwekwa katika Katiba za Washirika wa Muunagano na Kama Katiba za Washirika haitaweka, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itachukua precedence. | | |
| 52. | Usimamizi wa haki za binadamu | (i) Ibara hii ifupishwe na irudishwe katika Sehemu ya Kwanza ya sura ya Nne. | Uandishi mzuri wa sheria ni kuhakikisha vipengele vya aina moja vinapatikana sehemu moja kwa urahisi na kwa lugha nyepesi. | Ibara ya 52 inakuwa ya 54 na inabaki kama ilivyo |
| | | (ii) Ibara hii irekebishwe ili kuwe na uwezekano wa shauri la haki za kikatiba kufunguliwa katika mahakama za chini. | Kwa kuwa Mahakama Kuu haiko kila sehemu nchini. | |
| | | (iii) Katika Ibara ndogo ya (4) maneno "kwa mujibu wa sheria" yafutwe. | Rasimu kwa kuweka sharti la kufungua shauri kwa mujibu wa sheria | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Baraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | linaitelekeza hii ibara kwa vile sheria inaweza kutungwa inayoweka vikwazo kama sheria iliopo sasa inayolazimisha uwepo wa Majaji watatu. | |
| | | (iv) Ibara ndogo ya (4) iandikwe kama ifuatavyo: "(4) Mahakama Kuu iwe ndio yenye mamlaka katika Mashauri ya kudai haki za kikatiba kwa mujibu wa ibara hii". | | |
| | | (v) Iongezwe ibara ya 52(5) na isomeke "Taasisi au mtu mwenye ujuzi maalum, baada ya kupewa kibali na mahakama, anaweza kutokea na kuwasilisha maoni kama rafiki wa mahakama." | | |
| | | (vi) Iongezwe ibara ya 52(6) na isomeke "katika kutekeleza usimamizi wa haki za kikatiba mahakama haitafungwa na masharti ya kiufundi ya uendeshaji kesi " | | |
| 53. | Mipaka ya haki za binadamu | (i) Ibara hii ifupishwe na irudishwe katika Sehemu ya Kwanza ya sura ya Nne. | Uandishi mzuri wa sheria ni kuhakikisha vipengele vya aina moja vinapatikana sehemu moja kwa urahisi na kwa lugha nyepesi. | Ibara ya 53 inakuwa ya 55 na inabaki kama ilivyo |
| | | (ii) Katika aya ya (f) ya ibara ndogo ya (1) yaongezwe maneno "kulinda mila na desturi na usalama wa nchi". | | |
| | | (iii) Iongezwe ibara ndogo ya (3) | Pamoja na vigezo | |

| ***Ibara Na.*** | ***Kichwa cha Habari*** | ***Maoni ya Baraza*** | ***Sababu ya Maoni*** | ***Marekebisho ya Tume*** |
|---|---|---|---|---|
| | | ambayo itaeleza ulinzi wa jumla wa sehemu hii ya katiba kuwa isiwe na urahisi wa kubadilishwa na itakapolazimu kubadili basi mapendekezo ya mabadiliko yapigiwe kura ya maoni na pia sheria yoyote itakayokinzana na sehemu hii ya katiba iwe ni batili. | vilivyowekwa rasimu haijaweka ulinzi wa haki hizi kwa maana ya kuwa isiwezekane kuibadili haki zilizomo katika sehemu hii ya katiba bila kuwepo kwa kura ya maoni. | |

# SURA YA TANO YA RASIMU

## 5.1 URAIA KATIKA JAMHURI YA MUUNGANO

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Maoni* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| 54. | Uraia wa Jamhuri ya Muungano | (i) Ibara ya 54 hadi 56 ziandikwe upya ili zieleze kwamba kila raia wa Zanzibar na Tanganyika atahesabika moja kwa moja kuwa pia ni raia wa Shirikisho la Muungano wa Jamhuri za Tanzania. | Uraia ndio msingi wa uananchi. Nchi mbili ndio zilizoungana kuwa shirikisho. | 1. Ibara ya 54 inakuwa ya 56.<br>2. Katika ibara ndogo ya (1) maneno “raia wa Tanzania” yasomeke maneno “raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania” |
| | | (ii) Ibara hii irekebishwe ili kila nchi iwe na uraia wake. | (a) Ili kila mtu apewe uraia katika nchi yake.<br>(b) Kabla ya Muungano kila nchi ilikuwa na uraia wake. | |
| | | (iii) Ibara isomeke Jamhuri za Muungano wa Tanzania. | Muungano ni wa nchi mbili. | |
| | | (iv) Iongezwe ibara ndogo iatakayoweka tafsiri ya neno “Mtanzania”. | | |
| | | (v) Ibara hii irekebishwe ili Uraia wa nchi mbili usikubalike. | (i) Ili kuzuia mtu aliyezaliwa nje ya nchi asipate uraia.<br>(ii) Unaweza kutoa mwanya kuingiza watu wasio raia wa Tanzania.<br>(iii) Ili kuzuia mtu aliyezaliwa nje ya nchi asipate uraia. | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| | | (vi) Uraia usiwe suala la Muungano. | Kila nchi iwe na uraia wake. | |
| | | (vii) Ibara hii irekebishwe ili kuruhusu Uraia wa nchi mbili. | (a) Ili kupanua wigo wa watanzania kutumikia nchi na kutafuta maisha nchi za nje bila ya kupoteza Uraia.<br>(b) Kuwawezesha watanzania waishio nje ya nchi kunufaika na fursa zinazopatikana katika nchi walizomo ikiwa wataamua kuwa raia wa nchi wanazofanyia kazi.<br>(c) Kuwawezesha Watanzania waishio ughaibuni kunufaika na fursa zinazopatikana katika nchi walizomo ikiwa wataamua kuwa raia wa nchi hizo bila ya kulazimika kupoteza uraia wao wa Tanzania.<br>(d) Ni haki ya msingi na maslahi ya kiuchumi kwa nchi yetu.<br>(e) Ili kupanua wigo wa watanzania | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | kutumikia nchi na kutafuta maisha nchi za nje bila ya kupoteza Uraia. | |
| | | (viii) Ibara hii irekebishwe ili kuruhusu uraia wa nchi zaidi ya moja, lakini uwe na mipaka kuwa raia yeyote mwenye uraia wa nchi zaidi ya moja, mojawapo ikiwa Tanzania, hataruhusiwa kugombea na kushika nyadhifa yoyote ya dola; na haruhusiwi kuajiriwa kwa namna yoyote katika idara nyeti za Taifa, ikiwamo Usalama wa Taifa. | | |
| | | (ix) Ibara hii irekebishwe na itamkwe bayana kuwa raia wa Tanzania hatakuwa na uraia wa nchi nyingine. | Inapendekezwa hivyo kutokana na usalama wa nchi yetu na mazingira yanayotuzunguka.<br>Mathalan kwa mujibu wa Ibara ya 219/10 kila Raia analo jukumu la ulinzi na usama wa nchi yetu. Sasa, endapo mtu anakuwa na uraia anakuwa na uraia wa nchi nyingine na nchi hiyo ikaingia vitani na nchi yetu huyo raia atawajibika vipi chini ya sheria za nchi za nchi na za kimataifa, endapo ama atakataa kwenda vitani kupigana na nchi nyingine kwa vile ni raia wa nchi | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | hiyo na akipigana kwa upande wa nchi hiyo na akakamatwa mateka na majeshi ya Tanzania. Je atakuwa mhaini au mateka wa vita?<br>Endapo atachukuliwa kama mateka wa vita, je, baada ya vita kumalizika atapelekwa wapi? | |
| | | (x) Ibara ndogo ya (4) irekebishwe kwa kubadilisha umri wa mtoto uwe miaka minne na pia mtoto huyo apewe uraia wa kuandikishwa na si wa kuzaliwa ila akifika miaka 18 apewe fursa ya kuomba kupewa uraia wa kuzaliwa. | Haki hii inaweza kutumika vibaya hasa sehemu za mipakani wanapofika umri wa miaka saba ambao ni umri wa kuanza shule. | |
| | | (xi) Ibara ndogo ya (4) yaongezwe maneno "na endapo uraia wa asili wa mtoto huyo utagundulika au ukigundulika ulipatikana kwa udanganyifu, uraia wake utafutwa" mwisho wa sentensi. | | |
| | | (xii) Utaratibu wa uraia ubaki kama ilivyo sasa | | |
| | | (xiii) Kusiwe na matabaka kwenye uraia | | |
| | | (xiv) Uraia uwe wa Jamhuri ya Muungano na siyo Tanzania | Tanzania ni nchi na dola moja. | |
| | | (xv) Raia wa kuzaliwa asipoteze uraia wake kwa kuwa na uraia wa nchi nyingine | | |
| | | (xvi) Kuwe na uraia wa zaidi ya nchi moja lakini kwa masharti. | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | (xvii) Uraia na uhamiaji uondolewe kwenye mambo ya Muungano. | | |
| | | (xviii) Ibara ndogo ya (4) yaongezwe maneno "baada ya uchunguzi wa kina" baada ya neno "hawajulikani". | | |
| 55. | Uraia wa kuzaliwa | (i) Ibara hii ifutwe. | Kulinda umoja wetu. | 1. Ibara ya 55 inakuwa Ibara ya 57.<br>2. Kuwe na ibara ndogo itakayosomeka kama ifuatavyo:<br>"Ibara ndogo ya 4 imeboreshwa:<br>(a) Neno ''mipaka" limeondolewa na kuwekwa neno ''eneo"<br>(b) Neno ''kuzaliwa" limeondolewa na kuwekwa neno. ''kuandikishwa"<br>(c) Ibara ndogo ya 5 imerekebishwa na itasomeka ''Endapo uraia wa wazazi wa mtoto aliyepewa uraia chini ya masharti ya Ibara ndogo ya (4) utabainika kuwa si uraia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, uraia wa mtoto huyo utasita." |
| | | (ii) Katika Ibara ndogo ya (1) maneno "ni au alikuwa raia wa Jamhuri ya Muungano" yafutwe na badala yake isomeke "alistahili kuwa rais wa Jamhuri ya Tanganyika au Jamhuri ya Watu wa Zanzibar." | Kuondoa utata kuwa nani ni rais wa kweli wa kuzaliwa na nani si raia. | |
| | | (iii) Ibara ndogo ya (4) ifutwe. | (a) Inaweza kutumika vibaya.<br>(b) Kuondoa changamoto zinazoweza kujitokeza hasa katika maeneo ya mipakani mwa nchi.<br>(c) Nchi yetu ina makambi mengi ya wakimbizi, kwa hiyo ni rahisi sana wakimbizi hao kutelekeza watoto wao hapa nchini wakijua kwamba watatambuliwa kama ni raia.<br>(d) Katika mikoa ya mipakani, itakuwa ni rahisi sana kwa raia wa nchi jirani kuvuka mpaka na kutelekeza mtoto wake kwenye nchi yetu, ikizingatiwa | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | kwamba makabila mengi ya mipakani yanapatikana kwenye nchi mbili au zaidi na yanaongea lugha moja.<br>(e) Baada ya muda wa miaka kumi au zaidi, Taifa litakuwa na kundi kubwa la vijana ambao siyo raia halali wa nchi hii.<br>(f) Ikasomwa sambamba na Ibara ya 75(a) kuna uwezekano wananchi kuongozwa na mtu ambaye si mtanzania;<br>(g) Kwa sababu za kiusalama kwani nchi inaweza kujikuta inahalalisha uraia wa watu walioingia nchini isivyo halali. | |
| | | (iv) Ibara ndogo ya (4) irekebishwe ili kumfanya mtoto wa aina hii awe raia wa kuandikishwa. | Kwa sababu Ibara hii inaweza kuhatarisha usalama wa Nchi na inaacha mwanya kwa Jamhuri kukusanya watoto wengi hasa katika maeneo ya mipakani endapo nchi jirani itapata maafa na kusababisha wakimbizi, au maafa yoyote watu wanaweza kuwatupa watoto upande | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | wa Tanzania kwa makusudi. | |
| | | (v) Ibara ndogo ya (4) irekebishwe na ieleze kwamba umri wa mtoto wa aina hii uwe miaka minne na pia mtoto huyo apewe uraia wa kuandikishwa na si wa kuzaliwa ila akifika miaka 18 apewe fursa ya kuomba kupewa uraia wa kuzaliwa. | (a) Haki hii inaweza kutumika vibaya hasa sehemu za mipakani wanapofika umri wa miaka saba ambao ni umri wa kuanza shule<br>(b) Pamoja na kuwa rasimu imetaja mikataba ya haki za binadamu iliyoridhiwa na Tanzania kuwa ni sehemu ya katiba hii bado kuna umuhimu wa kuweka bayana haki ya afya katika upekee wake. | |
| | | (vi) Ibara ndogo ya (5) ihamishiwe katika Ibara ya 56 baada ya kuirekebisha kwa kuongeza maneno “kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Bunge” katika mastari wa tatu kati ya maneno “Muungano” na “kwa”. | Ibara ndogo 55(5) ihamishiwe chini ya ibara ya 56 kwani uraia utakaopatikana kwa njia hiyo ni wa kuandikisha | |
| | | (vii) Iongezwe ibara ndogo ya (6) ambayo iandikwe kama ifuatavyo:<br>“(6) Raia wa kuzaliwa hatapoteza uraia wake kwa kuwa amepata uraia wa nchi nyingine labda kama ataukana uraia wake wa Tanzania”. | | |
| | | (viii) Ibara ndogo ya (4) irekebishwe ili mtoto asihesabike kuwa raia wa Tanzania. | (a) Watoto wengi watatupwa na kuongezeka. | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | (b) Mtoto huyo hatokuwa na uzalendo wa nchi yake. | |
| | | (xix) Ibara (4) isomeke kuwa mkimbizi. | | |
| | | (xx) 55(5) iunganishwe na ibara ya 56 | | |
| | | (xxi) Uraia usitishwe ikigundulika kulikuwa na udanganyifu | Mtoto huyo hatokuwa na uzalendo wa nchi yake. | |
| | | (xxii) Katika 55(2) inapendekezwa kuwa ili mtu aliyezaliwa nje ya Tanzania awe raia wa Tanzania kwa kuzaliwa mzazi mmojawapo pia awe raia wa Tanzania kwa kuzaliwa. | | |
| | | (xxiii) 55(4) ifutwe kwa kuwa haina maslahi kwa Taifa | | |
| | | (xxiv) Umri wa mtoto huyo uwe chini ya miaka minne na akifika miaka 18 apewe fursa ya kupewa uraia wa kuzaliwa | Watoto wengi watatupwa na kuongezeka. | |
| | | (xxv) Kuwe na uraia wa kurithi | | |
| | | (xxvi) Ibara ndogo ya (4) irekebishwe ili mtoto awe raia wa kuandikishwa. | Upo uwezekano wa kuwa raia wa Tanzania. | |
| | | (xxvii) Ibara ibadilishwe ili mtoto aliyezaliwa mpakani apewe uraia wa kuandikishwa, na yule aliyeokotwa ndani ya mipaka apewe uraia wa kuzaliwa. | | |
| | | (xxviii) Ibara ndogo ya (5) iwekwe katika ibara ya 56. | Maudhui yake yanalingana. | |
| | | (xxix) Ibara ndogo ya (5) ifutwe. | Ili kuzuia mtoto wa kuasiliwa asiweze kuwa | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | raia wa Tanzania. | |
| 56. | Uraia wa kuandikishwa | (i) Ibara ndogo ya (1) hadi (4) zifutwe. | Kulinda umoja wetu. | 1. Ibara ya 56 inakuwa Ibara ya 58.<br>2. Ibara ndogo ya 1, imerekebishwa na itasomeka:<br>"Mara baada ya kuanza kutumika kwa Katiba hii, mtu ambaye amekuwa mkazi wa Jamhuri ya Muungano Tanzania na ambaye ametimiza masharti yote ya sheria za nchi anaweza kuomba kuandikishwa kuwa raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania"<br><br>Ibara ndogo ya 2, imerekebishwa na itasomeka:<br>"Mtu aliyefunga ndoa na raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ambaye:<br>(a) amedumu katika ndoa hiyo kwa kipindi cha miaka mitano mfululizo; na<br>(b) ametimiza masharti yaliyoainishwa katika sheria kwa mujibu wa Ibara ndogo ya (1), anaweza kuomba uraia wa kuandikishwa kuwa |
| | | (ii) Ibara ndogo ya (1) iandikwe upya na iandikwe kama ifuatavyo:<br>"(1) Mara baada ya kuanza kutumika kwa Katiba hii, mtu ambaye amekuwa mkazi wa Tanzania Bara au Zanzibar kwa muda uliowekwa, na ambaye ametimiza masharti yote, chini ya sheria ya Bunge la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, anaweza kuomba kuandikishwa kuwa raia wa Jamuhuri ya Muungano". | | |
| | | (iii) Katika Ibara ndogo ya (2) yaongezwe maneno "kwa kipindi cha miaka mitano" baina ya maneno "ndoa" na "na". | Kuepuka kutumiwa vibaya, hasa katika suala la umiliki wa ardhi. | |
| | | (iv) Iongezwe ibara ndogo mpya ya (2) ambayo itakayoandikwa kama ifuatavyo:<br>"(2) Raia wa kuandikishwa anaweza kufutiwa uraia wake iwapo:<br>(a) ameupata uraia kwa njia ya udanganyifu;<br>(b) amesaliti nchi wakati wa vita kwa kutoa siri za nchi kwa maadui;<br>(c) ameshiriki katika kitendo cha uhaini;<br>(d) ndani ya miaka mitano baada ya kupewa uraia ameshiriki katika makosa ya jinai na kufungwa kifungo kinachozidi | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | miaka mitano au adhabu nyingine kali”. | | raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania”.<br><br>3. Ibara ndogo ya 3, imerekebishwa na kwa kuweka maneno ‘’Watanzania” mbele ya maneno ‘’Uraia wake”:<br><br>4. Ibara ndogo ya 5, imerekebishwa na itasomeka:<br>‘’Mtoto aliye na umri wa chini ya miaka kumi na nane ambaye wazazi wake sio raia wa Tanzania, akiasiliwa na raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuasiliwa kwake huko, kutawezesha mtoto huyo kuwa raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa kuzaliwa”. |
| | | (v) Ibara ndogo ya (3) iandikwe upya na iandikwe kama ifuatavyo:<br>“(3) Endapo ndoa iliyorejewa katika Ibara ndogo ya (2) itavunjika, mtu huyo ataendelea kuwa raia wa Jamhuri ya Muungano, kama mtu huyo hakuukana uraia wake na kabla ya kuvunjika ndoa hiyo imedumu kwa muda uliowekwa na sheria ya Bunge la Tanzania”. | | |
| | | (vi) Ibara ndogo ya (3) iandikwe upya kama ifuatavyo:<br>“(3) Endapo ndoa iliyorejewa katika ibara ndogo ya (2) itavunjika, kama mtu huyo hakuukana uraia wake, na hakuwa na lengo la kupata uraia kisha avunje, ataendelea kuwa raia wa Jamhuri ya Muungano”. | | |
| | | (vii) Iongezwe ibara ndogo mpya ya (6) ambayo itaeleza kama ifuatavyo:<br>“(6) Kwa kuzingatia masharti ya Ibara ndogo zilizotangulia raia wa kuandikishwa anaweza kufutiwa uraia wake iwapo amejihusisha na vitendo vya kihaini au ameisaliti nchi kwa kutoa siri wakati wa vita kwa maadui n.k.” | | |
| | | (viii) Iongezwe ibara mpya mara baada ya ibara ya 56 itakayokuwa 57 ambayo itaeleza kama ifuatavyo: | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | *Haki ya kubaki na uraia wa kuzaliwa* “57. Raia wa kuzaliwa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania atakayepata uraia wa nchi nyingine atakuwa na haki ya kubaki na uraia wake kwa mujibu wa masharti ya sheria”. | | |
| | | (ix) Iongezwe ibara ndogo mpya itakayoeleza tofauti baina ya neno “uraia” na “mkazi wa kudumu”. | | |
| | | (x) Iongezwe ibara ndogo mpya itakayoruhusu uraia wa nchi mbili kwa Mtanzania mwenye uraia wa kuzaliwa. | | |
| | | (xi) Ibara ndogo ya (3) irekebishwe ili ndoa ikivunjika basi uraia nao ufutike. | Kuleta manufaa kwa Watanzania walio nje ya nchi na nchi yetu. | |
| | | (xii) Ibara ndogo ya (2) irekebishwe ili kuweka muda wa miaka mitano mtu aliyeoa raia wa Tanzania ndipo aweze kuomba uraia. | | |
| | | (xiii) Iongezwe ibara ndogo itakayoeleza masharti ya kuomba uraia kwa mgeni na kuweka muda maalum na muda huo ukimalizika bila ya kuomba uraia basi mgeni ashitakiwe. | Ili kuweza kumchunguza. | |
| | | (xiv) Iongezwe ibara ndogo itakayozuia raia wa kuandikishwa kuwa na haki ya kumiliki ardhi. | Ardhi ibaki kuwa mali ya wazawa. | |
| | | (xv) 56(2)kuwe na vigezo maalum kwa mtu alieolewa au kuoa mtanzania kupata uraia | | |
| | | (xvi) Kuwe na miaka mitano kabla ya mwenza wa ndoa kupata uraia | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | (xvii) Kuwe na tofauti ya uraia na makazi ya kudumu | | |
| | | (xviii) Uraia ukome ikiwa ndoa itavunjika | | |
| | | (xix) Uraia uendelee hata ndoa ikuvunjika | | |
| | | (xx) Kuwe na vifungu kuzuia watu kunyang'anywa uraia wao | | |
| | | (xxi) 56(2) Maana ya ndoa itafsiriwe | | |
| | | (xxii) 56(2) ianze na mme au mke | | |
| | | (xxiii) 56(3) isomeke "Endapo ndoa iliyorejewa katika Ibara ndogo ya (2) itavunjika, mtu huyo ataendelea kuwa raia wa Jamhuri ya Muungano, kama mtu huyo hakuukana uraia wake na kabla ya kuvunjika ndoa hiyo imedumu kwa muda uliowekwa na sheria ya Bunge la Tanzania." | | |
| | | (xxiv) Ndoa iwe miaka kumi na mwenza athibitishe hali ya ndoa | | |
| | | (xxv) Masharti ya kufutiwa uraia ikiwa aliuapta kwa udanganyifu, amesaliti nchi wakati wa vita; ameshiriki kwenye uhaini na ameshiriki katika makosa ya jinai na kufungwa au kuadhibiwa kisheria. | | |
| | | (xxvi) Kuwe na kipindi cha kuchunguzwa kabla ya mtu kupewa uraia | | |
| | | (xxvii) Ndoa iwe kwa kipindi kisichopungua miaka mitatu kabla ya mtu kupata uraia | | |

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Maoni* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| | | (xxviii) Kuwe na vifungu vinavyoruhusu watu wasio na uraia wa nchi yeyote na ambao wamekaa nchini kwa muda mrefu kuweza kuomba kuwa raia wa kujiandikisha kwa minajiri ya sababu hiyo. | | |
| | | | | Imeongezwa Ibara mpya ya 59 inayozungumzia ‘’Hadhi ya watu wenye asili au nasaba ya Tanzania” |

# SURA YA SITA YA RASIMU

## 6.0 MUUNDO WA JAMHURI YA MUUNGANO

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| 57. | Muundo wa Muungano | (i) Ibara hii ibaki kama ilivyo. | Muundo wa Serikali Tatu ni bora katika kudumisha Muungano.<br>(i) Serikali Tatu zitaongeza ajira kwa wananchi.<br>(ii) Serikali Tatu zitajenga msingi bora wa maelewano.<br>(iii) Maamuzi ya kuwa na Serikali Tatu yametokana na maoni ya wananchi wa Tanzania nzima.<br>(iv) Serikali Tatu zitaondoa manung'uniko na kilio cha muda mrefu kwa wananchi wa Zanzibar.<br>(v) Mfumo wa Serikali Tatu utasaidia kuongeza Vyanzo vya mapato.<br>(vi) Itakuwa rahisi kwa wageni kuacha mapato katika nchi husika.<br>(vii) Muundo wa Serikali Mbili hauna faida.<br>(viii) Muundo wa Serikali Tatu hautakuwa | 1. Ibara ya 57 inakuwa Ibara ya 60.<br>2. Katika Ibara ndogo ya (1)(c) na kila linapojitokeza neno "Tanzania Bara" lisomeke "Tanganyika".<br>3. Katika Ibara ndogo ya 3 neno "Tanzania Bara" lisomeke "Tanganyika", na kila linapojitokeza neno ''Washirika wa Muungano'' yasomeke ''Nchi Washirika". |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | na vurugu.<br>(ix) Muundo wa Serikali Tatu utasaidia Zanzibar kuwa huru.<br>(x) Serikali Tatu zitasaidia kupunguza gharama za uendeshaji.<br>(xi) Muundo wa Serikali Tatu utasaidia Tanganyika nayo kuwa huru kama ilivyo Zanzibar.<br>(xii) Kila nchi itanufaika kwa upande wake.<br>(xiii) Itakuwa vizuri kwa kila nchi kuweza kujitegemea.<br>(xiv) Mfumo wa Serikali Mbili haueleweki ni wa aina gani, ama ni "Unitary au Federation" hivyo, mfumo wa Serikali Tatu utaondoa utata uliopo.<br>(xv) Mfumo wa Serikali Tatu utasaidia Tanganyika kutambulika, kwani katika Serikali Mbili Tanganyika haitambuliki imemezwa na Muungano.<br>(xvi) Serikali iliyopo imepoteza Utanganyika.<br>(xvii) Serikali Tatu itapunguza idadi ya | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | Wabunge hivyo gharama zitapungua.<br>(xviii) Tokea mwanzo hakuna nchi inayoitwa Tanzania Bara.<br>(xix) Mfumo wa Serikali Tatu utarahisisha majukumu ya kisera na kisheria.<br>(xx) Muundo wa Serikali Tatu utarudisha heshima ya Tanganyika.<br>(xxi) Katika Serikali Tatu, Serikali ya Muungano itadhibiti Serikali ya Zanzibar na Serikali ya Tanganyika.<br>(xxii) Muundo wa Serikali Tatu utasaidia kuwa na mfuko maalum wa Serikali ya Muungano.<br>(xxiii) Zanzibar wanacho chombo cha kujisemea lakini Tanganyika hawana sehemu ya kujisemea, hivyo katika Serikali Tatu, Tanganyika itakuwa na chombo chake cha kujisemea.<br>(xxiv) Serikali Tatu zitarahisisha utendaji kazi.<br>(xxv) Katika Serikali Tatu, kutakuwa na usawa miongoni mwa watu wa | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | pande zote mbili kwa kuwa kila upande utakuwa na serikali yake.<br>(xxvi) Katika nchi zilizoungana ni kwa vipi nchi moja ina serikali wakati nchi nyengine haina serikali.<br>(xxvii) Kuwa na Serikali Tatu kutawafanya Wazanzibari na Watanganyika kuwa kitu kimoja.<br>(xxviii) Zanzibar kuna bendera, wimbo wa Taifa, Rais na Vikosi vya Usalama vinavyopokea maelekezo ya Rais wa Zanzibar hii inapelekea kutokuwepo kwa Serikali Mbili.<br>(xxix) Kuwepo kwa Serikali Tatu hakutakuwa na gharama kubwa kwani kitakachobadilika ni kuwepo kwa Rais wa Muungano.<br>(xxx) Kuwepo kwa Serikali Tatu kutapelekea kuwa na Bunge dogo ambalo hakutakuwa na gharama kubwa za matumizi.<br>(xxxi) Sasa ni wakati sahihi wa kurudisha | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | Serikali ya Tanganyika.<br>(xxxii) Zanzibar inayo Katiba yake wakati Tanganyika haina Katiba, hivyo ikitokea Muungano kuvunjika itapekelea Tanganyika kutotawalika hivyo ni sahihi kuwepo kwa Serikali Tatu ili Tanganyika iwe na Katiba yake.<br>(xxxiii) Kuwepo kwa uhalali wa Tanganyika kuonekana waziwazi kama ilivyo Zanzibar na kutoa fursa kwa wananchi wa Tanganyika kushiriki katika Serikali yao.<br>(xxxiv) Hoja ya kuwepo kwa Serikali Tatu ni hoja ya muda mrefu ambayo imeshawahi kupendekezwa na Tume mbalimbali zilizowahi kuundwa hapo kabla hivyo ni wakati muafaka wa kuwa na Serikali Tatu.<br>(xxxv) Pamoja na kwamba watu wachache ndio wanaotaka kuwepo kwa Serikali Tatu ni wakati muafaka wa kuamua kuwepo kwa muundo huo.<br>(xxxvi) Kuondoa | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | mgongano wa maslahi. (xxxvii) Kuondoa muingiliano wa majukumu. (xxxviii) Wananchi wanaimani na Tume ya Katiba iliyopendekeza Serikali Tatu. (xxxix) Uwepo wa Serikali Tatu hauna itikadi au sera. (xl) Kumekuwa na malalamiko ya siku nyingi hasa upande wa Zanzibar, jambo linaloashiria Zanzibar kutoridhika na muundo uliopo wa Serikali Mbili. (xli) Zanzibar ni dola kamili hivyo Serikali Tatu zitapelekea kuundwa kwa Tanganyika itakayokuwa na mamlaka yake kamili. (xlii) Serikali Tatu ni madai ya pande zote mbili za Muungano. (xliii) Serikali Tatu zitaleta umoja na utulivu na zitaepusha kero na changamoto katika Muungano. (xliv) Itampunguzia kazi Rais wa Shirikisho. (xlv) Serikali Tatu itapunguza mzigo wa siku | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | nyingi kwa Tanganyika.<br>(xlvi) Serikali Tatu zitaharakisha maendeleo.<br>(xlvii) Serikali Tatu zitaweka usawa wa utendaji kazi kwa kuwa na vyombo vya kutunga sheria kwa pande zote mbili.<br>(xlviii) Kuweka uwiano wa kazi kwa Marais wa Washirika.<br>(xlix) Hakuna uwiano wa malipo kwa Wabunge wale wanaowawakilisha watu wengi na wale wanao wakilisha watu kidogo.<br>Rais wa Muungano anapokea misaada kwa sehemu mbili, wakati Rais wa Zanzibar anapokea misaada yake kwa upande wake tu. | |
| | | (ii) Muundo wa Muungano waachiwe wananchi kuamua kwa kura ya maoni. | (a) Muungano uwe wa ridhaa ya wananchi wa pande mbili.<br>(b) Kupunguza kero za Muungano.<br>(c) Kuondoa upinzani wa Rasimu ya Katiba wakati wa kura ya maoni. | |
| | | (iii) Ibara hii irekebishwe ili kuwepo na muundo wa serikali moja. | (a) Kwa sababu za:<br>(i) Kiusalama;<br>(i) Kiitikadi; na | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | (ii) Kiuchumi.<br>(b) Serikali Mbili hazikusaidia na hata Tatu hazitosaidia kuondoa matatizo.<br>(c) Serikali Tatu zitaongeza gharama.<br>(d) Serikali moja italeta maana halisi ya Muungano.<br>(e) Serikali moja itajenga umoja zaidi.<br>(f) Mapato ya Tanganyika na Zanzibar yote yataenda Muungano.<br>(g) Zanzibar inachangia kidogo katika Muungano.<br>(h) Zanzibar inayo kila kitu mfano Amiri Jeshi Mkuu, hivyo ni bora awepo Amiri Jeshi Mkuu mmoja tu.<br>(i) Kitendo cha kuchanganya mchanga kati ya Zanzibar na Tanganyika, ni vigumu kuutenganisha mchanga huo.<br>(j) Serikali moja ndio ilikuwa nia na | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | kusudio la waasisi wa Muungano.<br>(k) Serikali Mbili zilizopo zimeshakomaa hivyo ziungane iwe moja. | |
| | | (iv) Kuwe na muundo wa Serikali Mbili.<br>(v) Aya (c) ya ibara ndogo ya (1) na Ibara ndogo ya (3) zifutwe ili shughuli za kiutendaji zinazohusu Tanzania Bara zisimamiwe na Serikali ya Jamhuri ya Muungano na zile za Zanzibar zisimamiwe na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. | Maoni haya yamezingatia mambo yafuatayo:-<br>(a) Kwenye mfumo wa Serikali tatu, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ataongoza nchi kwa kutegemea fadhila ya Rais wa Tanganyika na Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.<br>(b) Kwenye mfumo wa Serikali tatu, Rais wa Jamhuri atakuwa hana watu wa kuwatawala.<br>(c) Muundo wa Serikali tatu utaendeshwa kwa gharama kubwa kwa kuzingatia kwamba kutakuwa na marais watatu, Makamu wa Rais watatu, Mabunge | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | matatu.<br>(d) Kuanzisha muundo wa Serikali tatu maana yake ni lazima kwanza uvunje Muungano uliopo, ufanyike uchaguzi wa Tanganyika na Zanzibar na baada ya hapo ndipo achaguliwe Rais wa Muungano.<br>(e) Italeta amani na utulivu.<br>(f) Ndio msingi wa makubaliano ya Muungano.<br>(g) Kuepusha mkanganyiko.<br>(h) Malalamiko ya Muungano yapatiwe ufumbuzi.<br>(i) Serikali Tatu zitawayumbisha wananchi, kijamii, kiutawala na kisera.<br>(j) Serikali kamili inapaswa kuwa na ardhi na watu, hivyo iwepo Serikali ya Muungano na Serikali ya Zanzibar kama ilivyo sasa. | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | (k) Serikali Tatu hazitaweka uwiano baina ya Zanzibar na Bara hasa kwa upande wa Wabunge.<br>(l) Mchakato wa Katiba ya Tanganyika hauwezi kuanzishwa sasa.<br>(m) Hakuna uchumi wa kutosha kugharamia Serikali Tatu.<br>(n) Serikali Mbili hazina tatizo.<br>(o) Hakutakuwa na ushindani.<br>(p) Serikali Mbili ziendelee kuwepo ili kuendeleza serikali za mitaa.<br>(q) Hati ya Muungano ni Serikali Mbili.<br>(r) Serikali Tatu zitasababisha athari katika mikopo.<br>(s) Ni njia ya kudumisha Muungano.<br>(t) Mfumo wa Serikali Tatu ni mfumo mpya hapa Tanzania na duniani.<br>(u) Mfumo wa Serikali Tatu utawaacha nyuma wanawake.<br>(v) Mfumo wa Serikali | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | Tatu utaleta vurugu na kuhatarisha amani.<br>(w) Mfumo wa Serikali Tatu ni uroho wa madaraka kwa baadhi ya viongozi.<br>(x) Hakuna Katiba ya Tanganyika.<br>(y) Serikali Tatu zitavunja Muungano. | |
| | | | Sababu nyengine zilizotolewa za kutaka mfumo wa Muungano wa Serikali mbili<br><br>KISHERIA:<br><br>i. Msingi mkuu wa Muungano kati ya iliyokuwa Jamhuri ya Tanganyika na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar ni wa Serikali mbili kwa mujibu wa makubaliano ya mwaka 1964.<br>ii. Mfumo wa Serikali tatu utaleta urasimu na utata wa kisheria katika umiliki na uendeshaji wa shughuli za kiuchumi | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | na kijamii;<br>iii. Mfumo wa Serikali tatu utasababisha mgogoro wa kisheria kuhusu masuala ya uwakilishi katika Bunge la Jamhuri ya Muungano kwani majimbo ya uchaguzi yatakuwa mikoa kwa Bara na wilaya kwa Zanzibar wakati uundwaji wa mikoa na wilaya si jambo la Muungano.<br><br>KISIASA:<br><br>i. Serikali ya Jamhuri ya Muungano itaelea kimadaraka na kimamlaka kwa sababu haitakuwa na uwezo wa kushughulikia moja kwa moja masuala yanayowahusu wananchi kama elimu, afya, kilimo, maji na barabara kwani si kati ya mambo ya Muungano ingawa katika Rasimu hii ya Katiba yanazungumzwa kama sehemu ya | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | majukumu ya Serikali ya Muungano;<br>ii. Kutokana na ukubwa wa eneo na uchumi wa Tanzania Bara ni wazi kwamba Serikali ya Tanzania Bara itachangia zaidi kwenye uendeshaji wa Serikali ya Muungano.<br><br>KIUCHUMI:<br>i. Serikali ya Jamhuri ya Muungano itakuwa tegemezi kwa Serikali zinazounda Muungano hasa kwa Serikali ya Tanzania Bara ambayo uchumi wake ni mkubwa;<br>ii. Urasimu wa kibiashara na umilikaji ardhi utaongezeka kwa sababu biashara, ardhi na umilikaji mali wa aina nyingine si mambo ya Muungano;<br>iii. Gharama za uendeshaji wa Serikali zilizopo hivi sasa ni kubwa hivyo kuwepo kwa Serikali tatu kutakuwa ni gharama ya ziada na hivyo kuwa mzigo mkubwa kwa | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | wananchi.<br><br>KIJAMII:<br>Muundo unaopendekezwa utahatarisha amani, utulivu na utangamano wa kitaifa kwani watu wa pande mbili za Muungano wamekuwa na uhusiano na mwingiliano kwa miaka mingi. | |
| | | (vi) Iongezwe ibara ndogo mpya itakayoeleza usawa kati ya nchi zote mbili katika maeneo muhimu kama elimu ngazi zote, raslimali ardhi, rasilimali malikale maliasili nk. | | |
| | | (vii) Katika Ibara ndogo ya (1) neno 'Serikali" lifutwe na badala yake iandikwe "dola". | | |
| | | (viii) kila ilipotajwa "Serikali ya Zanzibar" iandikwe "Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar". | | |
| | | (ix) ibara ndogo ya (3) ifutwe. | | |
| | | (x) Kuwe na Rais mmoja na wakuu wa washirika wapewe majina mengine | | |
| | | (xi) Kuwe na serikali moja na Tanganyika na Zanzibar ziwe majimbo | | |
| | | (xii) Kuwe na serikali mbili kuelekea moja | | |
| | | (xiii) Katiba za nchi washirika | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | zielekezwe kwenda sambamba na masharti ya katiba ya Jamhuri ya Muungano. | | |
| | | (xiv) Kuwe na vifungu vinavyotamka kuwa: “Lengo la Katiba za Washirika ni kufanikisha malengo ya Muungano na kuweka masharti ambayo yanafanana na masharti ya Katiba hii na kwa vyovyote vile masharti yasiyo kinyume na masharti ya Katiba hii.” | | |
| | | (xv) Kuwe na msisitizo wa Ukuu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano na pawe na Ibara ndogo inayotamka kuwa ni sharti katiba za Tanganyika na Zanzibar zisikinzane na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. | | |
| | | (xvi) Sarafu na Benki Kuu visiwe mambo ya muungano | | |
| | | (xvii) Neno serikali liondolewe | | |
| | | (xviii) Ibara ya 57(10) iitwe serikali ya Mapinduzi Tanzania Visiwani. | | |
| | | (xix) Ibara ya 57(2)(c) iboreshwe kuweka maneno “Mahakama ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ishirikiane na TAKUKURU” | | |
| | | (xx) Mahakama ya Katiba Pekee iwe ni ya Muungano | | |
| | | (xxi) Shirikisho liwe kati ya serikali ya Tanganyika na Serikali ya Zanzibar na Kuwe na | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | Kamisheni ya mambo ya shirikisho | | |
| 58. | Vyombo vya utendaji vya Jamhuri ya Muungano | (i) Ibaki kama ilivyo. | | Ibara ya 58 inakuwa Ibara ya 61 na inabaki ilivyo. |
| | | (ii) Ibara ndogo (1) irekebishwe ili vyombo vya Muungano iwe kwa mambo ya Muungano tu. | | |
| | | (v) Serikali ya Muungano iwe na Mamlaka kwa ajili ya mambo ya muungano tu. | Maudhui yake hayaendani na muundo wa Serikali Mbili. | |
| | | (vi) Mahakama iwe ni kwa mambo ya muungano tu | Maudhui yake hayaendani na muundo wa Serikali Mbili. | |
| | | (vii) Kusiwe na Bunge la shirikisho bali kuwe na kamati ya kutathmini na kupendekeza uendeshaji bora wa mambo tuliyokubaliana kwenye shirikisho. | | |
| 59. | Mamlaka ya Serikali ya Muungano | (i) Iongezwe ibara ndogo mpya itakayoweka sharti kwa Serikali ya Muungano na Serikali za Nchi Washirika kushauriana na kushirikiana katika maeneo mbalimbali. | Kuepuka mgogoro baina ya Serikali ya Muungano na za Washirika. | 1. Ibara ya 59 inakuwa Ibara ya 62.<br>2. Katika Ibara ndogo ya 3, neno Tanzania Bara lisomeke Tanganyika. |
| | | (ii) ibara hii irekebishwe kwa kutaja Mambo ya Muungano, yasiyo ya Muungano na yale ambayo Washirika watakuwa na mamlaka sawa (concurrent jurisdiction). | | |
| | | (iii) Ibara ibadilishwe ili Katiba ya Jamhuri ya Muungano ijihusishe na mambo ya Muungano tu, mambo yasiyo ya Muungano waachiwe nchi | Ndilo jina sahihi. | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | washirika. | | |
| | | (ii) Katika Ibara ndogo ya (3) maneno "Serikali ya Zanzibar" yasomeke 'Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar". | (a) Ili kila upande uweze kufaidi rasilimali zake.<br>(b) Serikali za nchi Washirika zijisimamie wenyewe bila ya kuomba msaada kutoka kwa Serikali ya Muungano. | |
| | | (iii) Ibara ndogo ya (3) irekebishwe ili kuondoa uwezekano wa Serikali ya Muungano kutekeleza majukumu ya moja ya Serikali ya washirika kwa kubebesha mzigo wa gharama kwa Serikali nyingine, ibara hii irekebishwe kwa kutamka kwamba suala kama hili liwasilishwe kwenye Tume ya Baraza la Muungano kabla ya kupitishwa. | Maudhui yake hayaendani na muundo wa Serikali Mbili. | |
| | | (iv) Ibara ndogo ya (3) maneno "kwa makubaliano na masharti maalum baina yake na Serikali ya Zanzibar au Serikali ya Tanzania Bara – pia mamlaka ya Serikali ya Zanzibar na Serikali ya Tanzania Bara" yafutwe na badala yake isomeke "chini ya Washirika wa Muungano". | | |
| | | (v) Ibara zote zinazohusiana na muundo wa Muungano wa Serikali Tatu zifutwe. | | |
| | | (vi) Ibara zote zinazohusiana na muundo wa Muungano | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | zirekebishwe na ianzishwe Tanganyika. | | |
| | | (vii) Ibara ndogo ya (3) irekebishwe kwa kufuta neno "Tanzania Bara" na isomeke Tanganyika. | | |
| | | (viii) Ibara ndogo ya (3) irekebishwe ili Serikali ya Shirikisho kabla ya kukubaliana na Serikali ya mshirika kutekeleza mambo yasiyo ya Muungano, makubaliano hayo yaidhinishwe na Bunge la nchi mshirika wa Muungano. | | |
| | | (xii) Sheria za upande mmoja wa Muungano zitambulike upande mwingine | | |
| | | (xiii) Kuwe na orodha ya Mambo ya Muungano; Mambo yasiyo ya Muungano na Mambo ya pamoja(concurrent jurisdiction). | | |
| | | (xii) Sheria za upande mmoja wa muungano zitambulike upande mwingine | | |
| | | (xiii) Kuwe na orodha ya Mambo ya Muungano; Mambo yasiyo ya Muungano na Mambo ya pamoja(concurrent jurisdiction). | | |
| | | (i) 59(3) makubaliano yawekwe wazi | | |
| | | (viii) Ibara ya 59(3) ifutwe | | |
| | | (xiv)Iongezwe Ibara itakayotambua utekelezaji wa Sheria zinazotumika katika upande mmoja wa Muungano kutambulika upande mwingine | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | wa Muungano. | | |
| | | (xv)Isomeke, "Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haitaweza kuingia Mkataba wa Kimataifa ambao utaathiri nchi mshirika wa Muungano kabla ya kupata ridhaa ya nchi mshirika husika." | | |
| | | (xvi)Isomeke, "Bila kuathiri misingi ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaweza kuingia kwenye mkataba wa kimataifa wenye wanachama wengi kwa niaba ya mshirika wa muungano kama ikiombwa kufanya hivyo na nchi mshirika wa muungano. Ikitokea hivyo, gharama zote husika zitalipwa ma nchi mshirika wa muungano, na mkataba huo hautaathiri kwa namna yeyote nchi nyingine mshirika wa muungano. | | |
| | | (xvii)Mkataba wowote wa kimataifa ulioingiwa na Jamhuri ya Muungano hautakuwa na nguvu ya kisheria kama au kwa kadiri unavyokinzana na katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. | | |
| | | (xviii)Kila mshirika wa Muungano atalazimika kushauriana na Serikali ya Shirikisho kupitia Tume ya Uhusiano na Uratibu wa Serikali juu ya nia yake ya kuingia mkataba wa kimataifa. | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | Nchi mshirika wa muungano hataweza kuingia mkataba wa kimataifa kama:<br>1. Upande wa pili wa mkataba ni nchi au taasisi isiyotambuliwa na mahusiano ya kidiplomasia na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.<br>2. Mkataba huo unakinzana na sera ya kimataifa ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.<br>3. Mkataba huo unakinzana na masharti ya kimataifa ambayo yanatekelezwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. | | |
| | | (xix) Kuwe na ibara ndogo inayosomeka, "Ikitokea nchi mshirika wa muungano akaingia mkataba wa kimataifa kwa kukiuka ibara ndogo hapo juu, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itakuwa na wajibu wa kuzuia na kutowajibika na utekelezaji wa mkataba huo kulingana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania." | | |
| | | (xx)Mambo ya muungano yawe:<br>i. utumishi katika jamhuri ya muungano<br>ii. Mahakama ya jamhuri ya muungano<br>iii. Bunge la Jamhuri ya | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | muungano<br>iv. Tume za uwajibikaji<br>v. Uchaguzi na vyama vya siasa<br>vi. Fedha za jamhuri ya muungano<br>vii. Haki za binadamu<br>viii. Maliasili<br>ix. ardhi | | |
| | | (xxi)Mambo ya Muungano yaliyoko kwenye sheria yaorodheshwe kweye nyongeza kama mambo ya Muungano | | |
| | | Neno “yaliyoorodheshwa” libadilishwe na kuwa “ yanayo orodheshwa” | | |
| | | (xxii)Baraza la wawakilishi la Zanzibar liwe Bunge la Zanzibar | | |
| | | (xxiv)Ibara hii ifutwe. | | |
| | | (xxv)Ibara ndogo ya (3) maneno “kwa makubaliano na masharti maalum baina yake na Serikali ya Zanzibar au Serikali ya Tanzania Bara – pia mamlaka ya Serikali ya Zanzibar na Serikali ya Tanzania Bara” yafutwe na badala yake isomeke “chini ya Washirika wa Muungano”. | | |
| | | (xxvi)Ibara zote zinazohusiana na muundo wa Muungano wa Serikali Tatu zifutwe. | | |
| | | (xxvii)Ibara zote zinazohusiana na muundo wa Muungano zirekebishwe na ianzishwe Tanganyika. | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | (xxviii)Ibara ndogo ya (3) irekebishwe kwa kufuta neno "Tanzania Bara" na isomeke Tanganyika. | | |
| | | (xxix)Ibara ndogo ya (3) irekebishwe ili Serikali ya Shirikisho kabla ya kukubaliana na Serikali ya mshirika kutekeleza mambo yasiyo ya Muungano, makubaliano hayo yaidhinishwe na Bunge la nchi mshirika wa Muungano. | (a) Ili kupata ridhaa ya wananchi.<br>(b) Kuepusha ushawishi wa viongozi bila ya kuwashirika wananchi. | |
| 60. | Mambo ya Muungano | i) Mambo ya Muungano yaainishwe katika Ibara hii sio katika Nyongeza. | (a) Ili kuepuka tafsiri tofauti.<br>(b) Kuyapa uzito zaidi. | Ibara ya 60 inakuwa Ibara ya 63 na inabaki kama ilivyo. |
| | | ii) Inapendekezwa kwamba mambo ya Muungano yawe tisa kama ifuatavyo:-<br>1. Katiba na mamlaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.<br>2. Ulinzi na Usalama wa Jamhuri ya Muungano.<br>3. Uraia na Uhamiaji.<br>4. Sarafu na Benki Kuu.<br>5. Mambo ya Nje.<br>6. Usajili wa Vyama vya Siasa.<br>7. Ushuru wa bidhaa na mapato yasiyo ya kodi yatokanayo na mambo ya Muungano.<br>8. Elimu ya Msingi, Sekondari na Elimu ya Juu.<br>9. Masuala yote yanayohusu Ardhi. | Ili kubaki na muundo wa serikali mbili | |
| | | iii) Orodha ya Mambo ya Muungano katika Rasimu ya Katiba, kama iliyoonyeshwa katika Nyongeza, ijumuishe | Ili kuepuka kuwa na tafsiri tofauti. | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | mambo yote yenye sura ya Muungano yaliyotajwa kwenye Jedwali. Aidha, mipaka ya utekelezaji wake ibainishwe na yachambuliwe ili kila jambo la Muungano litajwe peke yake.<br>iv) Imetajwa kuwa Mamlaka ya Jamhuri ya Muungano ni jambo la Muungano. Zitajwe Asasi zilizo chini ya Mamlaka hiyo.<br>v) Badala ya kutaja Sarafu na Benki Kuu kuwa ni jambo la Muungano, yatajwe majukumu na siyo jina la Asasi.<br>vi) Suala la Haki za Binadamu lijumuishwe katika Mambo ya Muungano. Aidha, utolewe ufafanuzi wa mipaka ya utekelezaji wake. | | |
| | | vii) Ibara hii irekebishwe ili mambo yanayohusu Sarafu, Benki Kuu, Uraia, Uhamiaji na Usajili wa Vyama vya Siasa yawe chini ya mamlaka ya Washirika na yasiwe chini ya mamlaka ya Muungano. | Ni Mambo muhimu kwa maendeleo ya kiuchumi na kisiasa kwa Washirika. | |
| | | viii) Iongezwe ibara ndogo ya (2) ambayo itazungumzia chombo kitakachoshughulikia mambo ya Muungano.<br>ix) kuwepo na ibara nyengine ndogo ya (3) itakayoeleza kuwa Bunge litatunga sheria kusimamia | Ili masuala ya Muungano yapewe hadhi ya Kikatiba. | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | masuala yote yanayohusu Jamhuri ya Muungano. | | |
| | | x) Iongezwe ibara ndogo mpya itakayotoa mamlaka kwa washirika ama kupunguza au kuongeza mambo ya muungano.<br>xi) Masuala ya kimataifa yawe chini ya Serikali ya Muungano pekee<br>xii) Mambo ya nje yabaki kuwa ya muungano<br>xiii) uteuzi wa mabalozi uzingatie weledi na siyo uwiano | (a) Ili maamuzi yaweze kufanywa hata na upande mmoja tu wa nchi washirika pale uamuzi huo utakapoungwa mkono na Bunge la nchi mshirika, basi iwe moja kwa moja (automatic) jambo hilo linaondoka katika mambo ya Muungano.<br>(b) Pendekezo hili linatokana na matatizo yaliyopo sasa katika utaratibu wa kuondosha jambo la muungano; kwa mfano Zanzibar ilishafanya maamuzi toka mwaka 2009 kupitia Baraza la Mapinduzi na pia Baraza la Wawakilishi wa kuliondoa suala la mafuta na gesi asilia katika orodha ya mambo ya muungano, lakini kwa muda mrefu jambo hilo limeshindikana.<br>(c) Kuhusu kuongeza jambo la Muungano, inapendekezwa kuwa | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | jambo hilo kwanza likubaliwe katika mabunge ya nchi washirika. Hii itaondosha dhana ya mambo makubwa kama haya kuamuliwa bila ya kuvihusisha vyombo vikubwa vya nchi washirika kama vile Bunge na Baraza la Mawaziri, ambapo Zanzibar kwa mfano imekuwa kwa muda mrefu ikilalamika kuwa baadhi ya maamuzi yanayofanywa katika Bunge la Muungano hayapati ridhaa ya Baraza la Mapinduzi wala Baraza la Wawakilishi hasa ukizingatia kuwa hakuna utaratibu wa Kikatiba wala wa Kisheria wa vyombo hivi kufikisha maoni yake kupitia kwa Wabunge wa Bunge la Muungano kutoka Zanzibar. | |
| | | i) Inapendekezwa kuwa orodha ya mambo ya Muungano (Nyongeza I) isomeke hivi: | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | (a) (Bila mabadiliko) Katiba na mamlaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;<br>(b) (Bila mabadiliko) Ulinzi na Usalama wa Jamhuri ya Muungano;<br>(c) (Kirekebishwe) Uraia, Uhamiaji na Haki za Binadamu;<br>(d) (Bila mabadiliko) Sarafu na Benki Kuu;<br>(e) (Bila mabadiliko) Mambo ya Nje;<br>(f) (Bila mabadiliko) Usajili wa Vyama vya Siasa; na<br>(g) (Bila mabadiliko) Ushuru wa Bidhaa na Mapato Yasiyo ya Kodi yatokanayo na mambo ya Muungano. | | |
| | | ii) Ziongezwe ibara ndogo mpya kama ifuatavyo:<br>(a) Urais wa Jamhuri ya Muungano utakuwa ni wa kupokezana baina ya Tanganyika na Zanzibar kila baada ya miaka kumi.<br>(b) Chama chochote au mtu yeyote atakayekusudia kugombea Urais atalazimika kumpendekeza mtu yoyote kugombea nafasi ya Makamu wa Rais kutoka upande wa pili wa Muungano. | Utaratibu huu utaepusha Jamhuri ya Muungano kuongozwa na watu wa upande mmoja wa Muungano kwa kipindi kirefu. | |
| | | iii) Ibara hii irekebishwe ili kujumuisha elimu ya juu kuwa ni miongoni mwa mambo ya Muungano. | | |

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Maoni* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| | | iv) Katika Nyongeza ya Rasimu iliyotajwa katika ibara ya 60 iongezwe aya mpya zifuatazo:<br>**(a)** Maadili na Miiko ya Uongozi na Utumishi wa Umma;<br>**(b)** Haki za Binadamu na Wajibu wa Raia;<br>**(c)** Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi na masuala yote yanayohusu uchaguzi. | | |
| | | v) Ibara hii irekebishwe kwa kutaja taasisi zote zilizo chini ya Mamlaka ya Muungano;<br>vi) majukumu ya Benki Kuu yatajwe badala ya kutaja "Safaru";<br>vii) Haki za Binadamu zitajwe kuwa ni Mambo ya Muungano. | (a) Ibara hii inataja mambo ya Muungano kupitia Nyongeza ya Katiba kuwa ni 22, lakini Mambo yenye Sura ya Muungano yanayozungumziwa katika Rasimu ni zaidi ya hayo.<br>(b) Mambo yote hayo yatajwe kuwa ni Mambo ya Muungano.<br>(c) Mamlaka imetajwa kuwa ni jambo la Muungano.<br>(d) Rasimu imetaja jina la taasisi. | |
| | | viii) Mambo ya Muungano yaongezwe elimu, rasilimali, ajira na Utumishi. | | |
| | | ix) Sarafu, Benki Kuu, Uraia na Mambo ya Nje yaondolewe katika mambo ya Muungano. | (a) Haya ni mambo yaliyo katika mamlaka ya nchi husika.<br>(b) Kabla ya Muungano, | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | Zanzibar ilikuwa na sarafu yake. | |
| | | x) Sarafu, benki, uraia na Mambo ya Nje yaondolewe katika mambo ya Muungano. | Ili kila upande uweze kusimamia mamlaka yake kamili. | |
| | | xi) Afya, elimu, Jeshi la Polisi na hali ya hatari yawe mambo ya Muungano. | | |
| | | xii) Mambo ya Muungano yawe tisa kwa kuongeza rasilimali za taifa na Mitaala ya elimu katika ngazi zote. | (a) Rasilimali zitasababisha migogoro na kero mpya katika Muungano.<br>(b) Wasomi wa pande zote mbili watapata fursa ya kufanya kazi sehemu zote mbili.<br>(c) Sifa za ajira katika Muungano ziweze kufanana.<br>(d) Kufuta ubaguzi wa kielimu. | |
| | | xiii) Katika orodha ya Mambo ya Muungano iongezwe elimu ya Juu. | Kuongeza upeo wa elimu na kutoa nafasi zaidi ya ajira. | |
| | | xiv) Mambo ya Muungano yaainishwe katika Ibara hii sio katika Nyongeza. | (a) kuondoa tafsiri tofauti.<br>(b) Mambo ya Muungano yawe na uzito unaostahili. | |
| | | xv) Katika orodha ya mambo ya Muungano iongezwe Tume Huru ya Uchaguzi na Msajili wa Vyama vya Siasa. | Ili kuendana na mfumo wa Serikali Mbili. | |
| | | xvi) Ibara hii ibaki kama ilivyo. | Ili kila upande uweze | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | kujitawala. | |
| | | xvii) Uraia na uhamiaji yasiwe mambo ya Muungano. | (a) Ndio msingi wa wananchi.<br>(b) Kurahisisha kila nchi kuratibu mambo yanayowahusu raia wake.<br>(c) Kuweza kudhibiti uingiaji wa wageni kwa kuzingatia Zanzibar ni nchi yenye eneo dogo la ardhi.<br>(d) Itasaidi uhalali na upatikanaji wa Rais katika nchi Washirika.<br>(e) Kabla ya Muungano na mara baada ya Muungano Zanzibar ilikuwa na kadi zake za uraia.<br>(f) Utamaduni wa Zanzibar ni tofauti na Watanganyika, hivyo kuachia kuingia watu kiholela itasababisha kuharibu utamaduni wa Zanzibar. | |
| | | xviii) Mambo ya Nje isiwe suala la Muungano. | (a) Kujenga uwezo kwa nchi Washirika kuingia katika mahusiano na mikataba na mashirika ya | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | kimataifa.<br>(b) Ni utambulisho wa nchi kitaifa na kimataifa.<br>(c) Kuimarisha mahusiano yaliyokuwepo katika nchi Washirika kabla ya Muungano.<br>(d) Ili nchi Washirika waweze kuchagua nchi marafiki.<br>(e) Kutoa fursa kwa nchi Washirika kujiunga na Jumuiya za Kimataifa.<br>(f) Kuondosha usumbufu kwa wananchi wa upande mmoja wakati wa kuomba nafasi za kusafiri nchi za nje kutokana na kutokuwa na mabalozi. | |
| | | xix) Usajili wa Vyama vya Siasa lisiwe suala la Muungano. | (a) Masuala ya kisiasa ni ya nchi husika.<br>(b) Kabla ya Muungano Zanzibar na Tanganyika zilikuwa na vyama vyao vya siasa.<br>(c) Itaondoa nchi Washirika kuburuzwa katika | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | maamuzi.<br>(d) Kuzuia matumizi ya nguvu ya Serikali ya Muungano katika kulazimisha matokeo ya uchaguzi wa viongozi hasa kwa upande wa Zanzibar. | |
| | | xx) Ushuru wa bidhaa isiwe suala la Muungano. | (a) Suala la uchumi sio suala la Muungano.<br>(b) Nchi Washirika zinatofautiana katika mapato. | |
| | | xxi) Ibara hii isomeke mambo ya Shirikisho na sio mambo ya Muungano. | | |
| | | xxii) Mambo ya Muungano yawe kama ifuatavyo:<br>(a) Katiba ya Muungano wa Jamhuri za Tanzania.<br>(b) Mamlaka ya Jamhuri ya Muungano za Tanzania.<br>(c) Uratibu wa masuala ya Uraia na Uhamiaji.<br>(d) Uratibu wa Sera ya Mambo ya Nje.<br>(e) Uratibu wa mambo ya Usalama.<br>(f) Utumishi katika Serikali ya Jamhuri za Muungano za Tanzania.<br>(g) Mahakama ya Rufani ya Jamhuri za Muungano za Tanzania. | Kwa kuzingatia Muundo wa Muungano wa Serikali mbili. | |
| | | xxiii) Ibara hii isomeke mambo ya | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | Shirikisho na sio mambo ya Muungano. | | |
| | | xxiv) Mambo yote ya Muungano yaorodheshwe kwenye Ibara hii na siyo kwenye nyongeza | | |
| | | xxv) Tume ya Haki za Banadamu na utawala Bora na mipango ya uchumi, elimu, baraza la mitihani,maadili na miiko ya viongozi, utabiri wa haki ya hewa, usalama wa anga yawe mambo ya muungano | | |
| | | xxvi) Kuwe na usawa katika nafasi za ajira na uongozi kwa pande zote za Muungano. | | |
| | | xxvii) Mambo ya nje, polisi, usajili wa vyama vya siasa, ushuru wa bidhaa yasiwe mambo ya muungano | | |
| | | xxviii) Bunge la Jamhuri ya Muungano liwe jambo la muungano | | |
| | | xxix) Nchi washirika wawe na uwezo wa kuongeza au kupunguza mambo ya muungano | | |
| | | xxx) Jinsia iwe jambo la muungano | | |
| | | xxxi) Kuwe na kupokezana katika nafasi ya Urais baina ya washirika | | |
| | | xxxii) Mafuta na gesi visiwe mambo ya muungano | | |
| | | xxxiii) Usajili wa Vyama vya Siasa lisiwe suala la Muungano. | | |
| 61. | Washirika wa | (i) Ushuru wa bidhaa isiwe suala la | | 1. Ibara ya 61 inakuwa |

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Maoni* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| | Muungano | Muungano. | | Ibara ya 64 na inabaki kama ilivyo.<br>2. neno ''Tanzania Bara" lisomeke ''Tanganyika".<br>3. Mahali popote litakapotokea neno ''Washirika wa Muungano" lisomeke ''Nchi Washirika". |
| | | (ii) Mambo ya Muungano yawe kama ifuatavyo:<br>(h) Katiba ya Muungano wa Jamhuri za Tanzania.<br>(i) Mamlaka ya Jamhuri ya Muungano za Tanzania.<br>(j) Uratibu wa masuala ya Uraia na Uhamiaji.<br>(k) Uratibu wa Sera ya Mambo ya Nje.<br>(l) Uratibu wa mambo ya Usalama.<br>(m) Utumishi katika Serikali ya Jamhuri za Muungano za Tanzania.<br>(n) Mahakama ya Rufani ya Jamhuri za Muungano za Tanzania. | Kwa kuzingatia Muundo wa Muungano wa Serikali mbili. | |
| | | (iii) Ibara hii isomeke mambo ya Shirikisho na sio mambo ya Muungano. | | |
| | | (iv) Ibara ndogo ya (4) ibadilishwe na iandikwe kama ifuatavyo:<br>"(4) Washirika wa Muungano watatekeleza majukumu yao kwa kufuata masharti ya Katiba hii na Katiba zao". | | |
| | | (a) Katika ibara ya (5) itoe ufafanuzi wa neno "hadhi na haki sawa". | Kuondoa utata unaoweza kutokea. | |
| | | (vii) Ibara ndogo ya (4) na (5) zifutwe. | Kwa kuzingatia Muundo wa Muungano wa Serikali mbili. | |
| | | (vi) Maneno Serikali ya Tanzania Bara | | |

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Maoni* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| | | yabadilishwe na isomeke Serikali ya Jamhuri ya Muungano. | | |
| | | (vii) Neno Tanzania Bara lifutwe na badala yake lisomeke Tanganyika. | | |
| | | (viii) Ibara hii ibaki kama ilivyo. | Ili kukidhi muundo wa Serikali Tatu. | |
| | | (ix)Ibara ndogo ya (2) isomeke: Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itakuwa na mamlaka juu ya mambo yote yahusuyo Tanganyika na Zanzibar." | Ili kukidhi mfumo wa Serikali Moja. | |
| | | (x) Ibara ndogo ya (3) ifutwe. | Mfumo wa Serikali Moja. | |
| | | (xi) Ibara ndogo ya (5) Neno "Washirika" lifutwe na badala yake isomeke "wananchi". | | |
| | | (ix) Ibara ndogo ya (5) irekebishwe kwa kuongeza neno "haki sawa". | Ili ilingane na wingi wa watu. | |
| | | (xiii)Maneno hadhi na haki sawa yafafanuliwe. | | |
| | | (xiv)Usawa uwe kwa mambo yote | | |
| | | (xvi)Marginal note isomeke" mamlaka ya serikali ya muungano na serikali ya Zanzibar". | | |
| | | (xv)Ibara ya 61(4)(5) ziondolewe | | |
| | | 61(4) itumie maneno "kwa mujibu" badala ya "kwa kuzingatia' | | |
| | | (xvi)Neno usawa litumike badala ya uwiano | | |
| | | (xvii)Washirika wawe na kura ya turufu kulinda maslahi yao. | | |
| | | (xviii) Maneno Serikali ya Tanzania Bara yabadilishwe na isomeke Serikali ya Jamhuri ya Muungano. | | |
| | | (xix)Ibara hii ibaki kama ilivyo. | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | (xx)Ibara ndogo ya (2) isomeke: Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itakuwa na mamlaka juu ya mambo yote yahusuyo Tanganyika na Zanzibar.” | | |
| | | (xxi)Ibara ndogo ya (3) ifutwe. | | |
| | | (xxii)Ibara ndogo ya (5) Neno “Washirika” lifutwe na badala yake isomeke “wananchi”. | | |
| | | (xxiii)Ibara ndogo ya (5) irekebishwe kwa kuongeza neno “haki sawa”.<br>(xxiii) Iongezwe Ibara ndogo itakayoruhusu mshirika wa Muungano kuweza kujiondoa katika Muungano na inayoruhusu nchi nyengine kuweza kujiunga na Muungano. | | |
| 62. | Mamlaka ya Washirika wa Muungano | (i) Ibara hii ifutwe. | Kuruhusu nchi washirika kuingia mahusiano na taasisi za nje ni kukiuka Hati ya Muungano ianayotamka kuwa mambo ya nje ni ya Muungano. | 1. Ibara ya 62 inakuwa ya 65.<br>2. Iongezwe ibara ndogo ya 4 itakayoelekeza Bunge kutunga sheria itakayoainisha, pamoja na mambo mengine, “utaratibu wa namna ya utekelezaji bora wa masharti ya Ibara hii”. |
| | | (ii) Ibara hii irekebishwe ili nchi washirika ziwe na mamlaka kamili katika kuanzisha mahusiano na nchi za nje. | Hati za kisheria (Legal Instruments), ndizo zinazoanzisha jumuiya, taasisi na mashirika ya kimataifa ndizo zinazoweka sharti za nchi kuwa na Mamlaka kamili | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | (sovereign states) ili kuweza kukubalika kuwa mwanachama. | |
| | | (iii) Ibara hii irekebishwe kukidhi Muungano wa Serikali mbili na kutoa uwezo kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kujiunga na jumuiya za kimataifa. Hivyo maneno "kila Mshirika wa Muungano" yafutwe na badala yake yawekwe maneno "Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar." | Hii ni njia mojawapo ya kuondosha kero za Muungano katika muundo wa sasa wa Muungano. | |
| | | (iv) katika ibara ndogo ya (1) neno "mshirika" lifutwe na badala yake kiandikwe "Jamhuri ya Muungano". | | |
| | | (v) Ibara ndogo ya (2) irekebishwe ili kuruhusu Washirika waruhusiwe kujiunga au kupata "observer status" katika mashirika au jumuiya za kimataifa. | Kwa kuwa Ushirikiano wa Kimataifa si suala la Muungano. | |
| | | (vi) katika Ibara ndogo ya (2) maneno "kwa mujibu wa Katiba ya Mshirika wa Muungano" yafutwe. | Hayana athari yoyote. | |
| | | (vii) Aya ya (f) katika ibara ndogo ya (2) ibadilishwe na iandikwe kama ifuavyo:<br>"(f) kuwapandisha vyeo na kutoa kamisheni kwa maafisa wa vyombo vya ulinzi na usalama katika ngazi mbalimbali". | Katika kuunganisha sera za ndani, sera za kigeni na sera za kijeshi kuhusiana na usalama wa Taifa ili kuwezesha Taasisi za ulinzi na Usalama kushirikiana kikamilifu. | |
| | | (viii) Katika Ibara ndogo ya (3) maneno "inaweza kutoa" yafutwe na badala yake iandikwe "itatoa". | Ili kuilazimisha Serikali ya Muungano kutoa msaada pale unapohitajika. | |
| | | (ix) ibara ndogo ya (2) na (3) zifutwe. | (a) Kwa sababu inaeleza | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | masuala ya mambo ya nje, ambayo kwa mujibu wa katiba hii mambo ya nje ni mambo ya Muungano hivyo kutekelezwa kwa Ibara hizi ndogo ni utata hasa ikizingatiwa masilahi ya nchi washirika katika mashirikiano na nchi za nje. Tunatambua ushiriki wa nchi washirika kwa jumuiya za kimataifa kwa mambo yasio ya muungano ni za msingi lakini yatekelezwe na Jamhuri ya Muungano kwa kulinda umoja wetu.<br>(b) Kuondoa dhana ya uwepo wa Washirika wa Muungano.<br>(c) Zitaleta kero katika Muungano. | |
| | | (x) Maneno Serikali ya Zanzibar isomeke Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. | Kuondoa mgongano katika Bunge la Jamhuri ya Muungano kati ya Tanzania Bara na Zanzibar. | |
| | | (xi) Ibara ndogo ya (2) irekebishwe kwa kuongeza maneno yafuatayo | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | mwisho wa sentensi: "Ilimradi mambo hayo hayataingilia au kuleta athari kisiasa, kiuchumi, kijamii na kidemokrasia katika nchi Mshiriki wa Muungano na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania." | | |
| | | (xii) Ibara hii ibaki kama ilivyo. | Ili kukidhi muundo wa Serikali Tatu. | |
| | | (xiii) Ibara ndogo ya (3)(a) ifutwe. | (a) Inapingana na nyongeza ya Rasimu.<br>(b) Mahusiano ya Kimataifa ni jambo la Muungano. | |
| | | (xiv) Mabalozi wathibitishwe na Bunge | | |
| | | (xv) Ifanyiwe marekebisho kuendana na mfumo wa serikali mbili | | |
| | | (xvi) Washirika wawe na uwezo wa kushiriki katika mambo ya kimataifa | | |
| | | (xvii) Ibara ya 62(2) iwe "Bila ya kuathiri mipaka iliyowekwa na Katiba hii, kila Mshirika wa Muungano atakuwa na uwezo na uhuru wa kuanzisha mahusiano au ushirikiano na jumuiya au taasisi yoyote ya kikanda au kimataifa kwa mambo yaliyo chini ya mamlaka yake kwa mujibu wa Katiba ya Mshirika wa Muungano". | | |
| | | (xviii) 62(3) ishurutishe Jamhuri ya Muungano kukubali mashirikiano na washirika wa Muungano | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| | | (xix) Kuwe na nafasi sawa za ubalozi | | |
| | | (xx) Washirika wa muungano wasiruhusiwe kuruhusu ndoa za jinsia moja | | |
| | | (xxi) Kila mshirika awe na uwakilishi wake katika asasi za kimataifa. | | |
| | | (xxii) Kwenye 61(2), maneno 'yahusuyo Tanzania Bara' yaondolewe na iwe 'yahusuyo nchi yao' | | |
| | | (xxiii) 62(2) na (3) zifutwe | | |
| | | (xxiv) 62(1) neno 'pande' liondolewe na neno 'nchi' litumike | | |
| | | (xxv) 62(2)maneno ya mwisho yanayosomeka "kwa mujibu wa Katiba ya Mshirika wa Muungano" yaondoshwe. | | |
| | | (xxvi) Mamlaka ya kuingia katika mahusiano ya kikanda na ya kimataifa yawe katika Jamhuri ya Muungano. | | |
| | | (xxvii) Katika yale yasiyo ya muungano, washirika watatakiwa kushauriana, kupitia kuwasiliana au kwa ruhusa ya Serikali ya Muungano kwa sababu kwa mujibu wa sheria za kimataifa uwezo wa kuingia mikataba na nchi au taasisi za kimataifa ni moja ya uwezo wa dola huru (sovereign state as an international | | |

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Maoni* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| | | personality). | | |
| 63. | Mahusiano kati ya Washirika wa Muungano | (i) Katika ibara ndogo ya (2) neno “wanaweza” lifutwe na badala yake iandikwe “lazima”. | | 1. Ibara ya 63 inakuwa Ibara ya 66 na inabaki kama ilivyo<br>2. neno ‘’Tanzania Bara” lisomeke ‘’Tanganyika”<br>3. neno ‘’Washirika wa Muungano” lisomeke ‘’Nchi Washirika”. |
| | | (ii) Iongezwe ibara ndogo mpya itakayoainisha maeneo ya mashirikiano baina ya Serikali za Washirika. | | |
| | | (iii) Iongezwe Ibara ndogo mpya itakayotambua utekelezaji wa Sheria zinazotumika upande mmoja wa Muungano kutambulika na mshirika mwingine wa Muungano. | | |
| | | (i) Ibara hii ifutwe. | | |
| | | (ii) Ibara hii ibaki kama ilivyo, lakini kwa mfumo wa Serikali Mbili. | | |
| | | (iii) Ibara hii ibaki kama ilivyo. | | |
| | | Kuwe na mashauriano katika maeneo ya ushirikiano | | |
| | | Ushirikiano baina ya washirika uwe wa lazima | | |
| | | Neno ‘inaweza’ kwenye ibara ndogo ya 3 liwe’inawajibika’ | | |
| | | Serikali ya Muungano na Serikali Shiriki zote ziwe zinahusishwa katika mashauriano yanayohusu maeneo ya ushirikiano. | | |
| 64. | Mawaziri Wakaazi | (i) ibara hii ifutwe. | | 1. Ibara ya 64 inakuwa Ibara ya 67 na inabaki kama ilivyo.<br>2. Neno ‘’Tanzania Bara” lisomeke ‘’Tanganyika” na, |
| | | (ii) Ibara hii ibaki kama ilivyo. | | |
| | | (iii) Ibara hii irekebishwe ili kuainisha kazi za Mawaziri Wakaazi. | | |
| | | (iv) Ibara ndogo ya (2) ifutwe na badala yake iandikwe kama ifuatavyo: | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | "(2) Mawaziri Wakaazi watakuwa na ofisi katika nchi Washirika, Waziri Mkaazi wa Zanzibar ofisi yake itakuwa Tanganyika na Waziri Mkaazi wa Tanganyika ofisi yake itakuwa Zanzibar kwa ajili ya kukuza na kuendeleza mahusiano". | | 3. neno ''Washirika wa Muungano" lisomeke ''Nchi Washirika". |
| | | (v) Ibara ndogo ya (3)(a) ibadilishwe na iandikwe kama ifuatavyo:<br>(a) kushughulikia mambo yasiyo ya Muungano yanayohusu ushirikiano na mahusiano baina ya nchi washirika kimataifa". | | |
| | | (vi) Ibara hii ibaki kama ilivyo. | | |
| | | (vii) Mawaziri Wakaazi wasiwepo. | | |
| | | (viii) Mawaziri Wakaazi wawe na ofisi katika nchi za Washirika. | | |
| | | (ix) Mawaziri Wakaazi walipwe na Serikali zao. | | |
| | | (x) (v) Majukumu yao yabainishwe | | |
| | | (xi) Wasiwepo | | |
| | | (xii) Waitwe mawaziri wanaoshughulikia mambo ya muungano. | | |
| | | (xiii) Ibara ndogo ya (3)(a) ibadilishwe na iandikwe kama ifuatavyo:<br>(b) kushughulikia mambo yasiyo ya Muungano yanayohusu ushirikiano na mahusiano baina ya nchi washirika kimataifa". | | |
| | | (xiv) Ibara hii ibaki kama ilivyo. | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| 65. | Mamlaka ya wananchi | (i) ibara hii ibaki kama ilivyo. | | |
| | | (ii) ibara hii ifutwe na badala yake iandikwe kama ilivyo Sura ya Nane ya Katiba ya sasa. | | |
| | | (iii) Maelezo ya pembeni yabadilishwe na yasomeke kama ifuatavyo: "Mamlaka ya Wananchi juu ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa". | | |
| | | (iv) Ibara hii ifutwe. | | |
| | | (v) Inapendekezwa maneno "Tanzania Bara" yafutwe na badala yake yasomeke "Serikali ya Jamhuri ya Muungano." | | |
| | | (vi) katika Ibara ndogo ya (1) iishie katika neno "Katiba hii". | | |
| | | (vii) katika ibara ndogo ya (2) neno "Washirika" lifutwe na badala yake liandikwe neno "Jamhuri". | | |
| | | (viii) ibara ndogo ya (2) irekebishwe na isomeke kama ifuatavyo: "(2) Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itawajibika kugatua madaraka kwa serikali za Mitaa zitakazoanzishwa kwa mujibu wa Katiba hii." | | |
| | | (ix) Inapendekezwa kuwe na Sura nzima ya Serikali za Mitaa itakayoainisha mambo yafuatayo:<br>(a) Uanzishaji na mamlaka, aina mipaka na Muundo wa serikali za mitaa;<br>(b) Haki na uhalali wa Mamlaka za wananchi; | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | (c) Misingi na Malengo/Madhumuni ya serikali za Mitaa;<br>(d) Kazi na Majukumu ya Serikali za Mitaa;<br>(e) Uhuru wa Kujiamulia mambo yake kutegemeana na mazingira yake;<br>(f) Mahusiana baina ya serikali kuu na serikali za mitaa;<br>(g) Uchaguzi wa viongozi wa Serikali za Mitaa<br>(h) Utumishi katika Serikali za mitaa;<br>(x) Uwepo wa chombo cha wawakilishi cha Serikali za Mitaa kama ilivyo Katiba ya Afrika ya Kusini. | | |
| | | (xi) Ibara ibaki kama ilivyo. | | |
| | | (xii) Neno kugatua litolewe tafsiri. | | |
| | | (xiii) Ibara ndogo ya (1) isomeke "Serikali ya Shirikisho itapata madaraka kutoka Serikali za Washirika". | | |
| | | (xiv) Ibara hii ifutwe. | | |
| | | (xv) Irekebishwe kwa kufuta neno Tanzania Bara na badala yake isomeke Tanganyika. | | |
| | | (xvi) Iwe kama ilivyo Sura ya nane ya Katiba ya sasa | | |
| | | (xvii) Kusiwe na mgombea binafsi | | |
| | | (xviii) Maneno "Tanzania Bara" yaondolewe na badala yake yasomeke "Serikali ya Jamhuri ya Muungano." | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | (xix) Ibara ya 65(2) iboreshwe kuweka mfumo imara wa serikali za mitaa na dhana nzima ya ugatuaji wa madaraka. | | |
| | | (xx) Masuala ya serikali za mitaa yaachwe kwenye katiba za washirika | | |
| | | (xxi) "… kupitia uchaguzi huru, wa haki na kidemokrasia…." | | |
| | | (xxii) 65. (2) Mwishoni mwa Ibara hii ndogo yaongezwe maneno:<br>(xxiii) i) "Ilimradi serikali za mitaa zitapewa na kuwa na mamlaka kamili juu ya mambo ndani ya maeneo yao yaliyokasimiwa kwa serikali za mitaa kwa mujibu wa Katiba na sheria za Washirika na kuwezeshwa kifedha ipasavyo na Serikali Kuu za Washirika." | | |
| 66. | Wajibu wa kulinda Muungano | Ibara hii ifutwe na badala yake iandikwe kama ilivyo Ibara ya 46B ya Katiba ya sasa. | | Ibara ya 66 inakuwa Ibara ya 69 na inabaki kama. |
| | | (i) katika ibara ndogo ya (1) maneno "Washirika wa Muungano" yafutwe na badala yake yasomeke "Katiba ya Zanzibar". | | |
| | | (ii) Katika Ibara ndogo ya (3)(c) maneno "Rais wa Tanzania Bara" yafutwe na badala yake yawekwe maneno "Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano". | Marekebisho haya yanazingatia mapendekezo ya kuendelea kuwepo kwa nafasi ya Waziri Mkuu ambaye ni kiongozi wa shughuli za Serikali Bungeni. | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | (iii) Ibara ndogo ya (3) ifutwe na badala yake iandikwe kama ifuatavyo:<br>"(3) Viongozi Wakuu wanaohusika na masharti ya Ibara hii ni:<br>(a) Rais wa Jamhuri ya Muungano;<br>(b) Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano;<br>(c) Waziri Mkuu wa Tanganyika;<br>(d) Waziri Mkuu wa Zanzibar". | Nchi Washirika ziongozwe na Mawaziri Wakuu ili kuondoa urudiaji wa kuwepo kwa viongozi wengi kwa jina la Rais. | |
| | | (iv) katika Ibara ndogo ya (1) maneno "Washirika wa Muungano" yafutwe na badala yake yasomeke "Katiba ya Zanzibar". | | |
| | | (v) Katika Ibara ndogo ya (3)(c) maneno "Rais wa Tanzania Bara" yafutwe na badala yake yawekwe maneno "Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano". | | |
| | | (vi) Ibara ndogo ya (3) ifutwe na badala yake iandikwe kama ifuatavyo:<br>"(3) Viongozi Wakuu wanaohusika na masharti ya Ibara hii ni:<br>(e) Rais wa Jamhuri ya Muungano;<br>(f) Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano;<br>(g) Waziri Mkuu wa Tanganyika;<br>(h) Waziri Mkuu wa Zanzibar". | | |
| | | (vii) Ibara ndogo ya (3) aya (c) ifutwe. | | |
| | | (viii) Ibara hii ieleze kuwa wajibu wa kulinda Muungano ni wa Watanzania wote na viongozi | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | wanabaki na dhamana tu. | | |
| | | (ix) Aya (b) ya ibara ndogo ya (3) isomeke "Waziri Mkuu". | Serikali za Washirika zitaongozwa na Makamu wa Rais. | |
| | | (x) Iongezwe ibara ndogo mpya ya (4) itakayomwajibisha kiongozi atakayekiuka masharti ya Katiba. | | |
| | | (xi) Ibara hii ifutwe. | Ili kupunguza gharama. | |
| | | (xii) Katika ibara ndogo ya (1) yaongezwe maneno "wa nchi Washirika" baada ya neno "raia" na pia baada ya neno "Muungano" yaongezwe maneno "pale ambapo wananchi wanaridhika na Muungano". | | |
| | | (xiii) Ibara ndogo ya (1) yaongezwe maneno "pale patakapokuwa na maslahi". | (a) Kuonesha kuwa Muungano ni jambo la hiari.<br>(b) Nchi nyingine ziweze kuvutika kuweza kujiunga katika Muungano wetu. | |
| | | (xiv) Ibara ndogo ya (2) neno "Muungano" lifutwe na badala yake isomeke "umoja". | Kulinda umoja ni kulinda Muungano. | |
| | | (xv) Ibara hii irekebishwe ili kuwepo na Rais wa Tanzania, Rais wa Zanzibar na Rais wa Tanganyika. | | |
| | | (xvi) Maneno "Washirika wa Muungano, Viongozi Wakuu na Rais wa Tanzania Bara" yafutwe. | | |
| | | (xvii) Ibara hii ifutwe. | (a) Uwepo wa Marais watatu wataongeza gharama.<br>(b) Katiba itatetea | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | maslahi ya wakubwa. | |
| | | (xviii) Maneno "Rais wa Tanzania Bara" yasomeke "Rais wa Tanganyika". | | |
| | | (xix) Ibara ibadilishwe kwa kuweka Mawaziri Wakuu katika nchi Washirika badala ya Marais. | | |
| | | (xx) Ibara ndogo ya (3)(b) isomeke Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano. | Ili kuendana na mfumo wa Serikali Mbili. | |
| | | (xxi) Ibara ndogo (3)(a) na (b) zifutwe. | Kupunguza matumizi makubwa ya fedha. | |
| | | (xxii) Ibara ndogo ya (3) irekebishwe ili wajibu wa kulinda Muungano isiwe kwa viongozi tu, bali iwe mpaka kwa raia wa kawaida. | | |
| | | (xxiii) Itumike Ibara 46B ya Katiba ya sasa | | |
| | | (xxiv) b) Ibara 66(3) iwe<br>(xxv) Rais wa Jamhuri ya Muungano<br>(xxvi) Waziri mkuu wa Jamhuri ya Muungano<br>(xxvii) Waziri Mkuu wa serikali ya Tanganyika<br>(xxviii) Waziri mkuu wa serikali ya Zanzibar. | | |
| | | (xxix) Maneno, "Katiba za Washirika wa Muungano" yasomeke, "Katiba ya Zanzibar." | | |
| | | (xxx) Maneno, "Rais wa Tanzania Bara," yasomeke, "Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano." | | |
| | | (xxxi) Viongozi wakuu wa washirika waitwe Mawaziri Wakuu. | | |
| | | (xxxii) Marais wa washirika waape | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | kwa katiba zao | | |
| | | (xxxiii) iongezwe Ibara ndogo ya 66.(4) yenye maneno yafuatayo au kama hayo: "Kwa madhumuni ya kutekeleza kwa njia bora na muafaka maelekezo ya Ibara ndogo ya (3), Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania litatunga sheria kwa ajili hiyo." | | |
| | | (xxxiv) Marais wa nchi washirika wasifungwe kuutetea muungano | | |
| | | (xxxv) Viongozi wa serikali washirika wa muungano wawe na nyadhifa (titles) nyingine, mfano Gavana wa Tanganyika na Gavana wa Zanzibar au Waziri Mkuu wa Tanganyika na Waziri Mkuu wa Zanzibar | | |

# SURA YA SABA YA RASIMU

## 7.0 SEHEMU YA KWANZA: SERIKALI, RAIS NA MAKAMU WA RAIS

### (a) Serikali

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| 67. | Serikali ya Jamhuri ya Muungano | (i) Marginal notes isomeke "Serikali ya Jamhuri ya Muungano za Tanzania". | | 1. Ibara ya 67 inakuwa Ibara ya 70.<br>2. Ibara ndogo ya 2, imerekebishwa na inasomeka ''Mamlaka ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yatahusu utekelezaji na hifadhi ya Katiba hii na pia mambo mengine ambayo yameainishwa katika sheria za nchi." |
| | | (ii) Ibara ndogo ya (2) ibadilishwe kwa kuongeza kazi ya kushughulikia mambo yasiyo ya Muungano yanayohusu Tanzania Bara.<br>(iii) Ibara ndogo ya (3), na (5) zibaki kama zilivyo.<br>(iv) Ibara ndogo ya (4) Neno "wengine" lifutwe, | | |
| | | (v) 67(3) .Mwishoni mwa ibara isomeke"….yameainishwa katika sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania" | | |
| | | (vi) Ibara ndogo ya (3), na (5) zibaki kama zilivyo. | | |
| | | (vii) Katika Ibara ndogo ya (3) yaongezwe maneno "zitakazotungwa Kwa mujibu wa Sheria" mwishoni mwa ibara hii. | | |
| | | (viii) Ibara ndogo ya (4) Neno "wengine" lifutwe, yaongezwe maneno "zitakazotungwa kwa mujibu | Maneno "watu wengine" yameleta dhana kuwa Rais anaweza kukasimu madaraka yake kwa mtu | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | wa Sheria" mwishoni mwa ibara hii. | yeyote. | |
| | | (ix) 67(4).Maneno"Watu wengine wenye Madaraka" yaondolewe | Ibara ya 73(b-c) tayari zimeshaainisha. | |
| | | (x) katika ibara hii, Katiba iweke msingi wa usawa katika maamuzi na uendeshaji wa vyombo vya Muungano kama vile:<br>(a) nafasi ya Rais wa Muungano;<br>(b) Baraza la Mawaziri wa Serikali ya Muungano;<br>(c) Bunge la Muungano na uongozi wake;<br>(d) Mahakama za Muungano; na<br>(e) vyombo vyengine vya Muungano. | Katiba haikuweka wazi uendeshaji wa vyombo vya Muungano, ingawa inatambua kuwepo kwa washirika wa Muungano. | |
| | | (xi) 67(6) Iongezwe na isomeke "Rais achague viongozi wote wa Serikali ya Muungano kwa hadhi ya kinchi na usawa bila ya kujali ukubwa au udogo wa nchi husika" | Kifungu hiki kitaipa usawa na hadhi Jamhuri ya Muungano wa Tanzania | |

## (b) Rais

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| 68. | Rais wa Jamhuri ya Muungano | (i) Ibara hii irekebishwe Ili iwe na masharti ya kuweka utaratibu wa kupokezana Urais baina ya Tanganyika na Zanzibar. | Kutokana na udogo wa Zanzibar upo uwezekano wa kukaa kwa muda mrefu bila kutoa Rais.<br>Ili kuweka usawa baina ya | Ibara ya 68 inakuwa ya 71 na inabaki kama ilivyo. |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | washirika wa muungano. | |
| | | (ii) Katika Ibara ndogo ya (2) yaongezwe maneno " wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama" baina ya maneno "Mkuu" na "na". | | |
| | | (iii) Iongezwe aya mpya (a) katika ibara ndogo ya (2) itakayoeleza jukumu la Rais kusimamia na kulinda Katiba. | | |
| | | (iv) Iongezwe ibara ndogo mpya ya (3) itakayosema kama ifuatavyo: "(3) Rais atatekeleza majukumu yake kama ilivyoainishwa na Katiba hii na sheria nyingine zitakazotungwa na Bunge". | | |
| | | (v) Neno "nchi" libadilishwe liandikwe "Shirikisho". | | |
| 69. | Madaraka na majukumu ya Rais | (i) Ibara hii ifutwe. | (a) Viongozi walioainishwa katika Ibara hii tayari kuna vifungu vinavyohusu uteuzi wao;<br>(b) Kuna sheria ambayo inaeleza jinsi uteuzi utakavyokuwa;<br>(c) Kuepuka kuacha viongozi wengine ambao Rais ana jukumu la kuwateua. | 1. Ibara ya 69 inakuwa Ibara ya 72<br>2. Ibara ya 72(3)(d) imefanyiwa marekebisho kwa kuongezwa maneno ''na Naibu Makatibu Wakuu" mwisho wa Sentensi.<br><br>3. Ibara ndogo ya 72(3)(e) maneno ''Naibu Mwanasheria Mkuu yamefutwa" |
| | | (ii) 69(1) ibaki kama ilivyo kwa Rais kuendelea kuwa Mkuu wa Nchi (Head of State). | Inajitosheleza. | |

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Maoni* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| | | (iii) 69(2) b,c,d,e,Katiba itamke wazi kuwa atashauriana na Rais wa Zanzibar na Rais wa Tanganyika. | | 4. Ibara ndogo ya 72(3)(f) yameongezwa maneno "Wenyeviti, Makamu Wenyeviti, na Wajumbe" mbele ya neno kuwateua.<br><br>5. Iongezwe ibara ndogo ya 5 itakayompa Rais mamlaka ya kutenda majukumu mengine ya asili ya Mkuu wa nchi, Amiri Jeshi Mkuu na Kiongozi wa Serikali yanayoweza kutokea. |
| | | (iv) 69-Iongezwe Ibara ndogo ya (5) ambayo itaeleza kuwa licha ya majukumu ya Rais yaliyoainishwa katika ibara ndogo za (1), (2) na (3), Rais atakuwa na mamlaka ya kutekeleza majukumu mengine ya asili ya Mkuu wa Nchi, Amiri Jeshi Mkuu na Kiongozi wa Serikali ambayo hayakuainishwa katika Ibara hii na ambayo hayakiuki Katiba wala sheria za nchi. | Ibara ya 69(1), (2) na (3) inaweza kuacha baadhi ya majukumu ya Rais kama Mkuu wa Nchi, Amiri Jeshi Mkuu na Kiongozi wa Serikali. | |
| | | (v) Ibara hii ifutwe na badala yake iandikwe kama ilivyo Katiba ya sasa. | | |
| | | (vi) Ibara hii irekebishwe ili kutoa nafasi kwa Rais katika kuongoza masuala ya uchumi na fedha kama Mwenyekiti wa Baraza la Mawaziri haionekani. Madaraka hayo yaongezwe ikiwemo:kuteua Wakuu wa Mikoa; na Kuwasilisha Bungeni taarifa za Mpango wa Muda Mrefu na Muda Mfupi. | | |
| | | (vii) Katika Ibara ndogo ya (1)(a) ifutwe na badala yake iandikwe kama ifuatavyo:<br>(viii) "(a) kuheshimu Katiba ya Jamhuri ya Muungano na Katiba za Nchi Washirika"; | | |
| | | (ix) Aya (h) ya Ibara ndogo ya (1) ibadilishwe na iandikwe kama ifuatavyo: | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
| --- | --- | --- | --- | --- |
| | | (x) "(h) kuteua Mabalozi, Watu watakaoiwakilisha Tanzania nje ya nchi na wawakilishi wa nchi katika taasisi mbalimbali za kimataifa akishirikiana na vyombo husika kwa kuzingatia sifa maalum kwa mujibu wa sheria"; | | |
| | | (xi) 69(1)Vifungu vidogo (h),(i)na(j) vifutwe. | Mambo yaliyotajwa yatafanywa na Marais husika. | |
| | | (xii)(x)Aya ya (k) ya ibara ndogo ya (1) inapendekezwa ifutwe. | Adhabu ya kifo ni kinyume na haki za binadamu. | |
| | | (xiii) (xi)Aya (f) ya ibara ndogo ya (2) irekebishwe na isomeke kama ifuatavyo:-<br>(xiv) "(f) Kuwapandisha vyeo na kutoa kamisheni kwa maafisa wa vyombo vya ulinzi na usalama katika ngazi mbalimbali". | | |
| | | (xv) Ibara ndogo ya (3) irekebishwe ili Rais apewe madaraka ya kuteua Wakuu wa Mikoa na Wilaya. | (a) Wakuu wa Mikoa na Wilaya ni wawakilishi wa Rais katika maeneo yao;<br>(b) Wanasimamia shughuli za Ulinzi na usalama katika maeneo yao; | |
| | | (xvi) Katika Ibara ndogo ya (3) aya ya (c) maneno "Naibu Mawaziri" yafutwe. | Masuala ya Muungano si mengi na pia itasaidia kupunguza gharama za uendeshaji wa Serikali. | |
| | | (xvii) Katika Ibara ndogo ya (3) aya (e) maneno "na Naibu Mwanasheria Mkuu" yafutwe. | Hakuna nafasi ya Naibu Mwanasheria Mkuu. | |

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Maoni* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| | | (xviii) Iongezwe Ibara ndogo ya (4) itakayoeleza kama ifuatavyo:<br>(xix) "(4) Itakuwa ni marufuku kwa viongozi wa umma kutumia ofisi za umma au mali za umma kwa shughuli na faida ya vyama vya siasa au kwa masuala binafsi". | Ili kuzuia viongozi kutumia nafasi za uongozi kwa maslahi ya vyama vyao au maslahi binafsi. | |
| | | (xx) Ibara ndogo ya (4) ifutwe. | Katika mfumo wanachi yetu mara nyingi wenyeviti wa vyama vya siasa ndiyo wamekuwa wagombea Urais, hivyo wanaweza kuonekana kama wanajinasibisha kwa namna inayokiuka kifungu hiki. | |
| | | (xxi) 69(4) ibaki kama ilivyo. | Ili kuendana na masharti ya Ibara ya 68(2) inayompa Rais dhamana ya kukuza na kuhifadhi umoja wa kitaifa. | |
| 70. | Utekelezaji wa madaraka ya Rais | (i) Ibara za 70, 71, 72, 73 na 74 ziwe kama ilivyo katika Sura ya Pili, Sehemu ya Kwanza ya Katiba ya sasa. | | Ibara ya 70 itakuwa ya 73. Inabaki kama ilivyo |
| | | (ii) 70 ibaki ilivyo. | Inajitosheleza. | |
| | | (iii) Ibara hii ifutwe. | (a)Ibara hii inaondoa uwajibikaji wa Rais wa moja kwa moja kwa maamuzi anayoyafanya. Akilazimika kufuata ushauri hataweza kuwajibishwa au kuwajibika kwa maamuzi yake; | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | (b)Ibara ya 70(1) na (2) zinakinzana kwani Ibara ndogo (1) inamlazimisha Rais kufuata na kuzingatia ushauri atakaopewa ilhali Ibara ndogo (2) inasema Rais halazimiki kufuata ushauri. | |
| | | (iv)70(2)Kuweko na Tume maalum itakayowekwa kwa ajili ya kuteua viongozi wa juu wa umma ambao watafanyiwa usaili.Rais awe na majukumu ya kuwaapisha viongozi tu. | Ili kuleta ufanisi kazini,kuzuia upendeleo,kupata viongozi wenye vigezo na sifa stahiki na iwe rahisi kwa Rais kuwaadhibu watendaji wake inapobidi | |
| | | (v)Ibara ndogo ya (1) irekebishwe ili nafasi katika utumishi ziwe zinapatikana kwa ushindani na usaili. | Rais asiteue watu kushika nafasi za madaraka katika utumishi | |
| | | (vi)70(3).Viongozi wa ngazi hizi ni muhimu wakapatikana kwa njia ya ushindani na uwazi isiyotia shaka kuhusu uwezo wao. | Kuweka kipengele cha kumshauri Rais haisaidii na wala haijasaidia hadi leo. | |
| | | (vii)Ibara ndogo ya (3) ibadilishwe kwa kufuta neno "Mahakama" na badala yake iandikwe "Tume ya Utumishi ya Mahakama". | Mahakama haitoi ushauri ni chombo cha mwisho katika utoaji haki. Tume ya Utumishi wa Mahakama ndiyo yenye mamlaka ya kumshauri Rais kuhusu uteuzi katika mhimili wa Mahakama. | |
| 71. | Rais kuzingatia ushauri | (i) Ibara ndogo ya (1) ifutwe. | Rais asilazimishwe kufuata ushauri. | 1. Ibara ya 71 inakuwa ibara ya 74. |
| | | (ii)71(2)isomeke "kwa madhumuni ya | itawachanganya wasomaji | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | ibara ndogo ya kwanza(1) Rais hatalazimika kuufata ushauri aliopewa ambao unakwenda kinyume au kukiuka masharti ya katiba. | | 2. Kuwe na ibara ndogo itakayo elekeza kuwa "Rais hatalazimika kufuata ushauri aliopewa ambao unakwenda kinyume au kukiuka masharti ya Katiba hii na sheria za nchi". |
| | | (iii) 71(2).Ibara iongezwe maneno"Rais anapoamua kutofuata ushauri ni sawa,lakini analazimika kutoa sababu,na asifanye maamuzi yake binafsi,isipokuwa arudishe mchakato wa zoezi zima na uanze upya kwa kushirikisha chombo husika pamoja na kufuata utaratibu uliowekwa kulingana na miiko ya maadili ya uongozi wa nchi." | | |
| 72. | Rais kushindwa kumudu majukumu yake | 72-Ibara ya 72(5) na (6) iwe Ibara mpya ya 72A (1) na (2) ambapo Ibara ya 72A itakuwa na *"marginal note"* itakayosomeka "Utaratibu wa kujaza nafasi ya Rais kabla hajamaliza muda wake". | Ibara ya 72(5) ni suala mahsusi linalohusisha utaratibu wa kujaza nafasi ya Rais ambaye hajamaliza muda wake kwa sababu mbalimbali. | Ibara ya 72 inakuwa 75 na inabaki kama ilivyo. |
| | | (ii)Makamu wa Rais hakuchaguliwa kama Rais bali alichaguliwa kama mgombea mwenza wa Rais. | | |
| | | (iii) 72(6) (a na b).Rais aliyetokana na aina yoyote ya Mgombea ashauriane na Baraza la Ulinzi na Usalama la Taifa na sio Chama chake cha siasa anachotoka. | | |
| | | (iv) Kuendana na mapendekezo yaliyotolewa katika ibara ya 66(3). | | |
| | | | | Imeongezwa Ibara mpya ya 76 itakayozungumzia |

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Maoni* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| | | | | "utaratibu wa kujaza nafasi ya Rais kabla hajamaliza muda wake". |
| 73. | Utekelezaji wa majukumu ya Rais akiwa hayupo | (i) Inapendekezwa kuongezwa Ibara mpya mara baada ya Ibara ya 73, ambayo itazungumzia uanzishwaji wa chombo maalumu cha kumsaidia Rais katika masuala ya ushauri katika utekelezaji wa majukumu yake ya utendaji ya kila siku, *(The Constitutional Committee).* | Kwa nchi changa kama yetu na kwa kuzingatia uzoefu uliojitokeza siku za nyuma ni vema Kamati au Chombo Maalumu cha Kikatiba *(The Constitutional Committee)* kikawepo ili kumpatia ushauri Rais kwenye masuala ya Kikatiba na chombo hiki kitamsaidia katika kumlinda ili asikiuke Katiba. Kwenye nchi za wenzetu vyombo vya namna hii vimekuwa vikijumuisha majaji, marais wastaafu na watu wenye heshima na uzalendo kwa Taifa lao. | Ibara ya 73 inakuwa ibara ya 77.<br>Inabaki kama ilivyo |
| | | (ii) Ibara ndogo ya (1) irekebishwe ili kuweka utaratibu kama Rais hayupo madarakani Marais wa Nchi Washirika ndio wakaimu nafasi ya Urais wa Muungano. | | |
| | | (iii) Aya (a) ya Ibara ndogo ya (3) isomeke kama ifuatavyo:<br>"(a) Raisi wa nchi mojawapo washirika". | Ili kutoa nafasi kwa Rais mmoja wapo wa Nchi Washirika kukaimu nafasi ya Urais wa Muungano pale itakapotokea Rais wa Muungano hayupo kazini. | |

### (c) Uchaguzi wa Rais

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Maoni* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| | | (iv) Iongezwe ibara ndogo ya (5) ambayo ieleze kama ifuatavyo: "(5) Endapo Rais hataweza kukasimu madaraka yake kwa hati maalum aliyosaini kutokana na sababu za kiafya itahesabika kuwa mtu anayekaimu nafasi hiyo kwa mujibu wa ibara ndogo ya (1) amekasimiwa". | Ibara hii haijazingatia hali ambayo Rais hataweza kuandika hati maalum, mfano amepatwa na ugonjwa wa ghafla. | |
| 74. | Uchaguzi wa Rais | (i) Iongezwe ibara ndogo mpya ya (2) itakayoeleza kwamba Urais wa Jamhuri ya Muungano utakuwa kwa kupokezana baina ya nchi washirika na kwamba endapo katika kipindi kimoja Rais wa Jamhuri ya Muungano atatoka upande mmoja wa muungano, basi kipindi kinachofuata, Rais atatoka upande mwingine wa Muungano. | (a)Tanganyika na Zanzibar ni nchi huru zenye hadhi sawa.<br>(b)Kutapunguza misuguano baina ya Tanganyika na Zanzibar.<br>(c)Kutafanya Zanzibar ijisikie kuwa sehemu ya Muungano. | Ibara ya 74 inakuwa 78<br>na Ibaki kama ilivyo |
| | | (ii) Urais usiwe wa kupokezana. | (a)Rais apatikane kwa sifa zake;<br>(b)Ikiwa Urais utakuwa wa kupokezana kuna hatari kwa Rais wa Tanzania kutoka dini moja kwa kipindi kirefu.<br>(c)Katika muundo wa Serikali tatu, kupokezana Urais kunaweza kudhoofisha kupatikana kwa Rais wa JMT kwani nchi washirika zitakuwa katika harakati za | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | kuwania kupata viongozi wake; | |
| | | (iii) Ibara ndogo ya (3) iunganishwe na Ibara ya 75(2). | Uandishi mzuri wa sheria unataka mambo yanayofanana yawekwe pamoja. | |
| 75. | Sifa za Rais | (i) Aya (c) ifutwe na badala yake iandikwe "wazazi wake wote wawili wawe ni raia wa kuzaliwa". | Kuepusha nchi kuongozwa nan a mtu ambaye anaweza kuwa na uaminifu kwa nchi aliyotoka mmoja wa wazazi wake. | 1. Ibara ya 75 inakuwa 79.<br>2. Ibara hii imerekebishwa kama ifuatavyo:<br>(i) Ibara ndogo ya (e),(k) na (l) zimefutwa.<br>(ii) Imeongezwa Ibara ndogo (i) ambayo itaainisha sifa za uadilifu.<br>(iii) Awe na sifa zilizoainishwa katika Ibara ya 125(2),(e),(g) na (h). |
| | | (ii) Aya (d) iandikwe kama ifuatavyo:<br>"(d) Wakati wa kugombea awe na umri usiopungua miaka arobaini na usiozidi miaka sabini na tano". | | |
| | | (iii) Aya (d) iandikwe kama ifuatavyo:<br>"(d) Wakati wa kugombea awe na umri usiopungua miaka arobaini na usiozidi miaka sabini na tano". | | |
| | | (iv) 75(d)-Umri wa kugombea Urais uanzie miaka 40 na ukomo wa umri wa kugombea uwe miaka 70. | Baada ya miaka 75 mtu anakuwa amechoka kimwili na hivyo hawezi kumudu mikiki mikiki ya Urais licha ya kuwa mtu huyo anakuwa na busara, hekima na ukomavu. | |
| | | (v) Aya (d) iandikwe kama ifuatavyo:<br>"(d) Wakati wa kugombea awe na umri usiopungua miaka thelathini na tano." | | |
| | | (vi) Aya (c) ifutwe na badala yake iandikwe kama ifuatavyo:<br>"(c) Wazazi wote wa Rais lazima wawe raia wa Jamhuri ya | (a) Ili kupata kiongozi mwenye uzalendo.<br>(b) Ili kuepuka nchi kuongozwa na Rais | |

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Maoni* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| | | Muungano wa Tanzania kwa kuzaliwa". | ambaye utii na uaminifu wake upo katika nchi mbili. | |
| | | (vii) Aya ya (e) ifutwe. | Kuruhusu mtu aliyetumikia Ubunge kwa vipindi vitatu kugombea Urais. | |
| | | (viii) Katika aya (e) yaongezwe maneno "isipokuwa masharti ya Ibara ya 117(2)(a)" mwisho wa sentensi. | Ili kumwezesha Mbunge aliyeshika awamu tatu za Ubunge kuwa na sifa ya kugombea urais. | |
| | | (ix) Aya ya (j) ibadilishwe na iandikwe kama ifuatavyo:<br>"(j) Mwenendo wake binafsi hautiliwi shaka na jamii kwa kuzingatia maadili ya Taifa letu". | | |
| | | (x) 75(f)-Neno "angalau" lifutwe. | | |
| | | (x)75(f) Ibara ifafanue "Elimu ya Chuo kikuu kinachotambulika na Mamlaka itakayoamua kama Shahada /Chuo husika kinatambulika. | Elimu haimo katika masuala ya Muungano | |
| | | (xi) 75(g) Ibara hii ifutwe. | (a)Haina mantiki,<br>(b)Chama kisipewe nafasi. | |
| | | (xii) 75(k)-Upo umuhimu wa kutoa ufafanuzi wa kosa la jinai linalohusu kukosa uaminifu. | Ili kuondoa utata wa tafsiri. | |
| | | (xiii)Aya (l) irekebishwe kwa kufuta maneno "miaka mitano" na badala yake kuweka maneno "maisha yake yote". | | |
| | | (xiv) 75(l) yaongezwe maelezo yatakayomtaka Mgombea kuwa na hati iliyotolewa na Mamlaka | Ili kudhihirisha kuwa amekuwa mlipa kodi mwadilifu kila mwaka kwa | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | ya kodi. | miaka mitano mfululizo | |
| | | (xv) Aya (l) irekebishwe kwa kufuta maneno "miaka mitano" na badala yake kuweka maneno "kipindi chochote kile". | | |
| | | (xvi)Iongezwe ibara ndogo mpya ya (2) itakayoruhusu sifa zilizotajwa katika ibara hii kuratibiwa na Tume Huru ya Uchaguzi. | Kuipa mamlaka hiyo mamlaka ya kupokea na kuchambua sifa za wagombea. | |
| 76. | Haki ya kuchaguliwa tena | (i) Ibara ndogo ya (3) ifutwe. | | Ibara hii inakuwa ibara ya 79 na Ibakikama ilivyo. |
| | | (ii)76(3) Ibara irekebishwe na isomeke "Mtu aliyewahi kuwa Rais wa Tanzania bara au Zanzibar hataruhusiwa kugombea nafasi ya Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania". | Mtu huyo ameshaitumikia ikulu kwa kipindi chake kisheria, hakuna sababu ya kuruhusiwa kugombea awaachie wengine nafasi hiyo. | |
| | | (iii)Ibara hii haieleweki, hivyo ifafanue zaidi suala la la Makamu wa Rais kushika Urais kwa masharti ya Ibara ya 72. Ibara ya 40(4) ya Katiba ya sasa inajieleza vizuri zaidi kuhusu suala hili. | Ibara hiyo inazua maswali yafuatayo:<br>(a) Je, miezi hii 36 inahusu kipindi cha kwanza cha Umakamu wa Rais?<br>(b) Kama ndivyo, mtu aliyeshika Urais kwa masharti ya Ibara ya 72 kwa kipindi kilichozidi miezi 36 ya kipindi chake cha pili cha Umakamu wa Rais, anaweza kugombea nafasi ya Rais kwa kipindi kimoja au vipindi | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | viwili vijavyo vya Urais?<br>(c) Je, mtu aliyekamilisha vipindi viwili katika nafasi ya Makamu wa Rais anaweza kugombea nafasi ya Urais?<br>(d) Kwa kipindi kimoja au viwili? | |
| | | (iv) 76 ibaki kama ilivyo isipokuwa wakati wa kugombea asiwe amevuka umri wa miaka 70. | Inajitosheleza na baada ya miaka 75 mtu anakuwa amechoka kimwili na hivyo hawezi kumudu mikiki mikiki ya Urais licha ya kuwa mtu huyo anakuwa na busara, hekima na ukomavu. | |
| | | (v) Ibara ndogo ya (5) irekebishwe kwa kufuta neno “aliyechaguliwa” na badala yake kuweka maneno “Mtu aliyeshika nafasi ya madaraka”. | Mtu huyu hachaguliwi bali anashika nafasi ya Urais kwa mujibu wa Ibara ya 72. | |
| | | (vi) 76. Ibara imeandikwa kwa lugha ya kisheria zaidi, iwekwe katika lugha nyepesi. | | |
| | | (vii) 76(1) na (2), Ibara zibaki kama zilivyo. | | |
| | | (viii) 76. Ibara iwekewe kifungu kitakachoeleza kuwa nafasi ya Urais wa Muungano iwe ni ya kupokezana kati ya Zanzibar na Bara. | | |
| 77. | Utaratibu wa | (i) 77 (1) – (4) ibaki kama | Inajitosheleza. | 1. Ibara ya 77 |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | Uchaguzi wa Rais | ilivyo. | | imekuwa 81.<br><br>2. Ibara ndogo ya (6) imeongezwa neno 'halali' baada ya maneno asilimia hamsini ya kura zote. |
| | | (ii)Ibara ndogo ya (5) ibadilishwe na badala yake iandikwe kama ifuatavyo:<br>"Uchaguzi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano utafanyika siku iliyo ya kazi na itatambuliwa kuwa siku maalumu kwa kadri itakavyoteuliwa na Tume Huru ya Uchaguzi kwa mujibu wa sheria za nchi". | (a)Ili kuwapa fursa raia kushiriki uchaguzi kwa uhuru bila kuingiliwa muda wao wa ibada.<br>(b)Ili kuwapa fursa ya kutosha ya kushiriki katika uchaguzi. | |
| | | (iii)Katika Ibara ndogo ya (6) yaongezwe maneno "amepata zaidi ya theluthi moja ya kura zilizopigwa Zanzibar". | (a) Kuondosha uwezekano wa kiongozi huyo wa Jamhuri ya Muungano kuwa anapatikana kwa kuungwa mkono na upande mmoja tu wa Jamhuri ya Muungano.<br>(b) Utaratibu huu pia unatumika nchini Marekani ambapo mgombea wa urais wa nchi hiyo hupaswa kupata kiwango maalum cha kura katika baadhi ya majimbo ili aweze kushinda kiti cha urais. | |
| | | (iv)Ibara ndogo ya (7) ifutwe na badala | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | yake iandikwe kama ifuatavyo: | | |
| | | “(7) Endapo katika Uchaguzi wa Rais hakuna mgombea aliyekidhi masharti ya Ibara ndogo ya (6), basi mgombea aliyeshinda ataunda Serikali ya mseto kwa kushirikiana na vyama vyengine.” | | |
| | | Kuepuka kurudia uchaguzi na kupunguza gharama zisizo za lazima. | Kuepuka kurudia uchaguzi na kupunguza gharama zisizo za lazima. | |
| | | (vii) 77-Iongezwe Ibara ndogo ya (8) itakayotamka kuwa Tume itatakiwa kutangaza matokeo ya Urais ndani ya siku 7. | Ni muhimu kuwa na muda maalum ambao matokeo yatakuwa yametangazwa na kuondoa migogoro. | |
| 78. | Malalamiko kuhusu uhalali wa uchaguzi wa Urais | (i)Ibara ndogo ya (1) yaongezwe maneno “au mwakilishi wake” baada ya neno “mgombea”. | | 1. Ibara ya 78 imekuwa 82.<br>2. Ibara ya 82(2)maneno ‘wa siku saba’ yameondolewa na kuweka maneno ‘uliowekwa na sheria ya nchi’.<br>3. Ibara ndogo ya (3) ifanyiwe marekebisho; maneno ‘katika kipindi cha siku kumi na nne’ yameondolewa na kuwekwa ‘muda utakaoainishwa na sheria ya nchi’. |
| | | (ii) 78(4) Isomeke Mahakama ya Juu ikitoa uamuzi lazima itoe sababu.<br>(iii) Sifa za Rais zisichanganywe na sifa za ubunge<br>(iv) Kusiwe na muda maalum wa kutangaza matokeo ya Urais kwenye katiba. | Ili kuepusha uvunjifu wa amani wa uharibifu wa mali mara nyengine inaweza kutumika kigezo hiki ili kuharibu utaratibu | |
| 79. | Kiapo cha Rais | (i) Katika maelezo ya pembeni | Ibara inazungumzia kiapo | 1. Ibara ya 79 |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | (marginal note) yaongezwe maneno "na muda wa kushika madaraka". | na muda wa kushika madaraka. | inakuwa ibara ya 83.<br>2. Kuwe na marekebisho katika ibara ndogo ya (2) kwa kuondoa neno ‘"alipochaguliwa" na kuweka "tangu siku alipoapishwa"<br>3. Marginal Note isomeke "Kiapo cha Rais na muda wa kushika madaraka." |
| | | (ii) Ibara hii irekebishwe na ieleze kwamba Rais aapishwe baada ya siku thelathini tangu kutangazwa matokeo ya Urais, na endapo kabla ya kuapishwa Rais mteule atafariki, basi Makamu wa Rais aapishwe na ashike Urais kwa kipindi cha miezi sita tu na kufanyike uchaguzi mpya. | Ili kutoa muda wa kutosha wa kutoa malalamiko mahakamani na pia kupata muda wa kutosha kwa makabidhiano. | |
| | | (iii) Ibara ndogo ya (1) inatatanisha. Upande mmoja inasema Rais ataapishwa mapema iwezekanavyo, lakini kwa upande mwingine inasema kwa vyovyote vile hatashika madaraka kabla ya siku thelethini kupita. Inapendekezwa Ibara ndogo hii iandikwe upya na kwa ufasaha ni wakati gani Rais ataapishwa na kushika madaraka. | Kufafanua vizuri hasa wakati ambapo hakuna shauri la kuhoji uchaguzi wa Rais lililofikishwa Mahakamani; kuepusha ombwe la uongozi wakati ambapo Rais ameshaapishwa lakini hashiki madaraka, na kwa wakati huo huo Rais aliyekuwapo hawezi kuendelea kuongoza kwani Rais mteule ameshakula kiapo. | |
| | | (iv) Ibara ndogo ya (2) irekebishwe na isomeke kama ifuatavyo:<br>"(2) Rais mteule atashika nafasi ya madaraka ya Rais kwa muda wa miaka mitano tangu siku alipochaguliwa kuwa Rais, isipokuwa kama kiti cha Rais kitakuwa wazi kwa masharti yaliyoelezwa ndani ya Katiba hii." | Kujiuzulu au kufariki sio sababu pekee zinazoweza kumzuia Rais kushika madaraka kwa kipindi cha miaka mitano. | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | (v) Katika aya (a) ya ibara ndogo ya (3) yaongezwe maneno "na sasa" baina ya maneno "siku" na "ambapo". | | |
| | | (vi) Ibara hii irekebishwe na iweke utaratibu wa kumpata Rais pindi Rais Mteule anapofariki au kupoteza uwezo wa kumudu madaraka ya Rais kabla ya kuapishwa. | | |
| | | (vii) Iongezwe Ibara mpya itakayotamka kuwa "Rais ataapishwa tarehe 15 Desemba ya mwaka wa uchaguzi na kipindi cha miaka mitano ya uongozi kianze kuhesabiwa mara baada ya Rais Mteule kuapishwa. Miaka mitano si lazima iwe kamili, inaweza kupungua au kuongezeka.<br>Wakati wa kusubiri Rais Mteule kuapishwa, Rais anayeondoka awekewe ukomo wa mambo anayoweza kufanya, mfano azuiwe kufanya teuzi, labda kuziba nafasi wazi kutokana na vifo. | | |

### (d) Masharti Mahsusi kuhusu Mamlaka ya Rais.

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| 80. | Madaraka ya kutangaza vita | (i)Ibara hii haitekelezeki hivyo ifutwe. | Rais wa Jamhuri ya Muungano hana eneo la kijiografia na kisheria | 1. Ibara ya 80 inakuwa ibara ya 84. |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | analoweza kulifanyia maamuzi. Aidha, Rais wa Serikali ya Muungano hana mamlaka ya kutangaza vita kwani suala hilo halimo katika orodha ya mambo ya Muungano. Inapendekezwa Ibara hii iangaliwe upya kwa kuzingatia mapendekeo ya muundo wa Serikali mbili. | 2. Inabaki kama ilivyo. |
| | | (ii) Ibaki kama ilivyo. | Inajitosheleza na suala la ulinzi na usalama ni la Muungano na ni mamlaka ya Rais. | |
| | | (iii) 80(3).Isiwe kutaarifu tu, bali Bunge lipewe mamlaka ya kushauri na kuidhinisha. | | |
| 81. | Madaraka ya Rais kutangaza hali ya hatari | (i) Ibara hii haitekelezeki hivyo ifutwe. | Rais wa Jamhuri ya Muungano hana eneo la kijiografia na kisheria analoweza kulifanyia maamuzi. Aidha, Rais wa Serikali ya Muungano hana mamlaka ya kutangaza hali ya hatari kwani suala hilo halimo katika orodha ya mambo ya Muungano. Inapendekezwa Ibara hii iangaliwe upya kwa kuzingatia mapendekeo ya muundo wa Serikali mbili. | 1. Ibara ya 81 inakuwa 85.<br>2. Ibara ya 85(2) (b) neno “hasa” liondolewe na kuwekwa neno ‘ya wazi” na) neno “baa” liondolewe na kuwekwa neno ‘janga” . |
| | | (ii) 81 ibaki kama ilivyo. | Inajitosheleza na suala la | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | ulinzi na usalama ni la Muungano na ni mamlaka ya Rais. | |
| | | (iii) Maneno ya pembeni yaongezwe "na kupeleka majeshi katika ulinzi wa amani". | | |
| | | (iv) Katika ibara ndogo ya (1) yaongezwe maneno "au kupeleka majeshi katika ulinzi wa amani" na vivyo hivyo katika ibara ndogo (3) kati ya maneno "Muungano" na "Rais". | Inapendekezwa maneno hayo yaongezwe ili kutoa fursa kwa Rais kutoa tangazo kwa Spika wa Bunge pale anapoamuru majeshi yaende nje ya nchi katika operesheni za ulinzi wa amani. | |
| | | (v) Ibara ndogo ya (4) ifutwe na badala yake iandikwe ibara ya 32(2) ya Katiba ya sasa. | | |
| | | (vi) Ibara ndogo ya (5) iandikwe kama ifuatavyo:<br>"(5) Tangazo la hali ya hatari lililotolewa na Rais kwa mujibu wa Ibara hii litakoma kutumika iwapo litafutwa na Rais au Bunge lisipoidhinisha". | | |
| | | (vii) 81(6). Isiwe kutaarifu tu, bali Bunge lipewe mamlaka ya kushauri na kuidhinisha. | | |
| 82. | Mamlaka ya Rais kutoa msamaha | (i) Ibara ndogo ya (1) ifutwe. | Kazi hiyo iwe kwa mahakama ambao ni mhimili mwingine wa Dola. | 1. Ibara ya 82 inakuwa ibara ya 86.<br>2. Ibara 86(4) maneno 'Kamati ya taifa ya ushauri ' yaondoke na kuweka maneno |
| | | (ii) Ibara hii iangaliwe upya kwa kuzingatia kwamba Mahakama si mojawapo ya mambo ya Muungano. Hivyo haiyumkiniki | Mambo ya sheria, mahakama, magereza na msamaha si mambo ya Muungano na hivyo Rais | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | Rais wa jamhuri ya Muungano akawa na mamlaka ya kutoa msamaha kwa watu waliohukumiwa na vyombo vya kutoa haki ambavyo havimo katika orodha ya mambo ya Muungano. | wa Muungano hatakuwa na mamlaka ya kutoa msamaha kwa mtu aliyehukumiwa katika maeneo ya Washirika wa Muungano. | 'chombo kinachohusika na masuala ya msamaha wa wafungwa' |
| | | (iii) 82-Kwa adhabu ya kifo, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania awe ndiye mwenye mamlaka ya kubatilisha adhabu ya kifo na pia kutoa msamaha kwa makosa dhidi ya Jamhuri ya Muungano. Makosa mengine ambayo si dhidi ya Jamhuri ya Muungano, Marais wa nchi washirika wawe na mamlaka ya kutoa msamaha. | Rais wa Jamhuri ya Muungano ndiye mwenye raia kwani uraia wa Tanzania ni wa Jamhuri ya Muungano. | |
| | | (iv) 82-Kwa adhabu ya kifo, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania awe ndiye mwenye mamlaka ya kubatilisha adhabu ya kifo na pia kutoa msamaha kwa makosa dhidi ya Jamhuri ya Muungano. Makosa mengine ambayo si dhidi ya Jamhuri ya Muungano, Marais wa nchi washirika wawe na mamlaka ya kutoa msamaha. | Rais wa Jamhuri ya Muungano ndiye mwenye raia kwani uraia wa Tanzania ni wa Jamhuri ya Muungano. | |
| | | (v) Ibara ndogo ya (1) maneno "Rais kwa mamlaka ya Mkuu wa nchi" yafutwe na badala yake iandikwe "Rais kama Mkuu wa nchi | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | atakuwa na mamlaka". | | |
| | | (vi) Katika Ibara ndogo ya (1)(a) yaongezwe maneno "ya Rufani au Mahakama ya Juu" baada ya neno "Mahakama". | Ili kumpa Raisi mamlaka ya kuwasamehe wafungwa waliotiwa hatiani na mahakama za Jamhuri ya Muungano. | |
| | | (vii) Katika aya (b) ya Ibara ndogo ya (1) neno "kubatilisha" liandikwe "kubadilisha" na maneno "kuwa adhabu ya kifungo cha maisha" yafutwe na badala yake iandikwe "na kuwa adhabu tahafifu". | | |
| | | (viii) 82(1) (b). Adhabu ya kifo ifutwe kabisa kwenye Sheria za nchi. | Mwenye jukumu la kuua ni Mwenyezi Mungu. | |
| | | (ix) Ibara ndogo ya (2) ifutwe. | | |
| 83. | Kinga dhidi ya mashtaka ya Rais | (i)Ibara hii irekebishwe na iandikwe kama ifuatavyo:<br>"83(1) Wakati wote Rais akiwa madarakani na baada ya kuacha kushika madaraka hayo, Rais anaweza kushtakiwa kwa ajili ya kosa lolote la jinai chini ya sheria, au chini ya mkataba wowote wa kimataifa ambao Jamhuri ya Muungano ni mwanachama ambao unakataza kinga dhidi ya mashtaka ya Rais.<br>(2) Bunge la Jamhuri ya Muungano litatunga sheria itakayoweka utaratibu na masharti ya kufungua kesi ya jinai au mashauri ya madai dhidi ya Rais." | Mwelekeo wa sasa wa kikatiba – kama unavyoonyeshwa na Katiba Mpya za Kenya na Zimbabwe – ni kuondoa kinga dhidi ya mashtaka kwa Rais kwa makosa aliyoyafanya kabla na wakati akiwa Rais. Historia yetu halisi imethibitisha kwamba Rais anaweza kutenda uhalifu wa kijinai akiwa madarakani. Kwa hiyo, kuendelea kuwawekea marais wetu kinga dhidi ya mashtaka ya jinai sio tu kunapalilia uhalifu na | 1. Ibara ya 83 inakuwa ibara ya 87.<br>2. Inabaki kama ilivyo |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | matumizi mabaya ya madaraka ndani ya Ikulu, bali pia kunaenda kinyume na wimbi la mabadiliko katika nchi jirani na rafiki zetu ambazo zimeondoa dhana ya upendeleo kwa viongozi wao wakuu kwa kuwafanya wawe chini ya sheria za nchi. | |
| | | (ii) Ibara ndogo ya (3) irekebishwe kwa kuongeza maneno "isipokuwa kwa kutolipa kodi au kumsaidia mtu kutolipa kodi" baada ya neno "jinai". | | |
| | | (iii) Ibara ndogo ya (3) ifutwe na badala yake iandikwe ibara ya 46(3) ya Katiba ya sasa. | | |
| | | (iv) Ibara ndogo ya (3) ifutwe na badala yake iandikwe kama ifuatavyo:<br>"(3) Rais aliyemaliza kipindi chake cha uongozi anaweza kushitakiwa Mahakamani kwa makosa yoyote yale aliyoyafanya katika kipindi cha uongozi wake". | Ili kumfanya Rais kuwa makini wakati wa kutekeleza majukumu yake. | |
| | | (v) 83(3).Imependekezwa ibara hii ndogo ipanuliwe kueleza kuwa kinga hii inahusu maamuzi/matendo au kutotenda vinavyohusu mamlaka ya Rais, mfano; Rais anaruhusiwa kuendeleza shughuli zake binafsi (mfano | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | za kibiashara). Katika hali hiyo anaweza kutoa maamuzi yenye maslahi kwa biashara zake,lakini ambayo ni ya makosa. | | |
| | | (vi) Ziongezwe ibara ndogo mpya zitakazosomeka kama ifuatavyo: “(1) Ikiwa Rais alikuwa na shtaka la jinai linalodhaminika na ikiwa shitaka hilo litakua linaendelea kabla na wakati wa Kampeni basi shitaka hilo halitaendelea hadi hapo atakapokoma kuwa Rais. (2) Ikiwa Rais alifunguliwa shtaka katika Mahakama ya Uhalifu ya Kimataifa au mahakama nyingne ya kimataifa au ya kikanda kabla ya kuapishwa kuwa Rais basi Shtaka hilo litaendelea dhidi yake kwa mujibu wa uendeshwaji wa shtaka husika”. | | |
| | | (vii) 83-Ibara ibaki Kama ilivyo. | Kinga hii haitoi “absolute immunity” kwani hata akiwa madarakani, Rais anaweza kushtakiwa kwa kutumia Ibara ya 84. | |
| 84. | Bunge kumshtaki Rais | (i) Ibara ndogo ya (2) aya (a) neno “mkubwa” lifutwe. | Linaleta utata. | 1. Ibara ya 84 inakuwa ibara ya 88. 2. Ibara ndogo ya 7 (b) imerekebishwa na kusomeka “wabunge wengine sita kutoka Bunge la Jamhuri ya |
| | | (ii) Ibara ndogo ya (2) irekebishwe kwa kufuta maneno “Makosa makubwa ya jinai” na badala yake yawekwe maneno “Makosa ya jinai”. | Kosa lolote la jinai linatosha kutia doa wadhifa wa Rais. | |
| | | (iii) Ibara ndogo ya (2)(b) irekebishwe | Kuondoa utata katika | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | kwa kuainisha makosa makubwa ya jinai. | kutafsiri masharti husika. | Muungano, watatu kutoka kila upande wa Nchi Washirika watakaoteuliwa na Spika."<br>3. ibara ndogo ya 14 imerekebishwe kwa kuweka vifungu vidogo viwili:<br>a) kushika nafasi ya Rais, Makamu wa Rais Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais wa Tanganyika au Rais wa Zanzibar; na<br>b) kupata malipo yoyote ya uzeeni, posho wala kupata haki au nafuu nyingine anazopewa Rais au mtu aliyekuwa Rais kwa mujibu wa Katiba au sheria za nchi. |
| | | (iv) Ibara ndogo ya (2) irekebishwe kwa kufuta maneno "Makosa makubwa ya jinai" na badala yake yawekwe maneno "Makosa ya jinai". | Kosa lolote la jinai linatosha kutia doa wadhifa wa Rais. | |
| | | (v) Ibara ndogo ya (2)(b) irekebishwe kwa kuainisha makosa makubwa ya jinai. | Kuondoa utata katika kutafsiri masharti husika. | |
| | | (vi) Ibara ndogo ya (2)(b) irekebishwe kwa kuainisha makosa makubwa ya jinai. | Kuondoa utata katika kutafsiri masharti husika. | |
| | | (vii) Makosa yanayotajwa katika aya (b) ya ibara ndogo ya (2) yawekwe katika Sheria. | Ili kutoa tafsiri moja ya makosa hayo. | |
| | | (viii) Aya (h) ya ibara ndogo ya (2) maneno "ya kitaifa" yaongezwe mara baada ya neno "maadili". | | |
| | | (ix) Aya (b) ya Ibara ndogo ya (3) irekebishwe kwa kufuta maneno "asilimia ishirini na Tano" na badala yake kuweka maneno "asilimia 2/3". | 25% ni idadi ndogo sana ambayo kwa itikadi za kisiasa na mfumo wa sasa wa vyama vingi Rais anaweza kuondolewa kwa urahisi na hivyo kuathiri ustawi wa nchi. | |
| | | (x) Ibara ndogo ya (4) ifutwe na badala yake iandikwe kama ilivyo Ibara ya 46A(4) ya Katiba ya sasa. | | |
| | | (xi) Aya (b) ya ibara ndogo ya (7) ifutwe. | Hakutakuwepo Jaji Mkuu wa Tanzania Bara katika Mfumo wa serikali mbili. | |
| | | (xii) Ibara ndogo ya (3)(b) irekebishwe ili kuweka utaratibu wa kutoshitakiwa Rais mpaka | •25% ya wabunge ni idadi ya kutosha inayodhihirisha kuwa | |

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Maoni* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| | | ipatikane asilimia 25% ya kura kutoka kila upande wa Muungano. | kuna jambo linalotaka kufanyika.<br>•Kila upande wa Muungano kushiriki katika maamuzi mazito ya mustakabali wa nchi. | |
| | | (xiii) Aya (d) ya Ibara ndogo ya (7) iandikwe kama ifuatavyo:<br>“(d) wajumbe wengine watatu kutoka kila upande wa Muungano watakaoteuliwa na Spika”. | Haitakwamisha maamuzi. | |
| | | (xiv) 84(8)- iandikwe upya kwa kuongezwa maneno yafuatayo “atarejea tena kwenye nafasi yake ikiwa hatopatikana na makosa”. | Ili kuliweka suala hilo kuwa wazi zaidi. | |
| | | (xv) Ibara ndogo ya (12) ifutwe na badala yake iandikwe kama ilivyo Ibara ya 46A (9) ya Katiba ya sasa.<br>(xvi) kamati ya uchunguzi ijumuishe wabunge | | |
| | | (xvii) Katika Ibara ndogo ya (13) yaongezwe maneno “ndani ya muda wa masaa 24” baada ya maneno “Spika atamfahamisha Rais”. | | |
| 85. | Maslahi ya Rais | (i)Ibara hii irekebishwe ili kufuta uwezekano wa kutaja maslahi ya Rais na badala yake utaratibu wa sasa uendelee kutumika. | | Ibara ya 85 inakuwa 89. Inabaki kama ilivyo |
| | | (ii) 85-iongezwe Ibara ndogo ya (3) itakayosema “Bunge litatunga sheria itakayohusu Maslahi na Mshahara wa Rais”. | Kuweka uwazi na kuipa mwongozo Tume ya Utumishi wa Umma, inapopanga maslahi na mshahara wa Rais. | |

### (e) Makamu wa Rais

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| 86. | Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano | (i) Ibara hii irekebishwe ili kuweka utaratibu wa Marais wa Nchi washirika kuwa Makamu wa Rais wa Muungano. | Mfumo unaopendekezwa unamfanya Rais wa Jamhuri ya Muungano kutokuwa na mahusiano ya karibu na Marais kutoka Nchi Washirika hali ambayo inaweza kudhoofisha Muungano. Ni vyema Marais wa Nchi Washirika wakawa Wasaidizi Wakuu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano kwa kila upande wa Muungano na kwa hivyo, Marais wan chi Washirika wakawa pia na wadhifa wa Makamu wa Kwanza na Makamu wa Pili wa Rais wa Jamhuri ya Muungano. | 1. Ibara ya 86 inakuwa 90.<br><br>2. Katika ibara ndogo ya (2) Maneno “kusababisha utekelezaji” yafutwe na kuwekwa maneno “atawezesha au kusimamia utekelezaji”. |
| | | (ii) Ibara ndogo ya (2) irekebishwe kwa kufuta maneno “kusababisha utekelezaji” na badala yake kuweka maneno “atawezesha au atasimamia utekelezaji”. | Kuweka ufasaha wa Lugha ya Taifa. | |
| 87. | Upatikanaji wa Makamu wa Rais | (iii) Iwekwe maelezo ya pembeni (marginal note) yatakayosomeka “Upatikanaji wa Makamu wa Rais”. | | Ibara ya 87 inakuwa Ibara ya 91 na iwekewe “Marginal Note” ambayo itasomeka “Upatikanaji wa Makamu wa Rais. |
| | | (iv) Ibara ndogo ya (3) ifutwe na badala yake iandikwe ibara ya 47(3) ya Katiba ya sasa. | | |

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Maoni* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| | | (v) 87 Iongezwe ibara ya 87(4) itakayosomeka kwamba "Endapo mgombea wa uraisi atakua jinsi moja basi Makamu wa Rais atakua jinsia nyengine<br>(vi) Kuwe na ibara mpya itakayozungumzia upatikanaji wa Makamu wa Rais | Kuwepo na uwiano wa kijinsia katika nafasi za juu ya madaraka ya nchi kwa kuwa wana uwezo, elimu na wanawake ni wengi katika jamii kuliko wanaume | |
| 88. | Sifa za Makamu wa Rais | (i) Ibara ndogo ya (2) maneno "chama chochote" yafutwe na badala yake iandikwe "anaependekezwa na chama chochote au mtu yeyote", na maneno "Rais wa Tanzania Bara" yafutwe. | | Ibara ya 88 itakuwa ibara ya 92 na itabaki kama ilivyo |
| | | (ii) 88(3) Vifungu hivi viainishwe ili visilete ukinzani. | Kifungu hiki kinakinzana na ibara ya 86(1)(b) kwamba Makamu wa Rais atakua mwenyekiti wa Tume ya mahusiano ya Serikali. | |
| | | (iii) 88(4).Ibara ifafanue maslahi yake yatakuwaje kwa vile atakuwa hajakamilisha muda wake wa Urais wa Bara wala Zanzibar. | | |
| | | (ii) 88(3) Vifungu hivi viainishwe ili visilete ukinzani. | Kifungu hiki kinakinzana na ibara ya 86(1)(b) kwamba Makamu wa Rais atakua mwenyekiti wa Tume ya mahusiano ya Serikali. | |
| 89. | Kiapo cha Makamu wa Rais | 89 ibaki kama ilivyo | Imejitosheleza | Ibara ya 89 itakuwa ya 93 na itabaki kama ilivyo |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| 90. | Wakati wa Makamu wa Rais kushika madaraka | (i) Ibara ndogo ya (3) ifutwe na badala yake iandikwe kama ifuatavyo: "Makamu wa Rais atashika nafasi ya madaraka ya Makamu wa Rais kwa muda wa miaka mitano tangu siku Rais alipochaguliwa, isipokuwa kama nafasi ya Makamu wa Rais itakuwa wazi kwa masharti yaliyoelezwa ndani ya Katiba hii." | Makamu wa Rais hachaguliwi ila huteuliwa kuwa mgombea mwenza na kuwa kwake Makamu wa Rais kunategemea kuchaguliwa kwa Rais. | Ibara ya 90 itakuwa ya 94 na itabaki kama ilivyo |
| | | (ii) 90(3)(e).Kipengele hiki kisomeke"atakapotiwa hatiani kwa kosa lolote la Jinai" | | |
| | | (iii) Ibara ndogo ya (4) isomeke ''atakapotiwa hatiani kwa kosa lolote la jinai." | | |
| | | (iv) 90(4)(d).Ibara ifafanue Maslahi ya Makamu wa Rais yatakuwaje atakapoapishwa kuwa Rais.Aidha Maslahi ya Makamu wa Rais yatajwe. | | |
| | | (v) Vifungu vya ibara vibadilishwe na viwe na mpangilio ufuataoo:90(1),90(4),90(3) na mwisho imalizie ibara ya 90(2). | Ili kuwa katika mtiririko mzuri. | |
| 91. | Bunge kumuondoa Makamu wa Rais | (i) Ibara ndogo ya (1) aya (a) ifutwe na badala yake iandikwe kama ifuatavyo: "(a) Rais amewasilisha hati kwa Spika hati iliyopitishwa na Baraza la Mawaziri inayoeleza kwamba Makamu wa Rais ameacha au ameshindwa kutekeleza kazi za madaraka ya Makamu wa Rais". | | 1. Ibara ya 91 itakuwa ya 95.<br>2. Katika ibara ndogo ya (1) liongezwe neno "kumuondoa" mbele ya neno "kumshtaki". |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | (ii) Ibara ndogo ya (1) irekebishwe ili imtambue Waziri Mkuu.<br>(iii) Ibara ndogo ya kwanza iongeze neno "kumuondoa" baada ya neno kumshataki | | |
| | | (iv) 91. Ibara irekebishwe kwa kuingizwa ibara za 51, 52(1) na 53(2) za Katiba ya sasa. | Ili Waziri Mkuu awe ndiye kiongozi wa shughuli za Serikali Bungeni. | |
| | | (v) Iongezwe ibara mpya itakayoanzisha chombo huru kitakachokuwa na mamlaka ya kuteua Mawaziri, Mwanasheria Mkuu, Katibu Mkuu Kiongozi na Makatibu Wakuu. | | |
| | | (vi) 91-Ibara ndogo ya (3) iwekwe mwisho wa ibara hii na iwekewe "Marginal note" itakayosomeka "Upatikanaji wa Makamu wa Rais wakati nafasi hiyo inapokuwa wazi". | Ili iweze kueleweka vizuri. | |
| | | (vii) 91(4).Maneno yarekebishwe.Mwisho wa sentensi neno"wala" liondolewe na mwisho yaongezwe maneno "wala nafasi nyingine ya kugombea au kuteuliwa na Rais". | | |
| | | | | Inaongezwa Ibara mpya ya 96 ambayo inahusu "Upatikanaji wa Makamu wa Rais wakati nafasi hiyo inapokuwa wazi". |

## 7.1 SEHEMU YA PILI: BARAZA LA MAWAZIRI LA SERIKALI YA JAMHURI YA MUUNGANO

### (a) Baraza la Mawaziri

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| 92. | Kuundwa kwa Baraza la Mawaziri | i. Ibara hii irekebishwe na iandikwe kama ilivyo Ibara ya 54(1) ya Katiba ya sasa. | | 1. Ibara ya 92 itakuwa ya 97.<br>2. Ibara ya 97(1)(b) itaanza na maneno Waziri Mwandamizi na …………………<br>3. Ibara ya 97(2) neno “atahudhuria” limeondolewa na kuwekwa neno “ataongoza”. |
| | | ii. Katika aya (a) ya ibara ndogo ya (1) neno “Makamu wa Rais” lifutwe na badala yake liwekwe “Waziri Mkuu”. | | |
| | | iii. Inapendekezwa kabla ya Ibara ya 92 iwepo Ibara nyingine ambayo inahusu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano. Ibara hiyo itaitaja Ofisi ya Waziri Mkuu, kazi na mamlaka ya | Mfumo unaopendekezwa ni wa kibunge na wa Serikali mbili. | |
| | | iv. Waziri Mkuu, uwajibikaji wa Serikali kama ilivyo katika Ibara za 51, 52(1) na (3), 53(a) za Katiba ya sasa. | | |
| | | v. 92.Mawaziri Wakaazi wawe wajumbe wa Baraza la Mawaziri. | Wao ndio kiungo kati ya Serikali za Washirika na ile ya Muungano | |
| | | vi. Ibara ndogo ya (1) irekebishwe ili kuweka utaratibu wa kuwajumuisha Marais wa Nchi Washirika kuwa Wajumbe wa Baraza la Mawaziri. | | |
| | | vii. Ibara ndogo ya (1) irekebishwe kwa kuongeza maneno “Serikali ya” kati ya kiunganishi “la” na neno ”Jamhuri”. | | |
| | | viii. Ibara ndogo ya (1) itaje kwamba | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | Rais wa Jamhuri ya Muungano ndiye Mwenyekiti wa Baraza la Mawaziri kama ilivyo katika Katiba ya sasa. | | |
| | | ix. (i) Ibara ndogo ya (1) iongezwe aya mpya ya (a) inayosema kama ifuatavyo:<br>"(a) Rais atakuwa Mjumbe na Mwenyekiti wa Baraza la Mawaziri". | | |
| | | x. Iongezwe ibara ndogo itakayoeleza kwamba Barazaa la Mawaziri litajumuisha na Mawaziri wa nchi washirika. | Kuweza kuwakilisha nchi zao katika Baraza la Mawaziri na endapo pendekezo la kuwepo Makamu wa Rais wawili litakubaliwa. | |
| 93. | Uteuzi wa Mawaziri na Naibu Mawaziri | (i) Katika Ibara ndogo ya (2) inapendekezwa idadi ya mawaziri iwe 20 badala ya 15. | Kuzingatia ukubwa wa majukumu katika muundo unaopendekezwa wa Serikali mbili. | 1. Ibara ya 93 itakuwa ya 98.<br>2. "Katika Ibara ndogo ya 98 (2) yameongezwa maneno na Naibu Mawaziri mbele ya neno Mawaziri". |
| | | (ii) Ibara ndogo ya (4) irekebishwe ili kuweka idadi ya Naibu Mawaziri ambao wasizidi nusu ya Mawaziri. | Idadi ya Mawaziri na Naibu Mawaziri ilingane na idadi ya mambo ya Muungano. | |
| | | (iii) 93(4).Kusiwe na Naibu Mawaziri. | | |
| | | (iv) Ibara ndogo ya (4) irekebishwe ili Mawaziri na Naibu Mawaziri wateuliwe kwa utaalamu wao. | | |
| | | (v) iongezwe Ibara ndogo mpya itakayoeleza wazi kuwa uteuzi wa Mawaziri na Naibu Mawaziri wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania utakuwa ni wa uwiano sawa kwa Nchi washirika wa Muungano. | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | (vi) 93(4) -Neno "uwiano" lifafanuliwe kwa kuzingatia Washirika wa Muungano na jinsia. | Ili kupata tafsiri moja na fasaha. | |
| | | (vii) 93(5) Hati ya uteuzi iitwe"Barua ya Uteuzi". | Hati ya Uteuzi (Instrument) hutolewa kwa Waziri. | |
| | | (viii) iongezwe ibara ndogo mpya ambayo itakuwa kama ifuatavyo:<br>(ix) "Waziri atakayeshughulikia vyombo vya ulinzi na usalama ateuliwe kutoka miongoni mwa viongozi wa vyombo vya ulinzi na usalama". | | |
| | | (x) Ibara hii irekebishwe kwa kuongeza ibara ndogo mpya itakayokuwa kama ilivyo Ibara ya 58 ya Katiba ya sasa. | | |
| | | (xi) kuwe na ibara mpya itakayo anzisha ofisi ya Waziri Mwandamizi, namna atakavyoteuliwa na majukumu yake | | |
| | | | | Imeongezwa Ibara mpya ya 99 inayozungumzia "Uanzishwaji wa Ofisi ya Waziri Mwandamizi". |
| | | | | Imeongezwa Ibara mpya ya 100 ambayo inazungumzia "kazi na majukumu ya Waziri Mwandamizi". |
| 94. | Sifa za Mawaziri na | (i) Ibara ndogo ya (1) (a) irekebishwe | Katika suala hili kusiwe | 1. Ibara ya 94 |

| ***Ibara Na.*** | ***Kichwa cha Habari*** | ***Maoni ya Mabaraza*** | ***Sababu ya Maoni*** | ***Marekebisho ya Tume*** |
|---|---|---|---|---|
| | Naibu Mawaziri | na kusomeka "awe raia wa Jamhuri ya Muungano". | na tofauti ya aina ya uraia. | itakuwa Ibara ya 101.<br>2. Ibara ndogo ya 101(1(b) itasomeka "awe na Shahada ya Chuo cha Elimu ya Juu badala ya maneno ya Shahada ya Kwanza ya Chuo Kikuu".<br>3. Imeongezwa Ibara ndogo ya 100(1)(c) inayosomeka "awe na uweledi na uzoefu". |
| | | (ii) Aya (b) ya Ibara ndogo ya (b) ifutwe. | Rais ateue kulingana na uwezo wa anayemteua pamoja na mahitaji ya Serikali yake. | |
| | | (iii) Aya (b) ya ibara ndogo ya (1) ifutwe na badala yake iandikwe kama ifuatavyo:<br>"(b) awe na sifa mwelekeo na upeo". | Shahada haimfanyi mtu kuwa kiongozi bora. | |
| | | (iv) Ibara ndogo ya (1) (b) ibadilishwe kwa kufuta maneno "shahada ya kwanza" na badala yake iandikwe "shahada ya uzamili". | | |
| | | (v) Kuongeza aya zifuatazo katika ibara ndogo (1) kama ifuatavyo:<br>(c) ni mwadilifu na anafuata maadili ya Taifa;<br>(d) mweledi katika mambo yanayotekelezwa na wizara husika;<br>(e) mwenendo wake binafsi hautiliwi shaka na jamii;<br>(f) katika kipindi cha miaka mitano kabla ya tarehe ya kuteuliwa kwake hajawahi kutiwa hatiani kabla ya tarehe ya uchaguzi mkuu katika mahakama yoyote kwa kosa lolote la kukwepa kulipa kodi yoyote ya serikali". | Kuleta ufanisi katika utendaji kazi wa Mawaziri. | |
| | | (vi) Kuongeza aya zifuatazo katika ibara ndogo (1) kama ifuatavyo:<br>(a) ni mwadilifu, anaheshimu haki | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | za binadamu na asiyedharau wala kubagua watu kwa misingi ya kabila, jinsia, maumbile au hali zao katika jamii;<br>(b) hajawahi kupatikana na hatia ya kosa la jinai au kuwepa kodi ya Serikali;<br>(c) mwenye akili timamu;<br>(d) mwenendo wake binafsi hautiliwi shaka na jamii;<br>(e) ana uzoefu wa kutosha katika sekta ya umma au binafsi;<br>(f) awe na uelewa wa kutosha wa masuala ya kitaifa na kimataifa". | | |
| | | (vii) aya (b) ya Ibara ya (2) irekebishwe ili mtu aliyepatikana na hatia ya makosa mengine ya jinai apoteze sifa ya kuteuliwa kuwa Waziri au Naibu Waziri. | Yapo makosa mengi ya jinai yanayoweza kumuondolea mtu sifa ya uongozi. | |
| | | (viii) 94(2)(b).Yaongezwe na makosa ya kuua kwa kukusudia, kulemaza kwa kukusudia, ubakaji na kudhalilisha kijinsia,makosa ya jinai, madawa ya kulevya, ubadhirifu, rushwa , ufisadi na kuhatarisha usalama wa nchi. | | |
| | | (ix) Katika aya (b) ya Ibara ndogo ya (2) maneno "makosa ya ubadhirifu wa mali za umma" na badala yake kuweka maneno "makosa ya jinai na ukiukaji wa maadili." | (a) Ubadhirifu ni moja tu ya makosa ya jinai.<br>(b) Hivyo inahitajika kuongeza na ukiukwaji wa maadili. | |
| | | (x) Iongezwe ibara ndogo mpya | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | itakayoeleza kumwondolea sifa mtu aliyewahi kutiwa hatiani kwa makosa ya jinai ikiwemo rushwa, kukwepa au kusaidia kukwepa kodi na madawa ya kulevya. | | |
| | | (xi) ibara ndogo ya (4) ibadilishwe ili kuweka masharti kwamba uteuzi wa Mawaziri ufanywe na Rais kwa mashauriano na Marais wa nchi Washirika. | | |
| | | (xii) ibara hii irekebishwe ili iweke idadi ya Mawziri inayolingana na mambo ya Muungano. | | |
| 95. | Kiapo, muda na masharti ya kazi ya Waziri na Naibu Waziri | (i) Aya (a) ya ibara ndogo ya (4) irekebishwe ili iongezwe masharti yanayohusu kuugua na kuthibitika kushindwa kufanya kazi. | Kutoa fursa kwa matabibu kuthibitisha hilo. | Ibara ya 95 itakuwa Ibara ya 102 na itabaki kama ilivyo. |
| | | (ii) Ibara ndogo ya (3) ijitegemee na iwe na maelezo ya pembeni (marginal note) “Uwajibikaji wa pamoja wa Mawaziri” na isomeke kama ifuatavyo:<br>“(3) Kila Waziri anawajibika binafsi na kwa pamoja kwa Rais na kwa uamuzi wea Baraza la Mawaziri katika utekelezaji wa majukumu na katika kutumia madaraka ya Waziri ili kuhakikisha uwajibikaji wa pamoja wa Mawaziri, kwa mantiki hiyo:<br>(a) Waziri hatapingana au kumshambulia Waziri mwingine hadharani wala | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | kuifedhehesha Serikali;<br>(b) Mawaziri wote wana wajibu wa kutetea maamuzi ya Serikali na hawana uhuru wa kuyapinga nje ya vikao vya Serikali;<br>(c) Mawaziri wote wana wajibu wa kutunza siri za kumbukumbu na majadiliano ya Mikutano ya Baraza la Mawaziri na kwa vyovyote, Mawaziri hawatatoa nje siri za Baraza la Mawaziri;<br>(d) Mawaziri wanawajibika kuwa na kauli moja katika kutetea maamuzi ya Serikali;<br>(e) Kila Waziri, kabla ya kufikia uamuzi unaogusa sekta nyingine, atalazimika kwanza kushauriana kikamilifu na Mawaziri wanaohusiana na sekta hizo. | | |
| 96. | Utekelezaji wa shughuli za Serikali Bungeni | (i) Ibara hii ifutwe. | Kuzingatia mfumo wa kibunge unaopendekezwa. | Ibara ya 96 itakuwa Ibara ya 103 na itabaki kama ilivyo. |
| | | (ii) 96(1) ibara hii irekebishwe na kuruhusu mawaziri kushiriki vikao vya bunge | | |
| | | (iii) Katika ibara ndogo ya (2) maneno “Ibara ndogo ya (2)” yafutwe na badala yake iandikwe “ibara ndogo ya (1)(b)”. | | |
| | | (iv) 96(3) ibara hii irekebishwe na isomeke “Kila waziri atawajibika kwa utendaji wake ili kuongeza uwajibikauji” | Ili kuongeza uwajibikaji na ufanisi | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |

### (b) Mwanasheria Mkuu wa Serikali

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| 97. | Mwanasheria Mkuu wa Serikali | (i) Ibara hii irekebishwe na iandikwe kama ilivyo Ibara ya 59 ya Katiba ya sasa isipokuwa, Mwanasheria Mkuu wa Serikali asiwe Mbunge na asithibitishwe na Bunge. | | 1. Ibara ya 97 itakuwa Ibara ya 104.<br>2. Ibara ya 104(2)(c) imerekebishwa kwa kuwekwa maneno Mahakama Kuu ya Zanzibar au Mahakama Kuu ya Tanganyika badala ya neno Mahakama.<br>3. Ibara ya 104(2)(d) imerekebishwa na itasomeka ‘’Awe ni Mtumishi Mwandamizi katika Utumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano au Serikali za Nchi Washirika.<br>4. Imeongezwa Ibara ndogo mpya ya 6, ambayo itasomeka: |
| | | (ii) Ibara ndogo (1) irekebishwe na iandikwe kama ifuatavyo:<br>“(1) Kutakuwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye katika Katiba hii atatajwa tu kwa kifupi kama "Mwanasheria Mkuu" ambaye atateuliwa na Rais baada ya kupita kwenye mchakato wa wazi wa usaili mbele ya Tume ya Utumishi wa Mahakama na kuthibitishwa na Bunge”. | | |
| | | (iii) Aya (a) ya Ibara ndogo ya (2) irekebishwe na kusomeka “awe raia wa Jamhuri ya Muungano”. | | |
| | | (iv) Ibara ndogo ya (2) aya (c) liongezwe neno “Kuu” baada ya neno “Mahakama”. | | |
| | | (v) Katika aya (d) ya ibara ndogo ya (2) neno “mwandamizi” lifutwe na badala yake iandikwe “kwa kipindi kisichopungua miaka kumi na tano”. | | |
| | | (vi) 97(2)(b).Kipengele hiki | Sifa ya kuwa Wakili | |

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Maoni* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| | | kifafanuliwe kuwa ni "Shahada ya sheria ya Chuo kikuu kinachotambulika na vyombo husika vya Washirika…". | haitoshi hasa ikizingatiwa kuwa Uwakili sio suala la Muungano. | Mwanasheria Mkuu wa serikali hatashika nafasi ya madaraka ya Mwanasheria Mkuu mpaka awe ameapa mbele ya Rais kiapo cha utii na uaminifu na kiapo kingine chochote kinachohusu utendaji wa kazi yake kitakachowekwa kwa mujibu wa sheria za nchi. |
| | | (vii) Aya (e) ya Ibara ndogo (2) ifutwe. | Kwa sababu imemezwa katika ibara ndogo 2(d). | |
| | | (viii) Ibara ndogo ya (5) irekebishwe ili Mwanasheria Mkuu aingie katika Mahakama za Jamhuri ya Muungano tu. | Mwanasheria Mkuu wa Jamhuri ya Muungano hana nguvu na mamlaka ya kisheria kuingia na kusikilizwa na Mahakama Kuu ya Zanzibar. | |
| | | (ix) Iongezwe ibara mpya mara baada ya ibara ya 97 itakayoelezea kuhusu Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Inapendekezwa iandikwe Ibara ya 59B ya Katiba ya sasa na vilevile iandikwe kama ilivyo Ibara ya 56A (7) ya Katiba ya Zanzibar, ibara hiyo ieleze kwamba ikiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali anatoka upande mmoja basi Naibu Mwanasheria Mkuu atoke upande wa pili wa Muungano.<br>(x) Sifa za Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali ziwe sawa na sifa za Mwanasheria Mkuu wa Serikali. | | |
| | | (xi) Iongezwe ibara nyingine mpya itakayoeleza kuhusu Mkurugenzi wa Mashtaka ya Jinai na sifa. Inapendekezwa iandikwe Ibara ya 59B ya Katiba ya sasa na vilevile iandikwe kama ilivyo Ibara ya 56A (7) ya Katiba ya Zanzibar. | | |

### (c) Katibu Mkuu Kiongozi na Makatibu Wakuu

| ***Ibara Na.*** | ***Kichwa cha Habari*** | ***Maoni ya Mabaraza*** | ***Sababu ya Maoni*** | ***Marekebisho ya Tume*** |
|---|---|---|---|---|
| 98. | Katibu Mkuu Kiongozi | (i) Ibara ndogo ya (1) irekebishwe na iandikwe kama ifuatavyo:<br>"(1) Kutakuwa na Katibu Mkuu Kiongozi atakayeteuliwa na Rais baada ya kupendekezwa na Tume ya Utumishi wa Umma kutoka miongoni mwa watumishi waandamizi na kuthibitishwa na Bunge". | | 1. Ibara ya 98 itakuwa Ibara ya 105.<br>2. Ibara ndogo ya (1) imefanyiwa marekebisho na itasomeka " Kutakuwa na Katibu Mkuu Kiongozi atakayeteuliwa na Rais kutoka miongoni mwa Watumishi watatu waandamizi watakaopendekezwa na Tume ya Utumishi wa Umma na kuthibitishwa na Bunge.<br><br>3. Ibara ndogo ya (3) imefanyiwa marekebisho na itasomeka ifuatavyo:<br><br>Katika wadhifa wake wa Katibu wa Baraza la Mawaziri, Katibu |
| | | (ii) Ibara ya 98,Sifa za Katibu Mkuu kiongozi ziainishwe. | | |
| | | (iii) 98(1) isomeke "Rais atateua kutoka orodha ya watumishi wa Umma, Watumishi watatu waandamizi na kupigiwa kura na Bunge". | | |
| | | (iv) Ibara ndogo ya (2) na (3) zinazungumzia Mamlaka ya Katibu Mkuu Kiongozi kuwa Mkuu wa Utumishi wa Umma, lakini utumishi wa umma siyo suala la Muungano kwa mujibu wa ibara ya 60, ikisomwa pamoja na Nyongeza inayoelezea mambo ya Muungano. Ili kuimarisha Muungano na kupunguza gharama, inashauriwa kwamba suala la utumishi wa umma liongezwe kwenye mambo ya Muungano na pasiwepo mifumo sambamba kwenye serikali za washirika wa Muungano. | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | (v) Ibara hii irekebishwe ili Katibu Mkuu Kiongozi asithibitishwe na Bunge; | | Mkuu Kiongozi atakuwa Mtendaji Mkuu katika Ofisi ya Baraza la Mawaziri, na atatekeleza shughuli zifuatazo kwa kufuata maagizo ya jumla au maalum atakayopewa na Rais, yaani:<br>(a) kuandaa ratiba ya mikutano na kutayarisha orodha ya shughuli za Baraza la Mawaziri;<br>(b) kuandika na kuweka kumbukumbu za mikutano;<br>(c) kutoa taarifa na maelezo ya uamuzi wa Baraza la Mawaziri kwa kila mtu au chombo cha umma kinachohusika na uamuzi uliotolewa; na<br>(d) kutekeleza kazi na shughuli nyingine zozote ambazo Rais ameagiza. |
| | | (vi) Ibara hii irekebishwe kwa kueleza kazi za Katibu wa Baraza la Mawaziri kuwa ni Mkuu wa Utumishi wa Umma na Katibu wa Baraza la Ulinzi na Usdalama wa Taifa; | | |
| | | (vii) Iongezwe ibara ndogo mpya ya (5) itakayokuwa kama ifuatavyo:<br>"(5) Katika wadhifa wake wa Katibu wa Baraza la Ulinzi na Usalama wa Taifa, Katibu Mkuu Kiongozi atakuwa ndiye Mkuu na Mratibu wa Sekretarieti ya Baraza la Ulinzi na Usalama wa Taifa." | Kutambua nafasi ya Katibu Mkuu Kiongozi. | |

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Maoni* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| | | | | 4. Ibara ndogo ya (4) imefanyiwa marekebisho na itasomeka kama ifuatavyo:<br>Akiwa Mkuu wa Utumishi wa Umma, Katibu Mkuu Kiongozi atakuwa na mamlaka ya kutoa maelekezo ya mara kwa mara kuhusiana na masuala ya utumishi wa umma.<br><br>5. Imeongezwa Ibara ndogo ya (5) ambayo itasomeka:<br>Katika wadhifa wake wa Katibu wa Baraza la Ulinzi na Usalama wa Taifa, Katibu Mkuu Kiongozi atakuwa Mkuu na Mratibu wa Sekretarieti ya Baraza la Ulinzi na Usalama la Taifa.<br><br>6. Imeongezwa Ibara ndogo ya (6) |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | | ambayo itasomeka: Katibu Mkuu Kiongozi hatashika madaraka yake mpaka awe ameapa mbele ya Rais kiapo cha utii na uaminifu au kiapo kingine chochote kinachohusu utendaji wa kazi zake kitakachowekwa kwa mujibu wa sheria za nchi. |
| 99. | Makatibu Wakuu | (i) Imependekezwa kuwa makatibu wakuu na naibu katibu wakuu wathibitishwe na Bunge baada ya kuteuliwa. | Kutokana na unyeti wa majukumu waliyonayo. | 1. Ibara ya 99 itakuwa Ibara ya 106.<br><br>2. Marginal Note iongezwe maneno na ''Naibu Makatibu Wakuu.<br><br>3. Ibara ndogo ya (5) imerekebishwa na isomeke ''Katibu Mkuu au Naibu Katibu Mkuu hatashika |
| | | (ii) 99(1).Nafasi za Makatibu wakuu ziwe wazi na zishindaniwe kwa mujibu wa sifa.Utumike mfumo kama unaotumika Kenya kuwapata watendaji hawa. | | |
| | | (iii) 99- Marginal note isomeke "Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu". | | |
| | | (iv) Ibara ndogo ya (1) irekebishwe ili Makatibu Wakuu wasipendekezwe na Tume ya Utumishi wa Umma; | Tume haina uwezo wa kufanya upekuzi na vyombo vya kutambua watu wenye uwezo. | |
| | | (v) Katika ibara ndogo ya (3), maneno "kwa mapendekezo ya Tume ya Utumishi" yafutwe. | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | (vi) Katika ibara ndogo ya (4), kuongeza maneno "wa Wizara aliyopangiwa" baina ya maneno "Waziri" na "kwa". | | madaraka yake mpaka awe ameapa mbele ya Rais kiapo cha utii na uaminifu au kiapo kingine chochote kinachohusu utendaji wa kazi zake kitakachowekwa kwa mujibu wa sheria za nchi. |
| | | (vii) Ibara ndogo ya (5) irekebishwe ili kiapo cha Katibu Mkuu Kiogozi kihamie katika Ibara ya 98. | | |

## (d) Utendaji Kazi wa Baraza la Mawaziri

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| 100. | Kamati Maalumu ya Makatibu Wakuu | Maelezo ya pembeni (Marginal note) yabadilishwe na yaandikwe "Utekelezaji wa shughuli za Baraza la Mawaziri". | Kibebe maudhui. | Ibara ya 100 itakuwa ya 107 na itabaki kama ilivyo. |
| 101. | Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri | (i) Ibara ndogo ya (1) irekebishwe ili kuondoa maneno "Baraza la Mawaziri" na kuweka maneno "Katibu wa Baraza la Mawaziri". | | 1. Ibara ya 101 itakuwa ya 108.<br>2. Ibara ndogo ya 108(1), imeongezwa maneno ''Kama itakavyopangiwa na Katibu wa Baraza la |
| | | (ii) 101(1) Maneno yarekebishwe na yasomeke "….kama itakavyopangiwa na Katibu wa Baraza la Mawaziri". | | |

| ***Ibara Na.*** | ***Kichwa cha Habari*** | ***Maoni ya Mabaraza*** | ***Sababu ya Maoni*** | ***Marekebisho ya Tume*** |
|---|---|---|---|---|
| | | (iii)Katika Ibara ndogo ya (2) neno 'linaweza' lifutwe na badala yake liandikwe neno 'litatunga'. | | Mawaziri" badala ya maneno "kama itakavyopangiwa na Baraza la Mawaziri". |
| | | (v) Ibara ndogo ya (2) ifutwe. | Serikali huongozwa na miongozo, kanuni, taratibu na nyaraka mbalimbali za utumishi.<br>Ni vigumu kwa Bunge kutunga sheria ya jumla inayotoa utaratibu wa kutekeleza shughuli za Serikali. | |
| | | (v)Ibara hii iingie baada ya ibara ya 96 | | |

# SURA YA NANE YA RASIMU

## 8.0 URATIBU WA MAHUSIANO YA WASHIRIKA WA MUUNGANO

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Maoni* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| | URATIBU WA MAHUSIANO YA WASHIRIKA WA MUUNGANO | Katika Sura ya Nane isomeke kama ifuatavyo:<br>“UTARATIBU WA MAHUSIANO KATIKA MUUNGANO”. | Kukidhi matakwa ya Serikali mbili. | |
| 102. | Tume ya Mahusiano ya Uratibu wa Serikali | (i) Maneno ya pembeni yasomeke “Tume ya Uratibu wa Utekelezaji wa Masuala ya Muungano”. | | Ibara ya 102 itakuwa ya 109 na itabaki kama ilivyo. |
| | | (ii) Katika ibara hii neno “Tume” lifutwe na badala yake litumike neno “Baraza la Mahusiano”. | Kutokana na watu wanaunda Tume hii, likiwa Baraza litakuwa na nguvu zaidi. | |
| | | (iii) Ibara hii irekebishwe ili kuweka muundo mpya wa Tume ya Utaribu kama ifuatavyo:<br>a. Rais wa Muungano ndio awe Mwenyekiti;<br>b. Marais wa Nchi Washirika;<br>c. Wanasheria Wakuu wa Nchi Washirika;<br>d. Mawaziri Wakaazi;<br>e. Makatibu Wakuu Viongozi wa Nchi Washirika. | | |
| | | (iv) Ibara ndogo ya (1) ili kumfanya Rais wa Shirikisho ndiyo awe | Marais wa nchi Washirika wanapaswa kuwa na | |

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Maoni* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| | | Mwenyekiti wa Tume. | hadhi sawa na ile ya Makamu wa Rais. Kwa kuwa msingi wa Shirikisho ni Tanganyika na Zanzibar. | |
| | | (v) Ibara hii irekebishwe ili kuwafanya Mawaziri wa mambo ya Muungano kuwa wajumbe. | | |
| | | (vi) Katika Ibara ndogo ya (2) ziongezwe aya mpya zitakazoeleza kwamba, Mwanasheria Mkuu na Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania watakuwa Wajumbe wa Tume kwa nafasi zao (ex-officio members). | | |
| | | (vii) Ibara ndogo ya (2) iandikwe "Tume ya Uratibu wa Utekelezaji wa Masuala ya Muungano itaundwa na Wajumbe wafuatao". | | |
| | | (viii) Aya (d) ya ibara ndogo ya (2) iandikwe "Waziri mwenye mamlaka ya mambo ya Muungano". | Ili kusaidia kutoa ufafanuzi wa hoja husika. | |
| | | (ix) Iongezwe ibara mpya mara baada ya ibara ya 102 itakayokuwa 103 itakayoeleza mambo yafuatayo:<br>(x) Mtendaji Mkuu wa Tume ya Uratibu ya Muungano;<br>(xi) Sekretarieti; na<br>(xii) Masharti kuhusu nyenzo na rasilimali watu na fedha. | Kuiwezesha Tume kufanya kazi zake kwa ufanisi. | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | (xiii) Ibara hii irekebishwe kwa kuzingatia muundo wa Serikali mbili, na Kamati ifanye kazi zake ndani ya Mfumo wa Serikali. | Kutatua kero za Muungano. | |
| | | (xiv) Aya (e) ifutwe. | Hakutakuwa na Waziri wa Mambo ya Ndani. | |
| | | (xv) Kichwa cha habari kirekebishwe kisomeke "URATIBU WA MAHUSIANO YA MUUNGANO". | | |
| | | (xvi) Tume ya Mahusiano ibaki. | (a) Kuleta uwiano wa madaraka katika utendaji kazi.<br>(b) Kuratibu na kusimamia mahusiano katika Serikali Tatu. | |
| | | (xvii) Neno "Tume" lifutwe na badala yake iitwe "Wizara". | | |
| | | (xviii) Neno "Tume" lifutwe iitwe "Jopo". | | |
| | | (xix) Ibara hii ibaki kama ilivyo. | Ili kuweka uwiano kati ya Washirika wa Muungano. | |
| | | (xx) Neno Washirika wa Muungano lifutwe na badala yake isomeke Serikali ya Muungano. | | |
| | | (xxi) SURA yote ifutwe. | Kukidhi muundo wa Serikali Mbili. | |
| | | (xxii) Rais wa Muungano ndio awe Mwenyekiti wa Tume. | Ndiye Mtendaji Mkuu katika Serikali. | |
| | | (xxiii) Maneno "Rais wa Tanzania Bara" yasomeke Rais wa Tanganyika. | | |
| | | (xxiv) Kazi na majukumu ya Tume | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | yaelezwe katika sheria. | | |
| | | (xxv) Ibara ndogo ya (2)(a) ifutwe. | | |
| | | (xxvi) Ibara ndogo ya (2)(b) isomeke "awe Waziri anayeshughulikia Mambo ya Muungano". | | |
| | | (xxvii) Marais wa Washirika ndio wawe Makamu wa Rais. | Kila Makamu awe msaidizi wa Rais kwa upande wake. | |
| | | (xxviii) Waziri wa Mambo ya Nje asiwepo katika Tume ya Mahusiano. | (a) Mambo ya Nje lisiwe suala la Muungano.<br>(b) Mambo ya Nje ndio inayoifanya nchi kuwa na mamlaka kamili. | |
| | | (xxix) Ibara ya 102 hadi 104 zifutwe. | Malengo na majukumu yake hayatekelezeki. | |
| | | (xxx) Wajumbe wa Tume hii wajumuishe mawaziri wote wenye dhamana ya mambo ya Muungano. | | |
| | | (xxxi) Tume iwe na uwezo wa kumwalika waziri yeyote wa serikali ya Muungano kuhudhuria vikao vyake | | |
| | | (xxxii) Rais wa Jamhuri ya Muungano awe Mwenyekiti na wajumbe wengine wawe Marais wa washirika wa Muungano; Mawaziri Wakaazi; wanasheria wakuu na makatibu wakuu viongozi. | | |
| | | (xxxiii) 102(1) Marginal Note iwe, Tume ya Uratibu wa | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | utekelezaji wa masuala ya muungano” | | |
| | | (xxxiv) Marginal note (2) iwe, “Tume ya Uratibu Utekelezaji wa Masuala ya Muungano itaundwa na wajumbe wafuatao..,” | | |
| | | (xxxv) 102(2)(d) iwe, Waziri mwenye mamlaka ya mambo ya Muungano. | | |
| | | (xxxvi) Isiwepo kwa kuwa kuna Kamati ya Kuratibu Mahusiano ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya sasa ichukue | | |
| | | (xxxvii) Wajumbe wa Tume wawe pamoja na: Mwanasheria Mkuu na Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambao watakuwa ex-officio.<br>(xxxviii) Mawaziri wa fedha wawe sehemu ya Tume ya Uratibu wa Serikali.<br>(xxxix) Rais wa SHIRIKISHO awe ndiye Mwenyekiti wa Tume na sio Makamu wake. | | |
| 103. | Malengo ya Tume | (i) Ibara hii ifutwe. | (i) Katika mfumo wa sasa kuna kamati ya kuratibu utekelezaji wa Masuala ya Muungano ambayo inapendekezwa irasimishwe kikatiba.<br>(ii) Ibaki kama utaratibu | Ibara ya 103 itakuwa ya 110 na itabaki kama ilivyo. |

| ***Ibara Na.*** | ***Kichwa cha Habari*** | ***Maoni ya Mabaraza*** | ***Sababu ya Maoni*** | ***Marekebisho ya Tume*** |
|---|---|---|---|---|
| | | | unaotumika sasa, isipokuwa utaratibu huo uelezwe (urasimishwe) kwenye Katiba.<br>(iii) Ni msingi wa Serikali Tatu. Itasababisha migogoro kwani haikuonesha namna ya kuondoa migogoro hiyo. | |
| | | (ii) Katika aya (a) maneno “mashauriano na mshikamano baina ya Serikali ya Muungano na Serikali za Washirika wa Muungano” yafutwe na badala yake iandikwe “mambo ya Muungano baina ya Serikali”; | | |
| | | (iii) Aya (b) neno “Washirika” lifutwe na badala yake iandikwe “Serikali ya Muungano na Serikali ya Zanzibar”; | | |
| | | (iv) Katika aya (b) maneno “kwa lengo la kuwezesha kufanana kwa kiwango cha utoaji huduma kwa wananchi wote” yafutwe na badala yake yawepo maneno “kwa lengo la kuwezesha kubadilishana uzoefu”. | Kwa kuwa Serikali za Washirika ndizo zenye jukumu la kusimamia maendeleo ya uchumi na kiwango cha utoaji huduma kwa wananchi, kufanana kwa kiwango cha utoaji huduma kutategemea juhudi za nchi mshirika. | |
| | | (v) Aya (d) maneno “na Washirika wa Muungano” yafutwe na badala yake iandikwe “Serikali ya | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | Zanzibar"; | | |
| | | (vi) Iongezwe aya (e) itakayoandikwa kama ifuatavyo:<br>"(e) Tume hii itakuwa na majukumu mengine yoyote kama itakavyoelezwa na Katiba hii au sheria itakayotungwa na Bunge". | | |
| | | (vii) Ibara hii ibaki kama ilivyo. | (a) Ili kusaidia nchi Washirika wa Muungano.<br>(b) Inaimarisha Muungano na kuharakisha utatuzi wa migogoro. | |
| | | (viii) Ibara ya 103 na 104 ziunganishwe. | Kwa sababu zinafanana. | |
| | | (ix) Maneno katika 103(b), "kwa lengo la kuwezesha kufanana kwa kiwango cha utoaji huduma kwa wananchi wote" yaondolewe na iwe: "kwa lengo la kuwezesha kubadilishana" | | |
| | | (x) 103(a) iwe, mambo ya muungano baina ya serikali.' | | |
| | | (xi) Neno "washirika" liondolewe na badala yake liwekwe, " serikali ya muungano na serikali ya Zanzibar" | | |
| | | (xii) Iongezwe (e) itakayosomeka kuwa, "Tume hii itakuwa na majukumu mengine yeyote kama itakavyoelezwa na katiba hii au sheria itakayotungwa na Bunge " | | |
| | | (xiii) Ifutwe na badala yake kamati ya sasa ya Kuratibu utekelezaji wa | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | masuala ya Muungano irasimishwe kikatiba | | |
| | | (xiv) Ibara ya 103(b) ifutwe kwani inaipa Tume majukumu yakujihusisha na mambo yasiyo ya muungano | | |
| | | (xv) 103 (b & c): Nia ni nzuri lakini kila nchi Mshirika iwe na uwajibikaji katika kugharimia kulingana na kiwango chake cha uwakilishi katika Serikali ya Muungano, na kwa vyovyote vile itakavyokuwa, wajibu huo uainishwe bayana kwenye Katiba | | |
| | | (xvi) Yaongezwe maneno yaliyowekewa mkazo hapa: viwango bora vya utoaji huduma kulingana na viwango vya kikanda na kimataifa. | | |
| | | (xvii) Iongezwe: kulenga kujenga umoja kidemokrasia kwa kuongeza mambo ya Muungano na kuimarisha mahusiano na mashirikiano kwa njia, taratibu na vigezo wazi na muafaka. | | |
| 104. | Majukumu ya Tume | (i) Ibara hii ifutwe. | Katika mfumo wa sasa kuna kamati ya kuratibu utekelezaji wa Masuala ya Muungano ambayo inapendekezwa irasimishwe kikatiba. | 1. Ibara ya 104 itakuwa ya 111.<br>2. Katika Ibara ndogo ya 111(1)(c) mwisho wa sentensi isomeke ''nchi washirika"<br>3. Katika Ibara |
| | | (ii) Katika ibara (1)(a)(i) maneno "Washirika wa Muungano" yafutwe na badala yake iandikwe 'Serikali | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | ya Zanzibar" na neno "mashirikiano" lifutwe na badala yake iiandikwe "ushirikiano". | | ndogo ya 111(3) neno "Bunge linaweza" liondolewe na badala yake isomeke "Bunge litatunga". |
| | | (iii) Aya (i) ya ibara ndogo ya (1)(a) ifutwe. | | |
| | | (iv) Aya (a) na (b) ya ibara ndogo ya (1) zifutwe. | Majukumu ya Tume: Tunashauri Ibara ya 104(1)(a)(ii) na (b) zifutwe na ziondoshwe kabisa katika Rasimu Katiba. Hii ni kutokana na sababu ya kutoa uhuru kwa kila nchi mshirika wa Muungano awe na mamlaka ya kutunga sheria na sera zake wenyewe katika mambo yasiyo ya Muungano. | |
| | | (v) Katika ibara (1)(a)(i) maneno "Washirika wa Muungano" yafutwe na badala yake iandikwe 'Serikali ya Zanzibar" na neno "mashirikiano" lifutwe na badala yake iiandikwe "ushirikiano". | | |
| | | (vi) Katika aya (e) ya ibara ndogo ya (1) maneno 'Washirika wa Muungano" yafutwe na badala yake iandikwe "Serikali ya Zanzibar". | | |
| | | (vii) Aya (ii) ya ibara ndogo ya (1)(e) ifutwe. | | |
| | | (viii) Neno "utatuzi" katika aya (e) ya ibara ndogo ya (1) ifutwe. | | |
| | | (ix) Ibara ndogo ya (1) aya (b) ifutwe na badala yake iandikwe kama | | |

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Maoni* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| | | ifuatavyo:<br>"(b) kusimamia, kuratibu na kuhakikisha kwamba kuna kuwiana kwa sera na sheria za Washirika wa Muungano katika maswala yasiyo ya muungano". | | |
| | | (x) Ibara ndogo ya (3)(a) maneno 'Washirika wa Muungano" yafutwe na badala yake iandikwe "Serikali ya Zanzibar". | | |
| | | (xi) Inapendekezwa iongezwe ibara ndogo mpya ya (4) itakayoeleza kuanzishwa kwa Sekretarieti ya Tume ambayo itakuwa na uwakilishi sawa kutoka Nchi Washirika wa Muungano, ibara hiyo iandikwe kama ifuatavyo:<br>"(4) Kutakuwa na Sekretariati ya Tume yenye wajumbe kwa idadi sawa kutoka pande mbili za Muungano". | | |
| | | (xii) Ibara ndogo ya (1)(b) irekebishwe kwa kutoonyesha uwiano kati ya sera na sheria. | | |
| | | (xiii) Ibara hii ifutwe. | (a) Ili kuondoa migogoro itakayoweza kujitokeza.<br>(b) Itawabana watu wa upande mmoja wa Muungano. | |
| | | (xiv) Ushirikiano wa Washirika wa Muungano uwe wa lazima ili iweze kufanya kazi zake | | |
| | | (xv) Isomeke "kusimamia, kuratibu na | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | kuhakikisha kwamba kuna kuwiana kwa sera na sheria za Washirika wa Muungano katika maswala yasiyo ya muungano." | | |
| | | (xvi) Ibara 104(3)(b) iseme "Bunge litunge sheria kuanzisha Sekretarieti yenye wajumbe wenye uwiano sawa kutoka washirika wa muungano yenye mamlaka ya kiutendaji kuisaidia Tume ya Uhusiano na Uratibu wa Serikali. Mwenyekiti na Makamu mwenyekiti wasitoke nchi moja ya washirika wa Muungano na wawe na ukomo wa utumishi." | | |
| | | (xvii) Ibara ya 104(1)(b) ifutwe ili Tume isiwe na majukumu ya kuingilia masuala yasiyo ya muuungano. | | |
| | | (xviii) 104(1)(c) Maneno.. " kwa niaba ya nchi" yafutwe na iwe. " ...kwa mambo ya muungano" | | |
| | | (xix) Katika Ibara ya 104(1)(e), Tume isipewe kazi ya kushughulikia migogoro na badala yake ifanye kazi ya usuluhishi pekeee | | |
| | | (xx) Neno "utatuzi" liondolewe kwa kuwa Tume ya Uratibu wa Mahusiano ya Muungano ni chombo cha kisiasa zaidi na kwa muundo wake hakiwezi kufanya kazi ya utatuzi wakati wa migogoro baina ya pande za | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | muungano ambapo migogoro yenyewe inatarajiwa kuwasilishwa na hao wanaotarajiwa kufanya utatuzi.<br>(xxi) Kuwe na Baraza la Marais chini ya Rais wa shirikisho pamoja na Marais wa washirika wa Muungano wakisaidiwa na mawaziri waandamizi | | |
| | | | | Imeongezwa Ibara mpya ya 112, inayozungumzia ''Uanzishwaji wa Sekretarieti ya Tume ya Mahusiano na Uratibu" |

# SURA YA TISA YA RASIMU

## 9.0 SEHEMU YA KWANZA: KUUNDWA KWA BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO

| ***Ibara Na.*** | ***Kichwa cha Habari*** | ***Maoni ya Mabaraza*** | ***Sababu ya Maoni*** | ***Marekebisho ya Tume*** |
|---|---|---|---|---|
| | SURA YA TISA | Mpangilio wa Ibara za 128-132 uwe kama ifuatavyo:<br>Ianze ibara ya 129 ifuate ya 130, 132, 131, 129 na Ibara ya 131 iwe ya 132. | Mtiririko unaopendekezwa ni mzuri zaidi kiuandishi. | |
| 105. | Bunge la Jamhuri ya Muungano | (i) Katika ibara ndogo ya (2)(b) maneno "wenye ulemavu" yaongezwe mara baada ya maneno "Wabunge Watano" na maneno "kwa uwiano wa kuzingatia Washirika wa Muungano" yafutwe. | | 1. Ibara 105 itakuwa 113.<br>2. Ibara ya 113(2)(a) imerekebishwa na inasomeka "Wabunge sabini wa kuchaguliwa kupitia majimbo ya uchaguzi yatakayotangazwa na Tume Huru ya Uchaguzi, hamsini kutoka Tanganyika na Ishirini kutoka Zanzibar.<br>3. Ibara ndogo ya (3) imerekebishwa na itasomeka kama ifutavyo:<br>4. "katika kila jimbo la uchaguzi kutakuwa na |
| | | (ii) Ibara ndogo ya (2)(b) inapendekeza kuwa wabunge watano wateuliwe kupitia katika vyama vyao vya walemavu. | Ili kupata wawakilishi waliokusudiwa watakao wakilisha walemavu. | |
| | | (iii) Aya ya (b) katika ibara ndogo ya (2) irekebishwe na kiandikwe kama ifuatavyo: | (a) Aya ya (b) katika ibara ndogo ya (2) irekebishwe na kiandikwe kama ifuatavyo: | |
| | | "(b) Wabunge ishirini watakaochaguliwa kutokana na uwiano wa kura zilizopigwa kwa vyama vya siasa katika uchaguzi wa Bunge la Jamhuri ya Muungano, kwa kuzingatia uwiano sawa wa Washirika wa Muungano." | "(b) Wabunge ishirini watakaochaguliwa kutokana na uwiano wa kura zilizopigwa kwa vyama vya siasa katika uchaguzi wa Bunge la Jamhuri ya Muungano, kwa kuzingatia uwiano | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | sawa wa Washirika wa Muungano." | nafasi mbili za ubunge, moja kwa ajili ya mwanamke na moja kwa ajili ya mwanamme" |
| | | (iv) Aya (b) ya Ibara ndogo ya (2) irekebishwe ili kati ya hao wabunge watano wawakilishi wa watu wenye ulemavu wanawake wasipungue wawili. | Ibara hii pamoja na kwamba imetoa nafasi kwa kundi la watu wenye ulemavu kuingia bungeni lakini haijaweka wazi uwiano wa kijinsia wa watu hao watano watakaoteuliwa na Rais. | |
| | | (v) Aya (b) ya ibara ndogo ya (2) ifutwe. | Ili kuondoa mgongano wa kimakundi.<br>Walemavu wana nafasi sawa ya kugombea kwenye majimbo kama wabunge wengine na sio kutegemea nafasi za kuteuliwa na Rais kwani ikitokea mlemavu amechaguliwa na wananchi na pia anayo nafasi ya kuteuliwa basi watapata viti vingi vya uwakilishi. | |
| | | (vi) Ibara ndogo ya (3) ibadilishwe ili kuwepo na idadi sawa ya wabunge kutoka Zanzibar na Tanganyika. | Kuweka msingi wa usawa kwa washirika wa Muungano. | |
| | | (vii) Ibara ndogo ya (3) irekebishwe na iandikwe kama ifuatavyo:<br>"(3) Kwa madhumuni ya ibara ndogo ya (2)(a), kila mmoja wa Washirika wa Muungano atagawanywa katika majimbo kumi ya uchaguzi.<br>(4) Kwa madhumuni ya ibara | | |

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Maoni* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| | | ndogo ya (3) kila wilaya kwa upande wa Tanganyika na mkoa kwa upande wa Zanzibar litakuwa jimbo la uchaguzi". | | |
| | | (viii) Katika ibara ndogo ya (3) neno "Mkoa" iandikwe "Wilaya". | (a) Ili kuleta uwiano baina ya Tanzania Bara na Zanzibar.<br>(b) Kuepusha ugawaji wa majimbo kwa dhamira ya kisiasa. | |
| | | (ix) Ibara ndogo ya (3) irekebishwe ili kigezo kiwe ni idadi ya watu badala ya mkoa au wilaya. | (c) Kuepuka kero ya uwiano inayoweza kutokea. | |
| | | (x) Ibara ndogo ya (3), (4) na (5) zirekebishwe ili Wabunge wa Bunge la Muungano ukiondoa wale wanaowakilisha watu wenye ulemavu, wawe hamsini na kila mshirika wa muungano atoe wabunge 25. | Ili kupunguza gharama za uendeshaji wa muungano, wabunge hao wachaguliwe na mabunge ya nchi washirika kama utaratibu unaotumika sasa katika kuwapata wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki.<br><br>Isipokuwa kuwa wabunge hao wasiwe miongoni mwa wabunge wa mabunge ya nchi washirika ili kuongeza ufanisi kwa kutowatwisha wabunge majukumu mengi.<br>Hivyo kwa mujibu wa utaratibu huu unaopendekezwa kwamba, ibara nyingine kadhaa pia zirekebishwa | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | ili kukidhi utaratibu huu unaopendekezwa ikiwemo ibara ya 119. | |
| | | (xi) Ibara ndogo ya (4) ifutwe na badala yake iandikwe kama ifuatavyo:<br>“(4) Katika kila jimbo la uchaguzi kutakuwa na nafasi mbili za Ubunge.” | Kuondoa uwezekano wa watu wa jinsia moja iwe wanaume au wanawake kuweza kupata nafasi. | |
| | | (xii) Ibara ndogo ya(4) irekebishwe ili uwakilishi wa jimbo usitokane na usawa wa kijinsia bali wawakilishi wawili wa jimbo watokane na ushindani wenye mazingira ya fursa sawa. | Tunatambua umuhimu wa uwiano wa kijinsia kwenye vyombo vya maamuzi lakini uwakilishi uwe wa ushindani na kila mmoja awe na nafasi ya kuwa mwakilishi. | |
| | | (xiii) Ibara hii irekebishwe ili Rais awe sehemu ya Bunge. | Kuendana sambamba na mfumo wa kibunge.<br>Kutokana na nafasi yake ya kusaini Miswada ya Sheria. | |
| | | (xiv) 105(2) (a)-Idadi ya Wabunge iwe 75 ambapo 70 watakuwa wa kuchaguliwa kupitia majimbo ya uchaguzi ambapo Tanzania Bara watakuwa 50 na Zanzibar watakuwa 20 na watano watakuwa wa viti maalum vya walemavu. | Kuweka idadi kamili ya wabunge na kuipa Tume Huru ya Uchaguzi uwezo wa kugawa majimbo ya uchaguzi. | |
| | | (xv) 105(3)- Tume Huru ya Uchaguzi itakuwa na mamlaka ya kugawa na kutangaza majimbo ya uchaguzi kwa Tanzania Bara na Zanzibar. | Ili kuzuia nchi washirika kujiongezea mikoa au wilaya kwa madhumuni ya kuongeza majimbo ikitiliwa maanani kuwa suala la mikoa na wilaya | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | si la Muungano. | |
| | | (xvi) Ibara hii irekebishwe ili kuweka idadi sawa ya Wabunge toka pande za Muungano. | Kuleta uwakilishi uliyosawa. Kwa kuwa kila upande utakuwa tayari una Bunge/ Baraza lake. | |
| 106. | Muda wa Bunge | (i) Ibara ndogo ya (2) irekebishwe kwa kuongeza maneno "bila kuathiri haki ya Wabunge kulipwa mishahara kwa muda wote wa miaka mitano" katika tafsiri ya maneno "maisha ya Bunge". | Kuwawezesha wabunge kupata stahili zao hadi Bunge jipya litakapoapishwa. | Ibara 106 inakuwa 114.<br>Inabaki kama ilivyo. |
| | | (ii) Iongezwe ibara ndogo mpya ya (2) ambayo itasema "Mbunge ataendelea kuwa mbunge hadi pale atakapoapishwa mbunge mwingine kushika nafasi ya mbunge aliyemaliza muda wake". | | |
| 107. | Madaraka ya Bunge | (i) Ibara ndogo (2)(a) irekebishwe na iandikwe kama ifuatavyo:<br>"(2)(a) kujadili na kutoa maelekezo katika mambo yote yenye maslahi kwa taifa na umma wa Watanzania"; | | 1. Ibara ya 107 inakuwa 115.<br>2. Ibara ndogo ya 2(f) inakuwa ibara ndogo ya 2(a) na inasomeka kama ifuatavyo:<br>"kutunga sheria pale ambapo utekelezaji unahitaji kutungiwa sheria" |
| | | (ii) Katika ibara ndogo ya (2) aya (e) yaongezwe maneno "katika au nje ya Jamhuri ya Muungano" baada ya neno "serikali"; | | |
| | | (iii) Aya (h) ya Ibara ya (2) ifutwe. | (a) Kazi inayotajwa ya kujadili na kuridhia mikataba inayohusisha rasilimali na maliasili zinazosimamiwa na Serikali ya Jamhuri | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | ya Muungano si jukumu la Bunge bali ni la Serikali.<br>(b) Rasilimali na mali asili sio masuala ya Muungano.<br>(c) Litapunguza mvutano wa uwekezaji nchini. Pia, Serikali ndiyo mamlaka husika katika kuingia na kusimamia Mikataba na wawekezaji Bunge lisumamie matokeo ya Mikataba hii. | |
| | | (iv) Aya (h) ya Ibara ndogo ya (2) ibadilishwe kwa kuzingatia sababu zilizoelezwa. | (a) Serikali inaweza kushindwa kufanya kazi zake kikamilifu na pia inaweza kuvujisha siri za mikataba ya Serikali katika masuala ya rasilimali za Taifa.<br>(b) Shughuli za Serikali zinazohusu mikataba ya kibiashara zinahitaji usiri ili kuzuia hujuma za washindani, hivyo kuiweka mikataba hii katika mijadala ya Bunge usiri huo utatoweka. | |
| | | (v) Iongezwe aya mpya ya (i) katika ibara ndogo ya (2) ambayo iongeze | Kuzuia utendaji wa makosa ya wazi. | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | jukumu la kufuatilia utekelezaji wa mikataba hiyo. | | |
| | | (vi) 107 kiongezwe kifungu kidogo kitakachosomeka:<br>(vii) "Bunge litaunda kamati ya uteuzi wa Tume ya watu (12),watu (6) kutoka kila upande wa Muungano,Wawili ni Wanasheria kutoka Tanganyika na Wawili Wanasheria kutoka Zanzibar,Wabunge (4) kutoka Tanganyika na Wabunge (4) kutoka Zanzibar miongoni mwao wawili wawe ni Wanawake na wawili ni Wanaume.Kamati hii itakuwa na jukumu la kutafuta majina ya wajumbe wa Tume kwa mujibu wa sifa zitakazotajwa kwenye katiba kwa kila Tume.Wajumbe wa Tume hizo watapatikana baada ya kutangaza majina hayo kwa siku (30),na kutoa muda wa pingamizi(malalamiko) wa siku (15), kuwafanyia usaili wa hadharani,watakao faulu watapelekwa Bungeni kwa ajili ya kujadiliwa na kuthibitishwa".<br>(viii) Tume zitakazohusika na mchakato huu ni pamoja na Tume ya Utumishi wa Mahakama, Tume ya Sheria na Katiba, Tume ya Utumishi wa umma, Tume ya uchunguzi wa Rushwa na ubadhirifu wa mali za | | |

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Maoni* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| | | Serikali,Tume ya Maafa na Majanga ya Taifa na Tume ya Ulinzi na Usalama wa Taifa.Tume hizi zitawajibika kwa Spika wa Bunge. | | |
| 108. | Mipaka ya Bunge katika kutumia madaraka yake | (i) Ibara ndogo ya (1) irekebishwe na badala yake kuweka neno iandikwe kama ifuatavyo: "(1) Katika kutekeleza madaraka ya kuisimamia Serikali kwa mujibu wa Katiba hii, wajibu wa Bunge itakuwa ni kuielekeza Serikali na endapo Bunge halitaridhishwa na hatua zilizochukuliwa na Serikali katika utekelezaji wa suala lililotolewa ushauri, basi Bunge litakuwa na haki ya kuiwajibisha Serikali kwa mujibu wa madaraka iliyopewa katika Katiba hii". | | Ibara ya 108 inakuwa ibara ya 116 na inabaki kama ilivyo. |
| | | (ii) Ibara ndogo ya (2) irekebishwe na iandikwe kama ifuatavyo: "(2) Kwa madhumuni ya Ibara ndogo ya (1), Bunge halitachukua hatua yoyote ya kiutendaji ambayo, kwa desturi ni shughuli za Serikali, na halitatoa maagizo yoyote ya kiutendaji kwa Serikali na Watumishi wa Umma, isipokuwa Bunge litaelekeza kuhusu suala lolote lililo katika dhamana ya Waziri anayehusika". | | |
| 109. | Madaraka ya Bunge kutunga sheria | Ibara hii ifutwe na badala yake iandikwe ibara ya 64(1), (2), (3) na (4) ya Katiba ya sasa. | | Ibara ya 109 inakuwa ibara ya 117 na ibaki kama ilivyo. |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| 110. | Utaratibu wa kutunga sheria | (i) Ibara ndogo ya (1) irekebishwe na iandikwe kama ifuatavyo: "(1) Bunge la Shirikisho la Tanzania litatumia madaraka yake ya kutunga sheria kwa kujadili na kuipitishwa Muswada wa Sheria ambao utawekwa saini na Rais wa Shirikisho". | Jina la Bunge na pia kubainisha Rais anayetamkwa | 1. Ibara ya 110 inakuwa 118.<br>2. Imeongezwa ibara ndogo ya (4) na inasomeka; "Muswada wa sheria utahesabiwa kuwa umepitishwa na bunge iwapo utaungwa mkono kwa kura za wabunge wasiopungua theluthi mbili ya wabunge wote kutoka Tanganyika na wabunge wasiopungua theluthi mbili ya wabunge wote kutoka Zanzibar"<br>3. Ibara ndogo ya (4) imekuwa ya (5). |
| | | (ii) 110.Ibara itamke bayana:<br>(iii) (a)Kwamba Sheria na kanuni zake zitatungwa katika lugha ya Taifa (Kiswahili).<br>(iv) (b)Utaratibu ambao Serikali italazimika kuutumia ili kuwashirikisha wananchi wakati wa kuandaa muswada wa sheria.<br>(v) (c)Na utaratibu huo wa kushirikisha Wananchi ufuatwe bila ya kujali muswada wa sheria umetayarishwa na chombo kingine, mbali na Serikali. | | |
| | | (vi) Ibara ndogo ya (2) irekebishwe ili itowe haki kwa mbunge moja mmoja kuwasilisha muswada badala ya kikundi cha wabunge. | Kururuhu mbunge mmoja kuwasilisha muswada | |
| | | | (vii) 110(3) Neno 'kuhusu jambo lolote la Muungano litoke'. | |
| | | (viii) Aya ya (a) ya ibara ndogo ya (4) irekebishwe ili iruhusu upitishaji wa Miswada uwe kwa kura ya siri. | Ili Wabunge wawe huru zaidi, badala ya kufuata misimamo ya vyama vyao. | |
| | | (ix) Iongezwe ibara ndogo itakayoeleza | Kila upande wa mshirika | |

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Maoni* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| | | bayana kwamba utaratibu wa kutunga sheria utakuwa ni kwa Mswada wa sheria husika kupitishwa kwa kura zisizopungua theluthi mbili ya kura za Wabunge kutoka kila upande wa mshirika wa muungano. | wa muungano ushiriki katika kupitisha sheria. Kila upande uwe na nafasi sawa katika kupitisha sheria. | |
| 111. | Utaratibu wa kubadilisha Katiba hii na baadhi ya sheria | (i) Ibara ndogo ya (1) ifutwe. | Pendekezo hili linatolewa ili kuondoa mwanya kwa Bunge kuchezea Katiba, kama ambavyo tumekuwa tukishuhudia viongozi katika nchi nyingine, kwa kutumia Bunge, wanabadilisha katinba ili waendelee kuaka madarakani. | 1. Ibara ya 111 inakuwa ibara ya 119.<br>2. Ibara ndogo ya (2) maneno “au masharti ya sheria” yameondolewa. |
| | | (ii) 111. Ibara ianishe mambo ya msingi ambayo hayaruhusiwi kuguswa isipokuwa kwa ridhaa ya Wananchi kupitia kura ya maoni. | | |
| | | (iii) 111(2). Mabadiliko yoyote katika katiba hii, ni lazima kwanza yapitishwe na Mabunge ya Washirika kila mmoja kwa upande wake. | | |
| | | (iv) Ibara hii irekebishwe ili kuweka utaratibu wa kubadilisha Katiba uwe kwa idadi ya zaidi ya nusu ya kura za wajumbe kutoka kila upande wa Muungano. | Ili wajumbe wa kila upande washiriki kwa usawa katika kufanya mabadiliko ya Katiba. | |
| 112. | Utaratibu wa kubadilisha masharti mahususi | (i) Suala la kuongeza au kupunguza mambo ya Muungano liamuliwe na Bunge | | 1. Ibara ya 112 inakuwa 120.<br>2. Ibara hii |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | kwa maamuzi ya theluthi mbili ya wabunge wote kutoka Tanzania Bara na theluthi mbili kutoka Zanzibar. | | imeandikwa upya na itasomeka kama ifuatavyo: ‘’Bunge halitaweza kufanya mabadiliko ya Katiba kuhusu: (a) Masharti yaliyomo katika Sura ya Kwanza, Sura ya Pili na Sura ya Nne; (b) Masharti ya Ibara ya 60; (c) Masharti ya Ibara ya 79; (d) Kuongeza au kupunguza jambo lolote la Muungano yaliyoainishwa katika ibara ya 63; (e) Uwepo wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; (f) Masharti ya Ibara ya 116; Mpaka kwanza mabadiliko hayo yaungwe mkono na |
| | | (ii) Suala la kuwepo kwa Jamhuri ya Muungano liamuliwe na wananchi kwa kura ya maoni. | Uhai wa Jamhuri ya Muungano unahitaji uamuzi wa moja kwa moja wa wananchi na si kupitia kwa wawakilishi wao. | |
| | | (iii) Ibara iandikwe upya ili mamlaka ya kuitishwa, kusimamiwa na kuendeshwa kwa kura ya maoni ili kupata ridhaa ya maamuzi ya wananchi ya kuongeza au kupunguza jambo lolote la Muungano, uamuzi wa kuendelea kubaki au kujiondoa katika Muungano uendeshwe na mamlaka ya nchi husika kupitia Tume Huru ya Uchaguzi ya nchi mshirika na siyo Tume Huru ya Uchaguzi ya shirikisho kwa mujibu wa sheria ya kura ya maoni iliyotungwa na chombo cha kutunga sheria cha nchi mshirika. | | |
| | | (iv) Iongezwe aya mpya (c) ambayo itasomeka kama ifuatavyo: (v) “(c) Kuingeza au kupunguza hati ya haki za binadamu.” | | |
| | | (vi) Iongezwe aya mpya ya (c) itakayoeleza haki za msingi za binadamu; | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | (iii) Iongezwe aya mpya ya (d) itakayoweka ukomo wa mamlaka ya Bunge katika kurekebisha baadhi ya maeneo muhimu ya Katiba, mfano wa maeneo hayo ni:<br>(a) Mamlaka na madaraka ya nchi yatokanayo kwa wananchi;<br>(b) Katiba kuwa sheria kuu;<br>(c) Uwepo na nguvu za msingi ya mihimili ya dola na mgawanyo wa madaraka kati ya mihimili mikuu ya dola;<br>(d) Haki za binadamu na utawala wa sheria;<br>(e) Serikali kutokuwa na dini. (Mfano mzuri ni ibara ya 289 na 290 ya Katiba ya Ghana).<br><br>(iv) Ibara hii irekebishwe ili iwekwe masharti mahususi ya Katiba yaweze kurekebishwa baada ya kuungwa mkono na theluthi mbili ya wabunge wote. | (i) Kwa kuwa Katiba ni sheria kuu inayotokana na wananchi ambayo inasimamia utaratibu wa uendeshaji wa shughuli za nchi, serikali na watu wake na ambayo inatarajiwa kutumika kwa muda mrefu ujao, isiwe na utaratibu mwepesi sana kama ilivyo kwa sheria za kawaida.<br>(ii) Wakati wa kufanya mabadiliko ya Katiba ni vizuri kuwashirikisha wananchi kabla ya kubadilisha vipengele vinavyohusu misingi hiyo. | theluthi mbili ya wananchi wa Jamhuri ya Muungano kutoka kila upande wa Muungano kwa Kura ya Maoni itakayoendeshwa na kusimamiwa na Tume Huru ya Uchaguzi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa sheria itakayotungwa na Bunge. |
| 113. | Utaratibu wa kutunga sheria kuhusu mambo ya fedha | Ibara ya 113 ifutwe. | Inaondoa kabisa mamlaka ya Bunge na inawezesha Rais kutumia mfuko wa fedha vibaya. Hivyo kuwe na ibara itakayoonesha jinsi ambavyo Bunge linaweza kuielekeza Serikali kwenye masuala yahusuyo fedha. | Ibara ya 113 itakuwa ya 121 na itabaki kama ilivyo. |
| 114. | Madaraka ya Mkuu | (i) Neno “Mkuu” katika maneno ya | | 1. Ibara ya 114 |

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Maoni* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| | wa Nchi kuhusu Muswada wa Sheria | pembeni libadilishwe na iandikwe "Rais". | | itakuwa ya 122.<br>2. Ibara hii imefanyiwa marekebisho katika Ibara ndogo ya 6 kwa kuongeza maneno mbele ya neno Rais kuweka saini ambayo yatasomeka "Basi Katibu wa Bunge ataandika hati kuthibitisha kuwa mswada huo umekuwa sheria". |
| | | (ii) 114(1)-yaongezwe maneno "kwa nafasi ya Mkuu wa Nchi" baada ya neno "Rais" katika mstari wa pili. | Rais anaweka saini katika Muswada kwa nafasi yake kama Mkuu wa Nchi na sio Mkuu wa Serikali. | |
| | | (iv) Aidha, kifungu hiki kiboreshwe ili kuondoa uwezekano wa kumlazimisha Rais kusaini jambo lisilo na masilahi kwa Taifa. Hali hii ikitokea, suala iwasilishwe kwenye Tume ya Mawasiliano na Uratibu ili kupata muafaka unaotekelezeka. | | |
| | | (iv) Ibara ndogo ya (6) iandikwe kama ilivyo Ibara 97 ya Katiba ya sasa. | Kukosekana kwa ridhaa/idhini ya Rais kutafanya utekelezaji wa Sheria husika kuwa mgumu na kukosa tija. | |
| | | (v) Ibara ndogo ya (6) ifutwe na kuandikwa upya kama ifuatavyo:<br>"(6) Endapo Rais hatakubali muswada huo basi usipitishwe kuwa Sheria." | Ili kuondoa uwezekano wa kumlazimisha Rais kupitisha kuwa sheria muswada ambao hauna maslahi kwa nchi au wananchi hawautaki. | |
| | | (vi) Iongezwe Ibara ndogo mpya ya (7) itakayompa mamlaka Spika wa Bunge kusaini hati maalumu ya kuonesha kuwa mswaada uliokataliwa kusainiwa na Rais umekuwa sheria baada ya siku sitini toka ulipopitishwa kwa mara ya pili. | | |
| 115. | Kupitishwa kwa hoja za Serikali | (i) Ibara ndogo ya (2) ibadilishwe na iandikwe kama ifuatavyo: | Serikali haiwezi kuwa kuu mbele ya wawakilishi wa | Ibara ya 115 itakuwa ya 123 na inabaki |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | "(2) Serikali itawajibika kuyafanyia kazi mapendekezo ya Bunge kwa kadri itakavyowezekana na kisha kuwasilisha tena Bungeni hoja husika pamoja na maelezo ya utekelezaji wa maelekezo ya Bunge na endapo Bunge litakataa kwa mara ya pili hoja kuhusu Bajeti ya Serikali, basi hoja hiyo itafanyika kama ambavyo imeelekezwa na Bunge". | wananchi. | kama ilivyo. |
| | | (ii) Ibara ndogo ya (2) irekebishwe ili kama Bajeti haikupitishwa na Bunge Baraza la Mawaziri livunjwe. | | |
| | | (iii) Ibara ndogo ya (2) irekebishwe ili ikiwa mapendekezo ya Bunge yameshindikana kutekelezwa na Serikali, Rais atalihutubia Bunge kufafanua msimamo wa serikali na kuliomba tena likubali kupitishwa kwa Bajeti ya Serikali na mara baada ya Hotuba ya Rais Bunge litaijadili na kupitisha bajeti". | | |
| | | (iv) Ibara ndogo ya (2) irekebishwe kwa kueleza kuwa hoja au bajeti za serikali zitakapokuwa zimekataliwa na Bunge, zirudishwe serikalini kwa ajili ya marekebisho hata mara mbili au zaidi, na kama ikizidi mara tatu, basi hoja au bajeti hiyo iondolewe kabisa Bungeni hadi itakapoandaliwa upya. | Kulinda uwezo wa Bunge wa kuhoji na kupitisha/kutopitisha hoja za serikali | |

## 9.1 SEHEMU YA PILI:WABUNGE

### Uchaguzi wa Wabunge

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| 116. | Uchaguzi wa Wabunge | (i) 116(1-5) ibara irekebishwe na isomeke " 1.Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania watachaguliwa kutokana na ushindi wa viti vya Ubunge wa vyama vyao vya siasa katika Mabunge ya nchi shirikishi kwa utaratibu ufuatao:<br>(ii) Wabunge (10) kutoka chama chenye idadi kubwa ya viti vya Wabunge katika Mabunge ya nchi zao.<br>(iii) Wabunge (7) kutoka chama cha pili kwa idadi ya viti vya Ubunge katika nchi yao,<br>(iv) Wabunge (5) kutoka chama cha tatu kwa idadi ya viti vya Ubunge katika nchi yao,<br>(v) Wabunge watatu kutoka chama cha | | Ibara ya 116 itakuwa ya 124 na inabaki kama ilivyo. |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | nne kwa wingi wa viti katika Bune la nchi yao,<br>(vi) Ikiwa vyama vilivyopata viti vya Bunge ni viwili(2) tu katika nchi zao, watagawana kwa 60% kwa 40% ya viti ukitoa vya kuteuliwa,<br>(vii) Ikiwa vyama vyenye viti ni (3), Wabunge (12) watatoka chama chenye viti vingi, Wabunge (8) chama cha pili kwa idadi ya viti na Wabunge (8) kutoka chama cha tatu kwa wingi wa viti kwenye Bunge la nchi yao.<br>(viii) Kila chama kitakachotakiwa kutoa Wabunge watatunda utaratibu wao wenyewe wa kuwapata Wabunge hao.<br>(ix) Wabunge watakaochaguliwa wasiwe Wabunge katika Mabunge ya nchi zao, Mawaziri, Makatibu Wakuu, Manaibu Makatibu | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | Wakuu wala Wakurugenzi ndani ya nchi zao.<br>(x) Wabunge wa Bunge la Tanzania watakaa muhula mmoja wa miaka mitano na ukomo ni Mihula miwili.<br>(xi) Wabunge wataapa mbele ya Spika wa Bunge la Jamhuri ya Watu wa Tanzania." | | |
| | | (xii) Ibara ndogo ya (4) iandikwe kama ifuatavyo:<br>(xiii) "Endapo Mbunge yoyote atapoteza sifa za kuwa mbunge kwa sababu yoyote isiyokuwa ya Bunge kumaliza muda wake, Tume Huru ya Uchaguzi ya Jamhuri, kwa mujibu wa sheria ya uchaguzi itaitisha uchaguzi upya isipokuwa kama kipindi kilichobaki ni chini ya mwaka mmoja kabla ya Uchaguzi Mkuu kufanyika". | | |
| | | (xiv) Ibara ndogo ya (4) | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | ibadilishwe ili kuruhusu uchaguzi mdogo itakapotokea hali iliyoelezwa katika ibara ndogo hiyo. | | |
| | | (xv) Ibara ndogo ya (4) iandikwe kama ifuatavyo:<br>(xvi) "(4) Endapo Mbunge yoyote atapoteza sifa za kuwa mbunge kwa sababu yoyote isiyokuwa ya Bunge kumaliza muda wake, chama cha siasa ambacho Mbunge huyo anatoka kitateua mtu mwingine kujaza nafasi iliyoachwa wazi, isipokuwa kama kipindi kilichobaki ni chini ya mwaka mmoja kabla ya Uchaguzi Mkuu kufanyika". | Kuondoa uwezekano wa Wabunge kuhujumiana wenyewe kwa wenyewe. | |
| | | (xvii) Ibara ndogo ya (4) iandikwe kama ifuatavyo:<br>(xviii) "(4) Endapo mjumbe anayetokana na Chama cha Siasa au mgombea huru atapoteza sifa za | Mapendekezo haya yana lengo la kukuza demokrasia inayoheshimu matakwa vya watu, kuliko kuwateulia wananchi Mbunge ambaye hatokani na kura zao bali utashi wa Chama. | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | kuwa Mbunge kwa sababu yoyote isiyokuwa ya Bunge kumaliza muda wake, tume huru ya uchaguzi ya Jamhuri, itamteua na kumtangaza kuwa Mbunge mjumbe aliyeshiriki uchaguzi na kupata kura zilizofuatia katika wingi wa kura wakati wa uchaguzi wa awali ndiye awe mbunge mbadala.”<br>(xix) Ibara ndogo ya (5) iandikwe kama ifuatavyo:<br>(xx) “(5) Orodha ya majina ya wagombea walioshiriki katika Uchaguzi Mkuu ndiyo itakayotumiwa na Tume Huru ya Uchaguzi ya Jamhuri ya Muungano kwa madhumuni ya kujaza nafasi ya mbunge inapotokea kuwa wazi, wakati wowote wa maisha ya Bunge”. | | |
| | | (xxi) Ibara ndogo ya (5) ifutwe. | Ili kuruhusu uchaguzi mdogo. | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | (xxii) Ibara hii irekebishwe ili kuainisha vigezo vya kuanzisha majimbo. | | |
| 117. | Sifa za kuchaguliwa kuwa Mbunge | (i) Katika ibara ndogo ya (1) aya (a) maneno "ishirini na tano" yafutwe na badala yake yaandikwe "ishirini na moja". | Umri wa sasa wa miaka 21 hauna tatizo lolote. | 1. Ibara ya 117 itakuwa ya 125 na inabaki kama ilivyo.<br>2. Ibara ndogo ya (1)(a) imefanyiwa marekebisho kwa kuweka umri wa miaka 21 badala ya 25 kwa mtu anayetaka kugombea ubunge.<br>3. Ibara imeongezwa aya (h) katika kifungu kidogo cha pili ambayo itasomeka:<br>"Ikiwa katika kipindi cha miaka mitano kabla ya tarehe ya uchaguzi amewahi kutiwa hatiani katika mahakama kwa kosa la kukwepa kulipa kodi yoyote ya Serikali au makosa yanayohusu kukosa uaminifu"<br>4. Katika Ibara ndogo ya (5) kipengele (e) kimefanyiwa |
| | | (ii) Katika ibara ndogo ya (1) aya (a) maneno "ishirini na tano" yafutwe na badala yake yaandikwe "kumi na nane". | (a) Umri wa miaka kumi na nane ni umri wa mtu mzima.<br>(b) Kutoa fursa kwa vijana wenye uwezo wa kulitumikia Taifa na wazalendo waanze mapema. | |
| | | (iii) Katika ibara ndogo ya (1)(a) maneno "kidato cha nne" yasomeke "kidato cha sita". | | |
| | | (iv) 117(1)(b)-Kiwango cha chini cha mgombea Ubunge kiwe Shahada ya Kwanza inayotambulika na mamlaka ya elimu ya juu katika nchi washirika. | Bunge hili ni dogo na ni rahisi kuwapata Wabunge wenye sifa hiyo.<br>Bunge la Muungano litakuwa likijadili masuala mazito yanayohitaji elimu ya kutosha kwa Wabunge. | |
| | | (v) Ibara ndogo ya (1)(b) iandikwe kama ifuatavyo:<br>"(b) anajua kusoma na kuandika lugha ya Kiswahili au Kiingereza na ana elimu isiyopungua shahada ya kwanza". | Majukumu ya Bunge la Muungano ni makubwa hivyo yanahitaji watu wenye taaluma na weledi. | |
| | | (vi) Ibara ndogo ya (1)(b) iandikwe kama ifuatavyo:<br>"(b) anajua kusoma na kuandika lugha ya Kiswahili" | Kiingereza isiwe kigezo cha kumnyima haki ya kuchaguliwa Mtanzania yeyote. | |

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Maoni* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| | | (vii) Aya (b) katika ibara ndogo ya (1) neno "au" lifutwe na badala yake iandikwe "na". | Kulazimisha uelewa wa lugha zote mbili badala ya moja wapo. Kuweka urahisi kwa Wabunge wetu kushiriki Mabunge ya Nje. | marekebisho kwa kuondoa maneno na ''Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali"<br>5. Katika Ibara ndogo ya (5) kipengele (f), kimefanyiwa marekebisho na kitasomeka ''Katibu Mkuu Kiongozi, Mawaziri na Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu". |
| | | (viii) 117(1)(b). Kifungu kisomeke "Awe na elimu ya angalau kidato cha nne, na awe amejiandikisha kuwa Mpiga kura katika Jimbo analowania kugombea Ubunge"<br>(ix) Katika aya (b) ya ibara ndogo ya (1) neno "Kiingereza" liondolewe. | Mtu aliyemaliza kidato cha nne anauelewa mkubwa wa mambo. | |
| | | (x) Aya (e) ya ibara ndogo ya (1) irekebishwe ili mtu aliyetiwa hatiani kwa kosa lolote la jinai akose sifa za kugombea ubunge. | (a) Ni utaratibu wa utumishi wa kawaida | |
| | | (xi) Katika ibara ndogo ya 1 (b) maneno "kidato cha nne" yasomeke "kidato cha sita." | | |
| | | (xii) Aya (e) ya Ibara ndogo ya (1) irekebishwe ili mtu aliyetiwa hatiani kwa kosa lolote la jinai asiwe na sifa ya kugombea ubunge. | Mbunge kama kiongozi hapaswi kuwa na hatia ya kosa lolote la jinai kama ilivyo kwa viongozi wengine katika Rasimu hii ya Katiba. | |
| | | (xiii) Katika aya (e) ya ibara ndogo ya (1) maneno "miaka mitano" isomeke "kwa muda wote". | | |
| | | (xiv) 117(1)(e)- ihamishiwe katika Ibara ndogo ya (2) na iwe aya | Ibara ndogo ya (1) imeainisha sifa ambazo ni chanya ilhali aya ya (e) ina sifa ambazo ni hasi. | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | inayojitegemea na iongezwe « makosa yanayohusu utovu wa maadili ya kijamii (moral turpitude). » | | |
| | | (xv) 117(2)(a),Liongezwe neno"mfululizo kwa vipindi vitatu vya miaka mitano mitano". | | |
| | | (xvi) Ibara ndogo ya (2) ifutwe. | Uamuzi wa kuchaguwa nani awe mmbuge wao ni wa wananchi wenyewe. | |
| | | (xvii) Aya (a) ya Ibara ndogo ya (2) ifutwe. | Kwa kuwa nafasi ya ubunge ni ya uwakilishi ni vema wananchi wakaachiwa kuamua ukomo wa mwakilishi wao. | |
| | | (xviii) Katika aya (a) ya Ibara ndogo ya (2) maneno "vitatu vya miaka mitano" yafutwe na badala yake iandikwe "viwili vya miaka mitano". | | |
| | | (xix) Aya (c) ya ibara ndogo ya (2) irekebishwe kwa kujumuisha watu watakao hukumiwa nje ya nchi kwa makosa yanayotambulika nchini. | Kuondoa mwanya wa wahalifu waliohukumiwa nje kuwa na sifa ya kugombea. | |
| | | (xx) 17(2)(c).Kifungu kisomeke"Ikiwa amewahi kupatikana na hatia ya jinai na kuhukumiwa na Mahakama yoyote katika Jamhuri ya Muungano na kupewa adhabu ya kifungo gerezani kwa | Kuweza kuondoa utata katika tafsiri ya "Uaminifu". | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | muda usiopungua miezi sita”. | | |
| | | (xxi) Katika aya (e) ya ibara ndogo ya (2) maneno “miiko maalum” yatolewe tafsiri. | Kuepuka kutolewa tafsiri isiyokusudiwa na kuathiri watu wasiohusika. | |
| | | (xxii) 117(2) (e) Ibara ikataze mtu mwenye maslahi ya kimkataba na Serikali ya Jamhuri ya Muungano, kugombea Ubunge. | | |
| | | (xxiii) Iongezwe aya mpya (h) katika ibara ndogo ya (2) kama ifuatavyo:<br>“(h) Mtu ambaye hajafanya kosa la udanganyifu wa kuiba kura”. | | |
| | | (xxiv) Katika ibara ndogo ya (2)(f) maneno “Serikali ya Mapinduzi” yafutwe na badala yake iandikwe “Serikali ya Zanzibar”. | | |
| | | (xxv) Ibara ndogo ya (3) na (4) zisiwe katika Katiba bali katika Sheria. | Itakuwa ni rahisi kufanya marekebisho pale itakapoonekana inafaa badala ya kubaki katika Katiba ambayo utaratibu wake wa kufanya marekebisho ni mrefu. | |
| | | (xxvi) Katika Ibara ndogo ya (3) maneno “asichaguliwe” yafutwe na badala yake iandikwe “asiwe mgombea”. | | |
| | | (xxvii) Katika Ibara ndogo ya (4) maneno “Tanzania Bara” yafutwe. | | |
| | | (xxviii) Katika Ibara ndogo ya | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | (5)(b) maneno "Rais wa Tanzania Bara" yafutwe na maneno "Rais wa Zanzibar" yafutwe iandikwe "na Makamu wa wake". | | |
| | | (xxix)Katika aya ya (f) ya ibara ndogo ya (5) maneno "Katibu Mkuu" yafutwe na badala yake iandikwe "Katibu Mkuu Kiongozi". | Ndiyo wadhifa wake. | |
| | | (xxx) Katika ibara ndogo ya (5)(j) maneno "ya Washirika" yafutwe na badala yake iandikwe "ya Zanzibar". Aidha, viongozi wote watajwe kwa kuzingatia ukuu na nafasi zao katika mihimili ya dola. | | |
| | | (xxxi) Ibara ndogo ya (5)(c) na (d) zisomeke kama ifuatavyo:<br>"(c) Spika na Naibu Spika wa bunge watachaguliwa na wabunge kutoka miongoni mwa wabunge;<br>(d) Waziri na Naibu Waziri watateuliwa na Rais kutoka miongoni wa Wabunge". | | |
| | | (xxxii) Aya (m) ya ibara ndogo ya (5) na 118(a) na (b) zibadilishwe. | Zinakinzana. | |
| 118. | Watu wenye Madaraka Serikalini kukoma utumishi | (i) hii ifutwe. | (a) Ielezwe kwenye sheria.<br>(b) Suala la kukoma utumishi linahusu Kanuni na Taratibu za kawaida za Utumishi wa Umma. | Ibara hii imefutwa. |
| | | ii).118 ibaki kama ilivyo. | Inajitosheleza. | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| 119. | Utaratibu wa uchaguzi wa Wabunge | 119 Ibaki kama ilivyo. | Inajitosheleza. | Ibara ya 119 inakuwa 126 na inabaki kama ilivyo. |
| 120. | Kiapo cha Wabunge | (i) 120 itamke kuwa kila Mbunge ataapishwa na Spika wa Bunge. | Ndivyo utaratibu ulivyo. | 1. Ibara ya 120 inakuwa 127.<br>2. "Marginal Note" itabadilika na itasomeka "Kiapo na masharti ya kazi ya Wabunge"<br>3. Ibara ya 120, 121, 123 zimechanganywa na zitakuwa Ibara moja ya 127. |
| | | (ii) Ibara hii iandikwe kuonyesha kiapo na masharti ya kazi ya ubunge kama ifuatavyo:-<br>(1) Kila Mbunge ataapishwa kiapo cha uaminifu na Spika katika Bunge kabla hajaanza kushiriki katika shughuli za Bunge, lakini Mbunge anaweza kushiriki katika uchaguzi wa Spika hata kabla hajaapishwa.<br>(2) Wabunge watashika madaraka yao kwa mujibu wa Katiba hii, na watalipwa mshahara, posho na malipo mengine kama yatakavyopangwa na Tume ya Utumishi wa Umma kwa mujibu wa sheria za nchi.<br>(3) Wakati wowote wa madaraka yake, Mbunge atawajibika moja kwa moja kwa wapiga kura wake. | Inajitosheleza. | |
| 121. | Masharti ya kazi ya Wabunge | (i) Ibara hii irekebishwe ili Tume ya Utumishi wa Bunge ishughulikie mishahara wa wabunge. | Wabunge ni viongozi wa kisiasa hivyo washughulikiwe na Tume inayohusu masuala ya Bunge. | Ibara imeingizwa Ibara ya 127. |
| | | (ii) Tume ya utumishi wa umma ipange mishahara, posho na stahiki nyingine zozote za wabunge na kuziweka wazi kwa wananchi. Pia wabunge | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | walipe kodi kama watumishi wengine kwa mujibu wa sheria. | | |
| | | Ibara ya 121 iondolewe. | Inatoa masharti kwa Mhimili mmoja tu. | |
| 122. | Muda wa Wabunge kushika madaraka | (i) Maelezo ya pembeni yasomeke "Ukomo wa Wabunge kushika madaraka" | | 1. *Marginal Note* itabadilika na kusomeka "Kupoteza sifa za Ubunge"<br>2. Ibara ya 122 inakuwa ya 128.<br>3. Ibara ya 128(1)(g) imerekebishwa na inasomeka kama ifutavyo:- "Ikiwa kwa ridhaa yake atajiondoa au kujivua uanachama wa chama chake cha siasa, atafukuzwa au kuvuliwa uanachama na chama chake cha siasa."<br>4. Imeongezwa ibara ndogo nyingine (i) ambayo |
| | | (ii) Marginal note isomeke "Kupoteza sifa za Ubunge". | Kuendana na maudhui ya ibara. | |
| | | (iii) Neno "atakoma" lisitumike na badala yake litafutwe neno zuri zaidi. | Linaleta tafsiri isiyopendeza. | |
| | | (iv).122(1) (b) irekebishwe kwa:<br>(i) kufuta maneno "vikao vya";<br>(ii) kufuta neno "mitatu" na badala yake kuweka maneno "miwili". | Kuweka ufasaha. | |
| | | (v). 122(1)-Iongezwe aya mpya ya (h) itakayosomeka "kufariki dunia". | Kuweka ufasaha. | |
| | | Aya (b) ya ibara ndogo ya (1) irekebishwe ili kueleza muda uwe ni vikao vitano mfululizo katika Mkutano mmoja wa Bunge | Muda uliyopendekezwa ni mrefu mno ukizingatia jukumu alilonalo Mbunge kuwawakilisha wananchi Bungeni. | |
| | | (v) Aya (d) ya Ibara ndogo ya (1) irekebishwe kwa kuondoa maneno "afya ya mwili". | Ugonjwa usimuondolee mtu sifa ya kuwa Mbunge. | |
| | | (vi) Aya (d) ya Ibara ndogo ya (1) irekebishwe ili suala la | Magonjwa yote ni lazima yathibitishwe kwanza. | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | ugonjwa wa akili au afya ya mwili liwe kwa uthibitisho wa daktari. | | inasomeka "kufariki dunia" |
| | | (vii) Katika aya (d) ya ibara ndogo ya (1) maneno "kizuizini ndani ya" yafutwe na badala yake iandikwe "kifungo gerezani". | | |
| | | (viii) Iongezwe aya mpya (h) itakayoeleza kuwa mtu atakoma kuwa mbunge endapo atasema uongo bungeni na ikadhihirika kuwa alisema uongo huo makusudi na kwa nia ya kupotosha, kulihadaa Bunge, kuleta hofu kwa wananchi, kuleta uhasama katika jamii kutahatarisha usalama wanchi au kuchinganisha Serikali na wananchi. | Pendekezo hili linatokana na vitendo vya baadhi ya wabunge kutoa habari za uongo bungeni ambazo zinaweza kuleta athari kwa wananchi na taifa kwa ujumla. – Mfano kudai kuwa majeshi ya Kenya na Uganda yameingia nchini hadi ukerewe na kupiga wananchi.<br><br>Taarifa hii ingeweza kuleta hofu kwa wanchi, kuwachonganisha wananchi na serikali yao kwa wananchi kudhani kuwa serikali haijali usala wao au vyombo vya ulinzi na usalama ni dhaifu, au kuleta chokochoko kati ya Tanzania na nchi hizo | |
| | | (ix) Katika Ibara ndogo ya (1) iongezwe aya mpya ya (h) itakayosomeka kama ifuatavyo:<br>"(h) ikiwa atafariki akiwa madarakani." | | |
| 123. | Uwajibikaji wa Wabunge | (i) Ibara ndogo ya (1) na (2) irekebishwe kwa kuweka dhana kwamba Mbunge ni mwakilishi wa wananchi, hivyo awajibike kwao sio | | Ibara imeingizwa Ibara ya 127. |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | kwa chama. | | |
| | | (ii) 123(1)-Ibara iishie katika maneno “atawajibika moja kwa moja kwa wapiga kura wake”. | | |
| | | (iii) Ibara ndogo ya (1) irekebishwe kwa kuondoa neno “kwa wapiga kura wake” na badala yake kuweka “”jimbo lake la uchaguzi” na kuongeza maneno “taifa lake” kabla ya maneno “chama chake cha siasa”. | | |
| | | (iv) Ibara ndogo ya (2) irekebishwe ili Mbunge akipoteza uanachama wake kwa kufukuzwa au kujitoa uanachama achukuliwe kwamba amepoteza sifa ya kuwa Mbunge. | Kwa mbunge ambaye hakuwa mgombea huru, hoja inayoamua ubunge wake ni uanachama na siyo namna alivyopoteza sifa ya kuwa mwanachama. | |
| | | (v) Ibara ndogo ya (2) irekebishwe kwa kuzingatia upatikanaji wa nafasi za ugombea kupitia vyama au ugombea huru, hivyo itasomeka kama ifuatavyo;<br>“(2) Mbunge aliyependekezwa na Chama cha Siasa atapoteza Ubunge wake ikiwa Mbunge huyo atafukuzwa au kuvuliwa Uanachama wa Chama chake pia mgombea huru naye akiamua kujiunga na | | |

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Maoni* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| | | Chama chochote cha Siasa, atapoteza nafasi yake ya Ubunge". | | |
| | | (vi) Ibara ndogo ya (2) ifutwe na badala yake isomeke kama ifuatavyo: "(2) Mbunge aliyependekezwa na chama cha siasa atapoteza Ubunge wake ikiwa Mbunge huyo atafukuzwa au kuvuliwa uanachama wa chama chake cha siasa"; | | |
| | | (vii) Ibara ndogo ya (2) irekebishwe na isomeke "(2) Mbunge aliyependekezwa na chama chake cha siasa amefukuzwa au kuvuliwa uanachama sifa za kuwa mbunge na atakoma kuwa mbunge". | Sababu ni ili kulinda nidhamu ndani ya vyama vya siasa. Vyama vya siasa ni vyombo vya wananchi na vya kikatiba vya kuongoza nchi hivyo ni vyema vilindwe na pawepo nidhamu ndani ya taasisi hizi.<br>Katiba ikilinda haki ya ugombea huru na kuacha mlango wazi ili vyama vidharauliwe na viwe legelege, taifa litazaa fujo na litaporomoka.<br>Katiba isiruhusu uongozi mamluki na usio na nidhamu kwa kisingizio cha demokrasia.<br>Demokrasia lazima ilindwe na iwe na nidhamu.<br>Anayechagua kugombea kwa kupitia chama akubali utii na nidhamu ya chama na kamwe asiruhusiwe kula keki yake na bado kutaka awe nayo. | |
| | | (viii) 123(3) ihamishiwe katika Ibara ya 121 na ieleze pamoja na mambo mengine | Kuweka nidhamu ya chama na kuimarisha demokrasia kupitia vyama vya siasa. | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | kuwa Mbunge atapoteza ubunge ikiwa atavuliwa au kufukuzwa uanachama na chama chake cha siasa. | | |
| | | (ix) Katika ibara ndogo ya (3) neno "atasita" libadilishwe na iandikwe "atakoma". | | |
| | | (x) Iongezwe ibara ndogo mpya ambayo itasomeka kama ifuatavyo: "Endapo mbunge amefungua kesi kwenye mahakama za kisheria ya kupinga uamuzi wa chama chake cha siasa kwa kumvua uanachama, basi Mahakama itamaliza kusikiliza kesi hiyo ndani ya siku tisini za kufukuzwa kwake". | Sababu ni kuhakikisha kuwa wananchi wanawakilishwa na mbunge ambaye uhalali wa ubunge wake haubishaniwi. | |
| | | (xi) Iongezwe Ibara ndogo ya (4) itakayomtaka Mbunge kukutana na wananchi wake angalau mara nne kwa mwaka, kabla na/au baada ya kila kikao cha Bunge. | | |
| 124. | Haki ya wapiga kura kumwajibisha Mbunge | (i) Ibara hii ifutwe. | Wapiga kura watumie haki yao ya kumbadilisha Mbunge baada ya kipindi cha miaka mitano. | 1. Ibara ya 124 inakuwa ibara ya 129.<br><br>2. Ibara ndogo (1)(d),(e), (f),(g)na (h) zimeondolewa. |
| | | (ii) 124(1).Vigezo vya kutekeleza vipengele (a) hadi (c) vya Rasimu hii, vitamkwe wazi.<br>(iii) Ibara hii iandikwe upya kama ifuatavyo: | Kuepusha utata katika utekelezaji wake. | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | "Bila ya kuathiri masharti ya ibara ya 123 ya Katiba hii, wananchi wa jimbo la uchaguzi watakuwa na haki ya kumuondoa mbunge wao madarakani kwa sababu, na kwa kufuata utaratibu na masharti yatakayowekwa na sheria itakayotungwa na Bunge." | | |
| | | (iv) Ibara ndogo ya (1) irekebishwe kwa kufuta aya za (a) na (b). | (a) Hazina viwango na ni subjective.<br>(b) Ni mambo ya jumla mno na yatawanyima Wabunge haki ya kutetea maslahi ya Taifa;<br>(c) Masharti haya yanaweza kuweaondoa Wabunge wengi watetezi wa maslahi ya Umma. | |
| | | (v) Katika aya (a) ya ibara (1) maneno "kinyume na maslahi ya wapiga kura" yafutwee. | | |
| | | (vi) Ibara ndogo ya (1) iandikwe upya kama ifuatavyo:<br>"(1) Bila kuathiri masharti ya Ibara ya 123 ya Katiba, wananchi watakuwa na haki ya kumuondoa mmbunge wao madarakani endapo hatatekeleza madaraka yake vyema.<br><br>(2) Bunge litatunga sheria kuweka masharti ya namna ya kuendesha uchunguzi wa Mbunge atakayeshindwa | Sheria itapambanua bayana kuhusu uamuzi wa kama mtu ni mbunge, na kuwa watu/wapiga kura na kuwapa watu uwezo wa kufungua shauri mahakamani ili kujiridhisha na uhalali wa mbunge. | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | kutekeleza majukumu yake kwa wapiga kura wake nautaratibu wa kumuondoa mbunge huyo". | | |
| | | (vii) Aya (b) ya Ibara ndogo ya (1) irekebishwe ili kuweka vigezo vya jinsi ya kupima udhati wa uwakilishi na utetezi vitakavyothibitishwa na mahakama. | Ibara hii inaweza kutumika vibaya. | |
| | | (viii) Aya (c) Ibara ndogo (1) ifanywe kuwa moja ya sifa za mtu kuchaguliwa kuwa Mbunge. | Ibara hii inaweza kutumika vibaya. | |
| | | (ix) Ibara hii irekebishwe kwa kutenganisha mambo ambayo mengine yanapaswa kuwa katika Sheria au Kanuni. | | |
| | | (x) Katika aya (c) ya Ibara ndogo ya (1) yaongezwe maneno "isipokuwa iwapo mbunge ataacha kuishi jimboni mwake kwa sababu za kiafya na ambapo jopo la madaktari limependekeza kuwa aishi sehemu nyingine". | | |
| | | (xi) Aya (f) isomeke kama ifuatavyo:<br>"(f) kufanya biashara, kumiliki makampuni, kutetea maslahi binafsi Bungeni au kuwa na hisa katika makampuni | | |

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Maoni* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| | | ambayo yana mikataba au mahusiano ya biashara na taasisi za umma kwa namna ambayo inaleta mgongano wa kimaslahi;” | | |
| | | (xii) Katika aya (g), maneno “kutiwa hatiani kwa makosa haya yawe ni miongoni mwa mambo ambayo yanapoteza sifa za mtu kuwa Mbunge. | | |
| 125. | Uamuzi wa suala kama mtu ni Mbunge | (i) Ibara hii ifutwe na badala yake iwekwe katika Sheria husika ya uchaguzi. | Sheria itapambanua bayana kuhusu uamauzi wa kama mtu ni Mbunge na kuwapa wapiga kura uwezo wa kufungua shauri mahakamani ili kujiridhisha na uhalali wa Mbunge. | Ibara ya 125 inakuwa ibara ya 130 na inabaki kama ilivyo. |
| | | (ii) Aya (a) ya Ibara ndogo ya (1) inayohusu ukomo wa mtu kuwa spika iwapo atateuliwa kuwa mbunge iondolewe. | | |
| | | (iii) Aya (c) ya ibara ndogo ya (2) irekebishwe ili uwezo wa mahakama kupokea mashauri ya kupinga uchaguzi ushushwe kwenye ngazi ya mahakama za wilaya na mahakama za hakimu mkazi. | Ili kutoa fursa kwa wananchi wa kawaida kufikia vyombo vya kutafsiri sheria. | |
| | | (iv) Aya (b) ya Ibara ndogo ya (1) inapingana na Ibara ya 185(2), inapendekezwa mamlaka malalamiko ya uchaguzi yashughulikiwe na | Ndicho chombo cha kimahakama cha Muungano. | |

| ***Ibara Na.*** | ***Kichwa cha Habari*** | ***Maoni ya Mabaraza*** | ***Sababu ya Maoni*** | ***Marekebisho ya Tume*** |
|---|---|---|---|---|
| | | Mahakama ya Rufaa. | | |
| 126. | Tamko Rasmi la Wabunge kuhusu Maadili ya Viongozi | 126 ibaki kama ilivyo | Inajitosheleza. | Ibara ya 126 inakuwa 131 na inabaki kama ilivyo. |
| 127. | Wabunge kutoa taarifa ya mali | (i) Ibara ndogo ya (1) irekebishwe kwa kuongeza maneno “na watoto wake” mwishoni mwa Ibara hiyo. | | Ibara ifutwe masharti yake yapo katika ibara ya 17. |
| | | (ii) 127(1) mstari wa mwisho neno “mke” amependekeza iongezwe “au wake zake”. | | |
| | | (iii) 127 irekebishwe kwa: (a) Kufuta Ibara ya (2); (b) Mbunge kuwasilisha nakala moja ya taarifa rasmi; (c) mali ya mtoto aliye chini ya umri wa miaka 18 kutolewa taarifa. | | |
| | | (iv) 127 Inapendekezwa kuwa ;Taarifa kuhusu mali za Wabunge zitangazwe kila mwaka na ihusishe na Madeni yao. | | |
| | | (v) Ibara ndogo ya (1) irekebishwe ili kutompa mamlaka Katibu wa Bunge kupokea nakala ya taarifa za mali ya Mbunge. | Kuepuka uvujaji wa taarifa binafsi za Mbunge na kuacha Tume ya Maadili kusimamia sheria. | |
| | | (vi) Iongezwe ibara ndogo mpya | Masharti ya Ibara hii yatumike pia | |

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Maoni* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| | | itakayoeleza kama ifuatavyo: "Wabunge watoe taarifa za mali zao kabla ya Bunge kuvunjwa na kupisha uchaguzi". | kwa mbunge anayejiuzulu au anayepoteza sifa za kuwa mbunge kwa mujibu wa Katiba hii. | |

## 9.2 SEHEMU YA TATU:UONGOZI WA BUNGE

### (a) Spika na Naibu Spika

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| 128. | Spika na mamlaka yake | (i) Ibara ndogo ya (4) irekebishwe kwa kuongeza maneno "na watoto wake" mwishoni mwa Ibara hiyo. | | Ibara ya 128 itakuwa ibara ya 132.<br>Ibara ndogo ya (4) imefutwa. |
| | | (ii) Ibara ndogo ya (4) iandikwe kama ifuatavyo: | | |
| | | (iii) "(4) Spika atatakiwa kuwasilisha kwa Rais nakala mbili za taarifa rasmi ya maelezo ya mali yake, kadri itakavyokuwa, mali ya mke au mume wake au watoto wake". | | |
| | | (iv) 129.Iongezwe ibara inayojitegemea itakayoelezea sifa za mtu kuweza kuwa Spika,na sifa hizo zijumuishe kuwepo kwa hati inayotolewa na Mamlaka ya kodi kuthibitisha kuwa mtu anaetarajiwa kupigiwa kura kuwa , amelipa kodi zote stahiki kwa kipindi cha miaka mitano mfululizo. | | |
| | | (v) Katika Ibara ndogo ya (4) neno "Rais" lifutwe na badala yake liandikwe "Tume ya Maadili ya Utumishi wa Umma". | Rais ni muhimili mwingine hivyo itadhoofisha uhuru wa muhimili wa Bunge. | |
| | | (vi) Ibara ndogo ya (4) | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | irekebishwe na ielezwe kwamba Spika awasilishe tamko la mali yake kwa Tume ya Maadili ya Viongozi na Uwajibikaji kama ilivyo kwa viongozi wengine. | | |
| | | (vii) Ibara ndogo ya (4) irekebishwe kwa kuongeza kiunganishi "na" kati ya maneno "mali yake" na "kadri itakavyokuwa". | Kuweka lugha ya Kiswahili sawa sawa. | |
| 129. | Ukomo wa mamlaka ya Spika | (i) Maelezo ya pembeni yasomeke "Ukomo wa Mamlaka ya Spika". | (a) Maelezo ya pembeni hayawiani na maelezo ya Ibara hii.<br>(b) Ibara inamzungumzia Spika na si Bunge. | 1. Ibara ya 129 inakuwa ibara ya 133.<br>2. Marginal note isomeke « Ukomo wa Mamlaka ya Spika »<br>3. Iongezwe aya ya (h) itakayosomeka , "kufariki dunia." |
| | | (ii) Ibara ndogo ya (1) irekebishwe na isomeke kama ifuatavyo:<br>"(1) Spika atakoma kuwa Spika na ataacha nafasi ya madaraka ya Spika kama moja ya mambo yafuatayo likitokea:" | | |
| | | (iii) Iongezwe aya mpya katika ibara ndogo ya (1) itakayoeleza kwamba kifo ni moja kati ya mambo yatakayomfanya Spika kufikia ukomo wa Spika. | | |
| | | (iv) Aya (a) ya Ibara ndogo ya (1) ifutwe. | Utaratibu wa sasa wa mfumo wa kibunge uendelee kutumika ili Spika atoke miongoni mwa Wabunge kama ilivyo hivi sasa ndani au nje ya Bunge endapo Wabunge wataamua hivyo kwa kumchagua mtu asiye Mbunge. | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | (v) Katika aya (a) na (b) ya ibara ndogo (1) liongezwe neno "au" katika kila mwisho wa sentensi. | (vi) Katika aya (a) na (b) ya ibara ndogo (1) liongezwe neno "au" katika kila mwisho wa sentensi. | |
| | | (vi) Aya (c) ya Ibara ndogo ya (1) irekebishwe kwa kufuta maneno "Wabunge wote" na badala yake kuweka maneno "Wabunge wa kila Mshirika wa Muungano". | (vii) Aya (c) ya Ibara ndogo ya (1) irekebishwe kwa kufuta maneno "Wabunge wote" na badala yake kuweka maneno "Wabunge wa kila Mshirika wa Muungano". | |
| | | (vii) Ibara ndogo ya (2) irekebishwe na isomeke kama ifuatavyo:<br>"(2) Hakuna shughuli yoyote itakayotekelezwa katika bunge wakati wowote ambao nafasi ya madaraka ya Spika itakapokuwa wazi, isipokuwa shughuli ya kumchagua Spika". | (viii) Ibara ndogo ya (2) irekebishwe na isomeke kama ifuatavyo:<br>"(2) Hakuna shughuli yoyote itakayotekelezwa katika bunge wakati wowote ambao nafasi ya madaraka ya Spika itakapokuwa wazi, isipokuwa shughuli ya kumchagua Spika". | |
| 130. | Naibu Spika | (i) 130 iwekwe ibara ndogo mpya itakayomtaka Naibu Spika kuwasilisha taarifa ya mali yake kwa Tume kwa utaratibu utakaotumika kwa Spika. | Kumpa mhusika wajibu kuwasilisha taarifa zake binafsi. | 1. Ibara ya 130 inakuwa ibara ya 134.<br>2. Ibara ndogo ya (4) neno "atakoma" lisomeke "atasita." |
| | | (ii) 130 Ibara itamke kuwa "Naibu Spika asitokane na Chama chochote cha Siasa". | | |
| | | (iii) Ibara ndogo ya (2) irekebishwe ili Naibu Spika atokane na | Kwa kuwa Spika anaweza kutoka nje ya Bunge, ni vema Naibu Spika awe Mbunge kama ilivyo sasa. | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | Wabunge. | | |
| | | (iv) Ibara ndogo ya (4) ifutwe. | | |
| | | 130(4).Imependekezwa kuwepo kwa ibara inayojitegemea itakayoainisha sifa za mtu kuwa Naibu Spika; vile vile sifa za kupoteza nafasi hiyo ziwe sawa kwa Spika na Naibu wake.<br>(iv)131-Neno "kiapo" liwekwe katika marginal note. | Kuweka ufasaha. | |
| 131. | Utaratibu wa kumchagua Spika na Naibu Spika | (i) 131(4) Spika na naibu Spika watachaguliwa kwa masharti kwamba endapo spika atatoka upande mmoja wa washirika wa muungano naibu spika atatoka upande mwingine wa washirika wa muungano kwa kuzingatia jinsia<br>(ii) Ibara ndogo ya (5) ifutwe. | Suala la mtu kuchaguliwa kuwa Spika au Naibu Spika ni sehemu ya demokrasia ndani ya Bunge, hivyo ni vema Wabunge wachague Spika au Naibu Spika kwa kadri watakavyoona inafaa | 1. Ibara 131 inakuwa ibara ya 135.<br>2. Marginal note Isomeke "utaratibu wa kumchagua spika na naibu spika na kiapo"<br>3. Ibara ibaki kama ilivyo. |
| | | (iii) 131-Neno "kiapo" liwekwe katika marginal note. | | |
| | | (iv) Ibara ndogo ya (6) ifutwe na badala yake iwe ibara mpya ya 132 na iandikwe kama ifuatavyo:<br>*Kiapo cha Spika na Naibu Spika.*<br>(v) 132. Mtu yeyote atakayechaguliwa kuwa Spika au Naibu Spika atatakiwa, kabla ya kuanza kutekeleza madaraka yake, | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | ataapishwa na Jaji Mkuu kiapo cha uaminifu". | | |
| | | (vi) Baada ya marekebisho ya hapo juu, ibara zinazofuata zirekebishwe kwa mpangilio wake. | | |
| 132. | Sifa za mtu anayefaa kuchaguliwa kuwa Spika au Naibu Spika | (i) Aya (a) ya Ibara hii irekebishwe kwa kufuta maneno "kwa mujibu wa sheria za nchi". | | 1. Ibara ya 132 inakuwa Ibara ya 136.<br>2. Ibara ndogo ya (1)(c) imekuwa (1)(b) na (1)(b) imekuwa (1)(c)<br>3. Ibara ndogo ya (1)(c) isomeke bila ya kuathiri masharti ya aya (a) na (b), awe na sifa za kumwezesha kuchaguliwa kuwa mbunge.<br>4. Imeongezwa ibara ndogo ya (2) ambayo inasomeka "kwa madhumuni ya aya (d) kiongozi wa juu wa chama cha siasa ni mwenyekiti, makamu mwenyekiti, |
| | | (ii) Aya (a) ya ibara hii irekebishwe kwa kufuta maneno "angalau elimu ya Chuo Kikuu" na badala yake isomeke "angalau Shahada ya Kwanza". | Kwa sasa vyuo vikuu vinaendesha programu za mafunzo ya Cheti, Stashahada na Shahada. | |
| | | (iii) 132. Kwa kuwa Elimu si suala la Muungano, ni vyema ikaainishwa ni nani/chombo au vyombo gani vitathibitisha Elimu aliyonayo Mgombea wa Uspika au Unaibu Spika. | Inaweza kutokezea kuwa mmoja wa Washirika anakitambua Chuo fulani na Mshirika mwengine hakitambui | |
| | | (iv) Aya (d) ya ibara hii ifutwe. | Kwa mfumo tulionao ambapo kwa kaisi kikubwa Spika anatokana na chama cha siasa, ni vigumu kupata mtu mwenye sifa hizo ambaye hakuwahi kujihusisha na chama cha siasa. | |
| | | (v) 132(d)-Maneno "kiongozi wa juu" yapatiwe ufafanuzi. | Kuweka ufasaha. | |
| | | (vi) Iongeze aya zifuatazo katika ibara hii ambazo zitasomeka kama ifuatavyo:<br>"(e) awe ni mtu mwenye uzoefu | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | wa kutafsiri sheria na kanuni na kuweza kuendesha mijadala ya kidemokrasia;<br>(g) uzoefu wake usiopungua miaka kumi katika kazi;<br>(h) elimu ya Spika iwe angalau shahada ya uzamili". | | katibu mkuu, naibu Katibu mkuu au mjumbe wa chombo chochote cha kitaifa chenye mamlaka katika chama cha siasa." |

## (b) Ofisi ya Bunge

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| 133. | Katibu wa Bunge | (i) Ibara ndogo ya (1) irekebishwe kwa kufuta maneno "Katibu wa Bunge atateuliwa na Tume ya Utumishi ya Bunge" na badala yake yawekwe maneno "Tume ya Utumishi wa Bunge itapendekeza majina matatu kwa Rais ambaye atafanya uteuzi wa jina moja la Katibu wa Bunge kati ya majina yaliyopendekezwa." | Kwa kuwa Tume ya Utumishi ya Bunge inaundwa na wabunge, iwapo Tume hiyo ndiyo itakuwa na madaraka ya kumteua Katibu wa Bunge, Katibu huyo hataweza kutekeleza majukumu yake kwa uhuru na weledi unaotakiwa katika nafasi hiyo. | 1. Ibara ya 133 inakuwa ibara ya 137.<br>2. Ibara ndogo ya (1) itasomeka kama ifuatavyo:-<br>"Kutakuwa na Katibu wa Bunge ambaye atateuliwa na Rais kutoka miongoni mwa majina matatu ya watu wenye madaraka ya juu katika utumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano yatakayopendekezwa na Tume ya Utumishi wa Umma". |
| | | (ii) 133-Katibu wa Bunge ateuliwe na Rais kutoka miongoni mwa majina matatu yatakayopendekezwa na Tume ya Utumishi wa Umma. | Katibu wa Bunge ni Mtendaji Mkuu kama walivyo Mtendaji Mkuu wa Mahakama na Makatibu Wakuu wa Wizara. | |
| | | (ii) Ibara ndogo ya (1) | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | irekebishwe kwa kufuta maneno “Katibu wa Bunge atateuliwa na Tume ya Utumishi ya Bunge” na badala yake isomeke “Tume ya Utumishi ya Bunge itapendekeza majina matatu kwa Rais ambaye atafanya uteuzi”. | | |
| | | (iii) Ibara hii irekebishwe ili isomeke kama ifuatavyo:-<br>133.(1) Kutakuwa na Katibu wa Bunge ambaye atateuliwa na Rais kutokana na mapendekezo ya Tume ya Utumishi wa Bunge na kuidhinishwa na Bunge.<br><br>(2) Mtu hatateuliwa kushika nafasi ya Katibu wa Bunge isipokuwa tu kama ni:-<br>(a) mwenye weledi na uzoefu katika masuala ya Sheria au masuala ya Bunge;<br>(b) mtumishi mwandamizi katika utumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano; na<br>(c) Mwadilifu na mwenye tabia na mwenendo mwema. | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | (3) Katibu wa Bunge atakuwa ndiye Mtendaji Mkuu wa Ofisi ya Bunge na atawajibika kwa utendaji bora wa shughuli za Bunge kwa kuzingatia masharti ya Katiba hii na sheria za nchi". | | |
| | | (iv) Iongezwe ibara ndogo mpya itakayoanzisha Tume ya Utumishi wa Bunge ikijumuisha majukumu yake. | Kama ilivyo kwa Tume nyingine. | |
| | | (v) Iongezwe ibara mpya itakayoanzisha Mfuko wa Bunge kama ilivyo ibara ya 175 inayoanzisha Mfuko wa Mahakama. | | |
| | | (vii) Kutakuwa na katibu wa bunge ambaye atateuliwa na tume ya utumishi ya bunge kutoka miongoni mwa watu wenye madaraka ya juu katika utumishi wa serikali ya jamhuri ya muungano.na vikao vya bunge vitafanyika kwa haki na usawa kati ya nchi washirika,na ikulu ya Rais wa Muungano itakuwepo Zanzibar. | Vikao vya bunge kwa miaka 50 sasa havijafanyika Zanzibar kuwepo ibara hii italazimisha Serekali katika utendaji wa Bunge. | |
| 134. | Sekretarieti ya Bunge | (i) Ibara ndogo ya (1) irekebishwe kwa kufuta maneno "kutoka sehemu zote Washirika wa | | Ibara ya 134 inakuwa 138 na Ibara ibaki kama ilivyo. |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | Muungano". | | |
| | | (ii) Ibara hii irekebishwe kwa kuongeza Ibara ndogo itakayoeleza sifa za Katibu wa Bunge ambayo itasomeka kama ifuatavyo: "(4) Sifa za mtu kuteuliwa kuwa Katibu wa Bunge iwe ni shahada ya kwanza katika fani za sheria, utawala au mipango na awe na uzoefu katika fani hizo kwa muda usiopungua miaka saba". | | |
| | | (iii) 134. Ibara itamke bayana ni Chombo kipi ambacho Katibu wa Bunge atakuwa anawajibika nacho, na watumishi wa Sekreteriet wanawajibika kwa nani. | | |

## 9.3 SEHEMU YA NNE: UTARATIBU WA SHUGHULI BUNGENI

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| 135. | Kanuni za Kudumu za Bunge | (i) Katika Ibara ndogo ya (1) neno "linaweza" lifutwe na iandikwe "litatunga". | | Ibara ya 135 inakuwa 139 ibaki kama ilivyo. |
| | | (ii) Iongezwe ibara ndogo mpya ya (4) itakayosomeka kama ifuatavyo:<br>"(4) Katika kulihutubua Bunge katika kikao cha mwisho wa mwaka, Rais pamoja na mambo mengine, atatoa taarifa kuhusu deni la Taifa". | | |
| 136. | Rais kulihutubia Bunge | (i) Ibara hii irekebishwe kwa kueleza Kiongozi wa shughuli za Serikali Bungeni awe ni waziri Mkuu. | Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni hajatajwa sehemu yoyote ya rasimu hii wala uteuzi wake. | 1. Ibara ya 136 inakuwa ibara ya 140.<br>2. Ibara ndogo ya (3) imefutwa" |
| | | (ii) Ibara ya 136(2) irekebishwe kwa kufuta maneno "Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni" na badala yake kuweka maneno "Waziri Mwandamizi". | Katika mfumo unaopendekezwa hakuna Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni. | |
| | | (iii) Ibara ndogo ya (2) ifutwe na badala yake iandikwe kama ifuatavyo:<br>"(2) Bila ya kuathiri masharti ya ibara ndogo ya (1) Rais anaweza wakati wowote, ikiwa Bunge litapitisha azimio maalum kumwalika, | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | kulihutubia Bunge". | | |
| | | (iv) Mara baada ya ibara ya 136 ziongezwe Sura Mpya itakayoeleza kuhusu Uongozi wa Bunge ambayo itaeleza kama ifuatavyo:<br><br>*Tume ya Utumishi wa Bunge*<br>136.(1) Kutakuwa na Tume ya Utumishi wa Bunge ambayo itaundwa na Wajumbe wafuatao:-<br>(a) Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano ambaye atakuwa ni Mwenyekiti;<br>(b) Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano ambaye atakuwa Makamu Mwenyekiti;<br>(c) Waziri anayehusika na masuala ya Bunge;<br>(d) Waziri anayehusika na masuala ya Utumishi wa Umma;<br>(e) Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni au mwakilishi wake;<br>(f) Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano;<br>(g) Spika wa Bunge la Tanzania Bara;<br>(h) Spika wa Baraza la Wawakilishi, Zanzibar.<br>(2) Katibu wa Bunge atakuwa | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | Katibu wa Tume ya Utumishi wa Bunge.<br>(3) Tume inaweza kumualika mtu mwingine yeyote mwenye utaalam mahususi kushiriki kikao chochote cha Tume, isipokuwa mtu huyo hatakuwa na haki ya kupiga kura.<br>(4) Tume itaweka utaratibu wa kuendesha vikao vyake.<br><br>137.(1) Tume ya Utumishi wa Bunge itakuwa na wajibu wa kuendeleza, kuwezesha na kuhakikisha utekelezaji wa kazi na shughuli za Bunge, kwa ufanisi na uwazi.<br>(2) Tume ya Utumishi wa Bunge itatekeleza majukumu yafuatayo:-<br>(a) kupendekeza kwa Rais majina ya watu wanaofaa kuteuliwa kushika nafasi ya Katibu wa Bunge;<br>(b) kupendekeza masharti ya utumishi wa Katibu wa Bunge, ikiwemo masuala ya nidhamu na maslahi yake;<br>(c) kuweka masharti ya utumishi wa Watumishi wengine wa Bunge, ikiwemo masuala yanayohusu nidhamu, maslahi na maendeleo yao; | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | (d) kuajiri, kuthibitisha kazini, kupandisha vyeo na kusimamia nidhamu za watumishi wa Bunge, kuteua, kuajiri na kupokea malalamiko dhidi yao kwa mujibu wa sheria itakayotungwa na Bunge;<br>(e) kuandaa na kutekeleza mipango ya kujiendeleza kielimu kwa Watumishi wa Bunge;<br>(f) kuandaa na kupendekeza Serikalini, viwango vya mishahara, posho na marupurupu mengine kwa Wabunge na Watumishi wa Bunge;<br>(g) kupendekeza Serikalini maboresho ya Taasisi ya Bunge ili kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya kikatiba ya Bunge;<br>(h) kutekeleza majukumu yoyote yatakayowekwa kwa mujibu wa Katiba hii au sheria nyingine.<br><br>(3) Katika kutekeleza majukumu yake, Tume itazingatia:-<br>(a) uwazi katika mchakato wa uteuzi na ajira ya watumishi wa Bunge la Jamhuri ya Muungano; | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | (b) uwakilishi wa sehemu mbili za Washirika wa Muungano; na<br>(c) uwakilishi wa kijinsia.<br><br>(4) Katika kutekeleza majukumu yake, Tume inaweza kukasimu madaraka yake kwa kamati mbalimbali zitakazoundwa kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Bunge.<br>(5) Bunge litatunga sheria itakayoweka masharti ya utekelezaji wa majukumu ya Tume.<br><br>*Mfuko wa Bunge*<br>138.(1) Kutakuwa na mfuko utakaoitwa Mfuko wa Bunge la Jamhuri ya Muungano ambao utakuwa chini ya usimamizi wa Katibu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano.<br>(2) Mfuko wa Bunge la Jamhuri ya Muungano utatumika kwa ajili ya kugharamia shughuli za uendeshaji, pamoja na shughuli zingine muhimu katika utekelezaji wa majukumu ya Bunge la Jamhuri ya Muungano.<br>(3) Serikali itahakikisha | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | kwamba, katika kila bajeti ya mwaka wa fedha wa Serikali, inatenga kwa kiwango kinachotosha, fedha ambazo zitaingizwa katika Mfuko wa Bunge la Jamhuri ya Muungano.<br>(4) Bunge litatunga sheria itakayoweka masharti kuhusu uendeshaji wa Mfuko wa Bunge la Jamhuri ya Muungano." | | |
| 137. | Mikutano ya Bunge | Katika Ibara ndogo ya (2) neno "limegizwa" lisomeke "limeagizwa". | | 1. Ibara 137 inakuwa ibara ya 141.<br>2. Ibara inabaki kama ilivyo. |
| | | (ii) .Bunge liwe na Makao Makuu yake Rasmi,na litakiwe kukutana hapo tu si kwengineko. | Kupunguza gharama. | |
| 138. | Uongozi na vikao vya Bunge | 138 Ibaki kama ilivyo. | Inajitosheleza. | Ibara ya 138 inakuwa 142 na Inabaki kama ilivyo |
| 139. | Akidi ya vikao vya Bunge | (i) Ibara hii irekebishwe kwa kufuta maneno "Wabunge wote" na badala yake kuweka maneno "Wabunge wa kila Mshirika wa Muungano". | | 1. Ibara ya 139 inakuwa 143.<br>2. Ibara 139 (2) mwisho wa sentensi yameongezwa maneno yanayosomeka;- "isipokuwa kwa masuala yaliyowekewa masharti |
| | | (ii) Ibara ndogo ya (1) irekebishwe ili kuweka masharti ya angalau theluthi moja ya wabunge wote wa kila mshirika wa muungano wawepo ili kutimiza akidi. | Ili akidi ya Bunge izingatie uwepo wa wabunge wa pande zote za Muungano. | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | (iii) Katika Ibara ndogo ya (2) maneno "ya siri" yaongezwe baada ya neno "kura" hivyo kuwa "kura ya siri". | | mahususi chini ya katiba hii" |
| | | (iv) • 139-Ibara ya (3) iwe ya (2) na kinyume chake (vice versa). | Kupata mtiririko mzuri. | |
| | | (v) Ibara ndogo ya (2) irekebishwe kwa kuongeza maneno "linapaswa kuungwa mkono kwa zaidi ya 50% ya wabunge wote waliohudhuria na kupiga kura lakini kwa kuzingatia kuwa suala linaloamuliwa liwe linaungwa mkono na angalau theluthi moja ya wabunge kutoka kila upande". | Ili kuepusha maamuzi ya Bunge kufanywa na upande mmoja wa Muungano. | |
| 140. | Kamati za Bunge | Ibara ndogo ya (4) ifafanuliwe zaidi. | Haieleweki. | Ibara ya 140 inakuwa 144 na inabaki kama ilivyo. |

## 9.4 SEHEMU YA TANO:MADARAKA NA HAKI ZA BUNGE

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| 141. | Uhuru wa majadiliano Bungeni | (i) Ibara ya 141 ifutwe na irudishwe katika kanuni za Bunge. | Ibara hii inaweza kubadilika mara kwa mara hivyo kwa njia ya Kanuni ni rahisi kukidhi haja ya marekebisho kuliko kwenye Katiba. | Ibara ya 141 inakuwa 145 na Ibaki kama ilivyo. |
| | | (ii) 141(2).Neno"Hatatakiwa" lisomeke"Hatarajiwi". | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | (iii) Ibara ndogo ya (4) irekebishwe ili kuruhusu Wabunge kushtakiwa kwa kusema uongo. | Ili kudhibiti uhuru wa Wabunge na kudhibiti matumizi mabaya, hususan, kauli zenye kuleta uchochezi na kudhalilisha watu wengine nje ya Bunge. | |
| 142. | Mipaka ya majadiliano Bungeni | (i) Ibara hii ifutwe na irudishwe katika kanuni za Bunge. | Ibara hii inaweza kubadilika mara kwa mara hivyo kwa njia ya Kanuni ni rahisi kukidhi haja ya marekebisho kuliko kwenye Katiba. | Ibara ya 142 inakuwa 146 na Ibaki kama ilivyo. |
| | | (ii) Baada ya ibara hii iongezwe Sura mpya itakayoelezea Serikali ya Zanzibar kama ilivyo katika Sura ya Nne ya Katiba ya sasa. | | |
| | | (iii) 142(1).Ibara hii ifutwe. | Masharti yake yanatoa mwanya wa kuminya uhuru wa wabunge kujieleza na kutoa maoni yao. | |
| | | (iv) Ibara ndogo ya (2) irekebishwe ili kuruhusu mwananchi yoyote atakayeona kwamba amedhalilishwa na Mbunge wakati wa mjadala Bungeni aweze kumshtaki Mbunge huyo Mahakamani. | | |
| | | (v) Katika ibara ndogo ya (2) yaongezwe maneno "na Mahakama ya Kadhi" mwisho wa sentensi. | Ni muhimu Katiba iitambue Mahakama ya Kadhi na kuwa ni chombo kikuu cha kusimamia mahakama hiyo.<br>Mahakama ya Kadhi ianzishwe na ishughulikie mambo ya mirathi, ndoa, talaka waqfu, malezi ya watoto, hibba, wosia, biashara, bima, benki bila ya kuingiliwa na chombo chochote. | |
| | | | | Imeongezwa ibara |

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Maoni* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| | | | | mpya ya 147 inayohusu uanzishwaji wa "Tume ya Utumishi wa Bunge." |
| | | | | Imeongezwa ibara mpya ya 148 inayohusu "Majukumu ya Tume ya Utumishi wa Bunge." |
| | | | | Imeongezwa ibara mpya ya 149 inayozumngumzia "uanzishwaji wa mfuko wa Bunge" |

# SURA YA KUMI YA RASIMU

## 10.0 SEHEMU YA KWANZA: MISINGI YA UTOAJI HAKI NA UHURU WA MAHAKAMA

| ***Ibara Na.*** | ***Kichwa cha Habari*** | ***Maoni ya Mabaraza*** | ***Sababu ya Maoni*** | ***Marekebisho ya Tume*** |
|---|---|---|---|---|
| 143. | Kuanzishwa kwa Mahakama ya Tanzania | (i) Ibara hii irekebishwe ili kuweka mfumo wa kuwa na Mahakama moja tu ya Muungano. | Ili kupunguza gharama za Muungano. | Ibara ya 143 itakuwa ibara ya 150 na Ibaki kama ilivyo. |
| | | (iv) 143(2)-Mahakama ya Rufani isiwe ya Muungano bali iwe chini ya mamlaka ya nchi washirika. | Ni vema mamlaka za nchi washirika zikaamua kuwa na Mahakama ya Rufani au kutokuwa nazo. | |
| | | | | |
| 144. | Misingi ya utoaji haki | (i) Katika aya (a) yaongezwe maneno “rangi na jinsia”. | Ili kupanua wigo wa haki kulindwa na kutendeka. | 1. Ibara ya 144 inakuwa ibara ya 151.<br>2. Ibara ndogo ya (e) imalizikie kwenye maneno ‘masharti ya kiufundi’. |
| | | (ii) Aya (b) irekebishwe kwa kuweka muda maalumu wa kumalizika kwa kesi au mashauri ya aina zote. | | |
| | | (iii) Aya (f) irekebishwe na isomeke kama ifuatavyo:<br>“(f) Lugha ya Kiswahili itumike kikatiba katika nyaraka zote na iwe na usawa wa kutetea wote. | | |
| | | (iv) 144(e)-Maneno“yanayoweza kuchelewesha au kukwamisha haki | Kuweka ufasaha. | |

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Maoni* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| | | kutendeka". | | |
| 145. | Uhuru wa Mahakama | (i) Katika ibara ndogo (1) yaongezwe maneno "na sheria za nchi" mara baada ya maneno "Katiba hii". | | 1. Ibara ya 145 inakuwa ibara ya 152.<br><br>2. Ibara ndogo ya (6) imerekebishwa na isomeke:<br><br>''Jaji wa Mahakama ya Juu au Jaji wa Mahakama ya Rufani hatashtakiwa kwa jambo lolote alilolifanya au kutolifanya kwa nia njema katika utekelezaji wa shughuli ya utoaji haki kwa mujibu wa sheria za nchi". |
| | | (ii) 145(1)-(5) ibaki kama ilivyo. | Inajitosheleza. | |
| | | (iii) Iongezwe Ibara ndogo ya (2) itakayosomeka kama ilivyo ibara ya 165(5) ya Katiba ya Afrika ya Kusini. | | |
| | | (ii) Ibara ndogo ya (1) na (2) zirekebishwe kwa kuweka masharti yatakayosaidia kuthibiti uzembe wa Mahakama pale inapothibitika. | Kuhakikisha kuwa haki inatolewa kwa wakati. | |
| | | (iii) Ibara ndogo ya (3), (4) na (5) zifutwe na badala yake zielezwe kwenye Sheria. | | |
| | | (iv) Katika ibara ndogo ya (2), (3), (4) na (5) maneno 'Mahakama ya Juu na Mahakama ya Rufani" yafutwe. | Kinga ni kwa Majaji wote. | |
| | | (v) Ibara itaje nafasi za hao watumishi mfano, Jaji ambao hufanya shughuli za utoaji Haki. | Neno mtumishi yeyote liko pana sana. | |
| | | (vi) Katika ibara ndogo ya (6) neno "Mtumishi" lifutwe na badala yake iandikwe "Jaji au Hakimu". | Kuwaondolea kinga watumishi wengine ambao kwa asili ya majukumu yao hawafanyi kazi ya kutoa haki. | |
| | | Neno "mtumishi wa mahakama" litafsiriwe katika Ibara ya 238. | | |
| | | (vii) Katika ibara ndogo ya (6) neno "yeyote" lifutwe; | | |
| | | (viii) Ibara ndogo ya (6) ifutwe na badala yake iandikwe kama ifuatavyo: | Ili mtumishi wa mahakama akifanya kosa kwa kuamua kesi bila ya haki achukuliwe hatua | |

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Maoni* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| | | "(6) Mtumishi yeyote wa Mahakama anaweza kushitakiwa kwa jambo lolote alilolifanya au kutolifanya kwa makusudi katika utekelezaji wa shughuli ya utoaji haki kwa mujibu wa Sheria." | ya kushitakiwa. | |

## 10.1 SEHEMU YA PILI:MUUNDO WA MAHAKAMA

### (a) Mahakama za Jamhuri ya Muungano

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Maoni* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| 146. | Muundo wa Mahakama | (i) Katika ibara ndogo ya (1) maneno "Bila ya kuathiri masharti yoyote yaliyotangulia katika sehemu hii kutakuwa na" yafutwe. | | Ibara ya 146 inakuwa 153 na inabaki kama ilivyo. |
| | | (ii) Ama 146(1) ibaki kama ilivyo | Inajitosheleza. | |
| | | Au | | |
| | | 146(1)-Mahakama ya Rufani isiwe ya Muungano bali iwe chini ya mamlaka ya nchi washirika. | Ni vema mamlaka za nchi washirika zikaamua kuwa na Mahakama ya Rufani au kutokuwa nazo. | |
| | | (iii) Katika Ibara ndogo ya (1) ziongezwe aya (c) na (d) kama ifuatavyo:<br>"(c) Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano; na<br>(d) Mahakama za Mahakimu zitakazoundwa kwa mujibu wa sheria ya Bunge." | | |
| | | (iv) Iongezwe aya (c) mpya katika ibara ndogo ya (1) kama ifuatavyo:<br>"(c) Mahakama Kuu ya Kadhi". | Bila ya Mahakama ya Kadhi kutambuliwa na Katiba, itakuwa ni vigumu kuanzishwa kwa Mahakama katika Serikali ya Tanganyika ambayo haikuwapo kabla katika Katiba hii. | |
| | | (v) Ibara ndogo ya (2) ibara hii ifafanue nini maana ya Mahakama ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. | | |
| | | (vi) Ibara ndogo ya (2) ifutwe na badala yake iandikwe kama ifuatavyo:<br>"(2) Mahakama Kuu ya Jamhuri ya | | |

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Maoni* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| | | Muungano iliyopendekezwa katika ibara ya 146(1)(c) itashughulikia utoaji haki katika mambo ya Muungano na yasiyo ya Muungano kwa Tanzania Bara". | | |

### (b) Mahakama ya Juu ya Jamhuri ya Muungano

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| 147. | Mahakama ya Juu | (i) Katika aya (a) ya Ibara ndogo ya (1) neno "Rais" lifutwe na badala yake liwekwe "Jaji Mkuu Kiongozi". | | 1. Ibara ya 147 inakuwa 154.<br>2. Katika Ibara ndogo ya (1)(a) na (b), maneno Jaji Mkuu na Naibu Jaji Mkuu yafuatiwe na maneno "wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania." |
| | | (ii) Katika aya (b) ya ibara ndogo ya (1) maneno "Makamu wa Rais" yafutwe na badala yake iandikwe "Naibu Jaji Mkuu Kiongozi". | | |
| | | (iii) Ibara hii irekebishwe ili kufuta vyeo vya Urais na Makamu Rais katika mhimili wa Mahakama ya Juu. | Vyeo hivi vibadilishwe na kuweka Jaji Mkuu na Makamu wa Jaji Mkuu. | |
| | | (iv) Katika ibara hii neno "Rais" lifutwe na badala yake Jaji Mkuu abaki kuwa Jaji Mkuu wa Mahakama. | | |
| | | (v) Katika aya (c) ya ibara ndogo ya (1) maneno "wasiopungua saba" yafutwe na badala yake iandikwe "wasiopungua watano na wasiozidi saba". | Kuwepo ukomo wa idadi ya chini na ya juu ya Majaji katika Mahakama ya Juu. | |
| | | (vi) Katika ibara ndogo ya (2) maneno "uwakilishi wa sehemu mbili za Washirika wa Muungano" yafutwe na badala yake iandikwe "sheria za nchi". | | |
| | | (vii) Ibara ndogo ya (2) iishie katika maneno "Katiba hii". | | |
| | | (viii) Ibara ndogo ya (2) na Ibara ya 158(2) zifanyiwe marekebisho ili zitamke wazi Majaji wa Mahakama za Muungano watateuliwa kwa msingi wa usawa baina ya nchi washirika wa Muungano" na hivyo kuwa na idadi sawa ya Majaji kati ya Zanzibar na Tanganyika. | Maneno yaliyotumika kwenye Rasimu uwakilishi na uwiano hayakupewa tafsiri. | |
| 148. | Akidi ya vikao vya | (i) Ibara ndogo ya (2) ifutwe. | Kazi za Mahakama ni kazi | Ibara ya 148 |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | Mahakama ya Juu | | za kitaaluma na vigezo vya uwakilishi visitumike katika kupata akidi ya vikao vya Mahakama ya Juu. | inakuwa 155 na inabaki kama ilivyo. |
| | | (ii) Ibara ndogo ya (2) ifanyiwe marekebisho ili itamke ''Akidi ya majaji iwe ni idadi sawa baina ya nchi washirika wa Muungano. | Maneno ''uwakilishi wa sehemu mbili za Muungano" yanaweza kuleta utatanishi katika tafsiri. | |
| | | (iii) Katika Ibara ndogo ya (3) neno "uamuzi" lifutwe na badala yake iandikwe "au ushauri". | | |
| 149. | Madaraka ya Mahakama ya Juu | (i) Katika Ibara ndogo ya (1) neno "Washirika" lifutwe na badala yake iandikwe "Serikali ya Muungano na Serikali ya Zanzibar". | | 1. Ibara ya 149 inakuwa 156.<br>2. Ibara ndogo ya (1)(b) imefanyiwa marekebisho na itasomeka ''Kusikiliza na kuamua mashauri yatakayowasilishwa na wananchi, serikalini au serikali za nchi washirika kuhusu tafsiri au utekelezaji wa katiba hii"<br>3. Ibara ndogo ya (1)(e) mwisho wa sentensi yameongezwa maneno ''pale itakapoombwa" |
| | | (ii) 149(1)(c-e).Ibara ifafanue ni vipi migogoro hiyo itafikishwa katika mahakama hiyo, itaingiliaje migogoro hiyo na pia itatoa ushauri kuanzia wapi na kwa nani? | (ii) Kuepusha lawama katika utekelezaji wa majukumu yake. | |
| | | (iii) Aya (e) ya ibara ndogo ya (1) ifutwe. | (a) Kutoa maoni ya kiushauri si kazi ya kimahakama.<br>(b) Pia itakuwa inaingilia mhimili mwingine wa mahakama. | |
| | | (iv) 149 ibaki kama ilivyo. Isipokuwa Ibara ya 149(1)(e) irekebishwe kwa kuongeza maneno "pale itakapoombwa" baada ya maneno "Serikali za Washirika; na". | Inajitosheleza. | |
| | | (v) Aya (e) ya Ibara ndogo ya (1) ifutwe. | Ili kuzuia Mahakama ya Muungano kuingilia mamlaka za Nchi | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | Washirika. | 4. Katika Ibara ndogo ya 2 neno "zitabanwa" lisomeke "zitalazimika"<br>5. Maneno "Mahakama ya Jamhuri ya Muungano yasomeke "Mahakama ya Rufani". |
| | | (vi) Katika aya (c) ya ibara ndogo ya (1) maneno "kutoka Mahakama ya Rufani" yafutwe na badala yake iandikwe 'kwa mujibu wa sheria itakayotungwa na Bunge". | | |
| 150. | Madaraka ya Majaji wa Mahakama ya Juu | Ibara hii irekebishwe kwa kuzingatia Muundo wa Serikali mbili. | | Ibara ya 150 inakuwa ya 157.<br>Ibara ndogo ya (1) imefanyiwa marekebisho na itasomeka "Jaji yeyote wa Mahakama ya Juu atakuwa na Mamlaka ya kusikiliza na kuamua shauri lolote katika |

## (c) Uteuzi wa Majaji wa Mahakama ya Juu

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| 151. | Uteuzi wa Jaji Mkuu | (j) Ibara ndogo ya (1) ibadilishwe na iandikwe kama ifuatavyo:<br>"(1) Jaji Mkuu atateuliwa na Rais baada ya kupendekezwa na Tume | | Mahakama ya Juu".<br>1. Ibara ya 151 inakuwa ya 158.<br>2. Ibara ndogo ya (3) |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | ya Utumishi wa Mahakama na kabla ya kuapishwa jina lake litawasilishwa Bungeni kwa ajili ya kuthibitishwa na Bunge". | | imefanyiwa marekebisho na itasomeka:<br><br>(a) Awe raia wa kuzaliwa wa Jamhuri ya Muungano mwenye sifa ya uadilifu, tabia njema na uaminifu;<br>(b) Awe na shahada ya sheria kutoka katika Chuo kinachotambuliwa na Mamlaka zinazoshughulikia Elimu ya Juu katika Jamhuri ya Muungano; na<br>(c) Awe:<br>i. Amefanya kazi ya ujaji katika Mahakama ya Rufani au Mahakama Kuu za nchi Washirika; au<br>ii. Amefanya kazi ya utumishi wa Umma katika Jamhuri ya Muungano au anataaluma akiwa na sifa ya kusajiliwa kuwa Wakili au wakili na amekuwa na sifa hizi mfululizo kwa |
| | | (i) 151(1-3) ibara irekebishwe na isomeke "Jaji Mkuu atapendekezwa na Tume ya Utumishi wa Mahakama, Katiba na Sheria, baada ya kutangazwa nafasi hiyo kwa wananchi na kutoa siku (30) za kupeleka maombi, siku (15) za kuweka pingamizi au malalamiko kwa maandishi kwa Tume.Baada ya kufanyiwa usaili wa wazi na Tume kupata majina matatu yatapelekwa kwa Spika wa Bunge kwa kupigiwa kura ili kumpata mshindi mmoja tu.Jaji Mkuu ataapa mbele ya Rais". | | |
| | | (ii) Ibara ndogo ya (1) ifutwe na badala yake iandikwe kama ifuatavyo:<br>"(1) Jaji Mkuu atateuliwa na Rais kutoka katika majina ya Majaji wa Mahakama ya Juu au Majaji wa Mahakama ya Rufani yatakayopendekezwa na Tume ya Utumishi wa Mahakama na ataapishwa na Rais". | (a) Ili kuepusha siasa wakati wa uteuzi wa Jaji Mkuu;<br>(b) Mahakama ya Juu sio sehemu ya kufanyia majaribio. | |
| | | (iii) Ibara hii irekebishwe ili Tume ya Utumishi wa Mahakama iteue majina matatu yatakayopigiwa kura na Majaji wote na atakayeshinda ndiyo aapishwe na | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | Rais. | | muda usiopungua miaka kumi na tano. |
| | | (iv) Ibara hii irekebishwe ili Jaji mkuu na Naibu wake waombe hizi nafasi na wafanyiwe usaili wa wazi na wathibitishwe na Bunge na wananchi waruhusiwe kuweka pingamizi. | Mamlaka ya uteuzi wa Jaji yasiwekwe kwa Rais. | |
| | | (v) Ibara ndogo ya (3) maneno "miaka kumi na Tano" yafutwe na isomeke "miaka kumi". | Miaka kumi na tano ya sifa za ujaji ni nyingi sana. | |
| | | (vi) Ibara hii irekebishwe ili Jaji Mkuu asithibitishwe na Bunge. | Ni Mhimili mwingine wa Dola. | |
| | | (vii) Sifa za mtu atakayeteuliwa kuwa Jaji mkuu zibainishwe kama ifauatavyo:-<br>(a) [awe raia wa kuzaliwa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwenye sifa ya uadilifu, tabia njema na uaminifu;<br>(b) awe na shahada ya sheria kutoka katika chuo kinachotambuliwa na mamlaka inayoshughulikia elimu ya juu katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na<br>(c) awe:<br>(i) amefanya kazi ya ujaji katika Mahakama ya Rufani au Mahakama Kuu za Nchi Washirika; au<br>(ii) amefanya kazi ya utumishi wa umma katika Jamhuri ya Muungano au uanataaluma akiwa na sifa ya kusajiliwa kuwa wakili na amekuwa na sifa hizo | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | mfululizo kwa muda usiopungua miaka ishirini.] | | |
| 152. | Uteuzi wa Naibu Jaji Mkuu | (i) Ibara ndogo ya (1) irekebishwe ili Majaji wa Mahakama ya Juu wateuliwe kutoka Mahakamani. | Kuepusha watumishi kutoka kada nyingine kuteuliwa kuwa Jaji. | Ibara aya 152 inakuwa 159 na inabaki kama ilivyo. |
| | | (ii) 152(1).Sifa na kupatikana kwake iwe sawa na mapendekezo yaliyopo kwa Jaji Mkuu. | | |
| | | (iii) 152- Uteuzi wa Naibu Jaji Mkuu uzingatie kuwa: ikiwa Jaji Mkuu anatoka upande mmoja wa Muungano basi Naibu Jaji Mkuu atoke upande mwingine wa Muungano kwa kuzingatia sifa na weledi. | Kuweka uwiano wa pande mbili za Muungano. | |
| | | (iv) Ibara ya 152 ifanyiwe marekebisho ili Tume ya Utumishi wa Mahakama iteue majina matatu yatakayopigiwa kura na Majaji wote na majina hayo matatu yatokane na ushindani wa watu watakaoomba nafasi hiyo. | | |
| | | (v) Ibara hii irekebishwe ili Naibu Jaji Mkuu asithibitishwe na Bunge. | Ni Mhimili mwingine wa Dola. | |
| 153. | Uteuzi wa Majaji wa Mahakama ya Juu | (i) Ibara hii irekebishwe ili Majaji wa Mahakama ya Juu wateuliwa toka miongoni mwa Majaji wa Mahakama ya Juu. | | 1. Ibara ya 153 itakuwa ya 160.<br>2. Ibara ndogo ya (2) imefanyiwa marekebisho na itasomeka:<br><br>"(2)Mtu anaweza kuteuliwa kuwa Jaji wa Mahakama ya Juu |
| | | (ii) Ibara hii ifutwe na kuandikwa upya kama ifuatavyo:<br>"Mtu atakayeteuliwa kuwa Jaji wa Mahakama ya Juu sharti awe amekuwa Jaji wa Mahakama kuu ya Tanzania, Mahakama kuu ya | Ili kuondoa uwezekano wa mtu mwingine asiye na uzoefu wa mahakama kuteuliwa kuingia katika mahakama ya juu kabisa ya nchi ambayo ndiyo | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | Zanzibar au Jaji wa Majakama ya Rufaa". | inatoa uamuzi wa mwisho katika maswala ya kisheria yaliyo mahakamani. | endapo atakuwa na sifa zifuatazo:<br>(a) awe raia wa kuzaliwa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwenye sifa ya uadilifu, tabia njema na uaminifu<br>(b) awe na shahada ya sheria kutoka chuo elimu ya juu kinachotambuliwa na mamlaka inayoshughulikia elimu ya juu wa katika Jamhuri ya Muungano Tanzania; na<br>(c) awe:<br>(i) amefanya kazi ya ujaji katika Mahakama ya Rufani au Mahakama Kuu za Nchi Washirika; au<br>(ii) amefanya kazi ya utumishi wa umma katika Jamhuri ya Muungano au uanataaluma akiwa na sifa ya kusajiliwa kuwa wakili au wakili na amekuwa na sifa hizo mfululizo kwa muda usiopungua miaka kumi na tano." |
| | | (iii) Katika Ibara ndogo ya (2) liongezwe neno "weledi" baada ya maneno "atakuwa na sifa ya". | | |
| | | (iv) Ibara ibainishe sifa za mtu atakayeteuliwa kuwa Jaji wa Mahakam ya Juu.<br>[(1) Mtu anaweza kuteuliwa kuwa Jaji wa Mahakama ya Juu endapo atakuwa na sifa zifuatazo:<br>(a) awe raia wa kuzaliwa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwenye sifa ya uadilifu, tabia njema na uaminifu<br>(b) awe na shahada ya sheria kutoka katika chuo kinachotambuliwa na mamlaka inayoshughulikia elimu ya juu katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na<br>(c) awe:<br>(i) amefanya kazi ya ujaji katika Mahakama ya Rufani au Mahakama Kuu za Nchi Washirika; au<br>(ii) amefanya kazi ya utumishi wa umma katika Jamhuri ya Muungano au uanataaluma akiwa na sifa ya kusajiliwa kuwa wakili au wakili na amekuwa na sifa hizo mfululizo kwa muda | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | usiopungua miaka kumi na tano.] | | |
| | | (d) Katika aya (c) ya Ibara ndogo ya (2) maneno "miaka kumi" yafutwe na bada la yake iandikwe "miaka kumi na tano". | | |
| | | (e) Iongezwe ibara ndogo mpya itakayoeleza sifa za mtu kuteuliwa kuwa Jaji katika Mahakama za ngazi zote sifa zitofautiane katika umri. | | |
| | | (f) Ibara irekebishwe ili Majaji waombe nafasi kupitia kwa Tume ya Utumishi wa Mahakama na Jaji Mkuu mamlaka zaidi katika uteuzi wa majaji na wananchi waruhusiwe kuweka pingamizi. | | |
| | | (g) Ibara ndogo ya (3) ifutwe. | Rais asiwe na mamlaka ya kutengua masharti ya sifa za majaji. | |
| 154. | Kiapo cha Majaji wa Mahakama ya Juu | Ibara ya hii irekebishwe kwa kuongeza maneno "amethibitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano" kabla ya maneno "na ameapishwa." | (a) Ibara hii itashabihiiana na Ibara ya 151(1) inayohusu uteuzi wa Jaji Mkuu na Ibara ya 152(1) inayohusu uteuzi wa Naibu Jaji Mkuu na hivyo kuwafanya Majaji wote kuwa na viwango vilivyo sawa katika uteuzi na kushika madaraka.<br>(b) Pili, itwafanya Majaji walioteuliwa na | Ibara ya 154 inakuwa 161 na inabaki kama ilivyo. |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | kuthibitishwa na Bunge kuwa huru zaidi katika utekelezaji wa majukumu yao.<br>(c) Tatu, kutokana na umuhimu wa Majaji wa Mahakama ya Juu, ili kutambua uadilifu, weledi na kuweka imani kwa wananchi, ni vema Majaji wote wa Mahakama ya Juu wakathibitishwa na Bunge kwa kupigiwa kura na Wabunge kama ilivyo kwa wakuu wengine wa Taasisi zilizotajwa katika rasimu ya Katiba. | |
| 155. | Muda wa kuwa madarakani kwa Jaji Mkuu, Naibu Jaji Mkuu na Majaji wengine | (i) Ibara ndogo ya (1) irekebishwe kwa kupunguza umri na ubaki miaka sitini na tano. | Umri wa miaka sabini ni mkubwa unaweza kuathiri utendaji. | 1. Ibara ya 155 inakuwa 162.<br>2. Ibara imetenganishwa kwa kuelezea muda wa kuwa madarakani Jaji Mkuu na Naibu Jaji Mkuu na Majaji wa Mahakama ya Juu. |
| | | (ii) Ibara ndogo ya (3) ifutwe. | (a) Haijazingatia sababu zingine zinazoweza kusababisha mtu mwenye nafasi kama hiyo kukoma kazi kama vile kufariki dunia, kuteuliwa nafasi ya juu zaidi, matatizo ya kiafya au kuacha kwa hiari. | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | (b) Aidha, athari za kuongeza muda usio na kikomo unaweza kusababisha uzembe katika utekelezaji wa majukumu yake.<br><br>(c) Vile vile utaratibu huuu unaweza kusababisha majaji kulimbikiziwa au kujilimbikizia kazi nyingi sana au Jaji huyo kutokutoa maamuzi ya mashauri aloyonayo kwa wakati uanostahili huku akijua kuwa anakaribia kustaafu au hata baada ya umri wake wa kustaafu kuwadia na yeye kuendelea kushughulikia mashauri aliyo nayo. Ikumbukwe kuwa taarifa ya kustaafu haiji ghafla.<br><br>(d) Wafanyakazi wote wa Serikali wanafahamu muda wao wa kustaafu hivyo wanatakiwa kutekeleza majukumu | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | yao kwa wakati ili unapofika muda wa kustaafu wawe wamekamilisha kazi zao. | |
| | | (iii) Ibara ndogo ya (3) ifutwe. | Kuruhusiwa kukaa madarakani mpaka kumaliza mashauri waliyoyaanza au kazi nyingine | |
| | | (iv) ibara hii irekebishwe kwa kuweka muda maalum wa Jaji Mkuu, Naibu Jaji Mkuu, na Majaji wengine kuendelea kufanya kazi ili kukamilisha shughuli au mashauri waliyoanza kuyasikiliza kabla hawajatimiza umri wa kustaafu. | Kuondoa mianya ya kufanya kazi kwa muda mrefu baada ya kustaafu kwa manufaa yao binafsi. | |
| | | (v) Ibara hii irekebishwe ili umri wa kustaafu Majaji ulingane na watumishi wengine wa umma. | | |
| 156. | Utaratibu wa kukaimu katika Mahakama ya Juu | (i) Ibara hii irekebishwe ili Tume ya Utumishi ya Mahakama iwe na jukumu la kumteua kaimu Jaji Mkuu. | Rais asiwe na mamlaka haya. | Ibara ya 156 inakuwa ya 163 na inabaki kama ilivyo. |
| | | (ii)156 ibaki kama ilivyo. | Inajitosheleza. | |
| | | (iii) Iongezwe aya mpya (d) katika ibara ndogo ya (1) itakayoeleza kama ifuatavyo: “(d) Iwapo Jaji Mkuu na Naibu Jaji Mkuu hawapo ofisini Jaji wa Mahakama ya Juu Mwandamizi atakaimu nafasi hiyo”. | | |
| | | (iv)156(2).Kuwe na muda wa ukomo wa kukaimu nafasi ya Ujaji. | Isitumike vibaya | |

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Maoni* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| 157. | Utaratibu wa kushughulikia nidhamu ya Majaji wa Mahakama ya Juu | (i) Maelezo ya pembeni (marginal note) yaandikwe "Utaratibu wa kushughulikia nidhamu ya Majaji". | Hakuna haja ya kurudia utaratibu wa kushughulikia nidhamu ya Majaji wa Ngazi zote, hivyo ibara hii iwe sawa na ibara ya 167. | 1. Ibara ya 157 inakuwa ya 164.<br><br>2. Ibara imeandikwa upya kuelezea utaratibu wa kushughulikia nidhamu ya Majaji wa Mahakama ya Juu. |
| | | (ii) 157(1) ifutwe. | Utaratibu wa kushughulikia nidhamu ya Majaji umeelezwa katika Ibara ya 157(2)-(5). | |
| | | (ii) Aya (a) ya Ibara ndogo ya (3) ibadilishwe na iandikwe kama ifuatavyo:<br>"(a) Rais anaweza, baada ya kushauriana na Tume ya Utumishi wa Mahakama, kumsimamisha kazi Jaji huyo". | | |
| | | (iii) Katika aya (c) ya Ibara ndogo ya (3) na maneno "tabia mbaya" yafutwe na badala yake kuweka maneno "utovu wa nidhamu". | | |
| | | (iv) 157(2)-(6) ibaki kama ilivyo. | Inajitosheleza. | |
| | | (i) Aya (c) ya Ibara ndogo ya (3) ifutwe. | Masharti ya Ibara hii yaelezwe katika sheria. | |
| | | (ii) Ibara ndogo ya (4) irekebishwe kwa kufuta maneno "tabia mbaya" na badala yake kuweka maneno "utovu wa nidhamu". | | |

### (d) Mahakama ya Rufani ya Jamhuri ya Muungano

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Maoni* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| 158. | Mahakama ya Rufani | (i) Katika aya (b) ya Ibara ndogo ya (1) neno "wasiyozidi" lifutwe na badala yake kuweka neno "wasiyopungua". | | 1. Ibaki ya 158 inakuwa ya 165.<br><br>2. Katika Ibara ndogo ya (1) kimeongezwa kifungu (b) kinachotambulisha uwepo wa Makamu Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani. |
| | | (ii) 158(1)(b).Inapendekezwa idadi ya Majaji wa Mahakama ya Rufaa wapunguzwe. | | |
| | | (iii) Ibara ya 158(1)(b) inapendekezwa aongezwe Makamu Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani | | |
| | | (iv) 158(2) Ibara isomeke "Majaji wa Mahakama ya Rufaa wapendekezwe na Tume ya Utumishi wa Mahakama,baada ya kutangazwa nafasi hizo kwa siku (30) na siku (15) za kuweka pingamizi,kufanyiwa usaili na kuthibitishwa Bungeni".Majaji wa Mahakama ya Rufani wataapa Mbele ya Rais, | | |
| | | (v) Ibara ndogo ya (2) irekebishwe kwa kufuta neno "uwiano" na badala yake kuweka neno "usawa". | | |
| | | (vi) 158(2).Ibara ifafanue ni vipi uwiano huo utakuwa. | | |
| | | (vii) Ibada ndogo ya (2) irekebishwe kwa kufuta maneno "na uwiano wa uwakilishi wa sehemu mbili za Washirika wa Muungano". | | |
| | | (viii) Ibara ndogo ya (3) maneno "za Washirika wa Muungano" | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | yafutwe. | | |
| | | (ix) 158 ibaki kama ilivyo. | Inajitosheleza. | |
| 159. | Akidi ya vikao vya Mahakama ya Rufani. | (i) Aya (b) ya ibara ndogo ya (1) irekebishwe kwa kufuta neno “wasiozidi” badala yake isomeke “wasiopungua”. | | Ibara ya 159 inakuwa 166 na inabaki kama ilivyo. |
| | | (ii) Iongezwe ibara ndogo mpya ya (2) itakayosomeka kama ilivyo ibara ya 123(a) na (b) ya Katiba ya sasa. | | |
| | | (iii) 159 ibaki kama ilivyo. | Inajitosheleza. | |
| 160. | Mamlaka ya Mahakama ya Rufani | (i) ibara ya 160 ibaki kama ilivyo. | Inajitosheleza. | 1. Ibara ya 160 inakuwa 167.<br>2. Katika Ibara ya 167(1)(b) Imerekebishwa na itasomeka kama ifuatavyo:-<br>“Mamlaka ya kufanya mapitio ya maamuzi ya Mahakama Kuu au Mahakama yoyote ya chini iliyopewa mamlaka maalum ya kusikiliza mashauri ambayo kwa kawaida husikilizwa na Mahakama Kuu;” |
| | | (ii) Ibara 160(1)(b) irekebishwe ili isomeke kama ifuatavyo:-<br>“Mamlaka ya kufanya mapitio ya maamuzi ya Mahakama Kuu au Mahakama yoyote ya chini iliyopewa mamlaka maalum ya kusikiliza mashauri ambayo kwa kawaida husikilizwa na Mahakama Kuu;” | | |
| 161. | Mamlaka ya Majaji wa Mahakama ya Rufani | (i) Katika Ibara ndogo ya (2) maneno “za Washirika wa Muungano” yafutwe. | | 1. Ibara ya 161 inakuwa 166.<br>2. Ibara ndogo ya (1) imerekebishwa ili kutoa mamlaka kwa Jaji yeyote wa Mahakama ya Rufani |
| | | (ii) 161(2) Inapendekezwa kuwepo kwa Ukomo wa muda ambao atatakiwa kumaliza shughuli hizo, na kama hawezi,basi zihamishiwe kwa Jaji au | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | Hakimu mwengine katika Mahakama husika. | | kuweza kusikiliza shauri lolote katika Mahakama ya Rufani. |
| | | (iii) 161 ibaki kama ilivyo. | Inajitosheleza. | |
| | | (iv) Kichwa cha habari cha (e) kiandikwe<br>"(e) Uteuzi wa Mwenyekiti na Naibu Mwenyekiti". | | |
| | | (v) Ibara ya 161[(1) irekebishwe ili isomeke<br>'Mtu anaweza kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani endapo atakuwa na sifa zifuatazo:<br>(a) awe raia wa kuzaliwa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwenye sifa ya uadilifu, tabia njema na uaminifu;<br>(b) awe na shahada ya sheria kutoka katika chuo kinachotambuliwa na mamlaka inayoshughulikia elimu ya juu katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na<br>(c) awe:<br>(i) amefanya kazi ya ujaji katika Mahakama Kuu za Nchi Washirika; au<br>(ii) amefanya kazi ya utumishi wa umma katika Jamhuri ya Muungano au uanataaluma akiwa na sifa ya kusajiliwa kuwa | | |

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Maoni* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| | | wakili au wakili na amekuwa na sifa hizo mfululizo kwa muda usiopungua miaka kumi.] | | |

### (e) Uteuzi wa majaji wa mahakama ya Rufani

<table>
<tr><th>Ibara Na.</th><th>Kichwa cha Habari</th><th>Maoni ya Mabaraza</th><th>Sababu ya Maoni</th><th>Marekebisho ya Tume</th></tr>
<tr><td rowspan="5">162.</td><td rowspan="5">Uteuzi wa Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani</td><td>(i) Ibara ndogo ya (1) irekebishwe kwa kuongeza maneno “na kuthibitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano” mara baada ya maneno “Tume ya Utumishi wa Mahakama.”</td><td>Kujenga imani kwa wananchi na kumpa uhuru zaidi Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani katika utekelezaji wa majukumu yake.</td><td rowspan="5">1. Ibara ya 162 inakuwa 169.<br><br>2. Ibara ndogo ya (2) imefanyiwa marekebisho na inasomeka kama ifuatavyo:<br><br>Mtu anaweza kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani endapo atakuwa na sifa zifuatazo:<br>(a) awe raia wa kuzaliwa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwenye sifa ya uadilifu, tabia njema na uaminifu;<br>(b) awe na shahada ya sheria kutoka katika chuo kinachotambuliwa na mamlaka inayoshughulikia elimu ya juu katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na<br>(c ) awe:<br>(i) amefanya kazi ya ujaji katika Mahakama Kuu za Nchi Washirika; au</td></tr>
<tr><td>(ii) 162(1).Imependekezwa utaratibu kama unaotumika sasa kwenye katiba ya Kenya wa ushindani na uwazi (Meritocratic).</td><td>ili kuleta ufanisi</td></tr>
<tr><td>(iii) Ibara ndogo ya (1) irekebishwe na iandikwe kama ifuatavyo:<br>“(1) Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani atateuliwa na Rais baada ya kupendekezwa na Tume ya Utumishi wa Mahakama”.</td><td></td></tr>
<tr><td>(iv) Ibara ya 162 ifanyiwe marekebisho ili Tume ya Utumishi wa Mahakama iteue majina matatu yatakayopigiwa kura na Majaji wote. Atakayeshinda ndiyo aapishwe na Rais. Majina hayo matatu yatokane na ushindani wa watu watakaoomba nafasi hiyo.</td><td></td></tr>
<tr><td>(v) Iongezwe ibara ndogo mpya ya (1) itakayosomeka kama ifuatavyo:<br>“(1) Kutakuwa na Mwenyekiti na Naibu Mwenyekiti ambao watateuliwa na Rais”.</td><td></td></tr>
</table>

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | (vi) Ibara ya 162(1) irekebishwe na kusomeka kama ifutavyo:-<br>Mtu anaweza kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani endapo atakuwa na sifa zifuatazo:<br>(a) awe raia wa kuzaliwa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwenye sifa ya uadilifu, tabia njema na uaminifu;<br>(b) awe na shahada ya sheria kutoka katika chuo kinachotambuliwa na mamlaka inayoshughulikia elimu ya juu katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na<br>(c ) awe:<br>(i) amefanya kazi ya ujaji katika Mahakama Kuu za Nchi Washirika; au<br>(ii) amefanya kazi ya utumishi wa umma katika Jamhuri ya Muungano au uanataaluma akiwa na sifa ya kusajiliwa kuwa wakili au wakili na amekuwa na sifa hizo mfululizo kwa muda usiopungua miaka kumi. | | (ii) amefanya kazi ya utumishi wa umma katika Jamhuri ya Muungano au uanataaluma akiwa na sifa ya kusajiliwa kuwa wakili au wakili na amekuwa na sifa hizo mfululizo kwa muda usiopungua miaka kumi. |
| | | (iii) Katika Ibara ndogo ya (3) yaongezwe maneno “wa Mahakama ya Rufani” baada ya maneno “majina matatu”. | | |
| | | (iv) Aya (a) ya Ibara ndogo ya (3) irekebishwe kwa kufuta maneno “na mamlaka inayoshughulikia | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | elimu ya juu katika Jamhuri ya Muungano". | | |
| | | (v) 162(4) ifutwe. | Inaweza kutumika vibaya kwa upendeleo. | |
| | | 162(4) Imependekezwa iwe kama ilivyopendekezwa katika ibara ya 153(3) na 162(1). | | |
| | | (vi) Ibara ndogo ya (4) ifutwe. | (a) Kutoleta mkanganyiko kwenye masuala ya kutathmini malipo ya mafao kwa Majaji waliotumikia vipindi tofauti.<br>(b) Aidha, Rais anaweza kuitumia Ibara hiyo vibaya kwa kuingiza upendeleo.<br>(c) Ikiwa Rais ataweza kutengua mojawapo ya sifa zilizoainishwa itapelekea Rais kumteua mtu yeyote hata kama hana sifa ambazo ni msingi kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake ya kila siku.<br>(d) Hivyo, sifa zilizotajwa zizingatiwe katika uteuzi wa Majaji wa Mahakama ya Rufani.<br>(e) Kupunguza | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | uwezekano wa Rais kuteua mtu kwa upendeleo.<br>(f) Uteuzi wa Majaji unatokana na mapendekezo ya Tume ya Utumishi wa Mahakama na sio vinginevyo. | |
| | | (vii) Aya (c) ya Ibara ndogo ya (4) ifutwe | Haiko wazi na haibainishi kigezo muafaka bali inatoa mwanya kwa madaraka yasiyo na mipaka (*discretionary powers*). | |
| | | (viii) Ibara hii irekebishwe ili Rais asiwe na mamlaka ya uteuzi. | Aombe na kufanyiwa usaili. | |
| | | | | Imeongezwa Ibara mpya ya 170 inayozungumzia Uteuzi wa Makamu Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani. |
| 163 | Uteuzi wa Majaji wa Mahakama ya Rufani | (i) Ibara hii irekebishwe ili Rais aondolewe sifa za kuteua majaji. | Tume ya utumishi ya mahakama isimamie hili na waombe na kufanyiwa usaili. | 1. Ibara ya 163 inakuwa ibara ya 171.<br>2. Ibara ndogo ya (2) imerekebishwa na itasomeka "Mtu anaweza kuteuliwa kuwa Jaji wa Mahakama ya Rufani endapo atakuwa na sifa zilizoainishwa katika ibara ya 171(2)" |
| | | (ii) Katika ibara ndogo ya (1) maneno "Tume ya Utumishi wa Mahakama" yafutwe na badala yake iandikwe "kutoka Mahakama Kuu". | | |
| | | (iii) Ibara hii ibadilishwe ili Majaji waombe nafasi hizo kwa Tume ya Utumishi na Tume ya Utumishi iteue majina matatu yapigiwe kura na Majaji wote na | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | watakaoshinda waapishwe na Rais. | | |
| | | (i) Iongezwe ibara mpya yenye masharti ya uteuzi wa Makamu Mwenyekiti wa Mhakama ya Rufani itakayosomeka kama ifutavyo: 163.-(1) Makamu Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani atateuliwa na Rais kutoka miongoni mwa majina ya watu watatu yatakayopendekezwa na Tume ya Utumishi wa Mahakama. (2) Mtu atateuliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani endapo atakuwa na sifa zilizoainishwa katika Ibara ya 162(2).] [ | Inajitosheleza. | |
| 164. | Kiapo cha Majaji wa Mahakama ya Rufani | (i) 164 ibaki kama ilivyo. | Inajitosheleza. | Ibaki ilivyo |
| | | (ii) 164. Katiba itamke aina ya kiapo kwa nafasi zote zinazohitaji kiapo. | Ibara ya 164 inakuwa ibara ya 172 na inabaki kama ilivyo katika Rasimu. | |
| 165. | Muda wa kuwa madarakani kwa Mwenyekiti na Majaji wengine wa Mahakama ya Rufani | (i) 165 (1) na (2) ibaki kama ilivyo | zinajitosheleza | 1. Ibara ya 165 inakuwa ibara ya 173.<br>2. Ibara ndogo ya (2),neno "Naibu" limeondolewa na kuwekwa neno "Makamu".<br>3. Imeongezwa Ibara ndogo ya (4) ambayo itasomeka "Bila ya kuathiri masharti ya Ibara ndogo ya (3), |
| | | (ii) Ibara ndogo ya (3) irekebishwe ili kutoa fursa ya kuongezewa muda baada ya kustaafu ili kumalizia kesi na shughuli nyingine. | Inajitosheleza. | |
| | | (ii) 165 (3) ifutwe. | Kuepuka Majaji kujilimbikizia kesi kwa ajili ya kuendelea kuwapo kazini hata baada ya umri wa kustaafu kuwadia. | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | (iii) Katika ibara ndogo ya (3) yaongezwe maneno "kwa kipindi kisichozidi miezi kumi na mbili" mwisho wa sentensi. | | Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani aliyetimiza umri wa kustaafu,ataachia nafasi ya madaraka yake,isipokuwa ataendelea kutekeleza shughuli ambazo hajazikamilisha akiwa katika nafasi ya madaraka ya Jaji wa Mahakama ya Rufani mpaka atakapokamilisha shughuli hizo". |
| | | (iv) Iongezwe ibara ndogo ya (4) itakayoeleza muda wa kustaafu kwa Majaji atakapofikia umri wa miaka 60 kama ilivyo katika ibara ya 110(2) na 120(1) ya Katiba ya sasa. | | |
| | | (v) Iongezwe Ibara ndogo mpya itakayoeleza utaratibu wa kumuondoa Jaji Mkuu na Naibu Jaji Mkuu. | Hii ni kwa mujibu wa Ibara ya 155(1)(c) ambayo inatamka kuwa Jaji Mkuu na Naibu Jaji Mkuu atavuliwa madaraka kwa mujibu wa Katiba. | |
| | | (vi) Ibara hii irekebishwe kama ifuatavyo:<br>(a) umri wa kustaaafu wa Majaji ulingane na watumishi wengine wa umma;<br>(b) Jaji asipewe kesi mpya muda wake wa kustaafu unapokaribia;<br>(c) masharti ya Ibara hii yapelekwe katika sheria. | | |
| | | (vii) Iongezwe ibara ndogo itakayosomeka kama ifuatavyo:<br>(3) Bila ya kujali masharti ya Ibara ya ndogo ya (1) na (2), Jaji aliyetimiza umri wa kustaafu atalazimika kuendelea kufanya kazi baada ya kutimiza umri huo mpaka amalize kutayarisha na | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | kutoa hukumu au mpaka akamilishe shughuli nyingine yoyote inayohusika na mashauri ambayo alikwishaanza kuyasikiliza kabla hajatimiza umri wa kustaafu.<br>(4) Bila ya kuathiri masharti ya ibara ndogo ya (3), Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani aliyetimiza umri wa kustaafu, ataachia nafasi ya madaraka yake, isipokuwa ataendelea kutekeleza shughuli ambazo hajazikamilisha akiwa katika nafasi ya madaraka ya Jaji wa Mahakama ya Rufani mpaka atakapokamilisha shughuli hizo. ] | | |
| 166. | Utaratibu wa kukaimu katika Mahakama ya Rufani | (i) Ibara ndogo ya (1) (b) ifutwe. | | Ibara ya 166 inakuwa ya 174 na inabaki kama ilivyo |
| | | (ii) Ibara ndogo ya (1)(c) ifutwe na badala yake iandikwe kama ifuatavyo:<br>"(c) Naibu Jaji Mwenyekiti akiwa hayupo nafasi yake ishikwe na Jaji Mwandamizi wa Mahakama ya Rufani ambaye atakaimu nafasi ya Mwenyekiti". | | |
| | | (iii) Ibara ndogo ya (3) maneno "Jaji Mkuu" yafutwe na badala yake iandikwe "Tume ya Utumishi wa Mahakama". | | |
| | | (iv) Ibara ndogo ya (4) maneno 'kama muda haukutajwa basi mpaka uteuzi utakapofutwa na Rais" yafutwe na badala yake muda utajwe katika barua ya uteuzi. | | |

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Maoni* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| | | (v) 166(4) Imependekezwa kuwa na ukomo wa muda wa kukaimu usiozidi miezi 12. | Ili isiwe njia ya mkato ya watu kuwa Majaji. | |
| | | (vi) Ibara ndogo ya (5) inapendekezwa muda wa kumaliza mashauri usizidi miezi sita. | | |
| | | (vii) 166 ibaki kama ilivyo. | Inajitosheleza. | |
| 167. | Utaratibu wa kushughulikia nidhamu ya Majaji wa Mahakama ya Rufani | (i) Inapendekezwa ielezwe kama ilivyo kwenye ibara za 108 na 109 za Katiba ya sasa. | | 1. Ibara ya 167 inakuwa ya 175.<br>2. Ibara ndogo (1) imefutwa.<br>3. Katika Ibara ndogo ya (2) mbele ya maneno "Madaraka ya Jaji" yameongezwa maneno ya "Mahakama ya Rufani". |
| | | (ii) 167 (1) ifutwe. | Utaratibu wa kushughulikia nidhamu ya Majaji umeelezwa katika Ibara ya 157(2)-(5). | |
| | | (iii) Kiongezwe kichwa cha habari kipya kitakachoelezea kuhusu nidhamu ya Majaji, aidha kwa kuzingatia mtiririko uliopo katika Sheria ya Utumishi wa Mahakama, Ibara zinazohusu Mtendaji Mkuu wa Mahakama (170 na 171) zitangulie kabla ya zile zinazohusu Msajili Mkuu. | | |

### (f) Usimamizi wa Shughuli za Mahakama

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Maoni* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| 168. | Msajili wa | (iv) Masharti ya Ibara hii | | 1. Ibara ya 168 inakuwa |

| ***Ibara Na.*** | ***Kichwa cha Habari*** | ***Maoni ya Mabaraza*** | ***Sababu ya Maoni*** | ***Marekebisho ya Tume*** |
|---|---|---|---|---|
| | Mahakama | yapelekwe katika sheria.<br>(i) Ibara hii irekebishwe na nafasi usajili wa Mahakama itangazwe na usaili ufanyike.<br>(ii) Katika ibara ndogo (1) neno "Msajili" iandikwe 'Msajili Mkuu", aidha maneno "na baada ya kuidhinishwa na Bunge" yafutwe.<br>(iii) Ibara ibadilishwe kwa kuweka sharti kwamba Msajili ateuliwe na Tume ya Utumishi wa Mahakama.<br>(iv) Ibara ndogo ya (2) ifutwe na badala yake iandikwe kama ilivyo kifungu cha 27 cha Sheria ya Usimamizi wa Mahakama (Judiciary Administration Act Nam. 4/2011). | (a) Mahakama inawasajili wengi ambao wote wapo chini ya Msajili Mkuu.<br>(b) Kuidhinishwa na Bunge ni kuingilia Muhimili mwingine. | ya 176.<br>2. Katika ''Marginal Note" Neno Msajili wa Mahakama lisomeke 'Msajili Mkuu wa Mahakama'<br>3. Katika Ibara ndogo ya kwanza neno ''Msajili" lisomeke ''Msajili Mkuu wa Mahakama"<br>4. Ibara ya kwanza ikomee kwenye maneno ''Tume ya Utumishi wa Mahakama"<br>5. Katika Ibara ndogo ya (2), neno ''Msajili" lisomeke ''Msajili Mkuu wa Mahakama"<br>6. Imeongezwa Ibara ndogo ya 2(a) ambayo inasomeka ''Awe raia wa kuzaliwa wa Jamhuri ya Tanzania" |
| 169. | Majukumu ya Msajili wa Mahakama | (i) Ibara ibadilishwe ili Msajili awajibike kwa Jaji Mkuu. | a. Tume haikutani kila siku.<br><br>Kuwajibika kwake kwa Tume ya Utumishi wa | 1. Ibara ya 169 inakuwa ya 177.<br>2. Neno ''Msajili" lisomeke ''Msajili |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | Mahakama kunapunguza ukaribu na uwajibikaji. | Mkuu wa Mahakama" |
| | | (ii) Iongezwe aya mpya ya (d) katika ibara ndogo ya (2) itakayoweka sharti la kuwa na shahada ya Chuo Kikuu kinachotambulika na Serikali. | | |
| 170. | Mtendaji Mkuu wa Mahakama | (i) Ibara ibadilishwe ili nafasi ya Mtendaji Mkuu wa mahakama itangazwe, watu wenye sifa waombe na wafanyiwe usaili. | Uwazi na ushindani vitaongeza uhuru na uwajibikaji katika utumishi wa umma. | Ibara ya 170 inakuwa ya 178.<br><br>Katika Ibara ndogo ya 178(1) maneno "Tume ya Utumishi wa Mahakama" yasomeke "Tume ya Utumishi wa Umma". |
| | | (ii) 170(1)-Mtendaji Mkuu apendekezwe na Tume ya Utumishi wa Umma. | Ndio utaratibu wa kada hii ya utumishi. | |
| | | (iii) Ibara ibadilishwe ili Mtendaji Mkuu asiidhinishwe na Bunge. | Kunaingilia Mhimili mwingine. | |
| | | (iv) 170(2) ibaki kama ilivyo. | Inajitosheleza. | |
| 171. | Majukumu ya Mtendaji Mkuu wa Mahakama | (o) 171(1)(a),(c),(d) na (e) ibaki kama ilivyo. | Inajitosheleza. | Ibara ya 171 inakuwa 179 na inabaki kama ilivyo. |
| | | (ii) 171(1) (b)-Maneno "Afisa Masuuli" yapatiwe tafsiri. | Ili lieleweke kwa wengi. | |
| | | (iii) 171(2) ibaki kama ilivyo. | Inajitosheleza. | |

## 10.2 SEHEMU YA TATU:TUME YA UTUMISHI WA MAHAKAMA NA MFUKO WA MAHAKAMA

### (a) Tume Ya Utumishi Wa Mahakama

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| 172. | Tume ya Utumishi wa Mahakama | (i) Ibara ndogo ya (1) irekebishwe kwa jina la Tume kuwa Tume Huru ya Utumishi wa Mahakama. | | 1. Ibara ya 172 iwe 180.<br>2. Imeongezwa Ibara ndogo ya (1)(e) ambayo itasomeka Majaji Wakuu wa nchi Washirika.<br>3. Katika Ibara ndogo ya (1) (g) neno Vyuo Vikuu lisomeke Vyuo Vikuu husika. |
| | | (ii) Ibara ibadilishwe ili muundo wa Tume ujumuishe watu wa taaluma nyingine mbali ya taaluma ya sheria. | | |
| | | (iii) Ibara irekebishwe ili kuweka utaratibu wa kuzuia ukwamishaji wa rufani kutoka Mahakama za nchi Washirika kwenda kwenye Mahakama za Jamhuri ya Muungano. | | |
| | | (iv) Wawakilishi kutoka tume ya haki za binaadamu na watoa huduma ya msaada wa kisheria waongezwe. | Orodha haijitoshelezi kwa kuwa imeacha wawakilishi kutoka Tume ya haki za Binaadam na watoa huduma ya msaada wa kisheria | |
| | | (v) Aya (c) ya Ibara ndogo ya (1) ibadilishwe na iandikwe kama ifuatavyo:<br>"(c) Jaji mmoja wa Mahakama ya Juu aliyechaguliwa na Majaji wa Mahakama ya Juu". | | |
| | | (vi) 172(1)(c).Kipengele kiondolewe. | Kuna Jaji Mkuu. | |
| | | (vii) aya (d) ibadilishwe na iandikwe kama ifuatavyo:<br>"(d) Jaji mmoja wa Mahakama ya Rufani aliyechaguliwa na Majaji wa Mahakama ya Rufani." | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | (viii) 172(1)(d),Kipengele kirekebishwe na kisomeke "Naibu Jaji Mkuu". | | |
| | | (ix) ibara ibadilishwe kwa kutaja Chama cha Wanasheria wa Tanganyika. | Wajumbe wa Tume – chama cha wanasheria wa Tanzania bara hakipo. | |
| | | (x) iongezwe aya zifuatazo katika Ibara ndogo ya (1):<br>"(1) Watu wawili wasiokuwa wanasheria kutoka miongoni mwa wananchi watakaoteuliwa na taasisi za kidini na taasisi za kiraia kutoka Tanganyika na Zanzibar;<br>(2) Mtumishi mmoja wa umma atakayeteuliwa na Tume ya Utumishi wa Umma." | Ili kupata na kusikiliza malalamiko ya wadau na watumiaji wa Mahakama. | |
| | | (xi) Aya (f) ya ibara ndogo ya (1) ifutwe. | | |
| | | (xii) Aya (g) katika ibara ndogo ya (1) maneno "Wakuu wawili wa vitivo vya Sheria" yafutwe na iandikwe "Mkuu mmoja wa kitivo cha Sheria". | | |
| | | (xiii) 172(1)(g) irekebishwe kwa kufuta maneno "watakaopendekezwa na Jaji Mkuu". | Vitivo vipendekeze kupitia taratibu zao. | |
| 173. | Majukumu ya Tume ya Utumishi wa Mahakama | (i) Katika Ibara ndogo ya (2)(a) maneno "ya Juu na Mahakama ya Rufani" yafutwe na badala yake iandikwe "Mahakama mbalimbali". | | 1. Ibara ya 173 iwe 181.<br>2. Imeongezwa Ibara ndogo ya (5), ambayo itasomeka ''Bila ya kuathiri Masharti ya Ibara ndogo ya 2(b), Mapendekezo ya maslahi kwa Majaji na |
| | | (ii) 173(2).Imependekezwa kipengele hicho kitoe mamlaka kwa Tume ya Utumishi wa Mahakama, ya kuitisha maombi ya kujaza nafasi mbali | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | mbali za utumishi katika mahakama, zikiwemo za Ujaji na kupendekeza uteuzi ambao utathibitishwa na Bunge kabla ya Rais hajakamilisha. | | Watumishi wengine wa Mahakama yatawasilishwa kwenye chombo chenye jukumu la kusimamia maslahi ya Watumishi wa Umma". |
| | | (iii) iongezwe ibara ndogo mpya ya (6) kitakayoeleza kama ifuatavyo: "(6) Bila ya kuathiri masharti ya ibara ndogo (2)(b) mapendekezo ya masilahi kwa majaji na watumishi wengine wa mahakama yatawasilishwa kwenye chombo chenye jukumu la kusimamia masilahi ya watumishi wa umma". | | |
| | | (iv) 173(3)(a) iboreshwe kwa kumtaka Rais kuzingatia kuteua Majaji kutoka katika orodha ya majina iliyowalishwa na Tume ya Utumishi wa Mahakama na si vinginevyo. | Kuepuka kumpa Rais mwanya wa kuteua Majaji ambao hawajapendekezwa na Tume ya Utumishi wa Mahakama. | |
| 174. | Uanachama katika vyama vya siasa | (p) Katika ibara hii yaongezwe maneno "Jaji ya Mahakama Kuu, Mahakimu na Wasaidizi wa Sheria wa Majaji". | | Ibara ya 174 inakuwa 182 na inabaki kama ilivyo |
| | | (ii) 174 isomeke "Mara atakapoteuliwa aache uwanachama wa chama chake cha siasa; kwa muda ambao atakuwa jaji". | ili kila mtu awe na haki ya kikatiba ya kuwa mwanachama wa chama cha siasa "Freedom of Association" akichaguliwa Jaji asitishe uanachama mpaka hapo atakapoacha Ujaji. | |
| | | (iii) 174. bara ifafanue maana ya"Kuwa mwanachama wa chama chochote cha siasa" ni kuwa na kadi | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | ya chama husika, Kuhudhuria mikutano ya hadhara ya chama husika au Kuhudhuria shughuli nyingine zilizo wazi kwa umma za chama cha siasa. | | |
| | | (iv) 174 ibaki kama ilivyo. | Inajitosheleza. | |

*(b) Mfuko wa Mahakama*

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| 175. | Mfuko wa Mahakama | (i) katika Ibara ndogo ya (1) na (3) Suala la Mfuko wa Mahakama lisitajwe kwenye Katiba bali litajwe kwenye sheria itakayotungwa na Bunge kama ilivyo kwa mifuko mingine yote isipokuwa Mfuko Mkuu wa Hazina. | Mifuko ni mingi isimamiwe katika sheria na taratibu za mahakama. | 1. Ibara ya 175 inakuwa 183.<br>2. Katika Ibara ndogo ya (1) maneno "Mfuko utakaojulikana kama" yamefutwa.. |
| | | (ii) Ibara ndogo ya (3) irekebishwe ili iandikwe kama ifuatavyo:<br>"(3) Kila mwaka wa fedha, Mtendaji Mkuu wa Mahakama atawasilisha bajeti ya Mahakama Bungeni kwa ajili ya kuthibitishwa na Bunge, baada ya kuthibitishwa na Bunge, bajeti hiyo itaingizwa katika mfuko wa Mahakama kutoka kwenye mfuko mkuu wa hazina." | | |
| | | (iii) 175 ibaki kama ilivyo. | Inajitosheleza. | |

# SURA YA KUMI NA MOJA YA RASIMU

## 11.0 SEHEMU YA KWANZA: UTUMISHI KATIKA JAMHURI YA MUUNGANO

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Maoni* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| | SURA YA KUMI NA MOJA | SURA YA KUMI NA MOJA: Isomeke "UTUMISHI WA UMMA KATIKA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA". | | |
| 176. | Misingi Mikuu ya Utumishi wa Umma | (i) Ibara hii ifutwe. | Masharti yapelekwe katika Sheria za Utumishi wa Umma | Ibara ya 176 inakuwa 184.<br><br>Ibara inabaki kama ilivyo. |
| | | (ii) Ibara ndogo ya (1), isomeke: "(1) Kutakuwa na utumishi wa umma katika Jamhuri ya Muungano ambao utazingatia misingi na kanuni zifuatazo:" | | |
| | | (iii) Ibara ndogo ya (2), ongeza maneno "na katika kuchukua hatua za kinidhamu" katikati ya maneno "uongozi" na "katika". | | |
| | | (i) Ibara ndogo ya (1) iongezwe maneno "utumishi huo uzingatie usawa". | Nchi zote mbili zina hadhi sawa. | |
| | | (ii) Ibara ndogo ya (2) irekebishwe ili kuweka usawa katika Bunge. | Kuzingatia hadhi ya nchi na sio ukubwa na udogo wa nchi. | |
| | | Ibaki kama ilivyo | | |
| | | Isomeke, "Kutakuwa na utumishi wa umma katika Jamhuri ya Muungano ambao utazingatia | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | misingi na kanuni zifuatazo” | | |
| | | Ibara 176(2) isomeke, “misingi na kanuni za umma zilizoainishwa katika ibara hii zitazingatiwa na kutumika katika uteuzi wa kushika nafasi za madaraka ya uongozi na katika kuchukua hatua za kinidhamu.”<br><br>Ibara isomeke, “ Kutakuwa na utumishi wa umma katika Jamhuri ya Muungano ambao utazingatia misingi na kanuni zifuatazo” | | |
| | | 176(2) isomeke, “misingi na kanuni za umma zilizoainishwa katika ibara hii zitazingatiwa na kutumika katika uteuzi wa kushika nafasi za madaraka ya uongozi na katika kuchukua hatua za kinidhamu..” | | |
| | | Makosa yanayotendwa na watumishi yawekwe kwenye sheria | | |
| | | Neno rasilimali liboreshwe na kuwa raslimali | | |
| 177. | Masharti kuhusu utumishi katika Jamhuri ya Muungano | (i) Katika Ibara hii suala la uwiano halikufafanuliwa wala vigezo vyake havijabainishwa katika Rasimu. Inapendekezwa uwiano kati ya nchi Washirika uzingatie sifa na vigezo wazi na muafaka ikiwemo idadi ya watu katika nchi Washirika. | | 1. Marginal Note isomeke “Ajira na Uteuzi wa Viongozi wa Taasisi katika Serikali”<br><br>2. Ibara ya 177 inakuwa 185 na isomeke: |
| | | (ii) Katika Ibara hii uwiano baina | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | ya Washirika wa Muungano uwe wa haki. | | (1) Bila ya kuathiri masharti ya katiba hii, ajira katika utumishi wa umma na uteuzi katika nafasi za madaraka ya uongozi katika serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na taasisi zake, itatolewa na kufanyika kwa kuzingatia:<br>(a) Taaluma na uweledi; na<br>(b) Uwakilishi wa nchi washirika.<br>(2) Kwa madhumuni ya ibara ndogo ya kwanza, uteuzi wa viongozi katika serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania utafanyika kwa kuzingatia ushiriki wa kila upande wa nchi washirika. |
| | | (i) Katika Ibara hii itamkwe kwamba suala la Utumishi wa Umma ni moja kati ya mambo ya Muungano, ili kuwezesha mchanganyiko ambao hatimaye utaimarisha Umoja wa Kitaifa. | | |
| | | (ii) Ibara hii ifanyiwe marekebisho ili kuweka maelezo na ufafanuzi wa kina kwa mambo yafuatayo:<br>(a) Watumishi katika Serikali ya Muungano watakuwa kwa uwiano gani;<br>(b) Utaratibu wa mtumishi wa umma anayehamishwa kutoka Serikali ya Zanzibar au Serikali ya Tanganyika kwenda kufanya kazi Serikali ya Jamhuri ya Muungano;<br>(c) Maslahi ya wale ambao kabla ya kuanza kwa Katiba Mpya walikuwa ni watumishi wa Serikali ya Muungano. | | |
| | | (d) Iongezwe ibara ndogo itakayotoa tafsiri ya neno “uwiano”. | | |
| | | (e) Iongezwe ibara ndogo mpya ya (2) ambayo itakuwa kama ifuatavyo:<br>“(2) Bila ya kuathiri masharti ya Katiba hii, utumishi wa umma na uongozi katika Jamhuri ya Muungano utazingatia uwiano ulio | Ili kuondoa manung’uniko na hisia za kuwepo upendeleo wa udini na ubaguzi katika uteuzi wa nafasi katika utumishi wa umma. | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | sawa (50%) baina ya Waislam na Wakristo.” | | |
| | | (f) Neno “uwiano” lifutwe na badala yake iandikwe “usawa”. | | |
| | | Katika ibara hii neno “uwiano” lisomeke “usawa”. | Kuzingatia hadhi ya nchi na sio ukubwa na udogo wa nchi. | |
| | | Suala la Utumishi wa Umma liwe la Muungano ili kuimarisha Muungano. | | |
| | | Ibara ibaki ilivyo | | |
| | | Uwiano wa washirika wa Muungano katika utumishi ubainishwe | | |
| | | Ihaririwe kuzingatia muundo wa serikali mbili | | |
| | | Kuwe na nafasi sawa na mzunguko katika nafasi za uongozi na ajira | | |
| | | Kuwe na uwiano katika Muungano utolewe ifafanuzi, iwapo ni ni 50/50 au vinginevyo | | |
| | | Iongezwe “jinsi” itakayoelezea masharti ya utumishi katika Jamhuri ya Muungano ili isomeke “utoaji wa ajira na uteuzi wa viongozi utazingatia uwiano wa washirika wa muungano na jinsi” | | |
| | | uwiano kati ya nchi Washirika uzingatie sifa na vigezo wazi na muafaka ikiwemo idadi ya watu katika nchi Washirika. | | |
| | | Utaratibu wa kuunda Tume hii uwe ni wa wazi wa kutangaza nafasi, watu wenye sifa kuomba, | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | usaili, na Tume ya Utumishi wa Umma iteue, kisha Rais, na mwisho Bunge liidhinishe. | | |
| | | Utumishi wa umma uzingatie uwiano ulio sawa (50%)kati ya wakristo na waislamu | | |
| | | Katika ibara hii neno "uwiano" lisomeke "usawa". | Kuzingatia hadhi ya nchi na sio ukubwa na udogo wa nchi. | |
| | | | | |
| 178. | Tume ya Utumishi wa Umma | (i) Katika Ibara hii Tume ya Utumishi wa Umma Sura ya 11, kabla ya ibara ya 178 pawepo kichwa cha habari "Tume ya Utumishi wa Umma".<br>(ii) Aidha, masuala ya utumishi wa umma hayajapewa uzito unaostahili. Kwa mfano Tume kuwa na mamlaka ya kuwawajibisha wasimamizi wa waajiri ambao wanashindwa kuchukua hatua dhidi ya watumishi wanaowasimamia. | | 1. Ibara ya 178 itakuwa 186.<br>2. Ibara ndogo ya (3) imeandikwa upya na ibara ndogo ya (4) imefutwa. |
| | | (iii) Ibara hii iweke utaratibu wa kuunda Tume hii uwe ni wa wazi wa kutangaza nafasi, watu wenye sifa kuomba, usaili, na Tume ya Utumishi wa Umma iteue, kisha Rais, na mwisho Bunge liidhinishe. | | |
| | | (iv) Katika Ibara ndogo ya (4) neno "kuidhinishwa" lifutwe na badala yake iandikwe "kuthibitishwa". | | |
| | | (v) Ibara ndogo ya (4) irekebishwe ili Katibu wa Tume athibitishwe na | Utaratibu wa uthibitisho hufuata baada ya uteuzi. | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | Bunge baada ya kuteuliwa na Rais. | | |
| | | (vi) Ibara irekebishwe ili Katibu wa Tume asithibitishwe na Bunge. | (a) Ni mtendaji wa Mhimili wa Serikali.<br>(b) Hawajibiki Bungeni.<br>(c) Si nafasi ya kisiasa. | |
| | | (vii) Kuwe na kinga ya mashtaka dhidi ya Mwenyekiti, Wajumbe na Katibu kwa makosa waliyotenda katika utekelezaji wa majukumu yao. | | |
| | | (viii) Ibara hii irekebishwe ili ieleze dhana ya utumishi katika Serikali ya Muungano. | Ili kuondoa utata unaoweza kujitokeza. | |
| | | (ix) Ibara ndogo ya (1) na (4) ieleze:<br>(a) Mwenyekiti na wajumbe wapatikane kwa uwazi na ushindani;<br>(b) wajumbe na Katibu wasiidhinishwe na Bunge | Kuepuka Mhimili mmoja kuingia mwingine. | |
| | | (x) Katika ibara ndogo ya (4) maneno "baada ya" yafutwe. | Kuleta mtiririko wa mantiki. | |
| | | (xi) Ibara ieleze uhusiano baina ya Tume na Tume za Washirika au mamlaka zenye kufanana na hizo. | Kujua mipaka ya majukumu ya Tume. | |
| | | (xii) Ibara ieleze kwamba muda wa kukaa madarakani Mwenyekiti na wajumbe wa Tume uwe ni vipindi viwili vya miaka mitano mitano. | Ili kutoa muda wa kutosha kutathmini utendaji wao wa kazi. | |
| | | (xiii) Kuwe na uhuru wa Tume kutoingiliwa na mtu au mamlaka yoyote. | Kutoa uhuru kwa Tume na kuleta uwajibikaji. | |
| | | (xiv) Ibara hii iboreshwe kwa kuongeza ibara ndogo ambayo itaainisha sifa za Makamishna | | |

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Maoni* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| | | kulingana na unyeti wa majukumu ya kazi zao. | | |
| | | Ibara ndogo iongezwe itakayoainisha utaratibu wa kumuondoa Mwenyekiti na Wajumbe wa Tume. | | |
| | | Kabla ya ibara ya 178, kuwe na kichwa, "Tume ya Utumishi wa Umma." | | |
| | | Tume iwe na mamlaka ya kuwawajibisha wasimamizi na waajiri. | | |
| | | Katibu wa Tume ateuliwe miongoni mwa watumishi waandamizi katika Jamhuri ya Muungano. | | |
| | | Iitwe Tume ya Utumishi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. | | |
| | | Suala la utumishi liwe "utumishi katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano". | | |
| | | Katibu wa Tume asithibitishwe na Bunge. | | |
| | | Upatikanaji wa Mwenyekiti na wajumbe uwe wa ushindani na wasiidhinishwe na Bunge ili kuondoa mihimili kuingiliana. | | |
| | | Katibu wa Bunge asiidhinishwe na Bunge. | | |
| | | Sifa za Mwenyekiti ziwekwe wazi. | | |
| | | Apendekezwe na chombo fulani kwa Rais na kuthibitishwa na Bunge kabla ya uteuzi rasmi Rais. | | |
| | | Wajumbe sita wa Tume | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | wapendekezwe na chombo maalum, sifa zao ziwekwe wazi kwa vile chombo hicho kinabeba nguvu kubwa za Rais. | | |
| | | Katika ibara ya 178(4) Katibu wa Tume apendekezwe na chombo maalum kwa Rais kabla ya jina lake kupelekwa Bungeni kwa uteuzi rasmi. | | |
| | | Katibu wa Tume athibitishwe na Bunge. | | |
| | | Ibara ya 178(1) iseme, "Tume ya Uteuzi iliyoundwa chini ya ibara ya 182 itapendekeza majina ya watu wanaofaa kuteuliwa kuwa Wajumbe wa Tume ya Utumishi wa Umma na itatelekeza majukumu yake kwa mujibu wa ibara hiyo." | | |
| | | Ibara ya 178(1) iseme, "Tume ya Uteuzi iliyoundwa chini ya ibara ya 182 itapendekeza majina ya watu wanaofaa kuteuliwa kuwa Wajume wa Tume ya Utumishi wa Umma na itatelekeza majukumu yake kwa mujibu wa ibara hiyo." | | |
| | | 178(1) Ifutwe. | | |
| | | 178(1) iseme wajumbe sita; watatu wanawake na watatu wanaume | | |
| | | Sifa za wajumbe wa Tume zibainishwe ikiwemo uzoefu mkubwa wa kazi Serikalini na katika asasi za kiraia. | | |
| | | Idadi ya Wajumbe wa Tume iwe | Watumishi wanatoka | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | sawa kutoka kila Nchi Mshirika. | pande zote mbili za Shirikisho. | |
| | | | | Imeongezwa ibara mpya ya 187 inayohusu uanzishwaji wa nafasi ya Katibu wa Tume ya Utumishi wa Umma |
| 179. | Mamlaka na majukumu ya Tume | (i) Ibara hii ifanyiwe marekebisho ili:<br>(a) kuruhusu kutungwa kwa sheria ya Bunge itakayosimamia mambo yafuatayo-<br>(a) utayarishaji na utoaji wa taarifa za Tume;<br>(b) utayarishaji wa majukumu ya Tume;<br>(c) utoaji wa maamuzi na mapendekezo ya Tume;<br>(d) kinga kwa watumishi;<br>(e) masuala mengine muhimu ya Tume. | | 1. Ibara ya 179 itakuwa ibara ya 188.<br>2. Ibara ndogo ya 2(c) neno 'idara ya' limefutwa. |
| | | (ii) Tume iongezewe jukumu la kukagua rasilimali watu Serikalini na kutoa taarifa Bungeni. | Kufuatilia utendaji katika Utumishi wa Umma na kuleta ufanisi katika utoaji wa huduma. | |
| | | (iii) Ibara hii iweke masharti yanayohusu upatikanaji wa fedha, nyenzo na rasilimali watu za kutosha. | Majukumu ya Tume ni makubwa na mazito hivyo yanahitaji kutekelezwa kwa ufanisi mkubwa. | |
| | | (iv) Katika Ibara ndogo ya (2)(a) yaongezwe maneno "katika utumishi wa umma" mara baada ya neno "mbalimbali". | | |
| | | (v) Katika Ibara ndogo ya (2)(a) ieleze kwamba kazi ya Tume iwe ni | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | kupokea na kuchambua mapendekezo kutoka taasisi zinazohusika juu ya uteuzi wa viongozi wa taasisi mbalimbali na kumshauri Rais. | | |
| | | (vi) Ibara ya 179(2) (c), (d) na (e) irekebishwe kwani imechanganya kazi za utendaji na kazi za nidhamu. | Kuleta utendaji mzuri. | |
| | | (vii) Ibara 179(2)(g-h) irekebishwe kutokana na uzito wa suala Mishahara kwa Watumishi wa Umma, ni muhimu jukumu hili litekelezwe na chombo mahsusi cha kikatiba badala ya kuwekwa kama shughuli mojawapo tu ya Tume ya Utumishi wa Umma. Kwa hiyo Ibara ndogo (2) (g-h) ziondolewe chini ya Tume ya Utumishi wa Umma na ziwekwe chini ya chombo maalum cha kikatiba. | | |
| | | (viii) Neno “kusawazisha” liondolewe na badala yake yatumike maneno “kuoanisha na kuwianisha”. | Kwa sababu mishahara haiwezi kusawazishwa bali inawianishwa. | |
| | | (ix) Neno “masilahi” litumike badala ya “marupurupu”. | | |
| | | (x) Majukumu ya Tume yaangaliwe upya:<br>(a) yanaingiliana na ya Katibu Mkuu Kiongozi kama Mkuu wa utumishi wa Umma;<br>(b) ni makubwa mno, kupanga mishahara, uteuzi, kusimamia nidhamu za watumishi wa | (a) Yataleta mgogoro/ mgongano wa majukumu.<br>(b) Ni kinyume na Utawala Bora.<br>(c) Mfumo wake umeigwa Kenya, ambako tayari umeshaanza | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | umma na rufaa. | kulalamikiwa na baadhi ya makundi, ikiwemo Wabunge. | |
| | | Kazi ya Tume iwe ni kupokea na kuchambua mapendekezo kutoka Taasisi zinazohusika juu ya uteuzi wa viongozi wa Taasisi mbalimbali na kumshauri Rais. | | |
| | | Kuwe na chombo mahsusi kikatiba kushughulikia mishahara na maslahi ya viongozi na watumishi. | | |
| | | Neno "maslahi" litumike badala ya marupurupu. | | |
| | | Ibaki kama ilivyo. | | |
| | | Iangaliwe upya kuondoa migongano na Katibu Mkuu Kiongozi. | | |
| | | Itazamwe upya ili kutenganisha kazi za nidhamu na utendaji ili kuleta utendaji mzuri. | | |
| | | Ibara ya 179(g) na 179(h) zisomeke: | | |
| | | Isomeke, "Kuunda na kudurusu mishahara na marupurupu ya watumishi wa umma, ikiwemo viongozi wa juu wa nchi, viongozi wa kisiasa na wabunge, watumishi waliopo chini ya utumishi wa serikali, mahakama, Bunge, maofisa | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | wa majeshi ya ulinzi." | | |
| | | "Kusawazisha mishahara na marupurupu ya maafisa wote wa serikali ikiwemo viongozi wa juu wa nchi, viongozi wa kisiasa, Bunge, wabunge, mahakama, maofisa wa umma, maofisa wa majeshi ya ulinzi na usalama na askari wa majeshi ya ulinzi." | | |
| | | Katika ibara ya 179(1) Maneno yaongezwe maneno, " katika mamlaka ya Jamhuri ya Muungano." | | |
| | | Irekebishwe 179(2)(g) kwa maneno; "kuunda na kupitia mishahara na marupurupu ya viongozi wa juu wa nchi, viongozi wa kisiasa na Serikali. | | |

# SURA YA KUMI NA MBILI YA RASIMU

## 12.0 SEHEMU YA KWANZA: UCHAGUZI KATIKA VYOMBO VYA UWAKILISHI NA VYAMA VYA SIADA

### Uwakilishi wa Wananchi

| ***Ibara Na.*** | ***Kichwa cha Habari*** | ***Maoni ya Mabaraza*** | ***Sababu ya Maoni*** | ***Marekebisho ya Tume*** |
|---|---|---|---|---|
| 180. | Ushiriki katika vyombo vya uwakilishi | (i) Maneno ya pembeni yasomeke "Haki ya kujiandikisha na kupiga kura". | | 1. Ibara ya 180 inakuwa ibara ya 189.<br>2. Marginal note isomeke "Ushiriki katika uchaguzi na kura ya maoni".<br>3. 180(1)-Maneno "kwa ajili" yafutwe na badala yake yawekwe maneno "na kushiriki".<br><br>4. 180(2) (b) na (c)- Neno "mtu" lisomeke "raia".<br>5. 180(2)- Yaongezwe maneno "wa haki" baada ya maneno ""huru na".<br>6. 180(4)- Yaongezwe maneno "wa haki" baada ya maneno ""huru". |
| | | (ii) 180-marginal note isomeke "Ushiriki katika uchaguzi na kura ya maoni". | Kuendana na maudhui ya Ibara. | |
| | | (iii) Ibara ndogo ya (1) iandikwe kama ifuatavyo:<br>"(1) Kila raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwenye umri wa miaka kumi na nane au zaidi ana haki ya kujiandikisha na kupiga kura katika uchaguzi utakaofanyika Tanzania au kura ya maoni." | | |
| | | (iv) 180-marginal note isomeke "Ushiriki katika uchaguzi na kura ya maoni". | Kuendana na maudhui ya Ibara. | |
| | | (v) 180(1)-Maneno "kwa ajili" yafute na badala yake yawekwe maneno "na kushiriki". | Kuweka ufasaha. | |
| | | (vi) Ibara ya 180(2) (b) irekebishwe Kwa kufuta neno "ulemavu" na badala yake kuweka maneno "mahitaji maalum". | Ili kuweka usawa kwa kujumuisha watu wote wenye mahitaji maalum. | |
| | | (vii) 180(2) (b) na (c)-Neno "mtu" lisomeke "raia". | Kuweka ufasaha. | |
| | | (viii) 180(2) Inapendekezwa Ibara ndogo mpya baada ya Ibara ya 180(2)(c) na isomeke: | Kuhakikisha ushiriki sawa katika vyombo vyote wa uwakilishi. | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | "(c) Wanawake na waume watakuwa na fursa sawa za kushiriki katika vyombo vya uwakilishi". | | |
| | | (ix) Katika Ibara ndogo ya (2)(d)(iii) neno "haukuwa" libadilishwe na iandikwe "hautakuwa". | Kuweka ufasaha. | |
| | | (x) 180(2)- Yaongezwe maneno "wa haki" baada ya maneno "huru na". | Kuweka ufasaha. | |
| | | (xi) Katika Ibara ndogo ya (2) na (3)-<br>(a) Neno "Mamlaka ya Uchaguzi" itolewe tafsiri ili ijulikane kama ni Tume Huru ya Uchaguzi au ni chombo kingine;<br>(b) Majukumu yaliyotajwa katika Ibara za 180 (3) na 184 (1), (2) & (3) yaainishwe. | | |
| | | (xii) Katika Ibara ndogo ya (3), maneno "mamlaka ya nchi" yafutwe na badala yake iandikwe neno "Bunge". | | |
| | | (xiii) Katika Ibara ndogo ya (3)(f) yaongezwe maneno "kundi la wafungwa na mahabusu". | | |
| | | (xiv) Ibara ndogo ya (4) irekebishwe kwa kutaja muda wa siku 21 ya za kufungua mashauri ya uchaguzi. | | |
| | | (xv) Ibara ndogo ya (4) ifutwe. | Imeshaelezwa na Ibara ya 125(2). | |
| | | (xvi) 180(4)- Yaongezwe maneno "wa haki" baada ya maneno ""huru". | Kuweka ufasaha. | |
| | | (xvii) Iongezwe ibara ndogo mpya itakayoeleza kama ifuatavyo: | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | "Bunge litatunga sheria ya utaratibu na ukomo wa muda utakaofuatwa katika kutangaza matokeo ya uchaguzi wa Ubunge na ya Urais". | | |
| | | (xviii) Ibara ya 180(3) inapingana na Ibara ya 105(3).<br>(xix) Iongezwe Ibara mpya itakayozungumzia haki ya kupiga kura kwa raia ambayo isomeke:<br>(xx) kila raia wa Jamhuri ya Muungano aliyetimiza umri wa miaka 18 anayo haki na wajibu wa kupiga kura katika uchaguzi wowote uanaofanywa na Jamhuri ya Muungano.<br>(xxi) kutakuwa na Daftari la kudumu la wapiga kutra ambalo litatumika katika chaguzi zote za Jamhuri, na litatuzwa na/au kuwekwa mahali ambapo kila raia mwenye kutimiza umri ya miaka 18 ataweza kuandikishwa kama mpiga kura anapotimiza umri huo.<br>(xxii) (3) Bunge halitatunga Sheria kuzuia au kufifisha haki ya kupiga kura isipokuwa tu kwa sababu ya kukosa uwezo wa kisheria wa umri au ugonjwa wa akili.<br>(xxiii) Iandikwe kuwa: Bunge litatunga Sheria ya Uchaguzi itakayoweka masharti kuhusu mambo yafuatayo:<br>(a) Kutaja sehemu ambapo | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | Daftari la kudumu la wapiga kura litawekwa kwa ajili ya kuandikisha wapiga kura au kurekebisha yaliyomo katika Daftari hilo, na sehemu na nyakati za kupiga kura;<br>(b) Utaratibu wa kumwezesha mtu kujiandikisha sehemu moja na kupiga kura sehemu nyingine;<br>(c) Utaratibu wa kumwezesha raia anayeishi nje ya Jamhuri ya Muungano au aliyeko chini ya ulinzi wa vyombo au mamlaka ya usalama au hukumu au amri yeyote ya mahakama anapiga kura. | | |
| | | (xxiv) Iongezwe ibara mpya itakayokuwa na masharti yanayohusu ajira na uteuzi wa viongozi wa taasisi za serikali itakayosomeka kama ifuatavyo:<br>-(1) Bila ya kuathiri masharti ya Katiba hii, ajira katika utumishi wa umma na uteuzi katika nafasi za madaraka ya uongozi katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na taasisi zake, itatolewa na kufanyika kwa kuzingatia:<br>(a) taaluma na weledi; na<br>(b) uwakilishi wa Nchi Washirika. | | |

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Maoni* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| | | (2) Kwa madhumuni ya Ibara ndogo ya (1), uteuzi wa viongozi katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania utafanyika kwa kuzingatia ushiriki wa kila upande wa Nchi Washirika. | | |

## 12.1 SEHEMU YA PILI: TUME HURU YA UCHAGUZI

### (a) Muundo wa Tume Huru ya Uchaguzi

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya maoni* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| SURA YA KUMI NA MBILI | Sura ya Kumi na mbili (Ibara 180-187) Uchaguzi katika vyombo vya Uwakilishi na vyama vya siasa Inapendekezwa kwamba ibaki kama ilivyo. | | | |
| 181. | Kuundwa kwa Tume Huru ya Uchaguzi | (i) Jina pia liwe "Tume Huru ya Uchaguzi, Vyama vya Siasa na Mipaka". | | 1. Ibara 181 imekuwa ibara 190.<br>2. Ibara ndogo ya (1) imefanyiwa marekebisho na isomeke:<br>"Kutakuwa na tume huru ya uchaguzi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itakayokuwa na wajibu wa kusimamia na kuratibu shughuli za uchaguzi ambayo pia itaitwa "Tume Huru ya Uchaguzi"" |
| | | (ii) Ibara ndogo ya (2) - Tume Huru ya Uchaguzi iundwe, kwa utaratibu wa kutangaza, wahusika kuomba, usaili, Kamati ya uteuzi kufanya kazi yake, ndipo Rais ateue na Bunge kuidhinisha. | | |
| | | (iii) Ibara ndogo ya (1) irekebishwe kwa kuondoa masuala ya vyama vya siasa kama sehemu ya majukumu ya Tume Huru ya Uchaguzi. | (a) Kuipa nafasi Tume kushughulikia suala moja tu la kusimamia masuala ya uchaguzi.<br>(b) Kuongeza ufanisi katika utendaji wa vyombo hivyo;<br>(c) Kuondoa mifarakano ya kisiasa katika Tume Huru ya | |

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya maoni* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| | | | Uchaguzi. | |
| | | (iv) Ibara ndogo ya (1) irekebishwe ili kutenganisha masuala ya Tume ya Uchaguzi yakatenganishwa na Vyama vya Siasa. | | |
| | | (v) Tume hii haikutajwa kama moja ya Mambo ya Muungano. Kwa kuwa inahusika na chaguzi na Vyama vya Siasa, inapendekezwa kuwa iongezwe kwenye orodha ya Mambo ya Muungano. | | |
| | | (vi) Ibara ya 181(2) itamke kuwa Tume Huru ya Uchaguzi itaidhinishwa na Bunge. | Kuleta imani na kuimarisha uwajibikaji wa chombo hicho. | |
| | | (vii) Ibara ya 181(4)(b) irekebishwe kwa kuongeza maneno "za Washirika wa Muungano" mara baada ya maneno "Mahakama Kuu". | | |
| | | (viii) Ibara ndogo ya (4)(b), iandikwe upya na iandikwe "awe ni mtu mwenye shahada yoyote ya Chuo Kikuu". | | |
| | | (ix) Aya ya (b) ifanyiwe marekebisho ili:-<br>(a) sifa iwe ni shahada ya pili, hususan, ya sheria;<br>(b) uzoefu uwe ni miaka kumi na tano. | | |
| | | (x) Ibara ya 181(4)(b) iongeze masharti ya uzoefu wa Ujaji kwa kipindi kisichopungua miaka mitano. | Kuepuka kuteua Majaji wastaafu. | |
| | | (xi) 181(4)(b)-Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wawe na sifa ya kuwa mawakili na wamekuwa na sifa hiyo kwa | Kutanua wigo wa kupatikana kwa mtu anayefaa kushika wadhifa huo. | |

| Ibara Na. | Kichwa cha habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | muda usiopungua miaka kumi. | | |
| | | (xii) Ibara iboreshwe kwa kuonyesha uchaguzi wa serikali za mitaa. | | |
| | | (xiii) Aya (d) ya ibara ndogo ya (4) ifutwe. | Kipengele hiki kinaweka kibano ambacho kitakuwa kigumu kutekeleza. | |
| | | (xiv) Aya (d) ya Ibara ndogo ya (4) na badala yake iandikwe kama ifuatavyo:<br>"(d) awe na uzoefu wa utumishi wa umma au binafsi katika moja wapo ya nyanja za sheria, utawala, menejimenti, logistics na takwimu kwa kipindi kisichopungua miaka mitano". | Hakuna haja ya kuweka sifa za mtu kuwahi kuwa Jaji Mkuu. | |
| | | (xv) Katika Ibara ndogo ya (4)(e) yaongezwe maneno "kukosa uaminifu" baada ya maneno "linalohusiana na". | | |
| | | (xvi) Katika aya (c) ya ibara ndogo ya (6) kiwekwe uwiano kwa sifa za wajumbe wote. | Ambaye hajawa kwenye nafasi ya utumishi wa uma kwa muda wa miaka mitano kabla ya uteuzi huo. | |
| | | (xvii) Ibara ndogo ya (6)(c) ibadilishwe ili iandikwe kama ifuatavyo:<br>"(c) mtu ambaye anashika nafasi ya madaraka katika asasi zisizo za kiserikali". | | |
| | | (xviii) Aya ya (c) ya Ibara ndogo ya (6) ifutwe. | Haieleweki ni kwa nini iliwekwa kuwazuia watu walioshika madaraka | |

| Ibara Na. | Kichwa cha habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | kwenye asasi zisizo za kiserikali kuwa wajumbe wa Tume. | |
| | | (xix) Ibara ndogo ya (6) neno 'mtawalia" lifutwe na badala yake liandikwe neno "kwa kufuatana". | | |
| | | (xx) Ibara ndogo ya (7) neno 'uwiano" lifutwe na badala yake liandikwe neno "asilimia". | | |
| | | (xxi) Ibara hii irekebishwe ili Tume Huru ya Uchaguzi iundwe kuanzia ngazi ya Taifa hadi Wilaya. | (a) Kwa sasa, katika ngazi za Wilaya Msimamizi wa Uchaguzi ni Mkurugenzi wa Wilaya ambaye siyo mwajiriwa wa Tume ya Uchaguzi.<br>(b) Kuwepo kwa Tume Huru katika ngazi ya Wilaya kutawezesha kuendeshwa kwa uchaguzi huru na wa haki na kuondoa manung'uniko kwa vyama vinavyoshindwa kwenye chaguzi husika.<br>(c) Watendaji wote wa Tume Huru ya Uchaguzi siyo wanachama wa chama cho chote cha siasa hivyo watatenda haki kwa kila chama | |

| Ibara Na. | Kichwa cha habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | cha siasa na wananchi wataona hivyo. | |
| | | (xxii) Katika Ibara ndogo ya (8) tarakimu "(8)" ifutwe na kuweka tarakimu "(7)". | Masahihisho. | |
| | | (xxiii) 181(2-5) Ibara irekebishwe na isomeke :<br>2.Tume huru ya uchaguzi itaundwa na Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wengine (12) Sita kutoka Tanganyika na Sita kutoka Zanzibar.Mwenyekiti akitoka Tanganyika,Makamu wake atoke Zanzibar.Nafasi za Wajumbe zitatangazwa na Tume ya Utumishi wa Umma kwa muda wa siku (30),na kutangaza siku (15) kwa ajili ya pingamizi yoyote kwa Wagombea,Wagombea watafanyiwa usaili na watakaochaguliwa watapelekwa Bungeni kwa kuthibitishwa.Kila Mjumbe ni lazima apate kuanzia asilimia 51% ya kura za Wabunge.Wajumbe hao wataapa kwa Spika wa Bunge.Ikiwa kuna mgombea hakupata asilimia ya kura iliyowekwa,mchakato kwa nafasi hiyo utaanza upya.<br>3. Wajumbe wa Tume ya | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | Uchaguzi watafanya kazi kwa mihula miwili ya miaka mitano mitano bila ya kuhitajika kupigiwa kura tena baada ya muhula wa kwanza.<br>4. Tume itaweza kushitakiwa katika Mahakama ya juu na Mgombea binafsi ama chama chochote cha siasa ama mwananchi ambae amedhalilishwa ama kunyimwa haki ya kuandikishwa ama kupiga kura.<br>5.Wajumbe wa Tume watakuwa na sifa zifuatazo:<br>(a) Awe ni raia wa asili ya Tanzania, si wa kuomba au kuombewa na wazazi wake.Ikiwa aliombewa na babu ama bibi upande wa baba au mama ataweza kuwa Mjumbe.<br>(b)Awe ni mwenye akili timamu na hajawahi kuugua maradhi ya akili,<br>(c)Asiwe na maradhi makubwa ambayo yataweza kumzuilia kutekeleza majukumu yake,<br>(d) Awe ni mwenye elimu isiyopungua shahada ya kwanza,<br>(e)Asiwe amewahi kuhukumiwa kwa makosa ya uhaini au jinai,<br>(f) Asiwe mwenye | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | kujishirikisha katika biashara haramu ama vitendo vya uhalifu.<br><br>(xxiv) Ibara ndogo ya (2) ifutwe na badala yake iandikwe kama ifuatavyo:<br>“(2) Katibu Mkuu Kiongozi atakuwa Katibu wa Kamati ya Uteuzi”. | | |
| 182. | Kamati ya Uteuzi | (i) Ibara 182(1) irekebishwe kwa kongeza Katibu wa Tume ya Utumishi wa Umma katika kamati hiyo ili kuwa na uwakilishi wa mihimili yote mitatu. | | 1. Ibara ya 182 inakuwa 191.<br>2. Ibara ndogo ya (1)(g) isomeke “mwenyekiti wa Tume ya Maadili na Uwajibikaji”<br>3. Ibara ndogo ya (3) na (4) yameongezwa maneno “na waliopendekezwa” mbele ya neno “walioomba”<br>4. Ibara ndogo ya (6) yameongezwa meneno “wanaoweza kuteuliwa” mbele ya maneno “majina ya watu” |
| | | | Ili kutoa nafasi kwa Mkurugenzi wa Tume Huru ya Uchaguzi kuteuliwa na Tume na siyo yeye kushiriki katika kuwateua wajumbe wa Tume huru ya uchaguzi. | |
| | | (ii) Katika aya ya 182 inayohusu ‘Kamati ya Uteuzi’ kuongeza vipengele vifuatavyo baada ya kipengele (g) cha ibara ndogo ya (1):<br>(h) Wajumbe watakaowakilisha vyama vya mawakili wa kujitegemea vya Washirika wa Muungano;<br>(g) Wajumbe watakaowakilisha chama cha siasa chenye wawakilishi katika Bunge la Jamhuri ya Muungano au | Kuweka ufasaha. | |

| Ibara Na. | Kichwa cha habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | mabunge ya Washirika wa Muungano. | | |
| | | (iii) 182 (1)(g) isomeke Mwenyekiti wa Tume ya Maadili na Uwajibikaji. | | |
| | | (iv) Ibara ya 182 uteuzi wa Wajumbe kutoka Mhimili wa Serikali nao wawepo. | | |
| | | (v) 182(3) na (4)-Yaongezwe maneno "na waliopendekezwa" baada ya neno "walioomba". | | |
| | | (vi) Aya (d) na (e) ya ibara ndogo ya (4) zifutwe. | | |
| | | (vii) 182 ibaki kama ilivyo. | Inajitosheleza. | |
| 183. | Ukomo wa kushika madaraka ya Ujumbe wa Tume Huru ya Uchaguzi | (i) Ibara ndogo (2)(e) iandikwe kama ifuatavyo: "(e) kutiwa hatiani kwa kosa la kukosa uaminifu na adhabu yake ni kifungo gerezani kwa muda unaozidi miezi sita". | | Ibara ya 183 inakuwa ibara ya 192.<br><br>Ibara ibaki kama ilivyo. |
| | | (ii) Ibara ya 183 (2) irekebishwe kwa kuongeza aya mpya ya (g) itakayosema "kuzuia uiingiliaji na uvurugaji mchakato wa uchaguzi kinyume na sheria." | Kosa hili liwe sababu ya mtu kukoma kuwa mjumbe katika Tume. | |
| | | (iii) Ibara ndogo ya (3) neno 'Kamishna" lifutwe na badala yake liandikwe neno "Mjumbe". | Neno mjumbe ndilo lililotumika katika rasimu. | |
| | | | (iv) 183(4) Ibara irekebishe na isomeke 'apelekwe kwenye tume ya maadili ashughulikiwe na pia apelekwe mahakamani ili | |

| Ibara Na. | Kichwa cha habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | ahukumiwe. | |
| | | (v) Ibara ya 183(6) Katiba itamke kwamba utaratibu husika utawekwa na Sheria wala siyo Kamati kama ambavyo Rasimu inasema. | | |
| | | (v) Ibaki kama ilivyo. | Inajitosheleza. | |
| | | (vi) Maneno "utawala bora" yaondolewe. | Utawala Bora haushughulikiwi na Tume hii. | |
| 184. | Wajibu wa Tume Huru ya Uchaguzi | (i) Ibara ya 184(1) irekebishwe kwa kuongeza aya mpya za (g)na (h) zitakazosema: "(g) kuweka mipaka ya Majimbo kwa kufuata sheria; (h) Kutangaza matokeo yote ya uchaguzi kwa wakati muafaka (siku 5 baada ya siku ya uchaguzi) na kuyaweka wazi ili kuwapa wananchi nafasi ya kulinganisha na matokeo yanayotangazwa na Tume." | | 1. Ibara ya 184 inakuwa ibara ya 193.<br>2. Ibara ndogo ya (1) (e) isomeke "kusimamia fedha za vyama vya siasa.<br>3. Ibara ndogo ya (2) mbele ya maneno "mpiga kura" yamewekwa maneno "wakati wa" badala ya neno "katika" aidha mbele ya neno "kuratibu" yameongezwa maneno "utoaji wa elimu ya uraia kuhusu uchaguzi". Pia neno "wananchi" limeondolewa. |
| | | (ii) 184(1)(f)Neno "ruzuku" liondolewe na badala yake yawekwe maneno "fedha za vyama vya siasa". | Msajili asimamie fedha zote. | |
| | | (iii) 184(1)(d), (e) na (f) zihamishwe kwenda katika Ibara zinazohusu Ofisi ya Msajili wa Vyama. | Kutenganisha Msajili wa Vyama vya Siasa na Tume Huru ya Uchaguzi. | |
| | | (iv) Ibara ya 184 Wajibu uainishwe vizuri zaidi. | | |
| | | (v) Ibara ya 184 Tume iongozewe | Kuweka mamlaka ya | |

| Ibara Na. | Kichwa cha habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | jukumu la kuratibu sifa zilizoainishwa katika Ibara ya 75. | kuratibu sifa za wagombea | |
| | | (vi) Ibara ndogo ya (1)(a) hadi (c) zifutwe na badala yake zisomeke kama ilivyo ibara 74(6)(d) ya Katiba ya sasa. | | |
| | | (vii) 184(3)(b) kuwe na akidi maalum ya kutolea maamuzi,wawe si chini ya 5.Idadi ya wajumbe wanawake na wanaume ilingane. | Kuleta uwajibikaji na maamuzi yenye manufaa ya taifa na kuzingatia usawa wa kijinsia kwenye vyombo vya kutoa maamuzi. | |
| | | (viii) Ibara ndogo ya (3)(d) maneno "kwa kuzingatia uwakilishi wenye usawa na" yafutwe. | | |
| | | (ix) Ibara ndogo ya (4) ifutwe na iandikwe upya na iandikwe kama ifuatavyo:<br>"(4) Endapo suala la kumuondoa Mjumbe wa Tume huru ya Uchaguzi kwa kukiuka Kanuni za Maadili ya Uongozi wa Umma litajitokeza, jambo hilo litashughulikiwa na Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji". | | |
| | | (x) Ibara ya 184(1)(a) iboreshwe kwa kuongeza kusimamia uchaguzi wa viongozi wa serikali za mitaa. | | |
| | | (xi) 184(8)-Rejea iwe Ibara ndogo ya (7). | | |
| | | (xii) Ibara ya 184(8)(f) iboreshwe wasimamizi wote wa uchaguzi ambao ni waajiriwa wa Tume. | | |
| | | (xiii) Ibara ya 184 (4)(a) isomeka kwamba awe raia wa kuzaliwa". | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | (xiv) Iongezwe ibara ndogo ya (9) itakayosomeka kama ifuatavyo: "(9) Kwa madhumuni ya kulinda na kuhifadhi uhuru wa Tume na kuhakikisha uchaguzi unaosimamiwa na Tume unakuwa huru na wa haki, itakuwa marufuku kwa wasimamizi wote wa uchaguzi kuwa watumishi wa serikali." | | |
| | | (xv) Watendaji na Wakurugenzi wa Tume na katika (Taasisi za Muungano) wasiteuliwe na Rais peke yake. Iwe pia kwa njia ya mchakato wa kutangaza nafasi, wahusika kuomba, usaili na kuidhinishwa na Bunge. | | |
| | | (xvi) Ibara ya 184(5) irekebishwe kwa kufuta maneno "haitalazimika kufuata" na badala yake kuweka neno "haitofuata". | | |
| | | (xvii) Ibara ya 184(7) irekebishwe kwa kufuta neno "kujiunga" na badala yake kuweka neno "kuwa". | | |
| 185. | Malalamiko kuhusu uchaguzi | (i) Ibara ya 185(2) ikisomwa pamoja na Ibara ya 125 zina maelezo yanayokinzana juu ya Mahakama inayotakiwa kupokea shauri linalohusu malalamiko ya uchaguzi. Ibara ya 185(2) inaitaja mahakama ya Rufani ilhali Ibara ya 125 inaitambua Mahakama Kuu kama ngazi ya mwanzo ya kufungua shauri la uchaguzi. | Iwekwe bayana ni mahakama gani yenye mamlaka ya mwanzo wa kusikiliza shauri la uchaguzi. | 1. Ibara ya 185 itakuwa ibara ya 194.<br>2. Ibara ndogo ya (2) neno "mahakama ya rufaa" isomeke "Mahakama Kuu"<br>3. Ibara ndogo ya (3) imeondolewa. |
| | | (ii) Ibara ya 185(2) Ibara hii | Hakuna mamlaka hayo | |

| Ibara Na. | Kichwa cha habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | inakinzana na ya 160(1). | kwa Mahakama ya Rufani. | |
| | | (iii) Katika ibara ndogo ya (2) maneno “Mahakama ya Rufaa” yafutwe na badala yake iandikwe “Mahakama Kuu”. | | |
| | | (iv) Ibara ya 185(3) ifutwe. | Katiba isiweke idadi ya majaji wa kusikiliza shauri bali suala la idadi liwekwe kwenye kanuni za Mahakama. | |
| | | (v) Mahakama kuu iendelee kusikiliza mashauri ya wabunge na sio mahakama ya rufaa. | | |
| | | (vi) Iongezwe ibara mpya yenye masharti ya Uteuzi wa Mkurugenzi wa Uchaguzi itakayosomeka kama ifuatavyo:<br>“_(1) Kutakuwa na Mkurugenzi wa Uchaguzi atakayeteuliwa na Rais baada ya kupendekezwa na Tume ya Utumishi wa Umma na kuthibitishwa na Bunge.<br>(2) Mkurugenzi wa Uchaguzi atakuwa na sifa zifuatazo:<br>(a) awe ni raia wa kuzaliwa na angalau mmoja kati ya wazazi wake ni raia wa kuzaliwa wa Tanzania;<br>(b) awe ni mtu mwaminifu, mwadilifu, na mwenye mwenendo usiotiliwa shaka na jamii;<br>(c) asiwe kiongozi wa chama chochote cha siasa na hajawahi kushika wadhifa wowote wa kisiasa katika chama chochote cha kisiasa; | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | (d) awe na elimu ya shahada ya chuo cha elimu ya juu kinachotambuliwa kwa mujibu wa sheria za nchi; na<br>(e) awe ni mtu ambaye hajawahi kutiwa hatiani kwa kosa lolote la jinai linalohusu kukosa uaminifu. | | |
| | | (vii) Iongezwe ibara mpya itakayobainisha majukumu ya Mkurugenzi wa Uchaguzi itakayosomeka kama ifuatavyo:<br>"(1) Mkurugenzi wa Uchaguzi atakuwa ndiye msimamizi na mtekelezaji mkuu wa majukumu ya kila siku ya Tume Huru ya Uchaguzi kuhusiana na masuala ya uchaguzi, uandikishaji wa wapiga kura na uendeshaji wa kura ya maoni.<br>(2) Mkurugenzi wa Uchaguzi atatekeleza majukumu yake kwa kufuata utaratibu ulioainishwa na sheria za nchi kuhusu masuala ya uchaguzi.<br>(3) Mkurugenzi wa Uchaguzi atatekeleza majukumu yake kwa kusaidiwa na watendaji ambao ni watumishi wa umma kwa kadri ya idadi inayohitajika.<br>(4) Katika kutekeleza majukumu yake, Mkurugenzi wa Uchaguzi atawajibika kwa Tume Huru ya Uchaguzi. " | | |
| | | | | Imeongezwa Ibara mpya ya 195 inayozungumzia |

| Ibara Na. | Kichwa cha habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | | “uteuzi wa Mkurugenzi wa Uchaguzi” |
| | | | | Imeongezwa Ibara mpya ya 196 inayozungumzia majukumu ya Mkurugenzi wa uchaguzi |

## (b) Vyama vya siasa

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekeb isho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| 186. | Vyama vya siasa | (i) Iongezwe Ibara kuhusu mgombea huru. | Kuweka masharti ya kuzuia mgombea huru kuwa na sera za mrengo wa kuligawa taifa kwa misingi ya udini, ukabila, ukanda, rangi, jinsia au kuvunja Muungano. | 1. Ibara 186 itakuwa 197.<br>2. Ibara ndogo ya (2) neno “chombo” lisomeke “chama” |
| | | (ii) Ibara ya 186 ifutwe na vyama visiwe katika mambo ya Muungano. | | |
| | | (iii) 186-iweke masharti kwa vyama vya siasa kuzingatia uwiano wa kijinsia katika nafasi za uongozi. | Kuweka uwiano wa kijinsia. | |
| | | | (iv) 186(2)(c) “Nguvu” Neno “Nguvu” litafsiriwe | |
| | | (v) Ibara ndogo ya (2) aya (d) ifutwe. | | |
| | | (vi) Ibara hii irekebishwe kwa kuongeza ibara ndogo mpya itakayoruhusu Vyama vya siasa kuungana na kuunda muungano wa kisiasa siku 21 kabla ya tarehe ya mwisho ya kuanza rasmi kwa | Utaratibu huu, utasaidia kuunganisha vyama vidogo vidogo pia utakuza demokrasia. | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekeb isho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | kampeni za uchaguzi mkuu na muungano huo utasajiliwa bila ya kuathiri usajili wa chama husika. | | |
| | | (vii) 186(5)-Maneno "na sheria iliyotungwa na Bunge kwa ajili hiyo" yafutwe. | Sheria iliyotungwa na Bunge imetajwa katika Ibara ya 187(4). | |
| | | (viii) Iongezwe ibara mpya inayobainisha masharti ya uteuzi wa Msajili wa vyama vya siasa itakayosomeka kama ifuatavyo.<br>187 (1) Kutakuwa na Msajili wa Vyama vya Siasa atakayeteuliwa na Rais baada ya kupendekezwa na Tume ya Utumishi wa Umma na kuthibitishwa na Bunge.<br>(2) Msajili wa Vyama vya Siasa atakuwa na sifa zifuatazo:<br>(i) awe raia wa kuzaliwa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;<br>(ii) awe ni mtu mwaminifu, mwadilifu, na mwenye mwenendo usiotiliwa shaka na jamii;<br>(iii) awe ni mtu ambaye siyo kiongozi wa chama cha siasa na hajawahi kushika wadhifa wowote wa kisiasa katika chama chochote cha kisiasa; na<br>(iv) awe na elimu ya shahada ya chuo cha elimu ya juu kinachotambuliwa kwa mujibu | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekeb isho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | wa sheria za nchi. | | |
| | | (ix) Iongezwe ibara mpya itakayobainisha wajibu wa msajili wa vyama vya siasa na isomeke kama ifuatavyo:<br>188.-(1) Msajili wa Vyama vya Siasa atakuwa na wajibu wa:<br>(a) kusimamia na kuratibu uandikishaji na shughuli za vyama vya siasa kwa mujibu wa masharti ya Katiba na sheria za nchi;<br>(b) kutayarisha na kuchapisha ripoti za kila mwaka kuhusu ripoti za ukaguzi wa fedha wa kila chama cha siasa; na<br>(c) kusimamia fedha za vyama vya siasa.<br>(2) Msajili wa Vyama vya Siasa atatekeleza majukumu yake kwa kufuata utaratibu ulioainishwa na sheria za nchi kuhusu masuala yahusuyo vyama vya siasa. | | |
| | | | | Imeongezwa Ibara mpya ya 198 inayozungumzia uteuzi wa Msajili wa Vyama vya Siasa |
| | | | | Imeongezwa Ibara mpya ya 199 inayozungumzia Wajibu wa Msajili wa |

| ***Ibara Na.*** | ***Kichwa cha Habari*** | ***Maoni ya Mabaraza*** | ***Sababu ya Maoni*** | ***Marekeb isho ya Tume*** |
|---|---|---|---|---|
| | | | | Vyama vya Siasa |

### (c) Mkurugenzi wa uchaguzi na Msajili wa Vyama vya Siasa

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| 187. | Utekelezaji wa majukumu ya Tume Huru ya Uchaguzi | (i) Ibara ya 187 Ofisi ya Tume ya Uchaguzi na Msajili wa Vyama vya Siasa ziendelee kuwa taasisi mbili tofauti ili kuondoa mgongano wa masilahi ya kimajukumu. | | Ibara imefutwa |
| | | (ii) 187(5) isomeke "Mkurugenzi wa Uchaguzi na Msajili wa Vyama vya Siasa kila mmoja atateuliwa na Rais kutoka miongoni mwa majina ya watu watatu yaliyopendekezwa na Tume ya Utumishi wa Umma na kabla ya kuapishwa jina lake litawasilishwa Bungeni kwa ajili ya kuthibitishwa na Bunge." | Kada hii inahitaji uteuzi wa Rais. | |
| | | (iii) Ibara ya 187(2) isomeke:<br>• Jina la nafasi ya Mkurugenzi wa Uchaguzi libadilishwe kuwa Mkurugenzi wa Uchaguzi ili kuwezesha Wakuu wa Idara kufikia Vyeo vya Ukurugenzi.<br>• Pasiwepo na *Accounting Officers* wawili katika Insitution. Usajili wa Vyama uwe ni Idara ya Tume.<br>• Mkurugenzi wa Uchaguzi awe ndio *"Over All Incharge"*.<br>• Ili kuifanya Tume kuwa Huru awe ni Mwajiriwa wa Tume. | | |
| | | (iv) Ibara ya 187 Ifanyiwe marekebisho ili:<br>(a) kuainisha majukumu na sifa za Mkurugenzi na Msajili wa | (a) Majukumu yao ni mazito.<br>(b) Kuleta uhuru katika utendaji kazi wao. | |

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Maoni* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| | | Vyama vya Siasa;<br>(b) Wakurugenzi wa Halmashauri wasiwe wasimamizi wa Uchaguzi | | |
| | | (v) Ibara ndogo ya (5) maneno "baada ya" yafutwe na badala yake iandikwe "na". | | |
| | | (vi) Iongezwe ibara ndogo mpya itakayosomeka kama ifuatvyo: "Msimamizi wa uchaguzi wa Jimbo atatakiwa awe na sifa sawa na za kumuwezesha kuwa Mjumbe wa tume huru ya uchaguzi kwa mujibu wa Ibara ya 181(5)". | | |
| | | (vii) Iongezwe Ibara ndogo mpya itakayoainisha sifa za Mkurugenzi wa Uchaguzi na Msajili wa Vyama vya Siasa. | Mkurugenzi na Msajili wa Vyama vya Siasa wamepewa majukumu makubwa kwa mujibu wa Rasimu ya Katiba hii hivyo ni vyema sifa zikawekwa wazi. | |
| | | (viii) Iongezwe ibara mpya itakayotamka kuwa fedha za uendeshaji wa Tume ya Uchaguzi zitatoka mfuko Mkuu wa Hazina na utaundwa mfuko maalumu kwa ajili ya kuendesha shughuli za Tume ya Uchaguzi. | | |
| | | (ix) Ibara ifutwe,suala hili litazungumziwa katika Tume za washirika. | | |

# SURA YA KUMI NA TATU YA RASIMU

## 13.0 SEHEMU YA KWANZA:TUME YA MAADILI YA UONGOZI NA UWAJIBIKAJI

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| 188. | Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji | (i) Katika aya (c) inapendekezwa maneno "utumishi wa umma" yafutwe na yasomeke "uongozi". | | 1. Ibara ya 188 itakuwa ibara ya 200.<br>2. Ibara ndogo (2) maneno Tume ya Utumishi wa Umma yaondolewe na kuwekwa maneno "kamati maalum ya uteuzi"<br>3. Ibara ndogo (4)(a) isomeke "awe raia wa kuzaliwa wa Tanzania"<br>4. Imeongezwa ibara ndogo ya (3) ambayo itasomeka:<br>"Uteuzi wa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Tume, utafanywa kwa kuzingatia misingi kwamba endapo Mwenyekiti atateuliwa kutoka upande mmoja wa Jamhuri ya Muungano, basi Makamu Mwenyekiti |
| | | (ii) Uteuzi ufuate mchakato wa wazi kwa wote ikiwa ni pamoja na wajumbe wote; | | |
| | | (iii) TAKUKURU iingie kama kitengo ndani ya Tume hii, na pia iwe Kitengo huru. | | |
| | | (iv) Ibara ndogo ya (2) ifutwe na badala yake iandikwe kama ifuatavyo:<br>"(2) Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji watateuliwa na Rais baada ya kupendekezwa na Kamati Maalum ya uteuzi.<br>(3) Kutakuwa na Kamati ya uteuzi kwa madhumuni ya ibara hii ambayo itakuwa na wajumbe wafuatao:-<br>(a) Jaji Mkuu wa Mahakama ya Rufani;<br>(b) Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano;<br>(c) Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania;<br>(d) Jaji wa Mahakama Kuu ya | Taasisi hii ni nyeti na ya Kikatiba na inapaswa kuwa huru. Namna ya kuifanya iwe huru na ionekane kuwa iko huru ni kuanzia kwenye uwepo wa namna huru ya uteuzi wa wajumbe wake. Wajumbe walioainishwa wako huru kwanza wao binafsi na hata taasisi zao. | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | Zanzibar;<br>(e) Spika wa Bunge la Tanzania;<br>(f) Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar;<br>(g) Mwanasheria Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. | | atateuliwa kutoka upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano"; "<br><br>5. Ibara ndogo ya (5) (c) imerekebishwa na itasomeka "miaka kumi na tano" badala ya "miaka kumi"<br>6. Imeongezwa ibara ndogo ya (5)(e) ambayo inasomeka "awe hajawahi kutiwa hatiani kwa kosa la jinai au kosa la kukwepa kulipa kodi, rushwa, uhujumu uchumi, ubadhirifu wa mali ya umma au kutumia madaraka yake vibaya." |
| | | (v) Ibara ya 188(3) irekebishwe kwa kufuta maneno "kuthibitishwa na Bunge" na yawekwe maneno "kuapishwa na Rais". | (a) Wapo katika Mhimili wa Serikali.<br>(b) Si viongozi wa kisiasa.<br>(c) Hawawajibiki Bungeni. | |
| | | (vi) Ibara ya 188(4)(b) irekebishwe kwa kufuta maneno "kwa mujibu wa sheria za nchi". | | |
| | | (vii) Iongezwe ibara ndogo mpya ambayo itasema kama kifuavyo: "Iwapo Mwenyekiti anatoka upande mmoja wa Muungano, Makamu Mwenyekiti atoke upande mwingine wa Muungano". | | |
| | | (viii) Iongezwe Ibara nyingine itakayoelezea upatikanaji wa Wajumbe wengine wa Tume na sifa zao ambazo zitaeleza kama ifuatavyo:<br>1. Wajumbe wengine saba watateuliwa na Rais baada ya kupendekezwa na Tume ya Utumishi wa Umma.<br>2. Sifa za Wajumbe zitakuwa kama ifuatavyo:<br>(a) Awe raia wa Tanzania;<br>(b) Mtu mwenye shahada ya Chuo Kikuu | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | kinachotambulika kwa mujibu wa sheria za nchi;<br>(c) Mtu mwenye uzoefu kwenye uongozi kwa kipindi kisichopungua miaka saba;<br>(d) Mtu mwenye heshima, weledi, uaminifu, uadilifu na asiye na tabia au mwenendo wenye kutiliwa shaka. | | |
| | | (ix) Iongezwe ibara mpya itakayobainisha masharti ya uteuzi wa wajumbe wa kamati ya uteuzi ambayo itasomeka kama ifuatavyo:<br>" .- Kutakuwa na Kamati Maalum ya Uteuzi ambayo itakuwa na Wajumbe wafuatao:<br>(a) Jaji Mkuu wa Mahakama ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;<br>(b) Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;<br>(c) Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanganyika;<br>(d) Jaji wa Mahakama Kuu ya Zanzibar;<br>(e) Spika wa Bunge la Tanganyika;<br>(f) Spika wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar; na<br>(g) Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. | | |
| | | | | Imeongezwa ibara mpya |

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya maoni* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| | | | | 201 inayozungumzia "uteuzi na sifa za wajumbe wa Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji." |
| | | | | Imeongezwa ibara mpya ya 202 ambayo inazungumzia "uanzishwaji wa kamati maalum ya Uteuzi." |
| 189. | Majukumu ya jumla ya Tume | (i) Tume ya Haki za Binadamu ijulikane kwa jina la Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. | | 1. Ibara ya 189 inakuwa ya 203.<br>2. Ibara ndogo ya (2)(b) imerekebishwa na inasomeka: "kufanya upekuzi kwa kushirikiana na Taasisi nyingine"<br>3. Ibara ndogo ya (2)(e) imerekebishwa na inasomeka; kutoa ushauri juu ya masuala ya ubadhirifu wa fedha na mali za umma.<br>4. Ibara ndogo ya (2)(j) neno "kutoa maelekezo" lisomeke kutoa ushauri. |
| | | (ii) Ibara ya 189(2)(b),(c),(d),(e), (f),(g),(j) na (k) ziangaliwe upya. Majukumu makuu ya Tume yatajwe ndani ya Katiba na mengine yatajwe kwa kina katika sheria ya Bunge ili kuyaainisha vizuri zaidi kwa kuzingatia majukumu ya vyombo vingine ambavyo kazi zake zinaweza kufanana na za Tume hii. | (a) Tume imepewa majukumu mengi mno yanayoifanya iwe mpelelezi, mpekuzi, mwendesha mashtaka na kukaribia kutoa hukumu. Hii inakinzana na misingi ya utawala bora na utawala wa sheria.<br>(b) Sheria ina utaratibu mwepesi endapo mabadiliko yatahitahika kuliko utaratibu wa kurekebisha katiba. | |
| | | (iii) Kuwepo na masharti yatakayoleta ushirikiano na vyombo vingine vya dola kwa mambo ambayo yako nje ya majukumu ya Tume. | | |
| 190. | Muda wa kukaa madarakani wa Wajumbe wa Tume | Ibara ya 190 irekebishwe ili isomeke kama ifuatavyo:<br>190[(1) Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wengine wote | | 1. Ibara ya 190 inakuwa ibara ya 204.<br>2. Ibara imeandikwa upya na inasomeka kama |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | kila mmoja atashika madaraka yake kwa kipindi cha miaka mitatu au kipindi chengine cha chini ya miaka mitatu kama itakavyoainishwa katika barua ya uteuzi, ikizingatiwa kwamba uteuzi wa Wajumbe wa Tume utafanywa kwa namna ambayo Wajumbe wa Tume hawataanza au kumaliza muda wao kwa wakati mmoja.<br><br>(2) Bila ya kuathiri masharti ya ibara ndogo ya (1), Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti au Mjumbe wa Tume anaweza kuteuliwa tena kwa kipindi kingine kimoja tu cha miaka mitatu au vinginevyo vyovyote itakavyokuwa.<br><br>(3) Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wa Tume wakati watakapokuwa madarakani hawataruhusiwa kuteuliwa, kuchaguliwa au kushika wadhifa mwingine wowote katika nafasi ya utumishi wa umma.] | | ifuatavyo:<br>“204[(1) Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wengine wote kila mmoja atashika madaraka yake kwa kipindi cha miaka mitatu au kipindi kingine cha chini ya miaka mitatu kama itakavyoainishwa katika barua ya uteuzi, ikizingatiwa kwamba uteuzi wa Wajumbe wa Tume utafanywa kwa namna ambayo Wajumbe wa Tume hawataanza au kumaliza muda wao kwa wakati mmoja.<br>(2) Bila ya kuathiri masharti ya ibara ndogo ya (1), Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti au Mjumbe wa Tume anaweza kuteuliwa tena kwa kipindi kingine kimoja tu cha miaka mitatu au vinginevyo vyovyote itakavyokuwa.<br>(3) Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | | na Wajumbe wa Tume wakati watakapokuwa madarakani hawataruhusiwa kuteuliwa, kuchagulia au kushika wadhifa mwingine wowote katika nafasi ya utumishi wa umma. |
| 191. | Kuondolewa madarani kwa Wajumbe wa Tume | (i) Ibara ndogo ya (2) ifutwe na badala yake iandikwe kama ifuatavyo: "(2) Mwenyekiti, Makamu wa Mwenyekiti au mjumbe wa Tume anaweza kuondolewa madarakani kutokana na mapendekezo ya Kamati Maalum itakayoundwa na Rais". | | 1. Ibara ya 191 itakuwa ibara ya 205. 2. Ibara ndogo ya (1) na (2) ziongezewe maneno "Makamu wa Mwenyekiti au Mjumbe baada ya neno Mwenyekiti". 3. Ibara ndogo ya (3) imeandikwa upya na inasomeka: "Baada ya kupokea maombi hayo kutoka kwa wananchi au Tume ya Utumishi wa Umma, Rais ataunda kamati maalum itakayofanya uchunguzi kuhusu malalamiko hayo. |
| | | (ii) Ibara ndogo ya (3) ifutwe na badala yake iandikwe kama ifuatavyo: "(3) Baada ya kupokea maombi hayo kutoka kwa wananchi au Tume ya Utumishi wa Umma, Rais ataunda Kamati Maalum itakayofanya uchunguzi kuhusu malalamiko hayo". | Sababu za ujumla kwenye Ibara hizi ndogo ni kwamba Tume ya Utumishi wa Umma ikipokea maombi ya kuondolewa kwa wajumbe, ikaunda kamati na kuamua yenyewe itapingana na kanuni za haki za asili. | |
| 192. | Uhuru wa Tume | (i) Ibara ndogo ya (3) ifutwe na badala | Sababu za ujumla kwenye | Ibara ya 192 inakuwa ibara |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | yake iandikwe kamai ifuatavyo: “(3) Baada ya kupokea maombi hayo kutoka kwa wananchi au Tume ya Utumishi wa Umma, Rais ataunda Kamati Maalum itakayofanya uchunguzi kuhusu malalamiko hayo”. | Ibara hizi ndogo ni kwamba Tume ya Utumishi wa Umma ikipokea maombi ya kuondolewa kwa wajumbe, ikaunda kamati na kuamua yenyewe itapingana na kanuni za haki za asili. | ya 206 na ibaki kama ilivyo. |
| 193. | Uwezeshaji wa nyenzo na rasilimali | (i) Ibara ya 193 irekebishwe kwa kufuta maneno “kadri hali itakavyoruhusu”. | | Ibara ya 193 inakuwa ibara ya 207 na Ibaki kama ilivyo. |
| | | (ii) Ibara ndogo ya (1) hadi ya (5) ifutwe na badala yake iandikwe ibara ya 129 ya Katiba ya sasa. | Kulinda uhuru wa Tume. | |
| | | (iii) Maneno “kadri hali inavyoruhusu” yafutwe. | Ili Tume iweze kutelekeleza majukumu yake kwa ufanisi badala ya kutegemea fedha ‘kadri hali inavyoruhusu’. Neno hili linautata na kila mtu anaweza kulichukulia anavyotaka yeye na ile maana ya Kikatiba ikatoweka. | |

## 13.1 SEHEMU YA PILI:TUME YA HAKI ZA BINADAMU

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| 194. | Tume ya Haki za Binadamu | (i) Ibara ndogo ya (1) ibadilishwe na ieleze kwamba, "Wajumbe wateuliwe kwa kuzingatia jinsi ikiwa na wajumbe 4, jinsia nyingine iwe na Wajumbe 3. | | 1. Ibara ya 194 inakuwa ibara ya 208<br>2. Ibara ndogo ya (1) maneno "wajumbe wasiozidi saba" yasomeke "makamishna wasiozidi saba"<br>3. Imeongezwa Ibara ndogo ya (3) ambayo itasomeka:-<br>"Uteuzi wa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Tume, utafanywa kwa kuzingatia misingi kwamba endapo Mwenyekiti atateuliwa kutoka upande mmoja wa nchi mshirika, basi Makamu Mwenyekiti atateuliwa kutoka upande wa pili wa nchi mshirika;"<br>4. Ibara ndogo ya (6)(c) imeandikwa upya na kusomeka:-<br>(c) mtu mwenye uzoefu usiopungua miaka kumi ikiwa angalau |
| | | (ii) Ibara ndogo ya (2) irekebishwe na iandikwe kama ifuatavyo:<br>"(2) Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu watateuliwa na Rais baada ya kupendekezwa na Tume ya Utumishi ya Mahakama". | | |
| | | (iii) Ibara ya 194(3) maneno "kuthibitishwa na Bunge" yafutwe na kuweka maneno "kuapishwa na Rais". | (a) Wapo katika Mhimili wa Serikali.<br>(b) Si viongozi wa kisiasa.<br>(c) Hawawajibiki Bungeni | |
| | | (iv) Ibara ndogo ya (4)(a), Mwenyekiti na Makamu wake wawe raia wa kuzaliwa wa Tanzania. | | |
| | | (v) Ibara ndogo ya (4)(c) irekebishwe iandikwe kama ifuatavyo:<br>"(c) Mtu mwenye uzoefu wa utumishi wa umma, upeo mkubwa katika mambo ya haki za binadamu, utawala na mambo ya jamii kwa kipindi kisichopungua miaka kumi". | | |
| | | (vi) Ibara ndogo ya (4) aya (c) kiandikwe kama ifuatavyo:<br>"(c) mtu mwenye uzoefu wa | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | utumishi wa umma au katika taasisi binafsi zinazojishughulisha na maswala ya haki za binadamu kwa muda usiopungua miaka mitano". | | ana sifa ya masuala ya sheria, haki za binadamu, utawala, siasa na mambo ya jamii;<br><br>5. Imeongezwa Ibara ndogo ya (7) inayozungumzia sifa za makamishna wa Tume. |
| | | (vii) Iongezwe ibara nyingine itakayoeleza uteuzi wa Wajumbe na sifa zao kama ifuatavyo:<br>"(6) Wajumbe wengine watateuliwa na Rais baada ya kupita kwenye mchakato wa wazi kwenye Tume ya Utumishi wa Umma.<br>(7) Sifa za Wajumbe zitakuwa kama ifuatavyo:<br>**(a)** awe raia wa kuzaliwa wa Tanzania;<br>**(b)** mtu mwenye kuishi na kuheshimu haki za binadamu;<br>**(c)** mtu mwenye uzoefu usiopungua miaka saba ikiwa angalao ana sifa ya masuala ya sheria, haki za binadamu, utawala, siasa na mambo ya jamii;<br>**(d)** mtu mwenye heshima, weledi, uaminifu, uadilifu na asiye na tabia au mwenendo wenye kutiliwa shaka na jamii". | | |
| | | (viii) Iongezwe ibara ndogo mpya ambayo itaeleza kama ifuatavyo:<br>"Mwenyekiti akitoka upande mmoja wa muungano, itamkwe kuwa Makamu Mwenyekiti atatoka | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | upande mwingine wa Muungano". | | |
| | | Sehemu yote inayohusu Tume ya Haki za Binadamu iandikwe upya na iandikwe kama ifuatavyo:<br>*Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora*<br>"194.-(1) Kutakuwa na Tume itakayoitwa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora itakayoundwa na Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, na Makamishna wasiozidi watano.<br>(2) Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Makamishna watateuliwa na Rais baada ya kushauriana na Tume ya uteuzi kama itakavyoelezwa katika Katiba hii.<br>(3) Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti na Makamishna watashika nyadhifa zao baada ya kuthibitishwa na Bunge na kuapishwa na Rais.<br>(4) Sifa za Mwenyekiti wa Tume zitakuwa kama ifuatavyo;<br>(a) awe raia<br>(b) mtu mwenye shahada ya sheria, na sifa za kuteuliwa kuwa jaji;<br>(c) mtu mwenye uzoefu wa utumishi wa umma kwa kipindi kisichopungua miaka kumi; na<br>(d) mtu mwenye heshima, weledi, uaminifu, uadilifu na asiye na tabia au mwenendo wenye kutiliwa shaka na jamii.<br>(5) Sifa za Makamu Mwenyekiti | (a) Kutokana na Marekebisho ya 13 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 2000, (Bill Supplement No. 16 of 31st December, 1999) kwenye ukurasa wa kumi na moja (11) wa sheria tajwa, ilielezwa kuwa Tume ya Kudumu ya Uchunguzi (Ombudsman) haifutwi, kimajukumu ila inabakia na inajumuishwa na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.<br>(b) Majukumu ya Tume ya Kudumu ya Uchunguzi yamekuwepo kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (Sura 2 ya Sheria za Tanzania) na Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Na. 7 ya Mwaka 2001 (Sura | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | zitakuwa kama zilivyoainishwa katika Ibara ndogo ya (4) na kwamba iwapo Mwenyekiti anatoka sehemu moja ya Mshirika wa Muungano basi Makamu Mwenyekiti atatoka sehemu nyingine ya Mshirika wa Muungano.<br>(6) Makamishna watakuwa na sifa kama zilivyoainishwa kwenye Ibara hii:<br>(a) awe ni raia<br>(b) wawe na shahada kutoka vyuo vinavyotambulika na sheria ya nchi<br>(c) wawe miongoni mwa watu wenye ujuzi, uzoefu na upeo mkubwa katika mambo ya haki za binadamu, sheria, utawala, siasa au mambo ya jamii.<br>(d) Mtu mwenye heshima, weledi, uaminifu, uadilifu na asiye na tabia au mwenendo wenye kutiliwa shaka na jamii.<br>(7) Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ni Idara huru ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. | 391 ya Sheria za Tanzania).<br>(c) Hata Rasimu hii bado imeendelea kuainisha kazi za Ombudsman katika majukumu ya Tume ya Haki za Binadamu. Hivyo ili kuondoa mkanganyiko ni vema Tume ikaendelea na jina lake la awali kama lilivyo kwani kitendo cha kuliacha ni kufuta shughuli za “Ombudsman” chombo ambacho kimefanikiwa kwa kiasi kikubwa hapa nchini na Tanzania imekuwa ikipata sifa kwa kuwa nchi ya kwanza Afrika kuwa na Taasisi kama hii tangu mwaka wa 1965.<br>(d) Hivyo popote itakapotajwa Tume hii basi iandikwe kama Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.<br>(e) Inapendekezwa kuwa neno “Wajumbe” linaloonekana kwenye | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | Rasimu kuhusu Tume hii liondolewe na kuwepo neno "Kamishna" kwa sababu kulingana na Kanuni za Paris (Paris Principles) ambazo ndiyo chimbuko la Taasisi kama Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora duniani kote, Uongozi wa Juu wa Tume hizi kuanzia hizo za Kimataifa hadi za nchi wanachama, wanajulikana kwa jina la Kamishna. Awe Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti pamoja na wengine, wote huitwa Makamishna.<br>(f) Siyo vibaya kutofautiana au kufanya ubunifu lakini kwa Taasisi kama hizi mabadiliko ya majina haya yanaweza kuleta muonekano tofauti wa Tanzania na Taasisi yetu kwenye duru za Kikanda na kimataifa pia na kuonekana | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | kwenda kinyume na mfumo mzima ulioanzishwa na Kanuni za Paris na kuridhiwa na Baraza la Umoja wa Mataifa ambalo Tanzania ni mwanachama.<br>(g) Aidha kutokana na majukumu ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, pamoja na uzoefu tangu ilipoanzishwa, idadi ya Makamishna wasiozidi watano (5) ukiondoa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti na hivyo kufanya idadi yao kuwa saba (7) inatosha.<br>(h) Inapendekezwa kuwa Makamishna wote kutokana na asili ya majukumu, unyeti wake, na ile dhana ya kutokutofautiana kwa majukumu ya Tume kwa ujumla ni vema Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Makamishna wote kabla ya kushika madaraka yao | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | wathibitishwe na Bunge.<br>(i) Sifa za Makamishna pia zinapendekezwa kuwekwa bayana ili vigezo viwe wazi kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma pamoja na Kanuni za Paris (Paris Principles) ambazo zinataka mchakato wa upatikanaji wao uwe wazi, shirikishi na unaozingatia uwakilishi (Pluralism). | |
| | | | | Imeongezwa Ibara ya 209 inayozungumzia “Uanzishwaji wa Kamati ya Uteuzi” |
| 195 | *Kazi na majukumu ya Tume* | 195.(1) Kazi na majukumu ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora yatakuwa kama ifuatavyo:<br>(a) kuhamasisha hifadhi ya haki za binadamu na wajibu kwa jamii kwa mujibu wa Katiba na sheria za nchi;<br>(b) kupokea malalamiko juu ya uvunjwaji wa haki za binadamu kwa ujumla;<br>(c) kuchunguza uvunjwaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora;<br>(d) kufanya utafiti na kutoa elimu | Ili kuweza kuendana na Kanuni za Paris ambazo zilipitishwa na Baraza la Umoja wa Mataifa mwaka 1993 ambapo Tanzania ni mwanachama, kila taasisi kama Tume kote ulimwenguni ili kutekeleza majukumu yake vyema zinapaswa kusimamia kazi na majukumu yote yaliyoainishwa.<br>Kwa Tanzania kuacha | 1. Ibara ya 195 inakuwa ibara ya 210.<br>2. Ibara ndogo ya (1) imeongezewa aya ndogo (i),(j), (k), (l) na (m).<br>3. Aidha imeongezewa ibara ndogo ya (2) inayozungumzia mamlaka ya Tume ya Haki za Binadamu. |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | kwa umma kuhusu haki za binadamu na utawala bora;<br>(e) kufungua mashauri mahakamani ili kuzuia vitendo vya uvunjaji wa haki za binadamu au kurekebisha haki inayotokana na uvunjwaji huo wa haki za binadamu au ukiukwaji wa misingi ya utawala bora;<br>(f) kuchunguza mwenendo wa mtu yeyote anayehusika au taasisi yeyote inayohusika na masharti ya Ibara hii katika utekelezaji wa kawaida wa madaraka na kazi au majukumu yake au utekelezaji unaokiuka madaraka hayo;<br>(g) kutoa ushauri kwa serikali na vyombo vingine vya umma na vya sekta binafsi kuhusu haki za binadamu na utawala bora;<br>(h) kuchukua hatua zinazostahili kwa ajili ya kukuza na kuendeleza usuluhishi na suluhu miongoni mwa watu na taasisi mbali mbali wanaofika au kufikishwa mbele ya Tume;<br>(i) kutembelea magereza/ vituo vya polisi na mahala wanapozuiliwa watu au sehemu zinazofanana na hizo kwa madhumuni ya kutathmini na kukagua hali za watu wanamozuiliwa sehemu hizo na kutoa mapendekezo | kutekeleza kazi na majukumu tajwa hapo juu ni kwenda kinyume na makubaliano kwenye Baraza la Umoja wa Mataifa wakati wa kuridhia Kanuni tajwa na ni kuishushia heshima nchi yetu kwenye duru za kimataifa.<br>Aidha, kwa mara mbili mfululizo, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora imepata Alama "A" inayotolewa na International Coordinating Committee ya UN Human Rights Council baada ya kukidhi vigezo vilivyowekwa Kimataifa. Kitendo cha kupunguza majukumu yake ni kudhoofisha picha nzuri ya Tanzania kwenye anga za Kimataifa katika duru za ulinzi wa haki za binadamu na usimamizi wa misingi ya utawala bora.<br>Chombo cha mwisho cha utoaji haki ni Mahakama na maamuzi ya Tume hupelekwa Mahakamani kwa ajili ya kutiliwa nguvu. | . |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | yatakayowezesha kurekebisha kasoro zilizopo;<br>(j) kutoa mapendekezo yanayohusiana na sheria iliyokwisha tungwa au inayokusudiwa kutungwa, kanuni, au mambo ya kiutawala ili kuhakikisha zinakidhi viwango vya kimataifa na kikanda vya haki za binadamu;<br>(k) kuwasilisha taarifa na maoni huru kwenye vyombo na taasisi za kimataifa na za kikanda kuhusu hali ya haki za binadamu nchini pale inapobidi;<br>(l) kuihamasisha Serikali ya jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutia saini na kuridhia mikataba au makubaliano ya kimataifa yanayohusu haki za binadamu, kufuatilia na kutathmini utekelezaji, ndani ya Jamhuri ya Muungano, wa haki za binadamu zilizomo kwa mujibu wa Katiba hii, Katiba za Washirika wa Muungano, sheria za nchi na mikataba au makubaliano ya kimataifa ambayo Jamhuri ya Muungano inawajibika nayo;<br>(m) kwa kupitia Serikalini, kushirikiana na wawakilishi wa Umoja wa Mataifa, Mashirika ya Umoja wa Mataifa, Umoja wa | Nyongeza hii ya Majukumu au kazi za Tume ni kulingana na Kanuni za Paris (Paris principles) ambazo zinatabanahisha kinaga ubaga Majukumu ya Taasisi za namna hii ambayo Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ni mojawapo. | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | Nchi za Afrika, Jumuiya ya Madola na taasisi nyingine zenye mahusiano baina yao, miongoni mwao au ya kikanda na taasisi za nchi za nje ambazo zina uzoefu katika maeneo ya hifadhi na ukuzaji wa haki za binadamu.<br>(2) Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora itakuwa na mamlaka maalumu kama ifuatavyo:<br>(d) kumuita mtu yeyote mbele ya Tume na kumtaka awasilishe mbele yake nyaraka zozote, kumbukumbu au kitu chochote kilichopo chini ya miliki ya mamlaka yake kinachohusiana na jambo linalochunguzwa na Tume;<br>(e) kumtaka mtu yeyote kutoa taarifa anayoifahamu kwa Tume juu ya jambo linalochunguzwa na Tume;<br>(f) kutoa amri ya zuio la muda, kusubiri kumalizika kwa uchunguzi au utatuzi wa shauri unaofanywa na Tume;<br>(g) kwa kuzingatia sheria nyingine, kuingia na kukagua, jengo au mahali popote panapohusiana na uchunguzi wa Tume na kukamata nyaraka zozote husika au kitu chochote;<br>(h) kusababisha mtu yeyote anayekiuka maagizo yake au | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | taratibu za Tume kufunguliwa mashtaka ya jinai mahakamani.<br>(a) Iongezwe ibara ndogo ya (2) itakayosomeka kama ilivyo ibara 130(5) ya Katiba ya sasa.<br>(b) Iongezwe Ibara ndogo itakayoeleza kazi za Tume kama ifuatavyo:<br>(c) Kutembelea Magereza/ Vituo vya Polisi na mahala wanamozuiliwa watu au sehemu zinazofanana kwa madhumuni ya kutathmini na kukagua hali za watu wanamozuiliwa sehemu hizo na kutoa mapendekezo yatakayowezesha kurekebisha kasoro zilizopo.<br>(d) Kutoa mapendekezo yanayohusiana na sheria iliyokwishatungwa au inayokusudiwa kutungwa, kanuni, au mambo ya kiutawala ili kuhakikisha zinakubaliana na haki za binadamu.<br>(e) Kuihamasisha Serikali ya Jamhuri ya Muungano kuridhia/ | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | kutia saini mikataba au makubaliano yanayohusu haki za binadamu, kufuatilia na kutathmini utekelezaji, ndani ya Jamhuri ya Muungano, wa haki za binadamu zilizomo kwa mujibu wa katiba hii, Katiba za Washirika wa Muungano, sheria za nchi na mikataba au makubaliano ambayo Jamhuri ya Muungano inawajibika nayo.<br>(f) Kwa kupitia Serikalini, kushirikiana na wawakilishi wa Umoja wa Mataifa, Mashirika ya Umoja wa Mataifa, Umoja wa Nchi za Afrika, Jumuiya ya Madola na taasisi nyingine zenye mahusiano baina yao, miongoni mwao au ya kikanda na taasisi za nchi za nje ambazo zina uzoefu katika maeneo ya hifadhi na ukuzaji wa haki za binadamu. | | |
| 196 | *Muda wa kukaa Madarakani kwa Makamishna wa Tume.* | Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Makamishna wa Tume watakaa madarakani kwa kipindi kimoja cha miaka saba na wengine kwa utaratibu unaozingatia kwamba uteuzi wa | Namna hii ya kukaa madarakani kwa Tume ni nzuri kwa sababu kila mara katika uhai wa Tume, kutakuwepo na | 1. Ibara ya 196 inakuwa ibara ya 211.<br>2. Ibara imerekebishwa na inazungumzia muda wa kukaa |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | Makamishna hautamalizika kwa wakati mmoja;<br>(a) Mwenyekiti na Makamishna watatu watakaa madarakani kwa muda wa miaka saba kila mmoja;<br>(b) Makamu Mwenyekiti na Makamishna wawili watakaa madarakani kwa Miaka mitano;<br>(c) Tume ya Uteuzi itashauriana na Rais kuhusu Makamishna wawili watakaokaa madarakani kwa miaka mitano (5);<br>(d) Kwamba kama Mwenyekiti anatoka sehemu moja ya Mshirika wa Muungano, Makamu Mwenyekiti atatokea sehemu nyingine ya Mshirika wa Muungano. | Makamishna wenye uzoefu na taasisi na hivyo kutakuwa na nafasi ya kuelekezana na kupeana ujuzi wenyewe kwa wenyewe hivyo kupunguza gharama za kuwapeleka kwenye mafunzo.<br>Pili itapunguzia serikali na Tume yenyewe gharama za uteuzi wa Makamishna wengi kwa wakati mmoja.<br>Uteuzi utafanyika kwa wachache na baada ya muda mrefu ili tu kuziba mapengo. | madarakani kwa makamishna wa Tume. |
| 197 | *Kuondolewa Madarakani kwa Makamishna wa Tume.* | (1) Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Tume au Kamishna yeyote wa Tume anaweza kuondolewa madarakani kwa:<br>(a) kutokuwa na uwezo wa kutekeleza Majukumu yake kutokana na matatizo ya akili au kimwili;<br>(b) kukiuka kanuni za maadili ya viongozi wa umma;<br>(c) kukiuka miiko ya uongozi;<br>(d) kukosa weledi; na | Kwa asili ya kazi za Tume inapendekezwa kuwepo na chombo maalum kitakachoweza kupokea malalamiko na kupendekeza Makamishna kuondolewa madarakani tofauti na Tume ya Utumishi wa Umma.<br>Kuwepo kwa Tume ya Utumishi wa Umma kama chombo cha kuwapendekeza kuondolewa madarakani ni hatari kwa | 1. Ibara ya 197 inakuwa ibara ya 212.<br>2. Ibara imerekebishwa kwa kuweka neno “makamishna’ kila palipokuwa na neno “wajumbe”<br>3. Imeongezwa ibara ndogo ya (6) inayosomeka:<br>“Rais atachukua hatua kama atakavyoshauriwa na kamati maalum.” |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | (e) utovu wa nidhamu.<br>(2) Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti au Kamishna wa Tume anaweza kuondolewa madarakani kutokana na mapendekezo ya Kamati ya Uteuzi au kwa maombi ya mtu yeyote kwa Kamati ya Uteuzi, ambapo;<br>(a) maombi hayo yawe ya maandishi; na<br>(b) yaainishe masuala yanayolalamikiwa.<br>(3) Baada ya kupokea maombi hayo au endapo malalamiko yametolewa na Kamati yenyewe, Rais ataunda Kamati Maalum itakayofanya uchunguzi kuhusu malalamiko hayo.<br>(4) Baada ya kupokea ripoti ya Kamati Maalum, Tume ya Uteuzi itapeleka mapendekezo ya Kamati Maalum kwa Rais kwa uamuzi.<br>(5) Rais atalazimika kuchukua hatua kama atakavyoshauriwa na Kamati Maalum.<br>(6) Kwa madhumuni ya kuwakinga Makamishna kutokana na migogoro ya kimaslahi, mtu yeyote akiteuliwa kuwa Kamishna wa Tume atalazimika kuacha mara moja madaraka yeyote katika chama chochote cha siasa au madaraka ya aina nyingine yoyote itakayotajwa kwa ajili hiyo na sheria iliyotungwa na Bunge.<br><br>(7) Tume yaweza kutekeleza | mustakabali wa Tume na usimamizi mzima wa majukumu yake kwani Tume ya Utumishi wa Umma ni chombo ambacho kimsingi kipo chini ya Rais na kinaweza kutumiwa vibaya na watu wasiopenda au wanaochukizwa na utendaji kazi wa Tume yenyewe au Kamishna mmoja mmoja.<br>Pia upo uwezekano watendaji wa Tume ya Utumishi wa Umma yenyewe wakalalamikiwa na wakachunguzwa na Tume hivyo kutokea mgongano wa kimtazamo. Hivyo ni vema kukawepo chombo huru kitakachotajwa na Katiba hii kama ilivyokuwa hapo awali. | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | shughuli zake bila kujali kwamba kuna nafasi iliyo wazi miongoni mwa viti vya Makamishna au kwamba Kamishna mmoja hayupo. | | |
| | | (i) Ibara ndogo ya (1)(d) maneno "kukosa weledi" yafutwe na badala yake yasomeke 'kukosa uaminifu". | | |
| 198. | Uhuru wa Tume | (i) Ibara ndogo ya (1) iboreshwe kwa kutamka kuwa sheria zielekeze namna bora ya wananchi kupewa uhuru wa kuhoji utendaji wa Tume ya Haki za Binadamu pale itakaposhindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo.<br>(ii) Tume itakuwa huru; na kwa mantiki hiyo, haitaingiliwa na mtu yeyote au mamlaka yoyote katika utekelezaji wa Majukumu yake.<br>(iii) (2) Uchunguzi, mwenendo wa mashauri au mchakato wa Tume, hautakuwa batili kwa sababu tu ya makosa au upungufu kwenye taratibu, isipokuwa kwa sababu ya kutokuwa na mamlaka kisheria, hakuna uchunguzi, mwenendo, taratibu za uendeshaji mashauri au taarifa ya Tume itaweza kupingwa, kupitiwa upya, kufutwa au kuhojiwa katika mahakama yeyote.<br>(iv) (3) Hakutakuwa na mashtaka ya aina yoyote yatakayofunguliwa dhidi ya Makamishna, maafisa, na watumishi wa Tume na watu wengine waliopewa mamlaka na Tume, juu ya jambo lolote | | Ibara ya 198 inakuwa ibara ya 213 na inabaki kama ilivyo. |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | lililofanywa au kutofanywa wakati wa utekelezaji wa majukumu yao chini ya sheria hii isipokuwa pale itakapoonekana kwamba kitendo hicho au kutokufanyika huko kumefanywa au kuachwa kwa nia mbaya.<br>(v) Hakuna Kamishna au mtu mwingine aliyetajwa katika kifungu kidogo cha nne ataitwa kutoa ushahidi katika mahakama yoyote au katika mashauri yoyote yenye asili ya kimahakama kuhusiana na taratibu katika uchunguzi wowote au jambo lolote atakalolifahamu wakati wa utekelezaji wa majukumu yake chini ya Katiba hii.<br>(vi) Bila kuathiri ibara zilizotangulia, Tume itatoa Taarifa zake Bungeni kwa kujadiliwa si chini ya mara moja kwa mwaka kwa kupitia Kamati husika ya Bunge kuhusu utekelezaji wa Majukumu yake yaliyoainishwa kwenye Katiba hii.<br>(vii) Bunge litatunga sheria itakayoweka masharti kuhusu:<br>(viii) utaratibu wa utekelezaji wa Majukumu ya Tume;<br>(ix) utayarishaji wa Taarifa za Tume;<br>(x) utaratibu wa utoaji wa mapendekezo na maamuzi ya Tume;<br>(xi) watumishi wa Tume ; na<br>(xii) masuala mengine muhimu | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | yanayoihusu Tume. Ili Tume kuwa huru katika utendaji kazi wake ni lazima watumishi wake pia kuanzia ngazi ya Mwenyekiti hadi watendaji wake kuwa na kinga ili kuwalinda na hila mbaya ambazo zinaweza kufanywa na watu wenye nia mbaya au wavunja haki na misingi ya utawala bora ambayo Tume inasimamia.<br>Aidha kwa kujua kuwa Taasisi kama hizi zina wajibika kwa wananchi kupitia vyombo vyao vya uwakilishi kama Bunge, ni vema kuwa taarifa zote za Tume ziwasilishwe Bungeni kwa ajili ya kujadiliwa.<br>(xiii) Rejea Kanuni ya Tatu (3) (a) ya Paris inayozungumzia umuhimu wa kuwasilisha taarifa kwa ajili ya kujadiliwa Bungeni.<br>(xiv) Kwa kuwasilisha taarifa Bungeni, wananchi wanapata fursa ya kuielewa Tume na wajibu wake na kupata nafasi ya kuihoji pia. Aidha utoaji wa taarifa Bungeni kwa majadiliano ni fursa nyingine ya kuelimisha jamii ili kukuza, kuhifadhi na kutetea haki za binadamu na misingi ya utawala bora nchini. | | |
| | | (xv) Kabla ya ibara ndogo ya (2) iongezwe ibara ndogo nyingine ambayo itasomeka kama ifuatavyo.<br>(xvi) "(2) Tume itatoa taarifa Bungeni | (a) Tume ni chombo cha wananchi na kinapaswa kuwajibika kwa | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | kwa kujadiliwa si chini ya mara moja kwa mwaka kwa kupitia Kamati husika kuhusu utekelezaji wa majukumu yake yalioainishwa na katiba hii".<br>(xvii) Tume ya Uteuzi wa Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Makamishna.<br>(xviii) Iandikwe upya kama ifuatavyo: (1) Kutakuwa na Tume ya Uteuzi kwa madhumuni ya ibara hii ambayo itakuwa na wajumbe wafuatao:<br>1. Jaji Mkuu wa Mahakama ya Rufani;<br>2. Spika wa Bunge;<br>3. Jaji Mkuu wa Zanzibar;<br>4. Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar;<br>5. Jaji Mkuu wa Tanzania Bara;<br>6. Spika wa Bunge la Tanzania Bara;<br>7. Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ambaye atakuwa ndiye Katibu wa Kamati hii.<br>(xix) Kwa sababu ya unyeti wa majukumu ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, upo umuhimu wa kamati ya uteuzi au chombo cha uteuzi wa Makamishna hawa kuwa huru kwanza kibinafsi na pia kitaasisi.<br>(xx) Tume ya Utumishi inayopendekezwa kuwa ndiyo itakayoteua Makamishna wa Tume | wananchi hivyo wananchi wanapaswa kujua namna inavyotekeleza majukumu yake kwa kupitia kwa wawakilishi wao ambao ni wabunge.<br>(b) Pia hatua hii ni kuhakikisha uwepo wa uwazi na uwajibikaji wa Kitaasisi na Serikali katika kukuza, kulinda na kutetea haki za binadamu na misingi ya Utawala bora nchini.<br>(c) Uwasilishaji wa Taarifa Bungeni kwa kujadiliwa ni mojawapo ya masharti yaliyoainishwa na Kanuni za Paris (Paris Principles) ambazo ndio chimbuko la taasisi kama hizi ulimwenguni kote. | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | haiko huru kwani yenyewe iko chini ya Rais na kwa mantiki hiyo ni vigumu sana kuweza kuteua Makamishna bila kuwa na maslahi ya mamlaka iliyopo madarakani. Hii ni hatari kwa mustakabali wa Tume na hata uangalizi wa haki za binadamu na misingi ya utawala bora nchini.<br>(xxi) Aidha inapendekezwa kuwa ni vema kukawepo na Kamati Maalum ya Uteuzi yenye watu makini ambao watakuwa kwa ubinafsi wao ni huru na pia wapo huru kitaasisi kutokana na mchakato wa uteuzi wao ulivyo.Mchakato wa zamani wa uteuzi wa Makamishna unapendekezwa kuendelea ilimradi unazingatia mabadiliko yatakayoletwa na mfumo wa aina za serikali zitakazokuwepo. | | |
| 199. | Uwezeshaji wa nyenzo na rasilimali | *Uwezeshaji wa Nyenzo na Rasilimali Watu*<br>.(1) Serikali itahakikisha kuwa Tume ya haki za Binadamu na Utawala Bora inapatiwa fedha, nyenzo na rasilimali watu ya kutosha ili kulinda uhuru wake katika kutekeleza kazi na Majukumu yake kwa ufanisi.<br>(2) Katika kuhakikisha uhuru na ufanisi unaozungumziwa kwenye Ibara ya (1), fedha zote yaani, mishahara ya Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Makamishna, watumishi wote wa Tume na fedha kwa ajili ya utekelezaji wa | Kanuni za Paris zinataka Taasisi za namna hii kuwa huru kwenye kila nyanja na mojawapo ni uhuru wa kifedha ili kuweza kutekeleza majukumu yake ipasavyo.Kanuni ya Tano (5) ya Paris ambazo Baraza la Umoja wa Mataifa limeridhia ni kwamba Taasisi inapaswa kupewa fedha za kutosha (adequate | Ibara ya 199 inakuwa ibara ya 214 na inabaki kama ilivyo. |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | majukumu ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora zitoke kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina. | funding). Nanukuu kwa kimombo *"The national institution shall have an infrastructure which is suited to the smooth conduct of its activities, in particular adequate funding. The purpose of this funding should be to enable it to have its own staff and premises, in order to be independent of the Government and not be subject to financial control which might affect its independence".* Aidha uzoefu kwenye Taasisi nyingine Afrika na ulimwenguni umeonyesha kuwa utoaji wa fedha kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina ndiyo namna bora zaidi ya kutekeleza uhuru huu wa kifedha ili taasisi iweze kutekeleza majukumu yake kama yalivyoainishwa. Namna hii inatoa uhakika zaidi katika utendaji kazi wa Tume kwa ufanisi. | |

## 13.2 SEHEMU YA TATU:MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Maoni* | *Marekebiso ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| 200. | Uteuzi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali | (i) Ibara ya 200(1) irekebishwe na isomeke "Kutakuwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambaye atateuliwa na Rais." | (a) Tume ya Utumishi wa Umma ni mojawapo ya Taasisi zinazokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.<br>(b) Hivyo, kumpendekeza Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kutasababisha uwepo wa matakwa binafsi au mgongano wa kimaslahi.<br>(c) Aidha, CAG anapaswa sio tu kuwa huru bali kuonekana kuwa huru kwa mujibu wa Miongozo ya Umoja wa Mataifa.<br>(d) Hivyo, si sahihi kwa Tume ya Utumishi wa Umma kumpendekeza CAG. | Ibara ya 200 inakuwa ibara ya 215 na inabaki kama ilivyo. |
| | | (ii) Ibara ya 200(2) irekebishwe na isomeke "Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atashika wadhifa huo mara tu baada ya kuthibitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano na kuapishwa na Rais." | Ni muhimu Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za Serikali aapishwe kiapo cha kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria, uadilifu na kuilinda Katiba ya nchi | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebiso ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | na rasilimali zake. | |
| | | (iii) Ibara ya 200 ibadilishwe Mdhibiti Mkuu asithibitishwe na Bunge. | Awe huru, kwani Bunge nalo linakaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali | |
| 201. | Sifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali | (i) Ibara ya 201 irekebishwe kwa kufuta maneno “watumishi wa umma” na badala yake kuweka neno “Watanzania” | Kutoa haki sawa kwa Watanzania wote wenye sifa na uwezo wa kutekeleza majukumu ya Taifa katika nafasi ya Mdhibiti na Mkaguzi Muu wa Hesabu za Serikali ambao hawako katika Utumishi wa Umma. | 1. Ibara ya 201 inakuwa ibara ya 216<br><br>2. Imeongezwa aya (a) ambayo inasomeka “Awe raia wa Jamhuri ya Muungano.”<br><br>3. Imeongezwa kifungu (e) ambacho kinasomeka:<br><br>“Awe ni mtu ambaye hajawahi kutiwa hatiani kwa makosa ya ukwepaji wa kodi, rushwa, uhujumu uchumi, ubadhirifu, kutumia madaraka yake vibaya au kukosa uaminifu.” |
| | | (ii) Ibara ya 201(a) isomeke “awe amefuzu mafunzo ya juu ya uhasibu au fani yoyote inayohusiana na usimamizi wa fedha za umma na kusajiliwa na mamlaka husika.” | Mamlaka ya ukaguzi yamepanuka sana yakihusisha mambo zaidi ya ukaguzi wa hesabu kwa mfano ukaguyzi wa thamani ya fedha, mazingira, utambuzi, n.k. hivyo kubaki kama ilivyo katika Rasimu ni kuwanyima fursa Watanzania wengine wenye fani nyingine. | |
| | | (iii) Ibara ya 201(b) isomeke “ana uzoefu usiopungua miaka kumi na tano katika masuala yanayohusu usimamizi wa fedha za umma au ukaguzi wa hesabu.” | Maneno “katika utumishi wa umma” yanaleta ubaguzi na pia yanaondoa wigo mpana wa kupata Watanzania mahiri na waadilifu wanaoweza kutekeleza jukumu hili kwa ufanisi | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebiso ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | zaidi ambao hawapo katika Utumishi wa Umma. | |
| | | (iv) Ibara ya 201(c) ifutwe na badala yake isomeke "awe ni raia wa Tanzania wa kuzaliwa." | Ibara ya 201(b inajitosheleza na inajumuisha sifa zilizoainishwa kwenye Ibara ya 201(b) kama ilivyopendekezwa. Aidha, nafasi hii inapaswa kupewa mtu ambaye ni mzawa na asiwe pandikizi kutoka mataifa ya nje. | |
| | | (v) Ibara ya 201(c) irekebishwe kwa kufuta maneno "za Serikali". | | |
| 202. | Kazi na majukumu yake | (i) Jukumu la kuidhinisha kutolewa kwa fedha kutoka katika Mfuko Mkuu wa Hazina lisiwe jukumu la CAG kama ilivyoelezwa katika Ibara 202(1)(a). | CAG kama Mkaguzi wa Hesabu za Serikali atatakiwa kufanya ukaguzi wake katika hatua zote ikiwemo utaratibu uliotumika katika kuidhinisha matumizi ya fedha kutoka katika Mfuko Mkuu wa Hazina. Kwa hiyo akiidhinisha matumizi ya fedha kutoka katika mfuko huo atakuwa kama anajikagua mwenyewe | 1. Ibara ya 202 inakuwa ibara ya 217.<br>2. Ibara ndogo ya (1)(c) na zimerekebishwa na zinasomeka:<br><br>(c) angalau, mara moja kila mwaka, kufanya ukaguzi na kutoa taarifa juu ya ukaguzi wa hesabu:<br>(i) za Serikali ya Jamhuri ya Muungano;<br>(ii) zinazosimamiwa na watumishi wote wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano;<br>(iii) za Mahakama za Jamhuri ya Muungano; na<br>(iv) zinazosimamiwa na |
| | | (ii) Ibara ya 202(1) (c) irekebishwe kwa kumpa CAG mamlaka ya kufanya ukaguzi wa aina nyingine tofauti na ukaguzi wa hesabu kama atakavyoona inafaa. | Ukaguzi wa hesabu peke yake hautoshelezi kuimarisha uwajibikaji na thamani ya fedha katika kukusanya na | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebiso ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | kutumia rasilimali za umma. Hivyo, ni muhimu CAG kufanya kaguzi zingine zinazolenga kuleta tija kwa Taifa. | Katibu wa Bunge; na<br><br>3. Aidha Ibara ndogo ya (4) inasomeka: Kutayarisha ripoti ya mwaka na kuiwasilisha bungengi kwa ajili ya kujadiliwa na kutolewa mapendekezo.<br><br>4. Ibara ndogo ya (5) imerekebishwa na inasomeka kama ifuatavyo:-<br><br>"Baada ya kupokea taarifa hiyo, Rais atawaagiza watu wanaohusika wawasilishe taarifa hiyo kwenye kikao cha kwanza cha Bunge kitakachofanyika baada ya Rais kupokea taarifa hiyo na itabidi iwasilishwe katika kikao hicho kabla ya kupita siku saba tangu siku ile ulipoanza Mkutano huo, na iwapo Rais hatachukua hatua za kuwasilisha taarifa hiyo kwa Spika wa Bunge, basi Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali atawasilisha taarifa hiyo kwa Spika wa Bunge au kwa Naibu Spika iwapo nafasi ya madaraka ya Spika iko wazi, |
| | | (iii) Ibara ya 202(3) irekebishwe kwa kufuta maneno "Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kila mtumishi wa Serikali" na badala yake kuweka maneno "Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, mtumishi wa Serikali au mtu yeyote." | Kumpa uhuru CAG kuwatumia watu ambao wana utaalamu ambao si watumishi wa Ofisi ya CAG wa suala analolikagua kuweza kumsaidia kufanya ukaguzi wake. | |
| | | (iv) Ibara ya 202(8) isomeke:-<br>"Bunge linaweza kutunga sheria ya utekelezaji wa majukumu ya mdhibiti na mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali." | Maneno haya yanaweza kufungua mianya ya kutunga sheria itakayomkandamiza na kukinzana na uhuru wa CAG ulioainishwa katia Ibara ya 202(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano. | |
| | | (v) Majukumu ya udhibiti na ukaguzi wa hesabu za Serikali yatenganishwe. | (a) Udhibiti wa matumizi ya Serikali umeonyesha udhaifu mkubwa kama inavyodhihirishwa na ripoti za kila mwaka za Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali.<br>(b) Pesa zinazotengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebiso ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | zinachelewa kuwafikia watendaji. Hii imelalamikiwa sana katika Bunge na ni sababu mojawapo ya ucheleweshwaji wa utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa barabara. Hili ni suala la utekelezaji wa bajeti.<br>(c) Utekelezaji wa bajeti ya Serikali haujapewa umuhimu unaostahili katika ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali. Ripoti hizi zimejikita katika matokeo ya ukaguzi wa matumizi ambayo yamekwisha kufanyika baada ya muda mrefu, yaani mwaka. Udhibiti unaofanyika baada ya utendaji wa muda mrefu unakosa uharaka wa kuzuia udhaifu katika utekelezaji wa mipango na matumizi ya serikali; na<br>(d) Siyo rahisi kwa Mdhibiti na Mkaguzi | ambaye atawasilisha taarifa hiyo kwa Bunge." |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebiso ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | Mkuu kukosoa maamuzi ambayo anayafanya kuhusu udhibiti wa matumizi ya Serikali wakati akifanya kazi kwa kutumia kofia yake ya pili ya ukaguzi. Kunakuwepo mgongano wa wazi wazi wa maslahi ya muhusika.<br>(e) Hivyo, Sura ya 13, Sehemu ya 3 ya Rasimu ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ibadilishwe ili wawepo Mkaguzi Mkuu na Mdhibiti wa Bajeti.<br>Mdhibiti wa Bajeti:<br>(a) Ateuliwe na Rais kwa kupewa mapendekezo yaliyopatikana kwa njia ya uwazi na ushindani, na kuthibitishwa na Bunge;<br>(b) Sifa zake zifanane na zile za Mkaguzi Mkuu kama zilivyoanishwa katika aya ya 201 ya Rasimu; | |

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Maoni* | *Marekebiso ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| | | | (c) Kazi na majukumu yake viwe kama ilivyoainishwa katika aya ya 202 (1) (a), (b) na (2) ya Rasimu na aongezewe jukumu la kutoa taarifa kwa Bunge juu ya utekelezaji wa Bajeti kila baada ya miezi minne.<br>(d) Hii ina maana kuwa Mkaguzi Mkuu atabaki na kazi na majukumu yaliyoanishwa katika aya ya 201 (1), (c), (d) (2), (3), (6), (7) na (8); (4) na (5) ya aya hii vifutwe na badala yake kiwekwe kifungu cha kumtaka Mkaguzi Mkuu kutoa ripoti zake moja kwa moja kwa Bunge. | |
| 203. | Muda wa kukaa madarakani | (i) Ibara ya 203(1) isomeke "Muda wa kukaa madarakani kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za Serikali utakuwa ni kipindi cha miaka kumi mfululizo". | Katika Nyanja za kimataifa, kipindi cha CAG kuwa madarakani ni miaka mitano hadi kumi na tano, hivyo kipindi kinachopendekezwa cha miaka kumi ni sahihi. | Ibara ya 203 inakuwa ibara ya 218 na ibaki kama ilivyo. |
| | | (ii) Ibara ya 203(1) irekebishwe iwe vipindi viwili vya miaka mitatu mitatu. | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebiso ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| 204. | Kuondolewa madarakani | (i) Ibara ya 204 iboreshwe kwa kuongeze kipengele kinachohusu utaratibu wa kumwondoa kazini Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kama ilivyo katika Ibara ya 144(1)-(7) ya katiba ya Jamhuri ya Muungano ya 1977. | (a) Ni muhimu Katiba kutaja mazingira ambayo Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali ataondolewa madarakani.<br>(b) Awe huru, Tume ya Utumishi wa Umma nayo inakaguliwa na yeye. | 1. Ibara ya 204 inakuwa ibara ya 219.<br>2. Ibara ndogo ya (1)(a) sentensi imalizie na maneno "kama itakavyopendekezwa na taarifa ya daktari".<br>3. Aidha ibara ndogo ya (2) (3), (4) na (5) zimeandikwa upya na kusomeka kama ifuatavyo:<br><br>[(2) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anaweza kuondolewa katika madaraka ya kazi yake kwa sababu ya kushindwa kutekeleza kazi zake ama kutokana na maradhi au sababu nyingine yoyote au kwa sababu ya tabia mbaya, au kwa kuvunja masharti ya miiko na maadili ya Uongozi wa Umma na hataweza kuondolewa kazini isipokuwa kwa mujibu wa masharti ya ibara ndogo ya (4).<br>(3) Endapo Rais anaona kwamba suala la kumwondoa madarakani Mdhibiti na Mkaguzi |
| | | (ii) Ibara ya 204 1(d) na Ibara ya 204(1)(e) zifutwe. | Suala la maadili limeshazungumziwa kwa mapana kwenye kipengele cha Maadili na Miiko ya Uongozi ya Utumishi wa Umma, Sura ya Tatu kwenye Sehemu ya Kwanza inayozungumzia Maadili ya Viongozi wa Umma. | |
| | | (iii) Katika Ibara ndogo ya (2) maneno "Tume ya Utumishi wa Umma" yafutwe na badala yake iandikwe "Kamati Maalum itakayoundwa na Rais". | | |
| | | (iv) Katika Ibara ndogo ya (3) maneno "Tume ya Utumishi" yafutwe na badala yake iandikwe "Rais". | | |
| | | (v) Ibara ya 204(2), (3), (4) na (50 zifutwe na badala yake zisomeke:<br>"(2) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anawza kuondolewa katika madaraka ya kazi yake kwa sababu ya kushindwa kutekeleza kazi zake | Ibara hizi zinaondoa uhuru wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali wa kufanya kazi zake na zinaondoa maana ya Ibara zingine zote za | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebiso ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | kutokana na sababu zilizoainishwa katika Ibara ya 20 na Ibara ya 204(1) ya Katiba hii.<br>(3) Iwapo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atatakiwa kuondolewa katika madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya Ibara hii basi katika hali hiyo utaratibu utakuwa kama ifuatavyo:<br>(a) Rais atateua Tume maalum ambayo itakuwa na mwenyekiti na Wajumbe wengine wasiopungua wawili. Huyo Mwenyekiti na angalau nusu ya Wajumbe wengine wa Tume hiyo itabidi wawe watu ambao ni Majaji au watu waliopta kuwa Majaji wa Mahakama Kuu, Mahakama ya Rufani au Mahakama ya Juu katika nchi yoyote iliyomo kwenye jumuiya ya Madola;<br>(b) Tume hiyo itachunguza shauri lote na itatoa taarifa kwa Rais kuhusu maelezo ya shauri lote na itamshauri Rais kama huyo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali aondolewe kazini kwa mujibu wa masharti ya Ibara hii kwa sababu ya kushindwa kufanya kazi kutokana na masharti ya Ibara hii. | Rasimu hii zinazompa uhuru wa kufanya kazi bila ya kuingiliwa na mtu yeyote isipokuwa mahakama tu.<br><br>Hivyo basi, Ibara ya 144(2),(3) na (4) ya katiba ya sasa irudi kama ilivyo.<br><br>Aidha, taratibu za kumwondoa kazini CAG zishahabiane na taratibu za kuwaondoa kazini majaji wa Mahkama ya Rufani na Mahakama ya Juu oamoja na Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi kama ilivyoainishwa katika Rasimu. | Mkuu wa Hesabu za Serikali linahitaji kuchunguzwa, hivyo basi:<br>(a) Rais atateua Tume Maalum ambayo itakuwa na Mwenyekiti na Wajumbe wengine wasiopungua wawili, Mwenyekiti na angalau nusu ya wajumbe wengine wa Tume hiyo itabidi wawe watu ambao ni Majaji au watu waliopata kuwa Majaji wa Mahakama ya Juu, Mahakama ya Rufani au Mahakama Kuu za Nchi Washirika;<br>(b) Tume hiyo itachunguza shauri lote halafu itatoa taarifa kwa Rais kuhusu maelezo ya shauri lote na itamshauri Rais kama huyo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali aondolewe madarakani kwa mujibu wa masharti ya ibara hii kwa sababu ya kushindwa kufanya kazi kutokana na maradhi au sababu nyingine yoyote au kwa sababu ya tabia mbaya.<br>(4) Endapo Tume |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebiso ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | (4) Ikiwa Tume iliyoteuliwa kwa mujibu wa masharti ya Ibara ndogo ya (3) itamshauri Rais kwamaba huyo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu aondolewe kazini, basi Rais atamwondoa kazini.” | | iliyoteuliwa kwa mujibu wa masharti ya ibara ndogo ya (3) itamshauri Rais kwamba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali aondolewe madarakani kwa sababu ya kushindwa kufanya kazi kutokana na maradhi au sababu nyingine yoyote au kwa sababu ya tabia mbaya, basi Rais atamwondoa madarakani.<br>(5)Ikiwa suala la kumwondoa madarakani Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali limepelekwa kwenye Tume kwa ajili ya uchunguzi kwa mujibu wa masharti ya ibara hii, Rais anaweza kumsimamisha kazi huyo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, na Rais anaweza wakati wowote kufuta uamuzi huo wa kumsimamisha kazini, na kwa hali yoyote uamuzi huo utabadilika ikiwa Tume itamshauri Rais kwamba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa |
| | | (vi) Ibara hii ibadilishwe na iandikwe kama ilivyo Ibara ya 144 ya Katiba ya sasa. | Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali ndio inadhibiti na kukagua hesabu za Serikali, hivyo utaraibu wa kumuondoa Mdhibiti unapaswa kuwa wazi na ambao hautaathiri uhuru wake katika utendaji kazi zake. | |

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Maoni* | *Marekebiso ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| | | | | Hesabu za Serikali asiondolewe madarakani.] |
| 205. | Uwezeshaji wa nyenzo na rasilimali | (i) Ibara ya 205 isomeke:<br>"(a) Serikali kwa kupitia Bunge itahakikisha kuwa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi M kuu wa Hesabu za Serikali inapatiwa fedha, nyenzo na rasilimali watu ya kutosha ili kulinda uhuru wake katika kutekeleza kazi na majukumu yake kwa ufanisi;<br><br>(b) Kutakuwa na mfuko utakaojulikana kama Mfuko wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Jamhuri ya Muungano ambao utakuwa chini ya usimamizi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali;<br><br>(c) Mfuko wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali utatumika kwa ajili ya kugharamia shughuli za utawala na uendeshaji wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Jamhuri ya Muungano na shughuli zingine muhimu katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi | Kuipa ofisi ya CAG uwezo wa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa. | Ibara ya 205 inakuwa ibara ya 220 na inabaki kama ilivyo. |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebiso ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | Mkuu wa Hesabu za Serikali;<br><br>(d) Bunge litatunga sheria itakayoweka masharti kuhusu uendeshaji wa Mfuko wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Jamhuri ya Muungano." | | |
| | | (ii) Baada ya Ibara hii inapendekezwa kuwekwa Sura itakayoeleza Madaraka ya Umma. | Katika mfumo wa Serikali mbili, suala la Madaraka ya Umma ni muhimu kuelezwa katika Katiba. | |
| | | (iii) Inapendekezwa iandikwe kama ilivyo Sura ya Nne Ibara ya 145 na 146 ya Katiba ya sasa. | | |
| | | (iv) Kuwe na chombo kitakachosimamia maendeleo, hasa Tume ya Mipango. | | |
| | | (v) Ibara ya 206 ifutwe na badala yake iwekwe ibara ya 133 na 134 za Katiba ya jamhuri ya Muungano ya 1977 | | |

# SURA YA KUMI NA NNE YA RASIMU

## 14.0 MASHARTI KUHUSU FEDHA ZA JAMHURI YA MUUNGANO

### (a) Mfuko Mkuu wa Hazina na Fedha za Jamhuri ya Muungano

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Maoni* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| SURA YA KUMI NA NNE | Sura ya kumi nne (Ibara 206-218) Masharti kuhusu fedha za Jamhuri ya Muungano Inapendekezwa kwamba ibaki kama ilivyo | | | |
| 206. | Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano | (i) Maneno “zitakazopatikana kwa njia mbalimbali” yafutwe na kuweka maneno “fedha zote za Muungano zitawekwa kwa mujibu wa Ibara ya 215.” | | Ibara ya 206 inakuwa ibara ya 221 na inabaki kama ilivyo. |
| | | a) Ifanyiwe marekebisho kwa kufuta maneno “…zitakazopatikana kwa njia mbalimbali…” na kusomeka “…fedha zote za Muungano zitawekwa kwa mujibu wa Ibara 215,…”<br>b) Ibaki kama ilivyo<br>c) Ibara iondolewe na badala yake iwekwe Ibara ya 133 na 134 ya Katiba ya sasa ya Jamhuri ya Muungano kwa kuwa zinaendana na muundo wa serikali mbili. | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | d) Ibara hii ionyeshe wazi asilimia halisi ya mgawo wa wa fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina kwenda kwa washirika wa Muungano.<br>e) TAKUKURU ipewe nguvu ya kikatiba<br>f) Irekebishwe au kufutwa kabisa<br>g) Kuwe na ibara inayozungumzia wajibu wa kila mtu kulipa kodi na kuwajibisha serikali kukusanya kodi na kuwajibika katika matumizi yake.<br>h) Iishie…zitawekwa badala ya " isipokuwa"<br>i) kifungu (a) kiondolewe<br>j) Kifungu(b) kirekebishwe na kusomeka: " Taasisi za Serikali ya Shirikisho/ Muungano walioruhusiwa kwa mujibu wa sheria kukusanya fedha watawajibika kuomba fedha hizo kisheria kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina na Fedha za Shirikisho kwa ajili ya uendeshaji wa Taasisi hizo." | | |
| 207. | Masharti ya kutoa fedha za matumizi katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali | (i) Ibara ya 207(2) irekebishwe ili jukumu la kuidhinisha fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina au mifuko mingine ya Serikali lifanywe na mamlaka nyingine na si Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. | | Ibara ya 207 inakuwa ibara ya 222.<br>Ibaki kama ilivyo. |
| | | (ii) Ibara ndogo ya (2), ifanyiwe | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | marekebisho ili jukumu la kuidhinisha Fedha katika Mfuko Mkuu wa Hazina au mifuko mingine yoyote ya Serikali litekelezwe na Mamlaka nyingine tofauti na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. | | |
| | | (iii) Iongezwe Ibara mpya itakayoainisha masharti ya uhaulishaji wa fedha kutoka Serikali ya Muungano kwenda kwa Nchi Washirika na kinyume chake. | | |
| | | (iv) Kuwe na mfumo wa kitaasisi utakaosimamia utaratibu wa uchangiaji gharama za Muungano na mgawanyo wa mapato. | | |
| | | (v) Iongezwe Ibara ndogo katika itakayofafanua masharti ya Uhaulishaji wa Fedha kutoka Serikali ya Muungano kwenda kwa Washirika wa Muungano na kinyume chake. | | |
| | | (vi) Uwepo mfumo wa Kiasasi Kikatiba wa kuratibu uchangiaji wa gharama za Muungano na mgawanyo wa mapato. | | |
| | | (vii) Ibara ya 206 na 207 zibaki kama zilivyo. | | |
| | | (viii) Iongezwe Ibara mpya baada ya hii itakayofafanua masharti ya Uhaulishaji wa Fedha kutoka Serikali ya Muungano kwenda kwa Washirika wa Muungano na kinyume chake. | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| | | (ix) Kuwepo mfumo wa kitaasisi kwa ajili ya uhaulishaji wa mapato na kuratibu uchangiaji wa gharama za Muungano. | | |
| | | (x) Ibara ya 207(2) irekebishwe ili jukumu la kuidhinisha Fedha kutoka katika Mfuko Mkuu wa Hazina au Mifuko mingine yoyote ya Serikali litekelezwe na Mamlaka nyingine tofauti na ya Mdhibiti Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. | | |
| | | (xi) 207(2) iongezwe mwisho wa kifungu na isomeke: '…Hesabu za shirikisho za Seriakli ya Shirikisho la Tanzania.' | | |
| 208. | Utaratibu wa kuidhinisha matumizi ya fedha zilizomo katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali | (i) Ibara ya 208-Bunge likikataa kuidhinisha matumizi ya nyongeza, Serikali italazimika kujiuzulu. | | 1. Ibara ya 208 inakuwa ibara ya 223.<br>2. Ibara ndogo ya (2) neno kutawasilishwa lisomeke "Serikali itawasilisha" |
| | | (ii) Ibara ndogo ya (1) irekebishwe kwa kuondoa maneno "watu wanaohusika" na badala yake yawe Waziri wa Fedha. | | |
| | | (iii) 208(1) itaje ofisa wa serikali anayehusika ni Katibu Mkuu Kiongozi kwa sababu ni Mkuu wa Utumishi wa Umma | | |
| | | (iv) 208(1) itaje ofisa wa serikali anayehusika ni Katibu Mkuu Kiongozi kwa sababu ni Mkuu wa Utumishi wa Umma | | |
| | | (v) Ibara ndogo ianze na maneno, | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | "Rais atatoa maagizo kwa Katibu Mkuu Kiongozi kutayarisha na kuwasilisha kwenye Bunge…" | | |
| | | (vi) Ibara ibaki kama ilivyo | | |
| | | (vii) Ianishe wananchi kushirikishwa katika matayarisho ya bajeti ya serikali yao | | |
| | | (viii) Muswada wa sheria ya mapato na matumizi ya fedha ya serikali ya shirikisho la Tanzania. | | |
| 209. | Utaratibu wa kuidhinisha matumizi ya fedha kabla ya Sheria ya Matumizi ya Fedha za Serikali kuanza kutumika | (i) Ibara ndogo ya (1)- uidhinishaji wa fedha kutika Mfuko Mkuu wa Hazina unaofanywa na Rais uidhinishwe na Bunge. | | 1. Ibara ya 209 inakuwa ibara ya 224.<br>2. Ibara ndogo ya (1) neno "mpaka ipite miezi minne" lisomeke "ndani ya miezi minne".<br>3. Aidha ibara ndogo ya (2) maneno "Bunge linaweza kutunga" lisomeke "Bunge litatunga". |
| | | (ii) Ibara ya 209 iongezwe maneno "serikali za mitaa" baada ya maneno "Serikali Kuu". | | |
| | | (iii) Ibara hii irekebishwe ili kulipa Bunge mamlaka ya kupitisha bajeti ya mwaka unaofuata kabla ya mwaka wa fedha unaoishia kumalizikia. | | |
| | | (iv) Ibara hii ifutwe. | | |
| | | (v) Ibaki kama ilivyo | | |
| | | (vi) Bunge liwe na mamlaka ya kupitisha bajeti ya mwaka unaofuata kabla ya mwaka wa fedha unaoishia kumalizikia ili kuboresha mfumo wa matumizi wa fedha za Serikali. | | |
| | | (vii) Ibara ya 210(1) Katiba ielekeze kutungwa kwa sheria ya Bunge ambayo itadhibiti aina ya dharura zitakazijitokeza ili kuepusha ufisadi | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | (viii) 209. (1) Kuidhinisha matumizi kabla …… Asiachiwe mamlaka hayo Rais peke yake, yaidhinishwe na Bunge. | | |
| | | (ix) 209 (2) Bunge sio linaweza bali litatunga sheria …. | | |
| | | | | |
| 210. | Mfuko wa matumizi ya dharura | (i) Ibara ya 210 isomeke<br>(a) Mfuko wa matumizi ya Dharura;<br>(b) Mfuko wa Taifa wa Taasisi za Kiraia (NGO);<br>(c) Mfuko Rasmi wa Wakulima. | | Ibara ya 210 inakuwa ibara ya 225 na inabaki kama ilivyo. |
| | | (ii) Ibara ndogo ya (1) ielekeze kutungwa kwa sheria ya Bunge ambayo itadhibiti aina ya dharura zitakazijitokeza ili kuepusha ufisadi. | | |
| | | (iii) Ibara ya 210:<br>(a) Suala la dharura lihusishe Serikali ya Muungano na Washirika;<br>(b) Ibara ndogo ya (2) irekebishwe ili ngazi ya uidhinishaji wa matumizi ya dharura iwe ni Rais na Waziri Mkuu, kutegemea ukubwa wa dharura. | | |
| | | (iv) Ibaki kama ilivyo | | |
| | | (v) Suala la Dharura liwe linahusisha Serikali ya Muungano na Serikali za Nchi Washirika. | | |
| | | (vi) Iongezwe Ibara ndogo ya 210(4), ambayo itatoa ufafanuzi wa neno “Dharura” na mipaka yake. Aidha, | | |

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Maoni* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| | | Sheria itakayohusika itaje vyanzo vya mapato ya Mfuko huo. | | |
| | | (vii) Ibara 210(2) irekebishwe ili ngazi ya uidhinishaji wa Matumizi ya Dharura iwe Rais na Waziri mwenye dhamana ya Fedha kwa kuzingatia kiwango cha Dharura. | | |
| | | (viii) Ibara ya 210(1) Katiba ielekeze kutungwa kwa sheria ya Bunge ambayo itadhibiti aina ya dharura zitakazijitokeza ili kuepusha ufisadi | | |
| 211. | Mishahara ya baadhi ya watumishi kudhaminiwa na Mfuko Mkuu | (i) Ibara ya 211(5) irekebishwe kwa kuongeza maneno "Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali" kati ya maneno "Mjumbe wa Tume ya Haki za Binadamu" na maneno "na Watumishi wengine." | CAG ni kiongozi mwenye majukumu ya kuhakikisha kuwa mapato na matumizi ya rasilimali za umma zinatumika ipasavyo ndani ya Serikali.<br><br>Ili kiongozi huyo aweze kufanya kazi vizuri bila vikwazo vya namna yoyote ni lazima awe na uhakika wa upatikanaji wa maslahi yake kama ilivyo kwa viongozi wengine wa taasisi zinazotakiwa kuwa huru kama Mahakama.<br><br>Aidha, utaratibu huu si mpya kwani upo kwenye Katiba ya sasa na hata | 1. Ibara ya 211 inakuwa 226.<br>2. Ibara ndogo ya (5) mbele ya maneno "Tume ya Haki za Binadamu" yaongezwe maneno "Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali" |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | nchi jirani kama Uganda zina utaratibu huo. | |
| | | (ii) Ibara ya 211(5) –ihusishe wakuu wa Tume zote na taasisi za Serikali zinazojitegemea. | Ili wawe na imani na hivyo kuwa huru katika kutimiza majukumu yao. | |
| | | (iii) Katika ibara ndogo ya (5) aongezwe Mwenyekiti na wajumbe wa Tume ya utumishi wa Umma. | Wana majukumu nyeti na mazito. | |
| | | (iv) Ibara ndogo ya (5) iongezwe maneno "Jaji wa Mahakama Kuu na Mdhibiti Mkuu wa Serikali". | | |
| | | (v) Ibaki kama ilivyo isipokuwa 211(5) Iongeze Jaji wa Mahakama Kuu na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali | | |
| | | (vi) Ibaki kama ilivyo isipokuwa 211(5) Iongeze Jaji wa Mahakama Kuu na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali | | |
| | | (vii) Kuwe na masharti kuhusu ulipaji wa mishahara na posho kutokana na hali halisi ya Mtanzania | | |
| | | (viii) 211. (5) Ihusishe wakuu wa Tume zote na taasisi za Serikali zinazojitegemea ili wawe na imani na hivyo kuwa huru katika kutimiza majukumu yao. | | |
| | | (ix) Ibara ndogo ya (1) na (2) watumishi wanaodhaminiwa na Mfuko Mkuu watajwe na viwango wanacholipwa. | Kuondoa mgongano wa malipo na posho kwa watumishi wa umma | |
| | | (x) Ibara ndogo ya (1) na (2) | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | zirekebishwe ili watumishi wote walipwe kupitia Mfuko Mkuu wa Serikali. | | |

### (b) Deni la Taifa na Mikopo ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano

| Ibara Na. | Kichwa cha habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| 212. | Deni la Taifa | (i) Ibara ya 212(2) irekebishwe kwa kuongeza maneno "likihusisha deni la ndani na nje" baada ya maneno "deni lenyewe" na kufuta maneno "fedha zinazowekwa kwa ajili ya kulipa deni kwa awamu". | Kuhakikisha kuwa maelezo kuhusu deni la Taifa yanakidhi hali halisi ya deni hilo. | 1. Ibara ya 212 inakuwa ibara ya 227.<br><br>2. Ibara ndogo ya (2) imerekebishwa ili kuweka tafsiri ya deni la Taifa ambayo itajumuisha deni la serikali ya Jamhuri ya Muungano pamoja na deni lolote litakalodhaminiwa na serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. |
| | | (ii) Ibara ndogo ya (2) ifafanue maana ya deni la Taifa na isomeke kama ifuatavyo-<br>"deni lenyewe na pia riba inayolipwa juu ya deni hilo, malimbikizo ya deni na gharama zote zinazoambatana na usimammzi wa deni hilo. Kwa madhumuni ya Ibara hii, Deni la Taifa linajumuisha Deni la Serikali ya Muungano na madeni ya Serikali za Washirika wa Muungano yaliyodhaminiwa na yasiyodhaminiwa na Serikali ya Muungano." | | |
| | | (iii) Serikali isichukue mikopo yenye riba. | | |
| | | (iv) usimamizi wa "Deni la Taifa" ushirikishe pande zote | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | zinazohusika (Washirika). | | |
| | | (v) Aya ya (a) ifutwe. | (a) Shirikisho halina bidhaa kama chanzo cha mapato.<br>(b) Bidhaa za chanzo cha mapato zipo kwenye nchi Washirika. | |
| | | (vi) Ibara hii irekebishwe ili kila nchi iruhusiwe kukopa kwa mujibu wa haja na matumizi yake. | Shirikisho lisikope litachangiwa na nchi Washirika. | |
| | | (vii) Kuwe na tafsiri ya deni la Taifa | | |
| | | (viii) Ibaki kama ilivyo | | |
| | | (ix) Madeni ya Serikali ya Muungano yabaki kwake baada ya kuanza kutumika Katiba Mpya. | | |
| | | (x) Irekebishwe na kutaja; 'Deni la Serikali ya Shirikisho tu'. Ikizingatia mchango na tija ya mkopo wa deni hilo kwa mshirika husika. | | |
| | | (xi) Serikali isichukue mikopo yenye riba. | | |
| | | | | |
| 213. | Mamlaka ya kukopa ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano | (i) Serikali isichukue mikopo yenye riba. | | 1. Ibara ya 213 inakuwa ibara ya 228.<br>2. Imeongezwa ibara ndogo ya (2)(b) ambayo inasomeka: "itaweka ukomo wa deni la Taifa na madhumuni ya deni hilo" |
| | | (ii) Maelezo ya pembeni yabadilishwe na badala yake yasomeke "mamlaka ya kukopa na kulipa ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania". | | |
| | | (iii) Ibara ndogo ya (2) iandikwe: "(2) Bunge litatunga sheria ambayo:" | | |
| | | (iv) Ibara hii ifutwe | Shirikisho lisikope. | |

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Maoni* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| | | (v) Marginal note iboreshwe na isomeke “mamlaka ya kukopa na kulipa ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania” | | |
| | | (vi) Iwe ni jukumu la Serikali kulipa madeni na ulipwaji uwe wa wazi. | | |
| | | (vii) Taarifa za madeni yaliyolipwa na yaliyosamehewa ichapishwe kwenye gazeti la Serikali na pia ijadiliwe Bungeni. | | |
| | | (viii) Isomeke; “ kwa azimio maalum la Bunge linaweza kuizuia serikali kukopa endapo litaona kuwa kuna haja…” | | |
| | | (ix) Bunge liridhie mikopo kabla haijachukuliwa na serikali | | |
| | | (x) Neno “linaweza “ libadilishwe liwe “Bunge litatunga sheria ambayo…” | | |
| | | (xi) Katika ibara ya 213(2)(a) yaongezwe maneno “…na kuidhinisha ukopaji huo” | | |
| | | (xii) Pawepo kifungu kidogo kinachozungumzia udhibiti wa mikopo likiwemo sharti la kufanya uchambuzi wa mikopo kijinsia | | |
| | | (xiii) Bunge liweke utaratibu utakaofuatwa kwa mshirika kudhaminiwa na serikali ya shirikisho | | |
| | | (xiv) Kuwe na utaraibu wa washirkia kunufaika na mikopo ya shirikisho | | |
| | | | | |

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Maoni* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| 214. | Mamlaka ya Kukopa fedha kwa Serikali za Washirika wa Muungano | (i) Ibara ya 214 (1) na (2) iangaliwe vizuri ili kuepuka utegemezi wa Nchi Mshirika mmoja kwa mwingine. | | Ibara ya 214 inakuwa ibara ya 229 na ibaki kama ilivyo. |
| | | (ii) Ibara 214(1) itamke wazi kuwa deni la mshirika mmoja wa muungano halitaihusu Jamhuri ya Muungano. | | |
| | | (iii) Ibara ya 214 (2) ifanyiwe marekebisho ili-<br>(a) jukumu la kudhamini mikopo kwa Washirika wa Muungano liendane na uwezo wa kimapato wa Serikali ya Muungano.<br>(b) utaratibu wa kutoa dhamana ushirikishe Washirika wote na si Mshirika mmoja mmoja. | | |
| | | (iv) Ibara ya 214 (3) irekebishwe kwa kuongeza maneno "ilimradi Serikali Mshirika itakayodhaminiwa iwajibike kwa Serikali ya Muungano." Mwishoni mwa Ibara hiyo. | | |
| | | (v) Ibara hii ifutwe. | Inahusu uwepo wa Serikali Tatu. | |
| | | (vi) Ibara hii irekebishwe ili Bunge lipewe mamlaka ya kutunga Sheria kwa ajili ya kuweka utaratibu mzuri ambao utaainisha mfumo, viwango na sera ya serikali juu ya kudhamini nchi washirika wanapokopa. | | |
| | | (vii) Bunge lipewe mamlaka ya kuamua juu ya uwezekano wa | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | Serikali kusaidia serikali za washirika, pale inapotokea kuwa serikali za washirika zimeshindwa kulipa deni na sababu ya kufanya hivyo ikiwa imetolewa rasmi na baada ya Bunge kuijadili sababu hiyo kuwa ni kweli kuna haja ya Serikali kusaidia serikali za washirika katika kulipa deni husika. | | |
| | | (viii) Ibara ya 214:<br>(a) Ifanyiwe marekebisho kwa kuzingatia muundo wa serikali mbili.<br>(b) Tume ya Mipango iundwe kikatiba na majukumu yake yaainishwe;<br>(c) Kuwe na Ibara itakayoweka masharti kuhusu uchumi, mipango na fedha za Jamhuri ya Muungano. | | |
| | | (ix) Ibara ndogo ya (2) neno "inaweza" lisomeke "inawajibika". | Kutoa fursa kwa nchi Washirika kutekeleza mahitaji yake bila ya taabu. | |
| | | (x) Ibara ndogo ya (4) irekebishwe ili kuweka uwazi wa mikopo kwa ajili ya Serikali za Washirika na taarifa za mikopo zichapishwe katika magazeti. | Ili wananchi waweze kufahamu. | |
| | | (xi) Utaratibu wa kutoa dhamana kwa mujibu wa Ibara 214(2) ushirikishe Washirika wote wa Muungano badala ya kushirikisha Mshirika mmoja mmoja. | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | (xii) Ibara 214(2) inayohusu Tafsiri ya ya Deni la Taifa ifanyiwe marekebisho kama ifuatavyo:- Kwa kuondoa maneno “fedha zinazowekwa akiba kwa ajili ya kulipa deni kwa awamu” na badala yake kuweka maneno “malimbikizo ya madeni”. Na mwisho kuongeza maneno “na kwamba kwa madhumuni ya Ibara, Deni la Taifa linapewa tafsiri kuwa ni Deni la Serikali ya Muungano na madeni ya Serikali za Washirika wa Muungano yaliyodhaminiwa na yasiyodhaminiwa na Serikali ya Muungano”. | | |
| | | (xiii) Usimamizi ya Deni la Taifa ufanyike Kimuungano kwa kuwashirikisha Washirika. | | |
| | | (xiv) Iondolewe | | |
| | | (xv) Tume ya Mipango ianzishwe kikatiba | | |
| | | (xvi) Bunge lipewe mamlaka ya kutunga Sheria kwa ajili ya kuweka utaratibu mzuri ambao utaainisha mfumo, viwango na sera ya serikali juu ya kudhamini nchi washirika wanapokopa. | | |
| | | (xvii) Bunge lipewe mamlaka ya kuamua juu ya uwezekano wa Serikali kusaidia serikali za washirika inapohitajika | | |
| | | (xviii) Nchi Washirika wa Muungano zitakuwa na mamlaka ya | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | kukopeshana fedha kwa makubaliano | | |
| | | (xix) Serikali ya Jamhuri ya Muungano itakuwa na mamlaka ya kudhamini mikopo ya washirika wa muungano | | |
| | | (xx) Katiba iunde kamati maalum kuidhinisha mikopo ya serikali ya muungano, kuidhinisha matumizi ya dharurana kuchanganua na kuhimiza michango ya Washirika wa Muungano kwenda Serikali ya Muungano. | | |
| | | (xxi) Kamati hiyo iwe na wajumbe wafuataao:<br>(i) Waziri mwenye dhamana ya fedha wa serikali ya Muungano ambaye atakuwa Mwenyekiti;<br>(ii) Mawaziri wenye dhamana ya mambo ya fedha wa washirika wa Muungano. | | |
| | | (xxii) Serikali ya Jamhuri ya Muungano isikope fedha kwa matumizi ya kawaida(recurrent expenditure) | | |
| | | (xxiii) Ibara ya 214(3) iongezwe maneno '…kuzingatia kiwango cha michango na madeni yaliyopo ya mshirika muombaji" | | |
| | | | | Imeongezwa ibara mpya ya 230 inayozungumzia "masharti ya kutoza kodi." |

## (c ) Vyanzo vya Mapato ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| 215. | Vyanzo vya mapato vya Serikali ya Jamhuri ya Muungano | (i) Maelezo ya pembeni isomeke "Mikopo na misaada kutoka ndani na nje ya Jamhuri ya Muungano". | | 1. Ibara ya 215 inakuwa ibara ya 231.<br>2. Ibara ndogo (b) neno "maduhuli" lisomeke "mapato yasiyo ya kodi" |
| | | (ii) Vyanzo vya mapato katika Ibara ya 215 viongezwe kwa kujumuisha gawio la benki Kuu, misaada isiyo na masharti na mapato ya Muungano yasiyo ya kodi. | Kwa kuzingatia mfumo wa Serikali mbili unaopendekezwa hii ni sehemu ya maafikiano ya kuondosha kero za Muungano. | |
| | | (iii) Vyanzo vilivyoainishwa, licha ya kuwa si vya wazi, pia si vya uhakika. Ufafanuzi unahitajika na pia utaratibu muafaka kuwekwa;<br>(iv) Utaratibu wa kukusanya ushuru wa bidhaa ueleweke kwa kuwa ushuru utatokana na biashara ya ndani na nje ya serikali za Washirika. Hii inaweza kuwa chanzo cha kero;<br>(v) Kanuni ya Washirika kuchangia gharama za Muungano itengenezwe kitaalamu na vigezo vyake viwe wazi. | | |
| | | (vi) Ibara ya 215:<br>(a) Chanzo cha aya ya (a) si cha uhakika sana, vitafutwe vyanzo vyenye uhakika zadi.<br>(b) wigo na mipaka ya utozaji wa ushuru wa bidhaa viwekwe bayana;<br>(c) aya ya (c) ifutwe na vitafutwe vyanzo vingine vya mapato. Kama vile kodi ya mapato, ushuru wa forodha, n.k. | Ni bidhaa zisizo za lazima. | |

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Maoni* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| | | (vii) Ibara ya 215-ushuru wa bidhaa usiwe chanzo cha mapato ya Muungano. Ni vyema Serikali ya Muungano kuwa katika mfumo wa kuchangiwa na Serikali za nchi washiriki. Mapato ya ziada ni yale yatakayotokana na maduhuli ya taasisi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano. | Ili azma nzuri ya kuziimarisha nchi washiriki ifikiwe kwa haraka. | |
| | | (viii) Masuala ya mapato yawe kama yavyoonyeshwa kwenye nyongza namba 16 ya mambo ya Muungano. | | |
| | | (ix) Kuhusiana na gharama za Muungano<br>(a) utaratibu wa kugharamia Mambo ya Muungano uliopendekezwa kwenye Rasimu ya Katiba, utaratibu huu unakubalika.<br>(b) Chanzo cha mapato kutokana na Ushuru wa Bidhaa kinategemea matumizi ya bidhaa zisizo za lazima. Chanzo hiki kinaweza kuathirika iwapo hali ya uchumi itatetereka. Hivyo, kiangaliwe upya ili Mambo ya Muungano yagharamiwe na vyanzo vyenye uhakika zaidi.<br>(c) Wigo na mipaka ya utozaji wa Ushuru wa Bidhaa ufafanuliwe.<br>(d) Suala la kuzitaka Serikali | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | Shiriki kuchangia Gharama za Muungano, kwa mujibu wa Ibara 215 (c), linaweza kudhoofisha Mapato ya Serikali ya Muungano, iwapo Serikali Shiriki zitakuwa na hali mbaya ya kimapato. Hivyo, Kifungu hicho kifutwe na badala yake vitafutwe vyanzo vingine vya mapato, kwa mfano Kodi ya Mapato, Ushuru wa Forodha n.k.<br>(e) Maduhuli kama chanzo cha Mapato ya Muungano kinahitaji kufafanuliwa.<br>(f) Ibara 215(d) irekebishwe kwa kujumuisha Misaada isiyo na masharti. | | |
| | | (x) Aya (a) iandikwe "ushuru wa bidhaa na huduma". | | |
| | | (xi) Aya (b) ya yaongezwe maneno "kulingana na Sheria zitakazopitishwa na Bunge". | | |
| | | (xii) Aya (c) ifutwe. | | |
| | | (xiii) Ibara ya 215(c) ifafanuliwe kuwa michango itakuwa kwa misingi ya uwiano. | Kuepuka malalamiko toka kwa Washirika. | |
| | | (xiv) Iongezwe ibara ndogo mpya ambayo itatamka kuwa Bunge litatunga Sheria ambayo itaweka utaratibu mzuri wa serikali za washirika kuchangia asilimia kadhaa kwa ajili ya Serikali ya Shirikisho. | | |
| | | (xv) iongezwe Ibara ndogo ya (e) | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | inayosomeka kama ifuatavyo:- “mauzo ya rasilimali asili kama vile gesi/mafuta, madini, mazao ya baharini, wanyama, misitu, ushuru utokanao na kukodishwa kwa ardhi/uwekezaji”. | | |
| | | (xvi) Aya ya (a) na (d) zifutwe<br>(a) Ushuru wa bidhaa uwe chini ya nchi Washirika kwani ndio njia mama ya kupata na kutoa mchango kwa Shirikisho.<br>(b) Kuondoa usumbufu kwa wananchi kulipa ushuru mara mbili. | | |
| | | (xvii) Ibara hii ifutwe.<br>Vyanzo vya mapato viachiwe nchi Washirika, kasha nchi Washirika ndio wachangie Shirikisho. | | |
| | | (xviii) Aya (d) liongezwe neno “na misaada”. | Kuongeza mapato ya Muungano. | |
| | | (xx) Aya (a), (b) na (d) zifutwe. | Chanzo kikuu kiwe ni michango ya Washirika. | |
| | | (xxi) Ibara 215(b) ifafanuliwe kwa mapana kwa kuainisha aina za Taasisi zinazohusika. | | |
| | | (xxii) Iongezewe maneno: “Kulingana na Sheria zitakazopitishwa na Bunge.” | | |
| | | (xxiii) Isomeke, “mauzo ya rasilimali asili kama vile gesi/mafuta, mazao ya baharini, wanyama, misitu, ushuru utokanao na kukodishwa kwa ardhi/uwekezaji.” | | |
| | | (xxiv) Chanzo cha mapato kutokana | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | na Ushuru wa Bidhaa kinategemea matumizi ya bidhaa zisizo za lazima. | | |
| | | (xxv) Wigo na mipaka ya utozaji wa ushuru wa bidhaa ufafanuliwe. | | |
| | | (xxvi) Suala la kuzitaka Serikali Shiriki kuchangia Gharama za Muungano, kwa mujibu wa Ibara 215 linaweza kudhoofisha Mapato ya Serikali ya Muungano, iwapo Serikali Shiriki zitakuwa na hali mbaya ya kimapato. | | |
| | | (xxvii) Maduhuli kama chanzo cha Mapato ya Muungano kinahitaji kufafanuliwa. | | |
| | | (xxviii) Ibara 215(d) irekebishwe kwa kujumuisha Misaada isiyo na masharti. | | |
| | | (xxix) 215(d) isomeke ushuru wa bidhaa na huduma | | |
| | | (xxx) 215(d) isomeke, 'mikopo na misaada kutoka ndani na nje ya Jamhuri ya Muungano | | |
| | | (xxxi) Vyanzo vya mapato viongezwe vikiwemo<br>i. gawio la Benki Kuu;<br>ii.misaada isiyo na masharti na;<br>iii.mapato yasiyo ya kodi. | | |
| | | (xxxii) Pawekwe ibara ndogo ambayo itatamka kuwa Bunge litatunga Sheria ambayo | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | itaweka utaratibu mzuri wa serikali za washirika kuchangia asilimia kadhaa kwa ajili ya Serikali ya Shirikisho | | |
| | | (xxxiii) Pawekwe ibara ndogo ambayo itatamka kuwa Bunge litatunga Sheria ambayo itaweka utaratibu mzuri wa serikali za washirika kuchangia asilimia kadhaa kwa ajili ya Serikali ya Shirikisho | | |
| | | (xxxiv) Mchango kutoka kwa Washirika wa Muungano uwe 50/50 kama ilivyo katika masuala mengine | | |
| | | (xxxv) Kuwe na chanzo cha mapato kilicho chini ya madaraka ya serikali ya shirikisho yenyewe, na yaliyobaki yategemee ruzuku kutoka nchi za nje na vyanzo vingine vilivyotajwa kwenye ibara hii | | |
| | | (xxxvi) Ielezwe kuwa pia serikali ya shirikisho inaweza kuwasaidia washirika wa muungano na viwango vya mchango vitategemea makubaliano kati ya serikali tatu. | | |
| | | (xxxvii) Ushuru wa bidhaa usiwe chanzo cha mapato ya muungano | | |
| | | (xxxviii) Kuwe na mfumo wa | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | kuchangia serikali ya muungano kutoka nchi washirika na mapato ya maduhuli kutoka kwa taasisi za muungano. | | |
| | | (xxxix) 215(a) iongezwe, na huduma zitokanazo na Taasisi za Shirikisho la Tanzania' | | |
| | | (xl) iongezewe…asilimia 50 kwa 50 kwa kila mshirika wa shirikisho ambazo zitatolewa kwa muda utakaokubaliwa. | | |
| | | (xli) iongezewe…katika maeneo ya mambo ya shirikisho | | |
| | | (xlii) Benki Kuu | | |
| 216. | Manunuzi ya umma | (i) 216(1) irekebishwe ili Katiba itoe agizo la Bunge kutunga sheria kali au kuboresha iliyopo dhidi ya Ufisadi katika manunuzi ya Umma. | | 1. Ibara ya 216 inakuwa ibara 232.<br>2. Marginal Note imefanyiwa marekebisho na inasomeka "Ununuzi ya Umma" . |
| | | (ii) Ibara ya 216 irekebishwe ili kuongeza masharti ya jukumu la "usimamizi wa mali za umma" na udhibiti wa matumizi mengine ya umma. | | |
| | | (iii) Linaongozwa kwa misingi ya sheria, kanuni na taratibu za utekelezaji, liondolewe. | Halihitaji mwongozo wa Kikatiba. | |
| | | (iv) Ibara hii irekebishwe ili Jukumu la Manunuzi ya Umma lijumuishe pia Usimamizi wa Mali za Umma | | |
| | | (v) Udhibiti wa matumizi mengineyo ya umma lijumuishwe kwenye Katiba. | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | (vi) Iondolewe | | |
| | | (vii) Utaratibu wa 'value for money' uwekwe wazi na iwe ni marufuku kwa manunuzi yoyote makubwa kufanyika mfano kabla ya bajeti yake kuidhinishwa na Bunge. | | |
| | | (viii) Katiba itoe agizo la Bunge kutunga sheria kali au kuboresha iliyopo dhidi ya Ufisadi katika manunuzi ya Umma | | |

### (d) Benki Kuu

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| 217. | Benki Kuu ya Jamhuri ya Muungano | (i) Suala la manunuzi ya umma linaongozwa kwa misingi ya sheria, kanuni na taratibu za utekelezaji, hivyo liondolewe. | Halihitaji mwongozo wa Kikatiba. | Ibara ya 217 inakuwa ibara ya 233 na inabaki kama ilivyo. |
| | | (ii) Ibara ya 217 itoe mamlaka kwa Benki Kuu kuzuia biashara nchini kufanyika kwa fedha ya nje, isipokuwa tu pale inapobidi. | Ili kulinda thamani ya fedha yetu na uchumi kwa ujumla | |
| | | (iii) Ibara ya 217 irekebishwe na kuongezewa masharti ya Gavana na Manaibu Gavana pamoja na utaratibu wa upatikanaji wao, majukumu yao na muda wao wa kukaa madarakani. | Benki Kuu ni chombo muhimu kwa Taifa lolote, hivyo viongozi wake ni muhimu kutajwa. | |
| | | (iv) Aya (d) ya Ibara ndogo ya (1) ifutwe. | Ili kudhibiti usimamizi mzuri wa mzunguko wa sarafu na fedha. | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | (v) Iongezwe ibara mpya mbili ambazo zieleze mambo yafuatayo:<br>(a) Kuhusu malipo yote nchini yafanyike kwa kutumia sarafu tofauti za fedha za kigeni.<br>(b) Kuhusu jukumu mojawapo la benki kuu liwe ni kudhibiti mfumuko wa bei. | | |
| | | (vi) Ibara ya 217(1) iongezewe aya mpya ya (e) itakayokuwa na maneno "kuandaa na kusimamia sera za kifedha na sera za kibajeti." | Haya ni majukumu mazito katika kulinda uchumi wa nchi, hivyo ni muhimu yake kwenye taasisi yenye uhuru wa kiutendaji kama Benki Kuu. | |
| | | (vii) Ibara ndogo ya (2) irekebishwe na ieleze kwamba Benki Kuu haitaingiliwa na mtu yeyote katika utekelezaji wa majukumu yake isipokuwa Bunge. | | |
| | | (viii) Iongezwe ibara ndogo mpya itakayoeleza kwamba taarifa za utekelezaji wa kazi za Benki Kuu zitajadiliwa na Bunge angalau mara moja kila mwaka wa fedha na kwa kadiri itakavyoonekana sahihi kufanya hivyo. | | |
| | | (ix) Ibara hii ifutwe na badala yake iandikwe kama ifuatavyo:<br>217(1) Kutakuwa na Benki Kuu ya Jamhuri ya Muungano waTanzania itakayojulikana | (a) Jukumu la msingi la Benki Kuu popote duniani ni utayarishaji na utekelezaji wa sera za | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | kuwa "Benki Kuu " ambayo itakuwa na majukumu yafuatayo:<br>(a) Kutayarisha na kutekeleza sera za fedha;<br>(b) kutoa sarafu, kudhibiti na kusimamia mzunguko wa sarafu;<br>(c) kuandaa na kusimamia Sera na Mipango inayohusiana na sarafu;<br>(d) kudhibiti na kusimamia masuala ya fedha za kigeni;<br>(e) kutunza akaunti za fedha za Serikali husika.<br>(f) Kusimamia mabenki na taasisi za fedha nchini kwa mujibu wa Sheria zitakazopitishwa; na<br>(g) Kutoa ushauri kwa Serikali ya Muungano na zile za Washirika kuhusu masuala ya kiuchumi na fedha.<br>(2) Katika utekelezaji wa majukumu yake, Benki Kuu itakuwa huru na haitaingiliwa ama kwa kupewa maelekezo au kudhibitiwa na mtu au mamlaka yoyote.<br>(3) Bunge litatunga sheria itakayoweka masharti kuhusu muundo wa Benki Kuu itakayozingatia shughuli na utendaji wa Benki Kuu." | fedha. Hivyo jukumu hili linabidi libaki kuwa la Benki Kuu ya Muungano.<br>(b) Benki Kuu ndiyo chanzo pekee cha ukwasi (Liquidity) nchini kwa vile ndio taasisi iliyo na uwezo wa kuchapisha na kutoa sarafu ya Tanzania. Mahitaji ya Serikali ya ukwasi kupitia mkopo (advances) kila mwezi ni makubwa kwa vile matumizi yake kwa kawaida huwa lazima yafanyike kabla ya makusanyo ya mapato.<br>(c) Utekelezaji wa majukumu ya Benki Kuu, kwa mfano sera za fedha, zinazojumuisha kusimamia fedha za kigeni, kusimamia kiwango cha riba, ujazi wa fedha na mfumuko wa bei, ukiwa chini ya zaidi ya chombo kimoja unaweza kuleta utata | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | katika usimamizi. Mathalani, huwezi kuwa na misimamo tofauti inayohusu mwelekeo wa riba au ujazi wa fedha kwenye eneo au uchumi ambapo sarafu moja inatumika. Utaratibu unaotumika Marekani na Uswiss ni mifano mizuri ya hoja hii. | |
| | | (x) Katika Ibara za 217 na 216 majukumu yanayoainishwa katika Ibara hizi yanagongana na majukumu ya sasa ya Benki. | Kuna mgongano wa majukumu. | |
| | | (xi) Ibara hii ifutwe. | (a) Suala la uchumi sio suala la Muungano hivyo kila nchi Washirika iwe na Benki Kuu yake.<br>(b) Kila Nchi Washirika ijipangie mambo yake ya kiuchumi.<br>(c) Uchumi sio suala la Muungano.<br>(d) Uchumi wa nchi mbili unatofautiana, Zanzibar inategemea huduma na Tanganyika inategemea rasilimali.<br>(e) Uchumi wa nchi mbili | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | ni wa ushindani.<br>(f) Uchumi wa nchi unategemea Benki ambayo ndio muhimili mkubwa wa mapato.<br>(g) Kuzuia mfumuko wa bei. | |
| | | (xii) Iongezwe aya mpya (e) katika ibara ndogo ya (1) itakayosema "(e) kuandaa na kusimamia sera za kibajeti". | Kuongeza wigo wa wataalam wa bajeti katika Benki Kuu. | |
| | | (xiii) Isomeke: "Kutakuwa na "Benki Kuu " ambayo itakuwa na majukumu yafuatayo:<br>i. Kutayarisha na kutekeleza sera za fedha;<br>ii. kutoa sarafu, kudhibiti na kusimamia mzunguko wa sarafu; | | |
| | | (xiv) Kuwe na sarafu na Benki Kuu moja | | |
| | | (xv) Kuwepo bodi maalum ya kudhibiti pesa zote za Nchi Washirika | | |
| | | (xvi) Benki Kuu iwe na mamlaka ya kusimamia Benki zote | | |
| | | (xvii) Utaratibu wa sasa uendelee | | |
| | | (xviii) Ibara iongezewe kipengele (e) chenye maneno,"kuandaa na kusimamia sera za kifedha na sera za kibajeti." | | |
| | | (xix) Nchi washirika zisiruhusiwe kumiliki "Benki Kuu" zao hii ni hatari katika kudhibiti | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | mzunguko wa sarafu na usimamizi mzima wa maswala ya fedha. | | |
| | | (xx) | Ibara ya 217 iboreshwe na paongezwe ibara ndogo mbili, ya kwanza ni juu ya malipo yote nchini yafanyike kwa kutumia sarafu tofauti na hivi sasa ambapo malipo mengine hutumia fedha za kigeni na pili jukumu mojawapo la Benki Kuu liwe ni kudhibiti mfumuko wa bei. | | |
| | | (xxi) | Ibara ya 217(2) iboreshwe na itamkwe kwamba Benki Kuu haitaingiliwa na mtu yeyote katika utekelezaji wa majukumu yake isipokuwa Bunge. Taarifa za utekelezaji wa kazi za Benki Kuu zitajadiliwa na Bunge angalau mara moja kila mwaka wa fedha na kwa kadiri itakavyoonekana sahihi kufanya hivyo | | |
| | | (xxii) | Itamke kuwa kutakuwa na Gavana wa Benki Kuu. Tume ya Utumishi wa Umma ipendekeze majina matatu na Rais ateue mmoja wao. | | |
| | | (xxiii) | Gavana na Naibu Gavana wateuliwe na Rais kutokana na ushauri wa Tume ya utumishi na kuthibitishwa na Bunge. | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | (xxiv) Gavana na Naibu wake watoke pande tofauti za muungano na kuwe na kupishana katika madaraka. | | |
| | | (xxv) Ibadilishwe na kusomeka: Kutakuwa na 'Central Bank' ya Shirikisho la Tanzania. ambapo majukumu yake yatalenga mahitaji ya shughuli za kifedha za Shirikisho tu. | | |
| | | (xxvi) Kila nchi mshirika atakuwa na Benki Kuu yake itakazoshughulika na Sera ya "Mipango ya sarafu", na kusimamia na kudhibiti masuala ya fedha za kigeni. | | |
| | | (xxvii) Ibara hii ifutwe, na kipengele cha nne (4) cha Nyongeza ya Rasimu kirekebishwe ili kisomeke "sarafu, Fedha za Kigeni na Benki Kuu."<br>(xxviii) b) Benki Kuu Pekee iwe na jukumu la kusimamia sera za kifedha na Benki za Washirika wa Muungano zisihusike na jukumu hilo.<br>(xxix) c) Kuwepo bodi maalum ya kudhibiti pesa zote za nchi washirika<br>(xxx) d) Majukumu hayo yaondolewe kutoka Benki za Washirika b). Majukumu hayo yabaki kwenye Benki Kuu ili kulinda uchumi wa nchi.<br>(xxxi) e) Ibara hii ifutwe, kwa | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | kuwa hakuna haja ya kuwa na Benki za Serikali za Washirika kufanya hivi kunapingana na Ibara ya 60 ya rasimu ikisomwa kwa pamoja na Nyongeza ambapo swala la Sarafu na Benki Kuu ni jambo la 4 katika mambo 7 ya Muungano. | | |
| 218. | Benki za Serikali za Washirika | (i) Majukumu ya kusimamia sera za kifedha na benki za biashara yawe ya Benki Kuu. | Haya ni majukumu mazito katika kulinda uchumi wa nchi, hivyo ni muhimu yakae kwenye taasisi yenye uhuru wa kiutendaji kama Benki Kuu. | Ibara ya 218 inakuwa ibara ya 234 na inabaki kama ilivyo. |
| | | (ii) Inazuia udhibiti, usimamizi na uongozi kamili wa Benki Kuu katika benki za nchi Washirika na katika Nyanja nzima ya fedha na forodha nchi nzima;<br>(iii) Kiundwe chombo cha kuunganisha sera za mapato na matumizi (fiscal policies) za Serikali za Nchi Washirika na Muungano ili kuhakikisha mazingira sawa ya ushindani na kudhibiti deni la Taifa. | | |
| | | (iv) Ibara hii ifutwe. Utaratibu wa sasa uendelee. | (a) Hakuna haja ya kuwa na Benki Kuu za Serikali za Washirika.<br>(b) Ibara hii inapingana na Ibara ya 60 ikisomwa kwa pamoja na Nyongeza ambapo | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | swala la Sarafu na Benki Kuu ni jambo la 4 katika mambo 7 ya Muungano.<br>(c) Mapendekezo ya kuwa na Benki Kuu ya Muungano na Benki za Washirika hauendani na uhalisia katika utekelezaji wa majukumu ya Benki Kuu.<br>(d) Mapendekezo yaliyoko kwenye Rasimu hususan kuhusiana na kuundwa kwa Benki za Washirika yanakinzana na mwelekeo katika uendeshaji wa uchumi kikanda (Regional Integration) ambapo inakusudiwa kuwa na Benki Kuu na umoja wa sarafu moja katika Afrika Mashariki.<br>(e) Majukumu yaliyopewa benki za Washirika yanakinzana na uhuru wa Benki Kuu hivyo upo uwezekano wa kutokea | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | migongano.<br>(f) Benki Kuu iliyotajwa kwenye Rasimu inakosa majukumu ya Benki Kuu ya kawaida kwa sababu Benki za Washirika zina uhuru wa kutekeleza majukumu yote ya Benki Kuu isipokuwa kutoa na kudhibiti mzunguko wa Sarafu.<br>(g) Uwepo wa Benki za Washirika utaongeza gharama za uendeshaji zinazotokana na kila upande wa Muungano kuwa na shughuli zinazofanana ukizingatia kiuchumi tungali wachanga.<br>(h) Uwepo wa Benki za Washirika utaongeza gharama za uendeshaji zinazotokana na kila upande wa Muungano kuwa na shughuli zinazofanana ukizingatia kiuchumi tungali wachanga.<br>(i) Kama itakubalika kuwa na Benki Kuu | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | ya Muungano na Benki za Washirika, itakuwa vigumu sana kutekeleza majukumu ya kusimamia benki za biashara. Kwa mfano, nchi za Ulaya zimekumbwa na tatizo hilo miaka ya karibuni na sasa hivi ziko kwenye mchakato wa kuanzisha utaratibu utakaowezesha Benki Kuu ya pamoja kusimamia baadhi ya benki za biashara kulingana na viwango vitakavyokubaliwa chini ya mfumo wa Shirikisho. | |
| | | (v) Ibara ya 218 ibaki kama ilivyo. | | |
| | | (vi) Ibara hii ifutwe. | (a) Kila nchi Washirika iwe na Benki yake ya kutunza akaunti ya fedha zake za kuendesha Serikali yake.<br>(b) Kuwepo kwa Benki Kuu tatu kutasababisha kuyumba kwa sarafu kwa upande mmoja wa Serikali hizi. | |
| | | (vii) Kipengele cha nne (4) cha | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | Nyongeza ya Rasimu kirekebishwe ili kisomeke "sarafu, Fedha za Kigeni na Benki Kuu." | | |
| | | (viii) Benki Kuu Pekee iwe na jukumu la kusimamia sera za kifedha na Benki za Washirika wa Muungano zisihusike na jukumu hilo. | | |
| | | (ix) Kuwepo bodi maalum ya kudhibiti pesa zote za Nchi Washirika. | | |
| | | (x) Majukumu hayo yaondolewe kutoka Benki za Washirika b). Majukumu hayo yabaki kwenye Benki Kuu ili kulinda uchumi wa nchi. | | |
| | | (xi) Ibara hii ifutwe, kwa kuwa hakuna haja ya kuwa na Benki za Serikali za Washirika kufanya hivi kunapingana na Ibara ya 60 ya Rasimu ikisomwa kwa pamoja na Nyongeza ambapo swala la Sarafu na Benki Kuu ni jambo la 4 katika mambo 7 ya Muungano. | | |

# SURA YA KUMI NA TANO YA RASIMU

## 15.0 SEHEMU YA KWANZA: ULINZI NA USALAMA KATIKA JAMHURI YA MUUNGANO

### (a) Ulinzi na Usalama wa Taifa

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | SURA YA KUMI NA TANO | (i) Katika Sura ya 15 inayohusu Ulinzi na Usalama wa Taifa yametumika maneno "vyombo vya ulinzi na Usalama", Majeshi ya Ulinzi na Usalama", Majeshi ya Nchi" na Vyombo vya Dola hali hii inachangangia kuleta mkanganyiko kuhusu nani ni Jeshi la Ulinzi au nani ni chombo/taasisi ya usalama. Ili kuondoa mkanganyiko huu inapendekezwa popote pale katika Katiba inapotakiwa kuongelea vyombo vya hivi basi itamkwe kuwa ni "Jeshi la Ulinzi na "Idara za Usalama". | | |
| 219. | Usalama wa Taifa | (i) Katika aya ya 219(3)(a) inayohusu kanuni za ulinzi na usalama wa Jamhuri ya Muungano, kwa kufuta kipengele (a) na kuweka kipengele kipya kitakachosomeka kama ifuatavyo:<br>(a) Usalama wa taifa unaongozwa na wataalamu watakaokuwa chini ya usimamizi wa mamlaka za kiraia na watakaowajibika kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano. | | Ibara ya 219 inakuwa 235 na inabaki kama ilivyo. |
| | | (ii) Masharti ya Usalama wa Taifa yaandikwe kiujumla kama ilivyo | Masuala haya ni nyeti katika kulinda na | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | katika Sura ya Tisa ya Katiba ya sasa. | kutunza usalama. Hayafai kuwekwa hadharani. | |
| | | (iii) Masharti ya Usalama wa Taifa yaandikwe kiujumla kama ilivyo katika Sura ya Tisa ya Katiba ya sasa. | Masuala haya ni nyeti katika kulinda na kutunza usalama. Hayafai kuwekwa hadharani. | |
| | | (iv) Ibara ya 219(3)(b) irekebishwe kwa kufuta maneno "ikiwemo Sheria za Kimataifa". | | |
| | | (v) Iongezwe ibara ndogo ya (4) itakayosomeka: "Bila kuathiri Ibara ndogo ya (3) Jeshi la Ulinzi na Idara za Usalama wa Taifa watatekeleza majukumu yao bila kujali utamaduni wa aina mbalimbali pale ambapo itathibitika kwamba utamaduni huo unahatarisha usalama wa Taifa" | Ni muhimu kipengele hiki kikaongezwa ili kuzuia watu wenye nia mbaya kwa usalama wa taifa letu kutumia kisingizio cha utamaduni kufanya fujo, ghasia na kuhatarisha usalama wa nchi | |
| | | (vi) Iongezwe ibara ndogo mpya ya (4) ambayo itakuwa kama ifuatavyo: "(4) ni Marufuku kuanzishwa vikundi vya ulinzi na usalama visivyo rasmi." | Ili kudhibiti uanzishaji wa vikundi vya ulinzi nje ya vile vya Serikali. | |
| | | (vii) Ibara hii ibaki kama ilivyo. | | |
| | | (viii) Ibara ndogo ya (2) yaongezwe maneno "ikiwa ni pamoja na maziwa na nchi kavu". | | |
| | | (ix) Kuwepo na uwiano wa kiofisi katika nchi Washirika wa Muungano. | | |
| | | (x) Idara ya usalama iitwe Taasisi ya Usalama wa Taifa. | Kwa sababu Amiri Jeshi Mkuu ni Rais. | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | (xi) Ibara hii ifutwe. | Mambo ya usalama ni mambo ya ndani hivyo yaachiwe yawe katika nchi Washirika. | |
| | | (xii) Ulinzi na usalama uwe chini ya Jumuiya za Kikanda kupunguza gharama | | |
| | | (xiii) Masuala ya ulinzi na usalama yawe ya Muungano | | |
| | | (xiv) Popote pale katika katiba inapotamkwa vyombo vya ulinzi na usalama itamkwe, ni "Jeshi la Ulinzi" na "Idara za usalama." | | |
| | | (xv) Iongezwe, " bila kuathiri ibara ndogo ya (3) Jeshi la Ulinzi na Idara za Usalama wa Taifa watatekeleza majukumu yao bila kujali utamaduni wa aina mbalimbali pale ambapo itathibitika kwamba utamaduni huo unahatarisha usalama wa Taifa." | | |
| | | (xvi) Marginal Note, isomeke "Ulinzi na Usalama wa Taifa" | | |
| | | (xvii) 219(3)(a) kiondolewe ili Bunge lisihusike kwa kuwa baadhi ya taarifa ni siri | | |
| | | (xviii) Kipengele 3(a) kibadilishwe ili kuiweka idara ya usalama wa Taifa kuwa chini ya mamlaka ya kiraia na kuwajibika kwa Bunge | | |
| | | (xix) Iongezwe sehemu ya maziwa na mito | | |
| | | (xx) Suala la usalama lisiwe la | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | muungano | | |
| | | (xxi) Iboreshwe kuzungumzia idara ya usalama wa Taifa kufanya kazi kwa maslahi ya nchi | | |
| | | (xxii) Iongezwe uhaini na ugaidi | | |
| | | (xxiii) 219(3)(b) iwe kuzingatia sheria za nchi. "sheria za kimataifa" iondolewe. | | |
| | | (xxiv) Kila upande wa muungano uwe na idara yake ya ulinzi na usalama bila kuathiri mamlaka ya nchi | | |
| | | (xxv) Iwe ni marufuku kuanzishwa vikundi vya ulinzi na usalama visivyo rasmi | | |
| 220. | Taasisi za ulinzi na usalama wa Taifa | (i) Ibara ya 220(a)(c) yaongezwe maneno Jamhuri ya Muungano wa Tanzania baada ya jina la Taasisi;<br>(ii) Kiongezwe kipengele (d) chenye Idara ya Uhamiaji ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. | | 1. Ibara ya 220 inakuwa ibara ya 236.<br>2. Marginal note imerekebishwa na inasomeka "Vyombo vya Ulinzi na usalama wa Taifa".<br>3. Aidha neno "Taasisi za Ulinzi lisomeke "Vyombo vya Ulinzi". |
| | | (iii) Ibara ya 220(1) ifutwe na kuandikwa upya kuwa:<br>"220(1) Jeshi la Ulinzi na Idara za Usalama wa Taifa ni:<br>(a) Jeshi la Ulinzi la wananchi wa Tanzania;<br>(b) Idara ya Polisi; na<br>(c) Idara ya Usalama wa taifa | Pendekezo la kuifuta na kuiandika upya Ibara ndogo ya (1) linatokana na ukweli kwamba jinsi ilivyokaa itavinyima vyombo hivyo na watumishi wake uhuru wa kutekeleza kazi zao ipasavyo kulingana na matakwa ya kazi zao | |
| | | (iv) Ibara ya 220(1) iongezewe aya mpya ya (d) itakayosomeka:<br>"(d) Jeshi la Magereza." | Jeshi la Magereza ni muhimu katika kulinda amani na usalama na pia | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | Washirika wa Muungano hawataruhusiwa kuwa na vyombo vya Ulinzi na usalama ikihusisha pia Jeshi la Magereza. | |
| | | (v) Iongezwe ibara ndogo ya (2) na (3), isomeke:<br>"(2) Ni marufuku kwa mtu yeyote au shirika lolote au kikundi chochote, isipokuwa serikali ya Jamhuri ya Muungano kuunda au kuweka Majeshi ya ulinzi au Taasisi za usalama za aina yoyote Tanzania.<br><br>(3) Bila kuathiri ibara ndogo ya (1) na (2) kutakuwepo na Jeshi la Kujenga Taifa ambalo litakuwa na jukumu la kuwajenga vijana kizalendo na uzalishaji maji. | (a) Maneno usalama wananchi yasitumike ili kuondoa makanganyiko wa nani anawajibika na usalama wa wananchi kati ya Jeshi na Polisi.<br><br>(b) Jeshi la polisi liitwe Idara ya Polisi kwa sababu Jeshi la Polisi (Polisi Force) linatumika kwa polisi iliyokaa na kufanya kazi kijeshi (militasistic) na kishari (aggressive) eg polisi wa kikoloni, na haishirikishi jamii katika kutatua matatizo. Kwa upande mwingine Idara ya Polisi (Police Service) lengo lake ni kutatua matatizo katika jamii kwa amani, kwa kushirikisha jamii, jambo ambalo polisi | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | wa nchi hii wanaelekea kufanya – mfano Polisi Jamii, ulinzi shirikishi nk. | |
| | | (vi) Ibara ndogo ya (3) isomeke: (3) Katika utekelazaji wa majukumu yao, Jeshi la Ulinzi na Idara za Usalama na kila mtumishi wa Jeshi na Idara hizo watatekeleza majukumu yao kwa kuzingatia Sheria za nchi na Kanuni za taratibu zinazotawala kazi zao. | | |
| | | (vii) Katika aya ya 220(5) inayohusu mamlaka ya Rais juu ya taasisi za ulinzi na usalama, kwa kuongeza maneno yafuatayo baada ya neno 'Rais': "na zitawajibika katika Bunge la Jamhuri ya Muungano kwa utekelezaji wa majukumu yake" | | |
| | | (viii) Ibara ya 220 (6) -Mamlaka yasiwe kwa Rais na Baraza tu, bali pia Bunge lishauri na kuidhinisha. | | |
| | | (ix) Ibara ndogo ya (6) ifutwe. | Majeshi yaliyopo yanatosha. | |
| | | (x) Katika aya ya 220(6) ifutwe. | | |
| | | (xi) Katika Ibara ya 220 maneno "Jeshi la Wananchi wa Tanzania" yabadilishwe na yasomeke "Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania" na 'Jeshi la Polisi" yasomeke "Idara ya Polisi" kila linapotokea katika Rasimu. | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | (xii) Ziongezwe ibara ndogo nyingine mpya ambazo zitasomeka kama ilivyo Ibara ya 143(4) na 147(3) ya Katiba ya sasa. | | |
| | | (xiii) Ibara hii ibaki kama ilivyo. | | |
| | | (xiv) Ibara hii ifutwe. | Masuala ya usalama ni mambo ya ndani ya nchi Washirika. | |
| | | (xv) TAKUKURU iingizwe katika vyombo vya Ulinzi na Usalama vya Muungano. | | |
| | | (xvi) Ibara ndogo ya (2) maneno “watu wengine” yafutwe na badala yake isomeke “na raia wengine”. | | |
| | | (xvii) Uhamiaji iingizwe katika vyombo vya Ulinzi na Usalama. | | |
| | | (xviii) Jeshi la Polisi la Muungano lisiwepo, Polisi ibaki kuwa chini ya mamlaka ya Washirika. | | |
| | | (xix) Katika ibara ndogo ya (6) yaongezwe maneno “na kuthibitishwa na Bunge”. | Usalama wa raia ni jambo muhimu linahitaji uwazi. | |
| | | (xx) Neno anaweza lifutwe na badala yake isomeke “Rais ataunda”. | Ili kumpa uwezo Rais wa kuanzisha Vyombo vya Ulinzi na Usalama. | |
| | | (xxi) Iongezwe Jeshi la Magereza na Mgambo katika vyombo vya Ulinzi na Usalama. | Zote ni taasisi za ulinzi na usalama. | |
| | | (xxii) Ziongezwe ibara ndogo nyingine mpya ambazo zitasomeka kama ilivyo Ibara ya 143(4) na 147(3) ya Katiba ya sasa. | | |
| | | (xxiii) Ibara hii ibaki kama ilivyo. | | |
| | | (xxiv) Ibara hii ifutwe. | Masuala ya usalama ni | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | mambo ya ndani ya nchi Washirika. | |
| | | (xxv) TAKUKURU iingizwe katika vyombo vya Ulinzi na Usalama vya Muungano. | | |
| | | (xxvi) Ibara ndogo ya (2) maneno "watu wengine" yafutwe na badala yake isomeke "na raia wengine". | | |
| | | (xxvii) Uhamiaji iingizwe katika vyombo vya Ulinzi na Usalama. | | |
| | | (xxviii) Jeshi la Polisi la Muungano lisiwepo, Polisi ibaki kuwa chini ya mamlaka ya Washirika. | | |
| | | (xxix) Katika ibara ndogo ya (6) yaongezwe maneno "na kuthibitishwa na Bunge". | Usalama wa raia ni jambo muhimu linahitaji uwazi. | |
| | | (xxx) Neno anaweza lifutwe na badala yake isomeke "Rais ataunda". | Ili kumpa uwezo Rais wa kuanzisha Vyombo vya Ulinzi na Usalama. | |
| | | (xxxi) Iongezwe Jeshi la Magereza na Mgambo katika vyombo vya Ulinzi na Usalama. | Zote ni taasisi za ulinzi na usalama. | |
| | | (xxxii) Maslahi ya Taasisi yafanane | | |
| | | (xxxiii) Inspekta Jenerali wa Polisi ateuliwe kutoka ndani ya Jeshi la Polisi Tanzania | | |
| | | (xxxiv) Ifutwe na kuandikwa upya kama ifuatavyo:<br>(1) Jeshi la Ulinzi na Idara za Usalama wa Taifa ni:<br>a) Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania<br>b) Idara ya Polisi<br>c) Idara ya Usalama wa Taifa<br>(2) Iongezwe: marufuku kwa mtu au | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | shirika lolote isipokuwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano kuunda au kuweka Majeshi ya Ulinzi au Taasisi za Usalama za aina yoyote Tanzania.<br>(3). Kuanzishwa kwa JKT<br>(4). Itamkwe kuwa katika utekelezaji wa majukumu yao, Jeshi la Wananchi wa Tanzania na Idara za usalama watatekeleza majukumu yao kwa kuzingatia sheria za nchi.<br>(2) Jeshi la Polisi (Police Force) liitwe Idara ya Polisi (Police Service) ili kuifanya iweze kushirikiana na jamii katika utendaji wake tofauti na ilivyo sasa ambapo imekaa kama chombo cha mabavu. | | |
| | | (xxxv) 220(1) mpaka (3) ibaki kama zilivyo | | |
| | | (xxxvi) Ibara 147(3) na (4) ya katiba ya sasa viongezwe | | |
| | | (xxxvii) Ibara ya 220(5) iongezewe maneno yatakayozifanya Taasisi hizi kuwajibika kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano | | |
| | | (xxxviii) Ibara ndogo ya 220(6) ifutwe | | |
| | | (xxxix) Rais aongezwe kama taasisi mojawapo miongoni mwa Taasisi za Ulinzi na Usalama | | |
| | | (xl) Ibara ndogo ya (5) isomeke (4) na ibara ndogo (7) isomeke (5) . | | |
| | | (xli) Ibara ndogo ya (6) isomeke; | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | "itakuwa ni marufuku kuanzisha taasisi, kampuni, jumuiya au shirika linalohusina na ulinzi na usalama au ushirika wa kijeshi | | |
| | | (xlii) Ibara ndogo ya (7) isomeke, "Bunge linaweza kutunga sheria itakayoweka masharti ya kuanzisha taasisi, kampuni, jumuiya au shirika linalohusiana na ulinzi. | | |
| | | (xliii) Ibara ndogo ya 220 (6) ifutwe. | | |
| | | (xliv) Kiundwe chombo kidogo maalum cha kikatiba kitakachokuwa na mamlaka yanayofanana na ya kipolisi ya kuchunguza makosa makubwa yanayo tendeka ndani na nje ya nchi kikiundwa na wataalam wa fani mbalimbali | | |
| | | (xlv) Uongozi wa juu wa vyombo vyote vya ulinzi na usalama viwe kwa kupokezana kati ya washirika | | |
| | | (xlvi) 220 (6) Mamlaka yasiwe kwa Rais na Baraza tu, bali pia Bunge lishauri na kuidhinisha. | | |
| | | (xlvii) Neno "chombo" lielezwe maana yake kwenye katiba | | |
| | | (xlviii) Bunge liwezeshe kuanzishwa kwa chombo hicho cha ulinzi na usalama | | |
| | | (xlix) Kuwepo kamati ya Bunge kufuatilia utendaji wa chombo hicho. | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | (l) Kiwepo Chombo huru cha Kikatiba ambacho kitakuwa na nguvu kisheria katika kuzuia na kupambana na rushwa/ufisadi.<br>(li) Iongezwe ibara mpya itakayoanzisha "Kamati ya Vyombo vya Ulinzi na Usalama itakayoeleza kama ifuatavyo:<br>(lii) Kuwe na Kamati ya Ulinzi na Usalama ambayo itakuwa na Majukumu ya kulishauri Baraza la Usalama la Taifa. Kamati hiyo itakutana na kujadili masuala ya ulinzi na usalama kadri itakavyopangwa. Wajumbe wa Kamati hiyo watakuwa ni;<br>(a) Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi – Mwenyekiti;<br>(b) Mkuu wa Idara ya Polisi;<br>(c) Mkuu wa Idara ya Usalama wa Taifa;<br>(d) Mkuu wa Magereza;<br>(e) Mkuu wa Idara ya Uhamiaji;<br>(f) Mkuu wa Usalama na Utambuzi Jeshini – Katibu. | Ili kuzuia rushwa na ufisadi.<br><br>Mapendekezo haya yana lengo la kuhakikisha kwamba masuala ya ulinzi na usalama ni Mambo ya Muungano na yanabaki chini ya mamlaka pekee ya Jamhuri ya Muungano ili kwenda sambamba na matakwa ya aya za 59(1), 60 zinazohusu mamlaka ya Jamhuri ya Muungano juu ya mambo ya Muungano; na aya ya 61(2), (3) na (5) inayohusu mamlaka ya Washirika wa Muungano 'juu ya mambo yote yasiyo ya Muungano' yanayowahusu. Vile vile mapendekezo haya yana lengo la kuhakikisha kwamba vyombo vya ulinzi na usalama vinawajibika kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano kwa utekelezaji wa majukumu yao. | |
| 221 | Kuanzishwa kwa | (i) Ibara ya 221(1)(c) irekebishwe | Kwa mfumo | 1. Ibara ya 221 inakuwa |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | Baraza la Ulizi na Usalama la Taifa | kwa kufuta maneno "Rais wa Tanzania Bara" na badala yake kuweka maneno "Waziri Mkuu" | unaopendekezwa wa Serikali mbili hakuna Rais wa Tanzania Bara. | ibara ya 237.<br>2. Ibara ndogo ya (1)(a) imefutwa.<br>3. Ibara ndogo ya (2) imerekebishwa na inasomeka:<br>"Mwenyekiti anaweza kumwalika mtu yeyote kushiriki katika kikao cha Baraza la Usalama la Taifa"<br>Ibara ndogo ya (4) imerekebishwa na inasomeka:<br>"vikao vya Baraza la Ulinzi la usalama la Taifa vitaongozwa na Rais"<br><br>4. Imeongezwa Ibara ndogo (1)(m), ambayo imemuongeza Kamishna Mkuu wa Uhamiaji kuwa Mjumbe wa Baraza la Ulinzi na Usalama wa Taifa" |
| | | (ii) Ibara ya 221(1) iongezwe Waziri mwenye dhamana na uhamiaji na uraia. | Suala la uhamiaji na uraia ni muhimu na nyeti kwa Taifa. | |
| | | (iii) Aya ya (c) ya Ibara ndogo ya (1) ifutwe | | |
| | | (iv) Ibara ndogo ya (4) ifutwe na badala yake iandikwe kama ilivyo:<br>"(4) Mwenyekiti wa Baraza atakuwa ni Rais ambaye ndiye ataongoza vikao vya Baraza na endapo Rais hayupo vikao vitaongozwa na Makamu wa Rais". | | |
| | | (v) Baraza la Ulinzi na Usalama liwe na wajumbe wachache ambao ni Rais wa jamhuri ya Muungano, Makamu wa Rais, Rais wa Zanzibar, Waziri Mkuu na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar. Wengine wote wakaribishwe itakapohitajika. | Baraza la Ulinzi na Usalama dogo litaleta ufanisi, wepesi na uaharaka wa kufanya maamuzi. Linaweza kuita wataalamu au mawaziri wanaohusika pale itakapohitajika. | |
| | | (vi) Ibara ya 221(1) irekebishwe kwa kuongeza aya mpya ya (n) itakayosomeka:<br>"(n) Kamishna Mkuu wa Jeshi la Magereza." | Jeshi la Magereza ni muhimu katika ulinzi na usalama wa Taifa kwani linapokea wahalifu na washukiwa wa uhalifu. Hivyo, kuwaweka nje ya Baraza la Ulinzi na Usalama wa Taifa sio sahihi. | |
| | | (vii) Ibara ya 221 irekebishwe kwa kuongeza Ibara ndogo ya (7) | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | itakayosomeka "Bila ya kujali muundo uliotajwa hapo juu, Muundo wa Baraza la Taifa utakuwa na uwiano sawa wa Washirika wa Muungano." | | |
| | | (viii) iongezwe Ibara ndogo ya 7 inayosema "kuwe na chombo ndani ya baraza kinachoshughulikia maslahi ya vyombo vya ulinzi na usalama". | | |
| | | | | |
| | | (ix) Watendaji wakuu wa Washirika wawe wajumbe. | Kuwa na ushiriki mpana wa Washirika wa Muungano. | |
| | | (x) Mawaziri wa Fedha wa Washirika wawe wajumbe. | | |
| | | (xi) Ibara ndogo (2)(b) ifutwe. | Makamu wa Rais asiwepo katika Baraza la Ulinzi na Usalama. | |
| | | (xii) Maneno "Rais wa Tanzania Bara" yasomeke "Rais wa Tanganyika". | | |
| | | (xiii) Ibara ya 221(1)(c) irekebishwe kwa kufuta maneno "Rais wa Tanzania Bara" na badala yake kuweka maneno "Waziri Mkuu". | | |
| | | (xiv) Ibara ndogo ya (1)(c) ibaki kama ilivyo. | (a) Ili kuwezesha uwepo wa Serikali Tatu.<br>(b) Kufuatilia na kulinda ulinzi na usalama kwa ujumla. | |
| | | (xv) Ibara ndogo ya (4) irekebishwe ili Mwenyekiti awe mmoja wa Marais wa nchi Washirika kwa mujibu wa makubaliano ya Washirika. | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | (xvi) Wajumbe wafuatao waongezwe katika Baraza la Ulinzi:<br>(a) Mawaziri wenye dhamana na Mambo ya Nje wa nchi Washirika;<br>(b) Wanasheria Wakuu kutoka nchi Washirika.<br>(c) Mawaziri wenye dhamana na Fedha kutoka nchi Washirika.<br>(d) Wakuu wa Jeshi la Polisi kutoka nchi Washirika. | Kuweka usawa katika maamuzi na uwakilishi wa nchi Washirika. | |
| | | (xvii) Kuwe na chombo cha kushughulikia maslahi ya vyombo vya ulinzi na usalama | | |
| | | Ibaki kama ilivyo isipokuwa 221(1) iondolewe | | |
| | | (xviii) Ibara ndogo ya 221(1)(c) ifanyiwe marekebisho kuzingatia muundo wa serikali mbili | | |
| | | (xx) Maneno Waziri Mkuu yatumike badala ya Rais wa Tanzania Bara | | |
| | | (xxi) Baraza la Ulinzi na Usalama liwe na wajumbe wachache: Rais wa Jamhuri ya Muungano, Waziri Mkuu, Makamu wa Rais, Rais wa Zanzibar na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar. Udogo huo utaleta ufanisi na wepesi katika maamuzi. | | |
| | | (xxii) Neno 'Tanzania Bara' libadilike na lisomeke 'Tanganyika'; hivyo basi Ibara ya 221(1)(c) libadilishwe na lisomeke | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | 'Rais wa Tanganyika'. | | |
| | | (xxiii) Ibara ya 221(4) iboreshwe na ikiwa Makamu wa Rais hayupo basi vikao vya Baraza la Ulinzi na Usalama viongozwe na Rais wa Tanganyika au Rais wa Zanzibar na yeyote kati yao awe na mamlaka ya kufanya hivyo bila ya kuvunja itifaki kwa kuwa marais wa Tanganyika na Zanzibar wanayo hadhi sawa. | | |
| | | (xxiv) Ibara ndogo 1(m) zifutwe. Badala yake iwe Bunge linaweza kutunga sheria itakayoweka masharti ya kuanzisha vyombo | | |
| | | (xxv) Ibara ya 221(1) (b) iondolewe | | |
| | | (xxvi) Ibara ya 221(1)(c) isomeke "Waziri Mkuu wa Zanzibar" | | |
| | | (xxvii) Baraza la Ulinzi na Usalama liripoti kwenye Kamati Teule ya Bunge | | |
| | | (xxviii) Ibara ya 224 ifutwe na iandikwe kama ifuatavyo: "224(1) kutakuwa na Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi ambaye atateuliwa na Rais baada ya kushauriana na Kamati Maalum ya Ulinzi na Usalama wa Taifa. (2) Kamati Maalum ya Ulinzi na Usalama wa Taifa itakuwa na wajumbe wafuatavyo: (a) Makamu wa Rais; (b) Rais wa Zanzibar; | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | (c) Waziri mwenye dhamana ya ulinzi;<br>(d) Mkuu wa majeshi ya ulinzi;<br>(xxix) Mkurugenzi wa Idara ya Usalama wa Taifa. | | |
| | | (xxx) Kamati ya Ulinzi na Usalama wa Taifa itakuwa na wajumbe wafuatao:<br>(xxxi) Makamu wa Rais<br>(xxxii) Rais wa Zanzibar<br>(xxxiii) Waziri wa Ulinzi<br>(xxxiv) Mkuu wa Majeshi<br>(xxxv) Mkurugenzi wa Idara ya Usalama wa Taifa<br>(xxxvi) Rais asishauriane na Baraza laUlinzi na Usalama wa Taifa kwani baadhi ya wajumbe wa Baraza hilo hawajui sifa za Mkuu wa Majeshi<br>(xxxvii) Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi awe na mamlaka ya kuteua makamanda wa vikosi; Rais ateue makamanda wa Brigedi na Kamandi<br>(xxxviii) Kuwe na kamati ya uteuzi itakayokuwa ina mshauri Rais kuhusu uteuzi wa Mkuu wa Majeshi, Jeshi la Polisi na Idara ya Usalama wa Taifa. | | |
| 222. | Majukumu ya Baraza la Ulinzi na | (i) Rais atoe taarifa kisheria kwa wakati wowote tatizo | Kipindi cha mwaka mmoja ni kirefu mno. | 1. Ibara ya 222 inakuwa ibara ya 238. |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | Usalama la Taifa | litakapotokea, Rais atoe taarifa katika Bunge kwa miezi sita. | | 2. Ibara ndogo ya (1)(b) imerekebishwa na inasomeka; “kupokea, kutathmini na kuchunguza taarifa kutoka katika vyombo vya ulinzi na usalama wa taifa, taasisi za serikali kuhusiana na usalama wa nchi.”<br>3. Ibara ndogo ya (1) (c) imeongezwa na inasomeka:<br>“kutoa maelekezo mahususi kuhusiana na masuala ya ulinzi na usalama wa taifa kwa serikali ya Jamhuri ya Muungano, serikali ya nchi washirika na vyombo vya ulinzi na usalama wa taifa.”<br>4. Imeongezwa ibara ndogo (1) (e ) ambayo inasomeka: “kufanya kazi nyingine yeyote itayowasilishwa kwake na Rais”. |
| | | (ii) Kiongezwe kipengele (d) na kisomeke "Katika kutekeleza majukumu yake, vyombo vya usalama wa Taifa,havitatumia silaha yoyote kwa kushambulia wananchi wa Jamhuri ya Muungano wasio na silaha." | | |
| | | (iii) Rais apate mapendekezo ya Baraza la ulinzi katika utendaji wake wa kazi. | Ulinzi na usalama wa nchi ni jambo la kila siku.<br>Mwaka mmoja ni mrefu. | |
| | | (iv) Ibara ndogo iongezwe: (7) Bila ya kujali muundo uliotajwa hapo juu ya muundo wa Baraza la Usalama wa Taifa litakuwa na uwiano sawa wa Washirika wa Muungano. | | |
| | | (v) Ibara ndogo ya (2) yaongezwe maneno “Rais atatoa taarifa kwa Bunge kila baada ya miezi sita na kwa kadri atakavyoona inafaa kuhusiana na hali ya usalama.” | | |
| | | (vi) Rais atoe taarifa Bungeni kila Bunge linapokutana. | Mwaka mmoja ni muda mrefu sana. | |
| | | (vii) Rais atoe taarifa Bungeni kama ilivyo sasa. | | |
| | | (viii) Katika ibara ndogo ya (1)(b) maneno “kujitolea na hatari” yafutwe na badala yake isomeke “kukitokea”. | | |
| | | (ix) Ibara ndogo iongezwe: (7) Bila ya kujali muundo uliotajwa hapo juu ya muundo wa Baraza la | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | Usalama wa Taifa litakuwa na uwiano sawa wa Washirika wa Muungano. | | |

## (b) Jeshi la Wananchi wa Tanzania

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| 223. | Kuanzishwa kwa Jeshi la Wananchi wa Tanzania | (i) Ibara ya 223 ifutwe na kuandikwa kama ifuatavyo:<br>"223(1) Kutakuwepo na Jeshi la Ulinzi litakaloundwa na:<br>(a) Jeshi la Kudumu litakalojulikana kama Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania ambalo litakuwa na:<br>(b) Jeshi la Nchi Kavu;<br>(c) Jeshi la Anga; na<br>(d) Jeshi Jeshi la Maji.<br>(e) Jeshi la Akiba kama litakavyoidhinishwa katika Sheria itakayotungwa na Bunge;<br>(4) Idara na taasisi nyingine zitakuwa sehemu ya Jeshi la ulinzi pale tu na kwa muda ule tu ambapo watakuwa wamehamishwa (mobilized) au watakapokuwa wameitwa kufanya mafunzo au mazoezi ya pamoja na Jeshi la Ulinzi la wanachi wa Tanzania kwa mujibu wa Sheria iliyotungwa na Bunge."<br>(5) Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa | | 1. Ibara ya 223 inakuwa ibara ya 239.<br>2. Ibara ndogo ya (1) neno "mamlaka" lisomeke "jukumu". |

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Maoni* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| | | Tanzania litakuwa na mamlaka ya kusimamia ulinzi wa mipaka ya Jamhuri ya Muungano na Wananchi wake.<br>(6) Bila kuathiri ujumla wa Ibara ndogo ya (2), Jeshi la Ulinzi litakuwa na wajibu wa:<br>(a) Kulinda uhuru na mipaka ua Jamhuri ya Muungano;<br>(b) Kusaidia na kushirikiana na mamlaka nyingine wakati wa dharura au maafa;<br>(c) Kusaidia mamlaka au uongozi wa Serikali kutuliza ghasia, fujo au kurejesha hali ya utulivu, pale linapoitwa na mamlaka husika kufanya hivyo kwa mujibu wa Sheria iliyotungwa na Bunge;<br>(d) Kushirikiana na jumuiya ya kimataifa katika ulinzi wa amani<br>(e) pale itakapoonekana unafaa.<br>Rais anaweza kuanzisha vikosi vingine vya jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania kama atakavyoona inafaa. | | |
| | | Ibara vya 223(2) irekebishwe kwa kufuta neno “vingine”. | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | (i) Ibara ndogo ya (2) ifutwe. | | |
| | | (ii) iongezwe ibara ndogo ya (2) itakayoeleza kama ifuatavyo:<br>(iii) "(2) Kutakuwa na Jeshi la akiba la kudumu linalotokana na Wanajeshi Wastaafu wa Jeshi la Ulinzi wa Wananchi wa Tanzania". | | |
| | | (iv) Ibara ndogo ya (2) ifutwe na badala yake iandikwe kama ifuatavyo:<br>"(2) Rais anaweza kuanzisha vikosi vingine vya Jeshi la Wananchi wa Tanzania kama atakavyoona inafaa kwa kushauriana na Baraza la Ulinzi na Usalama na Bunge kuidhinisha vikosi hivyo na si vinginevyo." | | |
| | | (v) Ibara ndogo ya (2) iwe ya (3) na iwe kama ifuatavyo:<br>"(3) Rais anaweza kuanzisha Kamandi na Vikosi vingine vya majeshi ya ulinzi wa Wananchi wa Tanzania kama atakavyoona inafaa". | | |
| | | (vi) Iongezwe ibara ndogo mpya ambayo itakuwa kama ifuatavyo:<br>(vii) "Rais baada ya kushauriana na Baraza la Ulinzi na Usalama na kuidhinishwa na Bunge, anaweza kuunganisha au kufuta kikosi chochote cha ulinzi na usalama." | | |
| | | (viii) Ibara hii ibaki kama | Mwaka mmoja ni muda | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | ilivyo. | mrefu sana. | |
| | | (ix) Ibara hii isomeke "Uanzishaji wa Vikosi vya Ulinzi uthibitishwe na Bunge". | Vyombo vya ulinzi vianzishwe kwa uwazi. | |
| | | (x) Ibara ya 223(2) isomeke, "Rais anaweza kuanzisha vikosi vingine vya Jeshi la Wananchi wa Tanzania kama atakavyoona inafaa kwa kushauriana na Baraza la Ulinzi na Usalama na Bunge kuidhinisha vikosi hivyo na si vinginevyo." | | |
| | | (xi) Mamlaka ya Rais ya kuunganisha au kufuta kikosi chochote alichoanzisha awe nayo mara baada ya kushauriana na Baraza la Ulinzi na Usalama na Bunge kuidhinisha, Rais anaweza kufuta kikosi chochote alichoanzisha au kuunganisha vikosi. | | |
| | | (xii) Rais asiruhusiwe kuanzisha chombo chochote kingine cha ulinzi na usalama. | | |
| 224. | Uteuzi wa Mkuu wa Majeshi | (i) Ibara ya 224 ifutwe. | Rais awe huru kuteua kwa kuzingatia utaratibu na kanuni za uteuzi wa watendaji na watumishi wa vyombo vya ulinzi na usalama. | Ibara ya 224 inakuwa ibara ya 240 na inabaki kama ilivyo. |
| | | (ii) Katika aya ya 224 inayohusu uteuzi wa Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, kwa kuongeza maneno | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | yafuatayo baada ya neno 'Taifa': "na kuthibitishwa na Bunge." | | |
| | | (iii) Iongezwe ibara ndogo ya (2) itakayosomeka kama ifuatavyo:<br>"(2) Baada ya kuteuliwa jina lake litapelekwa katika Bunge la Jamhuri ya Muungano lithibitishwe au kutothibitishwa". | | |
| | | (iv) Iongezwe ibara ndogo ya (3), isomeke;<br>"(3) Bila kuathiri Katiba na Sheria itakayotungwa na Bunge, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi atakuwa na mamlaka ya kuteua Makamanda wa Vikosi". | Inapendekezwa Mkuu wa majeshi ateue makamanda wa vikosi ili kumpunguzia mzigo Rais na Amiri Jeshi Mkuu ambaye abakie kuwateua makamanda wa fomesheni ambazo ni brigedi na kamandi | |
| | | (v) Uteuzi wa Mkuu wa Majeshi uwe wa kupokezana baina ya Washirika wa Muungano. | (a) Kuwe na mzunguko wa madaraka katika nafasi ya Mkuu wa Majeshi kutoka kila upande wa nchi Washirika.<br>(b) Madaraka ya Amiri Jeshi Mkuu yapunguzwe. | |
| | | (vi) Ibara hii ibaki kama ilivyo. | | |
| | | (vii) Isomeke kama ifuatavyo:<br>"kutakuwa na Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi ambaye ataomba kazi na kuthibitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania". | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | (viii) Mkuu wa Jeshi la Ulinzi athibitishwe na Bunge. | Ili aweze kuwajibika Bungeni. | |
| | | (ix) Ibara ndogo 224(1) Iandikwe kuwa: "Kutakuwa na Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi ambaye atateuliwa na Rais baada ya kushauriana na Kamati Maalum ya Ulinzi na Usalama wa Taifa." | Vyombo vya ulinzi vianzishwe kwa uwazi. | |
| | | (x) Uteuzi wa Mkuu wa Majeshi kuthibitishwa na Bunge). | | |
| | | (xi) Ibara ibaki kama ilivyo | | |
| | | (xii) Vyeo hivyo vijazwe baada ya mapendekezo ya majina matatu kwa kila cheo kutoka Baraza la Ulinzi na Usalama la Taifa na Rais atateua kutoka katika mapendekezo hayo. Mkuu wa Polisi athibitishwe na Bunge | | |
| | | | | |
| | | (xiii) Uteuzi wa Mkuu wa Majeshi uthibitishwe na Bunge | | |
| 225. | Madaraka ya Amiri Jeshi Mkuu | (i) Ihamishiwe Ibara ya 69 baada ya kufanyiwa marekebisho yafuatayo:<br>(a) Katika Ibara ndogo ya (1) katika mstari wa saba yaongezwe maneno "ulinzi wa amani" kati ya maneno "hatari" na "mambo mengineyo"<br>(b) Katika Ibara ndogo ya (2)(b) neno "vikosi" lifutwe na kuwekwa neno "fomesheni";<br>(c) Katika Ibara ndogo ya (3) yaongezwe maneno "au kiongozi | Inapendekezwa ibara hii ihamishiwe ibara ya 69 inayohusu majukumu ya Rais kwa vile majukumu yaliyo katika Ibara ya 225 anayotekeleza vile vile kama rais kwa mujibu wa Ibara ya 68(2). | 1. Ibara ya 225 inakuwa ibara 240.<br><br>2. Ibara 241 imeandikwa upya ili kuelezea madaraka ya Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama ya Tanzania. |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | wake" baada ya maneno "Amiri Jeshi Mkuu" na maneno "kwa mujibu wa masharti ya ibara ndogo ya (1) na (2) ya ibara hii" yafutwe.<br>(ii) Ibara ya 225.-(1) Bila ya kuathiri masharti yatakayowekwa na sheria yoyote iliyotungwa na Bunge, miongoni mwa madaraka ya Rais akiwa Amiri Jeshi Mkuu ni kuyaamuru majeshi ya nchi yatende mambo yanayohusika na vita vya ulinzi wa Jamhuri ya Muungano, mambo ya kuokoa maisha na mali ya watu katika hali ya hatari na mambo mengineyo ambayo Amiri Jeshi Mkuu ataona inahitajika, na kwa ajili hiyo Amiri Jeshi Mkuu anaweza kuyaamuru majeshi hayo yatekeleze mambo hayo ama ndani au nje ya Tanzania.<br>(2) Bila ya kuathiri masharti yatakayowekwa na sheria iliyotungwa na Bunge, madaraka juu ya mambo yafuatayo yatakuwa mikononi mwa Amiri Jeshi Mkuu-<br>(a) madaraka ya kuwateua viongozi katika majeshi ya ulinzi ya Jamhuri ya Muungano;<br>(b) madaraka ya kuwateua wanajeshi watakaoongoza vikosi mbali mbali vya majeshi ya ulinzi; na | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | (c) madaraka ya kumwamuru mwanajeshi yeyote asitumie madaraka yoyote aliyokabidhiwa na ambayo yanaambatana na kuwa kwake mwanajeshi.<br>(3) Jambo lolote atakalotenda mwanajeshi yoyote kinyume cha amri iliyotolewa na Amiri Jeshi Mkuu kwa mujibu wa masharti ya ibara ndogo ya (1) na (2) ya ibara hii litakuwa batili. | | |
| | | (iii) Ibara ndogo ya (2)(b) iandikwe kama ifuatavyo:<br>"(b) madaraka ya kuwateua Wanajeshi watakaoongoza Kamandi na Vikosi mbalimbali vya majeshi ya ulinzi na usalama". | | |
| | | (iv) Iongezwe ibara ndogo mpya ya (4) itakayosomeka kama ilivyo Ibara ya 69(4) ya Rasimu. | | |
| | | (v) Ibara hii ibaki kama ilivyo. | | |
| | | (vi) Ibara hii isomeke kama ifuatavyo:<br>"Rais kwa kushauriana na Mkuu wa Majeshi atakuwa na madaraka ya kuwateua Viongozi katika Majeshi ya Jamhuri ya Muungano". | | |
| | | (vii) Ibara ndogo ya (2)(a) irekebishwe ili Mkuu wa Majeshi afanye uteuzi wa viongozi wa majeshi. | | |
| | | (vii) Ibara ndogo ya (2)(a) ibaki kama ilivyo. | | |
| | | (viii) Ihamishiwe Ibara ya 69 baada ya kufanyiwa | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | marekebisho yafuatayo: Ibara ndogo ya (1) iongezewe maneno "ulinzi wa amani" kati ya maneno "hatari" na "mambo "mengineyo" | | |
| | | (ix) Neno "vikosi" katika ibara ndogo ya (2) lifutwe na kuwekwa "fomesheni" | | |
| | | (x) Katika ibara ndogo ya (3) yaongezwe, "kiongozi wake" baada ya maneno "Amiri Jeshi Mkuu" na maneno "kwa mujibu wa masharti ya ibara ndogo ya (1) na (2) ya ibara hii yafutwe. | | |
| | | (xi) Ibaki kama ilivyo | | |
| | | (xii) Iwe marufuku kuwepo kwa kambi za jeshi lolote la nchi za nje nchini | | |
| | | Amiri Jeshi Mkuu asiweze kuamrisha majeshi yaende vitani nje ya nchi kabla ya Bunge | | |
| 226. | Tume ya Utumishi ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania | (i) Ibara ya 226- Tume ya Utumishi ya Jeshi la Wananchi – muundo na utaratibu wa uundaji wake uelezwe. | | Ibara 226 inakuwa ibara ya 242 na inabaki kama ilivyo. |
| | | (ii) Ibara ya 226 ifutwe na kuandikwa upya kuwa: "Kamati ya Majeshi ya Ulinzi – Kutakuwepo na Kamati ya Majeshi ya Ulinzi kama ilivyoainishwa katika Sheria iliyotungwa na Bunge yenye jukumu la kusimamia masuala yote ya Sera, Utawala na Utumishi wa | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | wanajeshi wa jeshi la ulinzi la wananchi wa Tanzania". | | |
| | | (iii) Ibara ndogo ya (1) iandikwe kama ifuatavyo:<br>(iv) "(1) Kutakuwa na Tume ya Utumishi ya Jeshi itakayokuwa na jukumu la kusimamia masuala yote ya utumishi wa Wanajeshi wa Majeshi ya ulinzi na usalama wa Tanzania, Kamandi na Vikosi vyake". | | |
| | | (iv) Iongezwe ibara nyingine mpya zitakayoeleza sifa za wajumbe wa Tume ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania, ambayo zitasomeka kama ifuatavyo:<br>(1) Mtu yoyote mwenye sifa ya kuwa Jaji wa Mahakama ya Juu;<br>(2) Wajumbe wawili ambao ni wanajeshi wa ngazi za juu wanaowakilisha fani mbalimbali jeshini; na<br>(3) Wajumbe wengine wawili waliotumikia umma kwa uadilifu na weledi mkubwa;<br>Mkuu wa Jeshi la Wananchi." | | |
| | | (v) Iongezwe Ibara ndogo mpya itakayosomeka kama ilivyo Ibara ya 199 ya Rasimu. | | |
| | | (vi) Ibaki kama ilivyo. | | |
| | | (vii) Tume ya Utumishi ya Jeshi ifutwe na liachiwe Bunge litunge sheria kusimamia Utumishi wa majeshi. | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | (viii) Ifutwe na kuandikwa upya, kama ifuatavyo: "Kutakuwepo na kamati ya ulinzi kama ilivyoainishwa katika sheria iliyotungwa na Bunge yenye jukumu la kusimamia maswala yote ya sera, utawala na utumishi wa Wanajeshi wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania | | |
| | | (ix) Ibara ya 1 isomeke: "Kutakuwa na Tume ya Utumishi ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania itakayokuwa na wajumbe wafuatao:<br>1. Mnadhimu Mkuu wa Jeshi, ambaye atakuwa Mwenyekiti;<br>2. Mkuu wa kikosi cha anga;<br>3. Mkuu wa JKT<br>4. Wakuu wa Brigedi;<br>5. Katibu Mkuu, wizara yenye dhamana ya ulinzi ambaye atakuwa Katibu wa Tume. | | |
| | | (x) Kazi na Majukumu ya Tume ya Utumishi wa Jeshi la Wananchi yatakuwa kama ifuatavyo:<br>1. Kutoa miongozo mbalimbali na kusimamia mchakato wa ajira katika utumishi wa Jeshi la wananchi;<br>2. Bila kuathiri masharti ya katiba hii, kuteua watu | | |

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Maoni* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| | | kuhudumu au kushikilia ofisi za kijeshi na za kiraia jeshini kwa muda, kuidhinisha uteuzi na kudhibiti nidhamu na kuwaondoa wanajeshi na watumishi wa kiraia jeshini wanaohudumu au kushikilia ofisi hizo;<br>3. Kusimamia na kuhamasisha utekelezaji wa misingi na kanuni za utumishi katika sekta zote jeshini;<br>4. Kusimamia maadili na uwajibikaji jeshini;<br>5. Kutoa elimu ya maadili ya wanajeshi kuhusu miiko na maadili ya viongozi jeshini;<br>6. Kushughulikia masuala ya ubadhirifu wa fedha na mali za umma;<br>7. Kuandaa kanuni za taratibu na matumizi ya mamlaka au utekelezaji wa kazi na majukumu ya Tume kama ilivyoelelekezwa na sheria;<br>8. Kuhamasisha hifadhi ya haki za binadamu na wajibu wa wanajeshi kwa jamii kwa mujibu wa katiba hii na sheria za nchi; | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | 9. Kuchunguza uvunjaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala wa sheria jeshini. na | | |
| | | 10. Ibara ya 226 isomeke. Tume ya Utumishi ya Jeshi la Wananchi – "Muundo na utaratibu wa uundaji wake uelezwe." | | |
| | | (v) Tume iwe na wajumbe wafuataao:<br>1. Mtu yeyote mwenye sifa ya kuwa Jaji wa Mahakama ya Juu.<br>2. Wajumbe wawili ambao ni polisi wa ngazi za juu wenye fani mbalimbali na weledi wa hali ya juu, heshima na nidhamu.<br>3. Wajumbe wengine wawili waliotumikia umma kwa uadilifu na weledi mkubwa. | | |
| 227. | Jeshi la Polisi la Tanzania | Polisi irejeshwe katika orodha ya Mambo ya Muungano. | Kwa mujibu wa Rasimu hii, polisi si suala la Muungano.<br>Jeshi la Polisi limekuwa tishio kwa Raia na mali zao kwa kutowajibika kikatiba na kupelekea liogopwe na raia kwa kubambika kesi | Ibara ya 227 inakuwa ibara ya 243 na inabaki kama ilivyo. |
| | | Ibara ya 227(1) isomeke kutakuwa na Jeshi la Polisi la JM | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | litakalokuwa na jukumu la ulinzi wa watu na mali zao bila kutumia nguvu chini ya masharti ya katiba hii. | | |
| | | (4) Ibara hii maginal note inasema Jeshi la Polisi Tanzania na kichwa cha habari cha Ibara ya 227 sura ya 15 kipengele (c) kinasema Jeshi la Polisi la Jamhuri ya Muungano, Ibara hii tunaona kuwa haifanani ili kuondoa mgongano tunapendekeza marginal note na Kichwa cha habari kisomeke JESHI LA POLISI TANZANIA. Na sehemu zingine zilizoandikwa Jeshi la Polisi la Jamhuri ya Muungano ISOMEKE "JESHI LA POLISI TANZANIA" | | |
| | | (vi) Ibara hii ibaki kama ilivyo. | | |
| | | (vii) Ibara ya 227 hadi 235 zifutwe. | (a) Kila nchi Washirika iwe na mamlaka yake ya ulinzi wa ndani.<br>Kupunguza gharama kwa nchi Washirika. | |
| | | (viii) Ibara ndogo ya (1) maneno "masharti ya Katiba hii" yafutwe na badala yake isomeke 'Katiba ya Jamhuri ya Muungano." | | |
| | | (ix) Marginal note itumie jina sahihi "Jeshi la Polisi la Jamhuri ya | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | Muungano wa Tanzania” | | |
| | | Ibaki kama ilivyo isipokuwa 227(1) iongezewe, “… na usalama” | | |
| | | 11. Polisi irejeshwe kwenye mambo ya Muungano | | |
| | | (x) Ibara hii ifutwe | | |
| | | 3. Itolewe katazo ndani ya Katiba au litolewe agizo la kutungwa sheria ya kupiga marufuku mauaji ya Raia yanayofanywa na Polisi | | |
| | | Ibara ya 227(1) isomeke “ kutakuwa na Idara ya Polisi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itakayokuwa na jukumu la kulinda haki za msingi za watu na itakayowajibika kwa wananchi kulingana na sheria” | | |
| 228. | Misingi ya utendaji wa Jeshi la Polisi | (i) Katika Ibara ya 228 (d) inapendekezwa kiundwe chombo maalumu kilicho huru ambacho kitakuwa na mamlaka ya kuzuia na kupambana na rushwa. | Maelezo ni kwamba chombo hicho kiwe huru na ambacho kinaweza kufanya uchunguzi wa kina na kuwa na jukumu wa kushtaki watuhumiwa mahakamani. | 1. Ibara ya 228 inakuwa ibara ya 244.<br><br>2. Ibara hii imeandikwa upya na inasomeka kama ifuatavyo:<br><br>“244(1)Katika utekelezaji wa majukumu yake, Jeshi la Polisi la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania litazingatia:-<br><br>a. Viwango vya juu |
| | | (ii) Katika Ibara hii tunapendekeza liongezwe neno “Kupambanana” mara tu baada ya neno “na” na kabla ya neno “ufisadi” ili isomeke “kuzuia rushwa na kupambana na ufisadi”. | | |
| | | (i) Iongezwe Ibara ya 228(f) isomeke: | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | (iii) Jeshi la polisi lifanye kazi kwa uadilifu bila kuonea Raia yeyote. | | vya kitaaluma na nidhamu miongoni mwa wafanyakazi wake;<br>b. Ulinzi na ukuzaji wa haki za binaadamu;<br>c. Kanuni za uwazi na uwajibikaji; na<br>d. Kukuza mahusiano na jamii.<br><br>(2).Jeshi la Polisi katika kutekeleza majukumu yake, litashirikiana na vyombo vinavyohusika na kupambana na uhalifu vya Nchi Washirika, katika kuufanya uchunguzi na kushughulikia makosa ya rushwa na ufisadi kwa Viongozi na watumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano. |
| | | a) Kiwepo Chombo huru cha Kikatiba ambacho kitakuwa na nguvu kisheria katika kuzuia na kupambana na rushwa/ufisadi<br>b) Ibaki kama ilivyo<br>c) ifutwe | | |
| | | (iv) Ibara hii ibaki kama ilivyo. | Vitu hivyo vimejitosheleza.<br>Kumpunguzia Rais kazi na madaraka.<br>Uwazi utavujisha siri za Polisi. | |
| | | (v) Aya (d) yaongezwe maneno "udanganyifu, uhujumu na ubadhirifu". | | |
| | | (vi) Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama wateuliwe na Bunge. | | |
| | | (vii) Ibara ya (1)(c) neno "Uwazi" lifutwe. | | |
| | | (ii) Iongezwe ibara ndogo itakayosomeka kama ifuatavyo:<br>(viii) "Mkuu wa Jeshi la Polisi atatekeleza majukumu yake kwa uaminifu na uadilifu." | | |
| | | (ix) Ibara hii ibaki kama ilivyo | | |
| | | (x) Ibara hii ifutwe | | |
| 229. | Uteuzi wa Mkuu wa Jeshi la Polisi | Ibara ya 229 ifutwe. | Rais awe huru kuteua kwa kuzingatia utaratibu na kanuni za uteuzi wa watendaji na watumishi wa vyombo vya ulinzi na usalama. | Ibara ya 229 inakuwa ibara ya 245 na inabaki kama ilivyo. |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | (iii) Katika aya ya 229 inayohusu uteuzi wa Mkuu wa Jeshi la Polisi la Jamhuri ya Muungano, kwa kuongeza maneno yafuatayo baada ya neno 'Taifa': "na kuthibitishwa na Bunge." | | |
| | | (iv) Ibara ya 229- Mkuu wa Jeshi la Polisi aidhinishwe na Bunge, Mchakato pia uwe wa wazi: wa kutangaza, wahusika kuomba, usaili, kupendekezwa, kuteuliwa na Rais na kuidhinishwa na Bunge. | | |
| | | (i) Ibara hii igawanywe katika Ibara ndogo (2) Ibara ya 1 isomeke kama ifuatavyo:-<br>(1) "kutakuwa na mkuu wa jeshi la polisi la jamhuri ya muungano wa tanzania ambaye atateuliwa na rais baada ya kushauriana na baraza la ulinzi na usalama wa taifa".<br>(2). "inspekta jenerali wa polisi atateuliwa kutoka ndani ya jeshi la polisi Tanzania". | | |
| | | (ii) Iongezwe ibara ndogo ya (2) itakayosomeka kama ifuatavyo:<br>"(2) Baada ya kuteuliwa jina lake litapelekwa katika Bunge la Jamhuri ya Muungano lithibitishwe au kutothibitishwa". | | |
| | | (iii) iongezwe ibara ndogo ya (3) itakayoeleza maana ya neno Polisi, kama ifuatavyo:<br>(v) "(3) Polisi maana yake ni kikundi | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | cha Raia wa Tanzania kilichofundishwa ukakamavu na kupewa silaha nyepesi kwa ajili ya ulinzi na usalama wa raia na mali zao na sio vinginevyo". | | |
| | | (vi) Uteuzi wa Mkuu wa Jeshi la Polisi uwe wa kupokezana baina ya Washirika wa Muungano. | Vitu hivyo vimejitosheleza. | |
| | | (vii) Uteuzi wa Mkuu wa Jeshi la Polisi uthibitishwe na Bunge. | Ili aweze kuwajibishwa na Bunge kwa manufaa ya umma. | |
| | | (viii) Ibara hii ibaki kama ilivyo. | | |
| | | Mkuu wa Jeshi athibitishwe na Bunge. | Uteuzi kufanywa na Bunge utafanywa kwa uwazi na kujenga imani kwa wananchi. | |
| | | (iv) Isomeke kama ifuatavyo:<br>(ix) "Kutakuwa na Mkuu wa Jeshi la Posili ambaye ataomba kazi katika Tume ya Utumishi ya Jeshi la Polisi na ataomba kazi kwa misingi ya uwazi na kuthibitishwa na Bunge". | | |
| | | (x) Ibara hii ifutwe | | |
| | | Ibara hii ibaki kama ilivyo | | |
| | | (v) Uteuzi wa Mkuu wa Jeshi la Polisi Kuthibitishwa na Bunge | | |
| | | (vi) Uteuzi wake upendekezwe na Baraza la ulinzi na usalama wa Taifa na kupitishwa na Bunge na kuhojiwa maswali yatakayo onyesha kuwa ana weledi mpana katika masuala ya ulinzi | | |
| | | (vii) Mkuu wa polisi anaweza kuondolewa na Rais pekee baada | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | ya uchunguzi huru na bunge kuridhia | | |
| | | Mchakato wa uteuzi uwe wa wazi: wa kutangaza, wahusika kuomba, usaili, kupendekezwa, kuteuliwa na Rais na kuidhinishwa na Bunge. | | |
| 230. | Majukumu na uhuru wa Mkuu wa Jeshi la Polisi | (i) Ibara ya 230 Haipo, Inapendekezwa kwamba iwekwe ambayo kimsingi ikiwekwa itaainisha shughuli za Mkuu wa Jeshi la Polisi Kikatiba. | | 1. Ibara ya 230 inakuwa ibara ya 246.<br>2. Inasomeka kama ifuatavyo:<br>3. 246 (1) Mkuu wa Jeshi la Polisi atatekeleza majukumu ya kazi zake kwa uhuru na bila woga, upendeleo wala chuki, kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii na sheria za nchi. |
| | | (ii) Izungumzie Majukumu na Uhuru wa Mkuu wa Jeshi la Polisi | | |
| | | (iii) Ibara ibakie na ieleze mchakato wa uteuzi wa Mkuu wa Jeshi la Polisi na madaraka yake | | |
| | | (iv) Ibara hii ifutwe | | |
| | | (v) Ibara ibaki kama ilivyo. | | |
| 231. | Tume ya Utumishi wa Jeshi la Polisi | (i) Ziongezwe ibara nyingine zitakazoeleza sifa za Wajumbe wa Tume ya Jeshi la Polisi kama ifuatavyo:<br>"(a) Mtu mwenye sifa ya kuwa Jaji wa Mahakama ya Juu;<br>(b) Wajumbe wawili ambao ni Polisi wa ngazi za juu wenye fani mbalimbali wenye weledi wa hali ya juu, heshima na nidhamu;<br>(c) Wajumbe wengine wawili waliotumikia umma kwa uadilifu na weledi mkubwa;<br>(d) Mkuu wa Jeshi la Polisi." | | Ibara ya 231 inakuwa ibara ya 247 na inabaki kama ilivyo. |
| | | (ii) Katika Ibara ndogo ya (2) | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | yaoengezwe maneno mwisho wa sentensi “na sheria ya Bunge”. | | |
| | | (iii) Iongezwe Ibara ndogo mpya itakaosomeka kama ilivyo Ibara ya 199 ya Rasimu. | | |
| | | (iv) Ibara hii ibaki kama ilivyo. | | |
| | | (v) Ibara ya (2)(c) maneno “Katiba hii” yafutwe na badala yake isomeke “Katiba ya Jamhuri ya Muungano”. | | |
| | | (vi) Ibara ya 231(1) Ibaki kama ilivyo | | |
| | | (vii) Katika Ibara ya 231(2) maneno…na sheria ya Bunge” yaongezwe | | |
| | | (viii) Katika Ibara ya 231(3) Iongezewe maneno kutoka Ibara ya 199 ya Rasimu | | |
| | | (ix) Miongoni mwa wajumbe wa Tume hii wawemo:<br>1. Mtu mwenye wadhifa wa Jaji wa Mahakama Kuu;<br>2. Polisi wawili wastaafu;<br>3. Watu watatu wenye maadili mema na amabao wamewahi kuwa watumishi wa umma<br>4. Mkuu wa polisi<br>5. Naibu Mkuu wa polisi | | |
| | | (x) Majukumu ya Tume iwe ni pamoja na kuajiri,kupandisha vyeo, kuhamisha vituo vya kazi na masuala ya nidhamu tu | | |
| | | (xi) Ibara ya 231. Tume ya Utumishi ya Jeshi la Polisi. Muundo, na utaratibu wa uundaji wake vielezwe. Mengine yawe kama | | |

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Maoni* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| | | katika 229. | | |
| | | (xii) Tume iwe na wajumbe wafuatao<br>1. Mtu yeyote mwenye sifa ya kuwa Jaji wa Mahakama ya Juu.<br>2. Wajumbe wawili ambao ni polisi wa ngazi za juu wenye fani mbalimbali na weledi wa hali ya juu, heshima na nidhamu.<br>3. Wajumbe wengine wawili walioytumikia umma kwa uadilifu na weledi mkubwa.<br>4. Mkuu wa Jeshi la Polisi | | |
| | | (xiii) Tume ya Utumishi ya vyombo vyote vya Ulinzi iwe moja | | |
| 232. | Polisi wa Washirika wa Muungano | (i) Ibara ya 232 ifutwe. | Utaratibu unaopendekezwa utasababisha mgongano wa kiutendaji na kiusalama.<br>Hivyo Jeshi la Polisi liwe moja tu. | Ibara hii imefutwa |
| | | (ii) Ibara ndogo ya (1) na (2) zifutwe na badala yake Ibara hii isomeke "Ni marufuku kwa nchi washirika wa Muungano kuanzisha vikosi vya Ulinzi na Usalama nje ya vikosi rasmi vya Ulinzi na Usalama vya Muungano. | Kwa mujibu wa ibara hii, vikosi vyote vya aina hiyo vilivyopo sasa vitaingizwa kwenye mfumo wa vyombo vya Ulinzi na Usalama. Ili suala la ulinzi na usalama liwe la muungano kwa asilimia mia moja. | |
| | | (iii) Ibara ya 232 (1)- Polisi liwe jambo la Muungano | Mlolongo wa madaraka/amri (*Chain of* | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | *command*) utaathirika kwa kutenguka na unaweza kuwa chanzo cha uhaini. | |
| | | (iv) Ibara ya 232 ifutwe. | Inarudia yaliyomo katika ibara ya 227. | |
| | | | (a) Mambo yote ya Ulinzi yawe chini ya Muungano.<br>(b) Kuepusha mgongano wa madaraka.<br>(c) Ulinzi na usalama ni jambo la Muuungano.<br>(d) Vikosi vya Polisi vitaleta chokochoko katika Muungano.<br>(e) Itaondoa hofu kwa nchi Washirika kuagiza vifaa vya Jeshi, Polisi nk. | |
| | | (v) Maneno "Washirika wa Muungano" yafutwe. | | |
| | | (vi) Ibara hii ibaki kama ilivyo. | (a) Ni haki na wajibu kila mshirika wa Muungano kuwa na kikosi chake cha ulinzi.<br>(b) Kudumisha na kuwaenzi waasisi wa Muungano kwa kuamua Zanzibar kuwa na vikosi vyake vya ulinzi. | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | (vii) Ibara hii ihamishiwe katika ibara ya 223. | (a) Ili kuondoa mgongano.<br>(b) Kupunguza mlundikano wa majeshi.<br>(c) Ili kuimarisha ulinzi kila upande. | |
| | | (viii) Kuwe na Jeshi moja tu la Polisi | | |
| | | (ix) Ibara hii ifutwe | | |
| | | (x) Itazamwe upya kuzingatia muundo wa serikali mbili | | |
| | | (xi) Polisi iongezwe katika masuala ya muungano | | |
| | | (xii) Itumike "vikosi vya usalama" badala ya "vikosi vya ulinzi" | | |
| | | (xiii) Ibara ya 232. Isomeke " Nchi Washirika haziwezi kuanzisha vikosi vyake. Mlolongo wa madaraka/amri (Chain of command) utaathirika kwa kutenguka na unaweza kuwa chanzo cha uhaini | | |
| | | (xiv) Washirika wa Muungano waruhusiwe tu kuanzishwa majeshi ya polisi | (d) | |
| | | (xv) Majeshi yote yawe chini ya Rais | (e) | |

## (c) Idara ya Usalama ya Jamhuri ya Muungano

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| 233. | Kuanzishwa kwa Idara ya Usalama | (i) Ibara ya 233-kazi ya kulinda Katiba iwe kazi ya Jeshi la Ulinzi | | Ibara 233 inakuwa ibara ya 248 na Inabaki kama ilivyo. |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | ya Taifa | wa Tanzania na siyo Idara ya Usalama wa Taifa. Idara ya Usalama iwe na jukumu la kulinda usalama wa nchi na viongozi wake kwa mujibu wa sheria. | | |
| | | (ii) Ibara ya 233(3) isomeke: Idara ya Usalama wa Taifa itekekeze majukumu yake kwa mujibu Katiba na ifanye kazi kwa manufa ya taifa. | | |
| | | (iii) Ibara hii ibaki kama ilivyo. | | |
| | | (iv) Ibara hii irekebishwe ili ajira itangazwe kwa wananchi wote. | (a) Ili kuondoa ajira kwa watoto wa viongozi.<br>(b) Kutoa fursa kwa raia wote kuajiriwa katika Idara hiyo.<br>(c) Kuondoa ubaguzi wa ajira katika Idara hiyo. | |
| | | (v) Ibara ndogo ya (2) maneno “kutii Katiba hii” yafutwe. | Hii ni Katiba ya Jamhuri ya Muungano. | |
| | | (vi) Itazamwe upya kuzingatia muundo wa serikali mbili | | |
| | | (vii) Kazi ya kulinda iwe kazi ya Jeshi la Ulinzi wa Tanzania na siyo Idara ya Usalama wa Taifa. Idara iwe na jukumu la kulinda usalama wa nchi na viongozi kwa mujibu wa sheria. | | |
| 234. | Uteuzi wa Mkurugenzi wa Idara ya Usalama wa Taifa | (i) Ibara ya 234 ifutwe. | Rais awe huru kuteua kwa kuzingatia utaratibu na kanuni za uteuzi wa watendaji na watumishi wa vyombo vya ulinzi na | Ibara 234 inakuwa 249 na inabaki kama ilivyo. |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | usalama. | |
| | | (ii) Katika aya ya 234 inayohusu uteuzi wa Mkurugenzi wa Idara ya Usalama wa Taifa, kwa kuongeza maneno yafuatayo baada ya neno 'Taifa': "baada ya kuthibitishwa na Bunge." | | |
| | | (iii) Ibara ya 234- Mkurugenzi Usalama wa Taifa, apatikane kwa kuidhinishwa na Bunge. | | |
| | | (iv) Kuwe na mgawanyo wa madaraka kwa kuzingatia pande zote mbili za Muungano. | | |
| | | (v) Ibara hii ibaki kama ilivyo. | | |
| | | (vi) Mkurugenzi wa Usalama wa Taifa athibitishwe na Bunge. | (a) Kujenga utumishi kwa umma;<br>(b) Wananchi kuwa na imani na mambo ya usalama. | |
| | | (vii) Ibaki kama ilivyo | | |
| | | (viii) Uteuzi wa Mkurugenzi wa Usalama wa Taifa uidhinishwe na Bunge | | |
| | | (ix) Mkurugenzi apendekezwe na Rais baada ya kushauriana na Baraza la Ulinzi wa Taifa na atathibitishwa na Bunge | | |
| | | (x) Bunge liwe na kamati za kusimamia usalama | | |
| 235. | Usalama wa Washirika wa Muungano | (i) Ibara ya 235 ifutwe. | Muundo unaopendekezwa katika Rasimu hii unaweza kusababisha mgongano wa kiutendaji hivyo kuhatarisha Muungano | 1. Ibara ya 235 inakuwa ibara ya 250.<br>2. Marginal Note inakuwa: "Usalama Katika Nchi washirika."<br>3. Ibara imeandikwa upya |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | badala ya kuulinda. | na itasomeka kama ifuatavyo:<br>249(1) "Bila ya kuathiri masharti ya sura hii, wakuu wa nchi washirika wanaweza kuagiza jeshi la polisi au idara ya usalama wa Taifa kuchukua hatua yoyote ambayo ni muhimu kwa ajili ya kulinda, au kuimarisha usalama wa eneo lolote la nchi mshirika husika."<br>(2) Bunge litatunga sheria itakayoainisha masharti yanayohusu namna bora ya utekelezaji wa ibara ndogo (1). |
| | | (ii) Ibara ya 235- Wajibu huu uwe katika mamlaka ya Muungano tu. Ni jambo la Muungano. | Ni hatari kwa usalama wa nchi Washirika na kwa Muungano kama hazifuati maelekezo ya vyombo vinavyosimamia ulinzi na usalama wa Taifa. | |
| | | (iii) Washirika wa Muungano wasiruhusiwe kuanzisha vyombo vya ulinzi bali suala hili liwe chini ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano | Ulinzi katika Taifa lolote ni mojawapo ya mambo ya msingi ambayo lazima yawe na sura ya Utaifa.<br><br>Hii ni kwa minajili ya kuimarisha Muungano. | |
| | | (iv) Ibara hii ifutwe. | (a) Kuondoa mgongano wa utendaji wa chombo cha usalama jambo litakalosababisha usumbufu kwa raia.<br>(b) Ili kuondoa ubaguzi kati ya vikosi vya Tanzania Bara na Zanzibar.<br>(c) Inakinzana na mambo ya Muungano | |
| | | (v) Ibara hii ibaki kama ilivyo. | (a) Itaimarisha usalama wa watu na mali zao katika serikali zote mbili na Serikali ya Muungano.<br>(b) Kabla ya 1984, kila upande wa | |

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Maoni* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| | | | Muungano ulikuwa na Idara yake ya Usalama wa Taifa na hakuna matatizo yoyote yoliyotokea. | |
| | | (vi) Ifutwe kwa kuwa ni jukumu la Serikali ya Jamhuri ya Muungano tu kuunda taasisi za usalama | | |
| | | (vii) Ibara hii itazamwe upya kuzingatia muundo wa Serikali mbili | | |
| | | (viii) Ifutwe kwa kuwa muundo huu unaweza kusababisha migongano ya kiutendaji na kuhatarisha Muungano. | | |

# SURA YA KUMI NA SITA YA RASIMU

## MENGINEYO

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Maoni* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| 236. | Masharti kuhusu utaratibu wa kukabidhi madaraka | (i) Ibara ya 236(1) ziongezwe Serikali za Mitaa;<br>(ii) Kiongezwe kipengele cha (e) kisomeke "iwapo kiongozi wa Serikali za mitaa atawasilisha kwenye mamlaka iliyomchagua". | | Ibara 236 inakuwa 251 na inabaki kama ilivyo. |
| | | (iii) Ibara ya 236(1) itaje na Mhimili wa Mahakama. | | |
| | | (iv) Ibara ya 236(3) ziongezwe Serikali za mitaa. | | |
| | | (v) 236 ibaki kama ilivyo. | Inajitosheleza. | |
| 237. | Masharti kuhusu madaraka ya kazi | (i) Ibara ya 237(1) itamke kuwa muda wa kukaimu madaraka kwa viongozi usizidi miezi 6. | Kukaimisha nafasi za uongozi kunazorotesha maendeleo. | Ibara 237 inakuwa 252 na Marginal Note imerekebishwa na inasomeka "Masharti kuhusu kukabidhi madaraka". |
| | | (ii) Katika Ibara ndogo ya (1) maneno "Jaji wa Mahakama ya Rufani" yafutwe na badala yake iandikwe 'Jaji wa Mahakama Kuu". | | |
| | | (iii) Muda wa kukaimu madaraka ya uongozi uwe ni mwaka mmoja. | Ni vigumu kuziba nafasi ya uongozi wa kisiasa kwa muda mfupi. | |
| | | (iv) Muda wa kukaimu uongozi wa kisiasa iwe ni mwaka mmoja na kwa watumishi wa umma iwe ni wiki mbili. | Ni vigumu kuziba nafasi ya uongozi wa kisiasa kwa muda mfupi. | |
| | | (v) 237 ibaki kama ilivyo. | Inajitosheleza. | |
| | | | | Imeongezwa ibara mpya 253 inayozungumza "zuio kwa |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | | baadhi ya watumishi wa umma kutogombea nyadhifa za kisiasa." |
| 238. | Ufafanuzi | (i) Ufafanuzi utolewe kwa maneno:<br>(a) msimamizi wa uchaguzi (Ibara ya 184(8)(f);<br>(b) kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni;<br>(c) mlemavu;<br>(d) miiko maalum;<br>(e) Jumuiya ya Madola.<br>(f) Naibu Waziri,<br>(g) Tamko,<br>(h) Kiongozi wa umma, | | Ibara ya 238 inakuwa ibara ya 254. |
| | | (ii) Ibara ya 238 (1) Inapendekezwa kwamba "Tanzania Bara" iondolewe na itambuliwe "Tanganyika"<br>Isomeke:<br>"Tanganyika" maana yake ni eneo lote la Jamhuri ya Muungano ambalo ndilo zamani lilikuwa eneo la Jamhuri ya Tanganyika. | | |
| | | (iii) Maneno "Naibu Waziri" yafafanuliwe; | | |
| | | (iv) Kuongeza tafsiri ya neno Utamaduni ambayo itasomeka kama ifuatavyo:<br>"Utamaduni maana yake ni mwenendo wa maisha ya kila siku ya jamii na taratibu zao za kuendesha mambo katika mazingira yao zinazowatofautisha wao na jamii nyingine, nazo hupatikana katika mila na desturi, | Ili kuweka wazi dhana ya maadili katika jamii, aidha inapendekezwa tafsiri hii iwekwe katika Sura ya Kwanza Sehemu ya Kwanza. | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | lugha, sanaa, maliasili, malikale, michezo, mapokeo na historia, uzalishaji mali, malezi, jando na unyago, imani, itikadi na miiko". | | |
| | | (v) tafsiri ya neno Jeshi ifutwe na badala yake iandikwe kama ifuatavyo: "Jeshi maana yake ni kundi la Raia wa Tanzania lililofundishwa mbinu za medani na utendaji wa kivita na kukabidhiwa silaha nzito kwa ajili ya ulinzi wa nchi na mipaka yake, dhidi ya aina yoyote za chokochoko za nchi za nje". | | |
| | | (vi) Tafsiri ya neno "Jaji" ifutwe na badala yake iandikwe kama ilivyo katika Katiba ya sasa. | | |
| | | (vii) Tafsiri ya neno "Serikali" ifutwe na badala yake iandikwe kama ilivyo katika Katiba ya sasa na mwisho yaongezwe maneno "kwa mujibu wa Katiba hii na sheria za nchi". | | |
| | | (viii) Tafsiri ya neno 'Zanzibar" ifutwe na badala yake iandikwe kama ifuatavyo: "Zanzibar" maana yake ni nchi ambayo eneo la mipaka yake ni eneo lote la Visiwa vya Unguja na Pemba pamoja na visiwa vidogo vilivyoizunguka bahari yake ambayo kabla ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ikiitwa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar". | | |
| | | (ix) Iongezwe tafsiri ya neno "Naibu | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | Waziri" ambayo itakuwa kama ifuatavyo: "Naibu Waziri" maana yake ni mtu au watu walioteuliwa na Rais kwa ajili ya kumsaidia Waziri katika kutekeleza majukumu yake na watafahamika hivyo na si vinginevyo". | | |
| | | (x) Neno "mahakama" lisomeke kuwa ni "mahakama yoyote yenye mamlaka katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na inajumuisha mahakama iliyoundwa kwa amri ya Jeshi". | | |
| | | (xi) Neno "jeshi" lisomeke kuwa ni "Jeshi la ulinzi la wananchi wa Tanzania". | | |
| | | (xii) Iongezwe tafsiri ya neno "Kiongozi wa juu" kama ilivyorejewa katika Ibara ya 132. | | |
| | | (xiii) Kuna haja ya kuongeza tafsiri ya maneno "uwiano" na "usawa". | | |
| | | (xiv) Neno shirikisho litafsiriwe kwenye Ibara ya 238 inayohusu ufafanuzi ili kuleta maana moja kwa watu wote. | | |
| | | (xv) Neno askari lisomeke "ni mtu aliyeandikishwa katika Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania au aliyeajiriwa katika Idara ya Polisi, idara ya Magereza na idara ya wanyama pori". | | |
| | | (xvi) Tafsiri ya neno" Serikali" iboreshwe ili isomeke kama ilivyo kwenye Ibara ya 6, 8 na 151 ya | (a) Lengo ni kufafanua zaidi na kuweka wazi misingi ya mamlaka | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | Katiba ya sasa. | kuwa ni ya watu,<br>(b) Kufafanua malengo makuu ya serikali,<br>(c) Kutaja serikali zilizomo ndani ya Muungano zikiwemo Serikali za Mitaa, na mtu yeyote anayetekeleza madaraka yoyote kwa niaba ya Serikali. | |
| | | (xvii) 238 Tafsiri ya "kiongozi wa umma" maana yake "Ni mtu yoyote ambaye anatumikia katika sehemu ya mamlaka ya serekali ya Jamhuri ya Muungano" | | |
| 239. | Jina la Katiba na kuanza kutumika | (i) ibara ndogo ya (1), ondoa tarakimu "2013" na weka maneno "mwaka ambao Katiba itaanza kutumika". | | Ibara ya 239 inakuwa ibara ya 255 inazungumzia jina la katiba na tarehe ya kuanza kutumika. |
| | | (ii) Ibara ndogo ya (2), ondoa maneno "kuzinduliwa rasmi" na weka maneno "kusainiwa na Rais". | | |
| | | | | |
| | | (iii) Tarehe ya kuanza kutumika iwe tarehe ya uzinduzi wa Katiba utakaofanywa na Rais. | | |
| 240. | Kufutwa kwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Mwaka 1977 | (i) Kabla ya ibara hii, iwepo Ibara mpya itakayoeleza kuhusu masharti ya mpito kabla ya kuanza kutumika rasmi Katiba Mpya. | Ili kuweza kuandaa mazingira ya kuifanya Katiba Mpya kufanya kazi sawa sawa.<br>Ili kutoa fursa ya kuandaa sheria zitakazoweka utaratibu kabla ya kuanza | Ibara ya 240 itakuwa ibara ya 256 ambayo inazungumzia "kufutwa kwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977.' |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | kutumika kwa katiba Mpya.<br>Ili kuondoa matatizo yanayoweza kujitokeza.<br>Ili kuweza kufanya marekebisho kwa sheria zilizopo na kuruhusu Katiba Mpya kuweza kufanya kazi ipasavyo. | |
| | | (ii) Katiba hii isitumike hadi pale nchi Washirika zitakapokuwa zimeunda Katiba zao kwa kuzingatia na kufuata masharti na maelekezo ya Katiba hii ya Muungano. | | |

## MAPENDEKEZO MAPYA

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Maoni* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| | Masharti yatokanayo na masharti ya mpito | (i) Kuwe na Kifungu chenye masharti na maelekezo mahsusi au juu ya utekelezaji wa Katiba hakipo kabisa. | | Imeongezwa sura mpya ya kumi na saba inayohusu masharti yatokanayo na masharti ya mpito. |
| | | (ii) Kuna haja ya kuwa na Ibara inayoweka utaratibu wa utekelezaji wa Katiba ikibainisha vyombo maalumu vya usimamizi, uratibu na uhakiki wa utekelezaji huo. Mfano Katiba ya Kenya inaunda vyombo viwili muhimu vinavyofanya kazi kwa kushirikiana vikihusisha na vyombo vingine vya dola kama itakiwavyo na Katiba. | | |
| | | (iii) Aidha, kuna maelekezo na masharti ya jumla kwenye Ib. 258 katika Sura ya 17 Mambo ya Jumla (General Provisions), kuhusu jambo hili muhimu. Hasa, katika Ib. 262, Sura ya 18 (Mambo ya Kipindi cha Mpito) na Nyongeza ya Sita ya Katiba ndipo Katiba imeunda: | | |
| | | (iv) Kifungu chenye masharti na maelekezo mahsusi au juu ya utekelezaji wa Katiba hakipo kabisa. | | |
| | | (v) Kuna haja ya kuwa na Ibara inayoweka utaratibu wa utekelezaji wa Katiba | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | ikibainisha vyombo maalumu vya usimamizi, uratibu na uhakiki wa utekelezaji huo. | | |
| | | (vi) Mfano Katiba ya Kenya inaunda vyombo viwili muhimu vinavyofanya kazi kwa kushirikiana vikihusisha na vyombo vingine vya dola kama itakiwavyo na Katiba. | | |
| | | (vii) Aidha, kuna maelekezo na masharti ya jumla kwenye Ib. 258 katika Sura ya 17 Mambo ya Jumla (General Provisions), kuhusu jambo hili muhimu. Hasa, katika Ib. 262, Sura ya 18 (Mambo ya Kipindi cha Mpito) na Nyongeza ya Sita ya Katiba ndipo Katiba imeunda: | | |
| | | (viii) Kuwe na Sura mahsusi kwa ajili ya kuanzishwa Jamhuri ya watu wa Tanganyika.<br>(ix) Inapendekezwa kuwepo na orodha ya sheria mpya au mabadiliko ya sheria na ratiba ya utekelezaji iwekwe kufuatana na Katiba Mpya;<br>(x) Inapendekezwa kuwa ndani ya miezi 12 sheria ya haki ya kupata habari na ile ya huduma za vyombo vya habari ziwe zimetungwa. | | |
| | Watendaji kuidhinishwa na Serikali | (i) Kuwe na ibara itakayoweka utaratibu wa Watendaji Wakuu wote wa muhimili wa | (a) Lengo ni kupunguza mlolongo wa wateule kuhitaji | Ibaki kama ilivyo. |

| ***Ibara Na.*** | ***Kichwa cha Habari*** | ***Maoni ya Mabaraza*** | ***Sababu ya Maoni*** | ***Marekebisho ya Tume*** |
|---|---|---|---|---|
| | | Serikali kiudhinishwa na Bunge. | kidhinishwa na Bunge.<br>(b) Rais aachiwe baadhi ya watendaji wakuu afanye uteuzi wake moja kwa moja ili asipunguziwe sana madaraka. | |
| | | (ii) Kiundwe chombo cha kusimamia mishahara na maslahi. | | |
| | | (iii) Iongezwe Ibara mpya itakayoelezea Waziri Mwandamizi, ambayo itakuwa kama ifuatavyo: | | |
| | Haki za Wanaume | Iongezwe Ibara mpya itakayoeleza haki za wanaume na haki hizo ni pamoja na:<br>(i) kuheshimiwa utu wake;<br>(ii) kuwa salama dhidi ya unyonyaji na ukatili;<br>(iii) kushiriki katika uchaguzi na ngazi zote za maamuzi bila ubaguzi;<br>(iv) kupata huduma ya juu ya afya inayopatikana;<br>(v) kupata ajira sawa na wanawake;<br>(vi) kulindwa ajira yake wakati wa ugonjwa na dhidi ya ubaguzi wa aina yoyote. | Kuondoa unyanyasaji wa wanaume kutokana na kutolindwa kisheria. | Ibaki kama ilivyo |
| | Haki ya Jamii Kumiliki Rasilimali za Asili | Iongezwe ibara mpya itakayosomeka kama ifuatavyo:<br><br>"Haki ya jamii kumiliki rasilimali | Ili kuhakikisha kwamba wananchi wanashirikishwa kikamilifu katika | Ibaki kama ilivyo |

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Maoni* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| | | za asili”<br>(1) Rasilimali asili zote, yaani ardhi, madini, mafuta na gesi asilia, maji na misitu na wanyama pori, ni mali ya Watanzania na zitatumika kwa manufaa ya watanzania.<br>(2) Itakuwa ni marufuku kwa mamlaka ya serikali ya Jamhuri ya Muungano au mamlaka za Washirika wa Muungano kutwaa rasilimali asili kwa malengo ya kuzigawa kwa wawekezaji au kwa malengo yoyote bila kwanza kupata ridhaa huru na ya ufahamu (free, prior informed consent) ya wananchi wanaoishi kwenye eneo zinapopatikana rasilimali hizo;<br>(3) Bunge litatunga sheria itakayoweka masharti na utaratibu wa wanachi wa maeneo zinapopatikana rasilimali asili kutoa ridhaa huru na ya ufahamu wakati mamlaka ya nchi inapofanya uamuzi wa kutwaa rasilimali hizo kwa wawekezaji au kwa malengo mengine yoyote;<br>(4) Sheria iliyotajwa katika ibara ndogo ya (3) itaweka masharti na utaratibu utakaowezesha wananchi wa maeneo hayo kufaidika na rasilimali zinazopatikana kwenye maeneo yao, pale zinapotwaliwa kwa | maamuzi yanayohusu rasilimali asili zinazopatikana katika maeneo yao na vile vile kufaidika na rasilimali hizo pale zinapotwaliwa kwa malengo ya uwekezaji au kwa malengo mengine. | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | wawekezaji au kwa malengo mengine yoyote;” | | |
| | Wajibu wa Waziri Mwandamizi. | (i) Kutakuwa na Waziri Mwandamizi atakayeteuliwa na Rais na kuidhinishwa na Bunge kutokana na sifa za kuwa Waziri kwa mujibu wa Katiba hii.<br>(ii) Waziri Mwandamizi atakuwa na madaraka juu ya udhibiti, usimamiaji, utekelezaji wa siku hadi siku wa kazi na shughuli za serikali ya Jamhuri ya Muungano.<br>(iii) Waziri Mwandamizi atakuwa kiongozi wa shughuli za serikali bungeni.<br>(iv) Waziri Mwandamizi katika utekelezaji wa madaraka yake, Waziri Mkuu atatekeleza au kusababisha utekelezaji wa jambo lolote au mambo yoyote ambayo Rais ataagiza kwamba yatekelezwe. | | Ibara mpya ya 99 kuhusu Waziri Mwandamizi imewekwa. |
| | | (v) Iongezwe Ibara itakayoruhusu mshirika wa Muungano kuweza kujiondoa katika Muungano na inayoruhusu nchi nyengine kuweza kujiunga na Muungano. | | |
| | Haki ya Kinga na Tiba ya Magonjwa | Iongezwe Ibara mpya itakayoeleza haki ya kinga na tiba ya magonjwa kwa watu wote itakayosomeka kama ifuatavyo:<br>« Kila mtu ana haki ya kupata | Lengo la ibara hii ni kuhakikisha wananchi wana afya njema kwa ustawi wa nchi na hasa makundi yaliyo katika | Ibaki kama ilivyo |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | kinga na tiba ya magonjwa bila kubaguliwa kwa misingi ya uwezo, dini, kabila, umri, rangi, ulemavu, jinsi au itikadi.<br>(2) Kwa madhumuni ya kuhifadhi haki ya mtu kupata kinga na tiba ya magonjwa, mamlaka ya nchi itaweka utaratibu wa kisheria kuhusu namna mtu atapata huduma ya kinga na tiba ya afya. » | mazingira magumu kama wazee, watoto, wajane, wagane, yatima, walemavu nk. | |
| | | (vi) Iongezwe Ibara itakayoruhusu mshirika wa Muungano kuweza kujiondoa katika Muungano na inayoruhusu nchi nyingine kuweza kujiunga na Muungano. | | |
| | Haki za Walaji | (a) Walaji wana haki ya:<br>(b) kupata huduma na bidhaa zenye ubora unaokubalika;<br>(c) kupata habari muhimu kuhusu manufaa ya huduma na bidhaa husika;<br>(d) kulindwa dhidi ya afya zao, usalama na haki za kiuchumi;<br>(e) kulipwa fidia pale wanapopata madhara kutokana na huduma au bidhaa zisizofaa.<br>(f) (2) Bunge litatunga sheria ya kuhakikisha walaji wanalindwa na matangazo yenye ukweli na uhalisia wa ubora wa bidhaa husika, | | Ibaki kama ilivyo |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | matangazo lazima yazingatie maadili ya Kitanzania.<br>(3) Sehemu hii itahusu bidhaa na huduma zinazotolewa na serikali, watu binafsi na taasisi nyingine za ndani na nje ya nchi. | | |
| | Haki Zingine | Ziongezwe ibara mpya zitakazozungumzia mambo yafuatayo:<br>(g) Haki ya kupata chakula;<br>(h) Haki ya makazi bora;<br>(i) Haki ya utamaduni;<br>(j) Haki ya wananchi kuandamana kudai haki;<br>(k) Haki ya kupata maji safi;<br>(l) Haki ya hifadhi ya jamii;<br>(m) Haki ya likizo yenye malipo na uhuru wa kuunda na kujiunga na chama cha siasa au kijamii;<br>(n) Haki ya kumiliki uchumi na rasilimali za nchi;<br>(o) Haki ya kupata chakula;<br>(p) Haki ya makazi bora;<br>(q) Haki ya utamaduni; | Ni haki za muhimu na za msingi kuainishwa katika Katiba. | Ibaki kama ilivyo |
| | | (r) Haki ya kuishi kwa amani na usalama.<br>(s) Serikali itaweka utaratibu wa kuhakikisha usalama na amani ya raia kwa kuhakikisha Taifa linalindwa na kuhifadhiwa.<br>(t) Haki ya Maendeleo.<br>(u) Kila raia ana haki ya maendeleo; | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | (v) Serikali itaweka miundombinu, sera na sheria zinazowezesha wananchi wake kupata maendeleo;<br>(w) Maendeleo hayo yatagawanywa katika uwiano sawa.<br>(x) Haki ya kuandamana na kukusanyika kutoa maoni.<br>(y) Kila mtu ana haki ya kukusanyika kwa amani bila silaha, kuandamana, kugoma na kupeleka malalamiko yao kwa maandishi kwa mamlaka husika.<br>(z) Haki ya kuwa na familia<br>(aa) Familia ni mahali pa kwanza pa makuzi na mahusiano ya kijamii ambayo Serikali inapaswa kutoa ulinzi;<br>(bb) Kila mtu mzima kwa hiari yake ana haki ya kuunganika na mtu wa jinsi tofauti kwa lengo la kukuza mahusiano ya ndoa, kuendeleza uzazi na kuanzisha familia;<br>(cc) Wanandoa wana haki sawa wakati ndoa inapoanza, inapoendelea na hata inapovunjika;<br>(dd) Bunge litatunga sheria kulinda na kuongoza | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | mahusiano ya ndoa.<br>(ee) Haki ya afya.<br>(ff) Kila mtu anahaki ya kupata:<br>(gg) Huduma bora za afya ikiwepo na kufikika kwa huduma za afya ikiwemo afya ya uzazi;<br>(hh) Kupata nyumba yenye viwango vinavyokubalika;<br>(ii) Kuwa huru na njaa na kuhakikisha lishe bora inapatikana kwa watu wote;<br>(jj) Kupata maji safi na salama kwa kiwango kinachohitajika;<br>(kk) Kupata hifadhi ya jamii;<br>(ll) Kupata elimu ya kutosha na taarifa mbalimbali kuhusu masuala ya afya na lishe.<br>(mm) (2) Mtu yeyote hatanyimwa haki ya kupata huduma za dharura za afya.<br>(nn) (3) Serikali itatoa huduma za hifadhi za jamii kwa watu wasiojiweza na wategemezi wao. | | |
| | Idara ya Takwimu za Taifa | (i) Iongezwe Ibara mpya itakayohusu kuanzishwa kwa idara ya Takwimu za Taifa ambayo itakuwa kama ifuatavyo:<br>(ii) Serikali itaanzisha Mamlaka ya Taifa ya Takwimu.<br>(iii) Kipengele cha dini katika | Rasimu itoe uzito unaostahiki katika suala la takwimu za Taifa na sense ili kuwe na umakini wenye kuleta tija katika zoezi la sensa. | Ibaki kama ilivyo |

| *Ibara Na.* | *Kichwa cha Habari* | *Maoni ya Mabaraza* | *Sababu ya Maoni* | *Marekebisho ya Tume* |
|---|---|---|---|---|
| | | sensa ya watu na makazi kiwepo. | | |

## NYONGEZA

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya "Tume |
|---|---|---|---|---|
| 249. | Nyongeza | (i) Katika orodha ya mambo ya Muungano, aya ya kwanza ifutwe na badala yake isomeke "Katiba na Mihimili ya Dola ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania". | | Ibaki kama ilivyo |
| | | (ii) Mambo ya Muungano yawe kama ifuatavyo:<br>(a) Mahakama ya Rufaa na Mahakama ya Juu;<br>(b) Utumishi wa Umma katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano;<br>(c) Polisi;<br>(d) Mamlaka juu ya mambo ya Muungano;<br>(e) Mikopo na biashara za nje;<br>(f) Usafiri na usafirishaji wa anga;<br>(g) Utabiri wa Hali ya Hewa;<br>(h) Takwimu;na<br>(i) Kodi ya mapato inayolipwa na watu binafsi, ushuru wa forodha na ushuru wa bidhaa zinazotengenezwa nchini usiosimamiwa na idara ya forodha. | | |
| | | (iii) Mambo yafutayo yaongezwe | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya "Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | katika orodha ya mambo ya Muungano:<br>(a) Utumishi wa Umma;<br>(b) Bunge la Jamhuri ya Muungano;<br>(c) Mahakama Kuu na Rufani;<br>(d) Tume ya Haki za Binadamu;<br>(e) Tume Huru ya Uchaguzi; na<br>(f) Uhamiaji. | | |
| | | (iv) Uraia na Uhamiaji, mambo ya nje na usajili wa vyama vya siasa viondoshwe katika orodha ya mambo ya Muungano. | (a) Kwanza kabisa kuipa uwezo wa kisheria Zanzibar kujiunga na Mashirika na Taasisi za kimataifa ulimwenguni kama vile Umoja wa Mataifa, Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, Shirikisho la Mpira wa Miguu Ulimwenguni n.k.<br>(b) Kutoa na kukuza fursa kwa nchi washirika wa Muungano hususan Zanzibar kujitangaza kimataifa ulimwenguni, fursa ambayo Zanzibar imeikosa kwa kipindi kirefu sana licha ya kuhitajika uwepo | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya "Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | | wake.<br>(c) Kuiwezesha Zanzibar kurudisha uhusiano wake wa kibalozi na mataifa mbali mbali uliokuwepo kabla ya Muungano wa 1964.<br>(d) Kuna umuhimu mkubwa wa kuilinda Zanzibar kutokana udogo wa eneo lake, uhaba wa ardhi na rasilimali nyinginezo. Uhamiaji wa kawaida tu unaweza ukasababisha mfadhaiko mkubwa juu ya matumizi ya rasilimali ardhi.<br>(e) Vile vile kwa upande wa kuenzi na kutunza utamaduni, mila, desturi na demografia ya Wazanzibari, suala la kudhibiti kwa kuratibu uhamiaji lina umuhimu wa kipekee Zanzibar. | |
| | | (v) Aya ya 4 katika orodha ya mambo ya Muungano iandikwe "sarafu, fedha za kigeni na Benki Kuu". | | |
| | | (vi) Sarafu na Benki Kuu zifutwe na ziondoshwe katika orodha ya | (a) Ili kutoa uwezo, mamlaka na fursa | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya "Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | Mambo ya Muungano. | kwa Nchi washirika wa Muungano katika kujipangia, kudhibiti na kuratibu sera za Uchumi kikamilifu hatimae kuharakisha maendeleo katika mambo yote yahusuyo uchumi.<br>(b) Vipau mbele vya uchumi vya nchi washirika wa Muungano vinatofautiana, hali ambayo inaleta mvutano wa ukuzaji wa vipaumbele vya uchumi na mgawanyo wa faida inayotokana na shughuli za Benki Kuu. | |
| | | (vii) Mambo ya Nje yabaki katika orodha ya mambo ya Muungano, lakini inapendekezwa kuwa Rasimu ya Katiba ioneshe wazi kuwa mambo yote ya nje yatakuwa ni ya uwiano sawa kwa asilimia mia moja kiuwiano katika mambo yote husika baina ya washirika wa Muungano. Kwa mfano, uteuzi wa mabalozi, Mawaziri 8 wa Nchi katika Afisi za Ubalozi wa Nje, mgao wa misaada mbali mbali, mikopo na masuala | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya "Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | yote yatayohusiana na Mambo ya Nje. | | |
| | | (viii) Makubaliano ya Muungano "Articles of the Union" yatajwe kama ni jambo la kwanza katika orodha ya mambo ya Muungano. | Katiba iweke utaratibu wa wazi wa jinsi makubaliano ya Muungano yatakavyokuwa yanarekebishwa. | |
| | | (ix) Mambo yafuatayo yaongezwe katika orodha ya mambo ya Muungano:<br>(a) Mikataba ya kimataifa ambayo Tanzania imeridhia;<br>(b) Mambo ya Nje;<br>(c) Elimu ya Juu na Baraza la Taifa la Mitihani;<br>(d) Utabiri wa hali ya hewa na usafirishaji wa anga na majini;<br>(e) Haki za binadamu;<br>(f) Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora<br>(g) Mahakama ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano;<br>(h) Mahakama ya Rufaa ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;<br>(i) Polisi;<br>(j) Utumishi katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano;<br>(k) Takwimu;<br>(l) Mamlaka ya Juu ya mambo ya hatari; | | |

| Ibara Na. | Kichwa cha Habari | Maoni ya Mabaraza | Sababu ya Maoni | Marekebisho ya "Tume |
|---|---|---|---|---|
| | | (m) Utafiti;<br>(n) Posta na simu;<br>(o) Udhibiti na usimamizi wa usafi wa mazingira. | | |
| | | (x) Mambo ya Muungano yaendelee kuwa 22. | | |
| | | (xi) Masuala ya Mipango na uchumi yaongezwe katika mambo ya Muungano. | Ili utekelezaji wa Dira na Mipango ya Maendeleo vifanywe kwa pamoja. | |
| | | (xii) Katika Orodha ya mambo ya Muungano yaongezwe mambo yafuatayo:<br>(a) Mahakama ya Jamhuri ya Muungano.<br>(b) Hifadhi ya Mazingira.<br>(c) Haki za Binadamu.<br>(d) Bunge.<br>(e) Tume ya Uchaguzi.<br>(f) Tume ya Maadili na Uwajibikaji.<br>(g) Utumishi katika Serikali ya Muungano.<br>(h) Tume ya Uratibu wa Mahusiano na Uratibu wa Serikali. | Masuala haya yanazungumziwa katika Katiba lakini hayamo katika Orodha ya Mambo ya Muungano. | |